Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA KUMI NA MBILI

**Kikao cha Thelathini na Moja - Tarehe 24 Julai, 2003**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Pius Msekwa) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge kabla hatujaanza katika *gallery* yetu leo tuna wageni wanaosikiliza majadiliano yetu nao ni pamoja na Mheshimiwa Rodney Phillip, Mwakilishi wa *UNICEF* hapa nchini pamoja na maafisa wake.

Vile vile tunaye Mheshimiwa Spika wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar na tunaye Balozi Ali Mchumo, ambaye anatuwakilisha Jumuiya ya Afrika Mashariki, huko Arusha. *(Makofi)*

Kikao cha 31 Waheshimiwa Wabunge kinaanza.

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:**

Hotuba ya Waziri wa Nishati na Madini kwa Mwaka wa Fedha 2003/2004.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA UWEKEZAJI NA BIASHARA:**

Taarifa ya Kamati ya Uwekezaji na Biashara kuhusu utekelezaji wa Wizara ya Nishati na Madini katika mwaka uliopita, pamoja na maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2003/2004.

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 299

**Sheria ya Udhibiti wa Usafiri wa Majini**

**MHE. DR. WILLIAM F. SHIJA** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali imepitisha sheria ya kudhibiti usafiri wa majini, na kwa kuwa usafiri katika Ziwa Victoria bado ni hafifu:-

(a) Je, ni matatizo gani yaliyojitokeza katika utekelezaji wa sheria hiyo hasa kwa wasafirishaji binafsi kama vile *M/S Claud Getg* wa Kamanga, *M/S Songoro* wa Kirumba ambao wamekuwa wakitoa huduma nzuri sana kwa wakazi wa Wilaya ya Sengerema, Geita, Mwanza na kwingineko?

(b) Je, Serikali inafanya nini kuwasaidia wasafirishaji katika kutimiza matakwa ya sheria hiyo mpya hatua kwa hatua?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dr. William Shija, Mbunge wa Sengerema, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa Serikali imepitisha Sheria ya Kudhibiti Usafiri wa Nchi Kavu na Majini *(SUMATRA)* Na. 9 ya mwaka 2001. Hivi sasa tunamalizia maandalizi ya chombo kitakachosimamia sheria hii.

Mheshimiwa Spika, sheria inayosimamia usafiri wa majini ni hii Sheria Na. 43 ya mwaka 1967, *The Merchant Shipping Act.* Sheria hii iliandaliwa kwa kuzingatia viwango vya usalama wa safari za meli na inalenga kuboresha huduma za safari za meli. Muswada wa sheria hiyo umepitiwa na kukubaliwa katika ngazi husika na umeshachapishwa katika gazeti la Serikali la tarehe 27 Juni, 2003 na tunategemea kuleta Bungeni katika Bunge lijalo.

Mheshimiwa Spika, Wizara haijapokea matatizo yoyote kwa wasafirishaji binafsi kama *M/S Claud Getg* wa Kamanga na *M/S Songoro* wa Kirumba ambayo yamewafanya washindwe kutekeleza kazi zao.

Mheshimiwa Spika, kwa maelezo haya napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa, Sheria ya Udhibiti wa Usafiri wa Majini zinazoendelea kutungwa zina lengo la kuondoa mapungufu ya sheria zilizopo ili kuimarisha usafiri na usalama wa huduma za vyombo vya majini.

**MHE. DR. WILLIAM F. SHIJA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja tu la nyongeza.

Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, napenda kumwuliza kwamba je, kuna mpango gani ambao umekuwepo kwa muda mrefu wa kuongeza *ferry* nyingine katika njia ya Busisi/Kigongo ambapo kwa maana ya sheria hiyo huwa kuwa msongamano mkubwa na huwa kuna hatari ya kuweza kutokea kwa sababu *ferry* iliyopo sasa hivi imezeeka sana, kuna mpango gani huo?

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, katika Bajeti ya Wizara ya Ujenzi ilihusisha pia *ferry* ya kutoka Busisi kwenda Kigongo. Katika mpango wa mwaka 2003/2004 kuna fedha ambazo zimetengwa kwa ajili ya kuifanyia matengenezo makubwa *ferry* inayotumika katika kuvusha kivuko kati ya Busisi na Kigongo. Lakini pia katika Bajeti ya mwaka huu kuna mpango wa kuangalia uwezekano wa kupeleka *ferry* nyingine itakayosaidiana na *ferry* inayovusha katika sehemu hiyo ya Busisi. *(Makofi)*

**MHE. JAMES P. MUSALIKA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa katika usafirishaji wa majini katika vivuko vya Kamanga na Busisi shehena za mafuta ambazo ni hatari petroli na dizeli huwa zinasafiri pamoja na abiria na kwa kuwa kuna hatari siku moja moto unaweza ukatokea katikati ya maji, je, Serikali inaonaje ingetenga usafirishaji wa mafuta tofauti na ule wa abiria na mizigo? *(Makofi)*

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa kwamba zinapokuwa zinavusha abiria huwa pia zinapakia magari yaliyobeba bidhaa za mafuta. Lakini huu ni ukweli pia unaolingana na uwezo wa nchi kwa sababu hatuwezi tukanunua *ferry* kwa ajili ya kuvusha mafuta tu halafu tukanunua *ferry* kwa ajili ya kuvusha abiria tu. Lakini kitu kikubwa ambacho huwa kinachukuliwa ni pamoja na tahadhari kwani magari haya yanayovusha mafuta bado huwa yana tahadhari ikiwa ni pamoja na *fire extinguisher* na mambo mengine ambayo yanaweza kuzuia hatari ambazo zinaweza kujitokeza.

Mheshimiwa Spika, hatari inayoweza kujitokeza katika gari hilo likiwa na mafuta ni hiyo hiyo hatari ambayo inaweza ikatokea kwa magari haya yanapopita kwenye sehemu za abiria, za watu na za

mizigo. Kwa hiyo, tahadhari ni lazima zichukuliwe katika kuhakikisha kwamba hatari hizo hazitokei. *(Makofi)*

Na. 300

**Kuunda Vikosi Maalum vya Uokoaji Kwenye Ajali Mbalimbali**

**MHE. PARMUKH SINGH HOOGAN** aliuliza:-

Kwa kuwa katika miaka ya hivi karibuni tumeshuhudia ajali nyingi na mbaya sana kama vile *MV Mtwara, MV Bukoba,* Kivuko cha Kilombero, ajali ya Mererani na ajali mbaya ya Treni - Dodoma; na kwa kuwa Serikali imeeleza mengi juu ya tahadhari zinazochukuliwa pindi ajali kama hizo zikitokea:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuunda vikosi maalumu vya uokoaji kwenye ajali kama hizo badala ya kuacha jukumu hilo kwa wapiganaji peke yao?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuviwekea Bima vyombo hivyo pamoja na watu wanaovisafiria?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Parmukh Singh Hoogan, Mbunge wa Kikwajuni, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Serikali chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Kitengo cha Maafa, inafanya utafiti wa kuandaa mbinu bora za uokoaji ikiwezekana kwa kutoa mafunzo kwa watu wote kuhusu mbinu za kujiepusha na ajali na kama ajali imetokea kujua mbinu za kupunguza madhara ya ajali hiyo, pamoja na mbinu za kuwasaidia wahanga wa ajali. Mkakati huu unalenga katika kutoa mafunzo kwa makundi maalum.

Aidha, mafunzo ya maafa yanayoendeshwa na Chuo cha Ardhi *(UCLAS)* ni moja ya shughuli za mradi wa kuimarisha uwezo wa Taifa kukabiliana na maafa. Katika hatua za awali (mwaka 2002) kwa kushirikiana na Idara ya Maafa kituo cha kutoa mafunzo ya maafa pale *(UCLAS)* kiliendesha mafunzo ya wiki nne kwa watumishi 40 (mmoja kutoka katika kila Mkoa Tanzania Bara na wengine toka Wizara za Kisekta).

Pia mafunzo mengine juu ya maafa ya wiki moja yameendeshwa ngazi za kanda, mwaka 2003 kuanzia mwezi Mei kimeanza kuendesha mafunzo na semina kwa Wakurugenzi Watendaji wa Halmashauri, tunategemea mafunzo ya *Disaster Responder Course* yatatolewa mwezi Julai, 2003 kwa ajili ya washiriki mbali mbali na Serikali inaangalia uwezekano wa kuwa na somo la uokoaji katika mitaala ya elimu hasa Elimu ya Msingi.

(b) Mheshimiwa Spika, mkakati huu ukifanikiwa utalipunguzia Jeshi la Wananchi jukumu la kuwa washiriki pekee wa uokoaji. Aidha, kuhusu Bima za vyombo, hili ni suala la kisheria kuwa kila mmiliki wa chombo cha uchukuzi wakiwemo wamiliki wa meli wanatakiwa kuwa na Bima *Third Party Insurance* ambapo kisheria zinapaswa kutoa fidia kwa yeyote anayepata ajali. Aidha, Sheria ya Bima inawashauri pia watu binafsi kujiwekea Bima ili kupata fidia ya kutosha inapotokea ajali.

**MHE. PARMUKH SINGH HOOGAN:** Mheshimiwa Spika, badala ya kutoa ushauri wa kuweka Bima kwa nini hamliweki sheria ya kudhibiti vyombo vikawa na Bima?

**SPIKA:** Inaelekea Mheshimiwa Naibu Waziri hakulipata vizuri swali lako unaruhusiwa kulirudia.

**MHE. PARMUKH SINGH HOOGAN:** Mheshimiwa Spika, badala ya kutoa ushauri wa Bima kwa nini Mheshimiwa Waziri hafanyi mpango ikaundwa sheria ya kudhibiti vyombo hivyo viweze kuwa na Bima?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, sheria ya kuweka Bima nadhani ipo na ndiyo maana tunawekea Bima vyombo vyetu vingi. Labda ni suala la kuwasiliana tu Wizara zinazohusika ili kukamilisha taratibu hizo.

**MHE. CAPT. THEODOS J. KASAPIRA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi kuuliza swali moja dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, tumeambiwa hapa kwamba katika Ofisi ya Waziri Mkuu kuna kitengo kinachoshughulikia maafa pamoja na uokoaji. Lakini kwa maafa yaliyotokea Kilombero tuliweza kuona tu Jeshi la Wananchi wa Tanzania pamoja na Wizara ya Ujenzi. Je, kitengo hiki kimeshughulikia kiasi gani matatizo yaliyotokea Kilombero, hatukuweza kukiona kabisa?

**SPIKA:** Mheshimiwa anayehusika ni Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, jibu swali.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI):** Mheshimiwa Spika, katika Ofisi ya Waziri Mkuu ni kweli kuna Kitengo cha Idara ya Maafa, lakini hakuna Kitengo cha Uokoaji. Kitengo hiki cha Maafa kinafanya kazi ya uratibu. Hawa Idara ya Maafa ndio walioandaa *logistics* na kuhamasisha Jeshi la Wananchi na kuratibu na kusimamia shughuli ile na kuhamasisha Jeshi la Wananchi, Idara ya Ujenzi na Idara nyingine kwa pamoja walishirikiana katika kufanya kazi ya uokoaji. Kwa hiyo, kitengo hiki kinaratibu tu, watekelezaji wako katika sekta mbalimbali. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, ni kwamba shughuli mojawapo ya Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania kutokana na utaratibu wa utendaji kazi, ni kutoa msaada kwa mamlaka za kiraia. Kwa hivi sasa hata kama Kitengo cha Uokoaji kingeundwa kama ni ngazi mojawapo ya kushughulikia bado kazi ya Jeshi la Ulinzi wa Wananchi wa Tanzania itaendelea kusaidia wananchi wakati wa maafa. *(Makofi)*

Na. 301

**Kuporomoka Kwa Zao la Korosho**

**MHE. LYDIA T. BOMA** aliuliza:-

Kwa kuwa kuanzia mwaka 2000 - 2002 Serikali imekuwa ikisikika kwenye vyombo vya Habari hususan Redio na kuandikwa kwenye magazeti juu ya jitihada zake za kuweka mikakati ya kuboresha baadhi ya mazao yanayolimwa nchini kama vile Pamba, Kahawa na kadhalika; na kwa kuwa tarehe 8 Aprili, 2003 Naibu Waziri wa Ushirika na Masoko alipokuwa anajibu swali Bungeni alisema kwamba mpaka sasa utafiti wa mazao ya Pamba, Tumbaku na Pareto umeshafanyika na taarifa za utafiti huo zinaandaliwa; na kwa kuwa katika maelezo yake hakutaja utafiti wa zao la korosho:-

(a) Je, Serikali inasema nini kwa wakulima wa zao la Korosho nchini hasa kwa Mkoa wa Mtwara ambao zao lao linazidi kuporomoka bei mwaka hadi mwaka?

(b) Je, zao la Korosho linaipatia Serikali pato gani na kwa kiwango kipi?

**NAIBU WAZIRI USHIRIKA NA MASOKO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ushirika na Masoko, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Lydia Boma, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikihimiza kilimo cha Korosho na kuandaa mazingira yanayowezesha kuiuza kwa lengo la kuboresha miasha ya wananchi wanaohusika moja kwa moja na zao la Korosho kama inavyofanya kwa mazao mengine aliyoyataja Mheshimiwa Mbunge.

Pamoja na Utafiti wa gharama za ununuzi na uuzaji unaofanywa kwa mazao ya Pamba, Tumbaku na Pareto, Serikali imekuwa ikifuatilia kwa karibu sana mwenendo wa bei ya Korosho ambayo imekuwa ikibadilika mara kwa mara katika soko la dunia kiasi cha kuwaathiri wakulima wa zao la Korosho.

Kutokana na hiyo bei ya Korosho anayopata mkulima kwa hivi sasa inapangwa kwa pamoja na wadau wote wa zao la Korosho kulingana na mwenendo wa bei katika soko la dunia pamoja na gharama zinazohusu uuzaji na ununuzi wa Korosho, jambo linaloendana na sera za hivi sasa katika kuuza mazao ya wakulima.

Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha mkulima wa Korosho analindwa katika mazingira ya soko la aina hii Serikali imekuwa ikihakikisha kwamba mkulima anapata bei ambayo haiendi chini ya kiwango cha bei ya kuanzia majadiliano yaani *floor price* kinachokubaliwa na wadau wa zao la Korosho wanapopanga bei.

Kwa kuwa wakulima au vyama vya ushirika vya kuuza Korosho vinatakiwa kupatana bei na wanunuzi, bei hii inakuwa ni msingi wa kuanzia majadiliano ya bei. Hivyo kulingana na upatikanaji wa Korosho na pia ubora wake, mkulima anaweza kupata bei kubwa zaidi. Kwa mfano katika msimu wa 2002/2003 katika Wilaya za Masasi, Nachingwea na Ruangwa bei ya Korosho daraja la kwanza ilipanda kutoka shilingi 360 kwa kilo na kufikia kati ya shilingi 400 na shilingi 425 kwa kilo. Bei ya Korosho daraja la pili iliongezeka kutoka shilingi 290 hadi shilingi 300 kwa kilo.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa utaratibu huu wa kupanga bei ya kuanzia majadiliano unaonekana kumlenga mkulima, Serikali itaendelea kusimamia ili uendelee kutumika. Jambo la muhimu kwa wakulima wetu ni kuhakikisha kuwa wanazalisha Korosho zenye ubora unaohitajika katika soko na kuhakikisha kwamba wanapanga Korosho katika madaraja yaliyo sahihi. Aidha, Serikali inahimiza ubanguaji wa Korosho ili kupanua wigo wa soko la Korosho kwa lengo la kumuongezea mkulima bei ya Korosho zake.

(b) Mheshimiwa Spika, katika kuuza Korosho nchi za nje zao la Korosho limeingiza jumla ya dola za Kimarekani milioni 45.5 baada ya kuuza tani 79,523 katika msimu wa 2002/2003. Mapato kutokana na mauzo ya Korosho nje ya nchi yameongezeka kwa asilimia 29.8 ikilinganishwa na msimu wa 2001/2002 ambapo dola za Kimarekani milioni 35.1 zilipatikana baada ya kuuza takriban tani 73,174. Kwa sababu hiyo zao la Korosho lina mchango mkubwa katika kukuza uchumi wa Taifa kwa kuliingizia fedha za kigeni.

**MHE. LYDIA T. BOMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu ya Naibu Waziri nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Kwa kuwa zao hili la Korosho Waziri amesema kwamba linachangia pato kubwa kwa Tanzania. Bado wananchi hawa wa Mkoa wa Mtwara kwa sababu natoka huko hali yao ya kiuchumi bado siyo nzuri. Serikali inafanya mpango gani wa kuwasaidia wakulima hawa kwa sasa hivi hasa suala la pembejeo wanawake wanalima zao hili lakini pembejeo kwao limekuwa ni tatizo?

La pili, wakulima mara nyingi wanakosa pembejeo kwa maana hiyo inakuwa tatizo kwa sababu zao lilishashuka bei na uzalishaji kutokana na ukungu. Je, Serikali inawasaidiaje hawa wakulima wadogo wadogo?

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba wakulima wa zao la Korosho wanahitaji msaada mbalimbali ikiwa ni pamoja na upatikanaji wa pembejeo ili waweze kuinua kipato chao. Hii ndiyo sababu ya msingi kabisa kwamba hivi sasa Serikali ina Mfuko wa Pembejeo ambao unawasaidia wakulima kwa mazao yote ikiwemo na hili la Korosho.

Mheshimiwa Spika, isitoshe vile vile kama ambavyo tulitaarifiwa wiki iliyopita hapa katika suala zima la ubanguaji ili kuwasaidia wakulima wadogo wadogo wenzetu wa Wizara ya Viwanda na Biashara wameanzisha mfuko wa kusaidia viwanda vidogo vidogo kwa ajili ya ubanguaji wa Korosho ili uuzaji wa Korosho uwe rahisi katika kuwasaidia wakulima wadogo wadogo ili uweze kuinua kipato cha mazao yao.

Na. 302

**Uendelezaji wa Wanawake**

**MHE. MZEE NGWALI ZUBEIR** aliuliza:-

Kwa kuwa shabaha kubwa ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto ni kuwapa wanawake uwezo zaidi wa kiuchumi, kielimu na kisiasa ili waweze kutoa mchango mkubwa zaidi katika kuendeleza familia na uchumi wa Taifa:-

(a) Je, wanawake hao wamewekewa mikakati gani ya kiuchumi ya moja kwa moja itakayoweza kuwasaidia?

(b) Je, ni elimu gani zaidi ambayo hutolewa ili kumsaidia mwanamke wa kijijini kuondokana na umaskini?

(c) Ukiacha kando nafasi za Viti Maalum vya Ubunge, je, zipo nafasi nyingine za Viti Maalum za kisiasa kwa wanawake Tanzania?

**NAIBU WAZIRI MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mzee Ngwali Zubeir, Mbunge wa Nungwi, lenye sehemu (a) , (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, katika suala zima la kuwawezesha wanawake kiuchumi, kielimu na kisiasa, Serikali yetu inazingatia Dira ya Maendeleo ya Taifa hadi kufikia mwaka 2025 ambayo inaelekeza kuwa na mikakati na sera ambazo zitawezesha kuwepo usawa wa kijinsia na kuwapa fursa wanawake kushiriki kikamilifu katika masuala yote ya kijamii, kiuchumi, kisiasa na kiutamaduni. Serikali imekuwa na mikakati ya moja kwa moja ya kuwawezesha wanawake kiuchumi. Badhi ya mikakati hiyo ni kutoa fedha za mikopo kupitia Mfuko wa Maendeleo wa Wanawake *(WDF)* unaoratibiwa na Wizara yangu.

Mfuko huu unatoa mikopo yenye masharti nafuu tangu mwaka 1993/1994 kwa wanawake wa vijijini na mijini ambapo riba inayotozwa ni asilimia kumi. Hadi kufikia mwaka 2002/2003, Wizara imekwishapokea jumla ya shs. bilioni 1.8. fedha hizi zimegawiwa kwa Halmashauri zote za Tanzania Bara.

Aidha, Serikali inatambua matatizo wanayoyapata wafanyabiashara wadogo wakiwemo wanawake katika kupata mikopo kwa ajili ya shughuli zao za kibiashara kutoka Benki za Biashara. Kwa kuzingatia hali hiyo, katika mwaka 2003/2004 Serikali imetenga fedha kwa ajili ya kudhamini mikopo ya sekta hiyo ya shughuli ndogo ndogo za kibiashara *(small and micro-enterprises)*.

Aidha, Wizara imekuwa ikishirikiana na Mfuko wa Fursa Sawa kwa Wote *(EOTF)* kuwawezesha wanawake kutoka Wilaya zote za Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar kushiriki katika Maonesho ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam tangu mwaka 1997, kwa kutoa mafunzo ya biashara, uboreshaji wa bidhaa na utafutaji wa masoko.

Pia Serikali ilipitishwa Sheria ya Ardhi ya mwaka 1999 ambayo inatoa fursa kwa wanawake kuweza kumiliki ardhi, ambayo ni muhimu katika kuendeleza uchumi hususan shughuli za kilimo, viwanda, maliasili, utalii na madini.

(b) Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inatoa mafunzo ya stadi mbalimbali za ushonaji, upishi, useremala, ufundi magari, uzazi salama, mbinu za kuanzisha na kuendesha biashara, uanzishaji wa vikundi vya miradi, afya ya jamii, utunzaji na uhifadhi wa mazingira, udereva na kilimo kupitia Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Canada *(CIDA)* imekuwa ikiendesha mafunzo ya muda mrefu na mfupi kwa wanawake tangu mwaka 1995. Hadi kufikia Machi, 2003 jumla ya Wanawake 272 walio katika ajira isiyo rasmi wamepata mafunzo kwa vikundi kuhusu stadi za biashara. Aidha, kutokana na mafunzo hayo vikundi vya wanawake vifuatavyo viliundwa. Vikundi hivyo ni *CRETA* - Pwani, *MGEDET* na *MWETU* - Mbeya na *SOWETU* - Ruvuma na kadhalika.

(c) Mheshimiwa Spika, kwa kutambua kwamba wanawake wanao mchango mkubwa katika kuchangia maendeleo ya nchi yetu, Serikali imeongeza idadi ya Viti Maalum vya Udiwani kutoka asilimia 25 mwaka 1995 hadi 33.3 mwaka 2000.

Aidha, mwaka 2002, Halmashauri Kuu ya Chama cha Mapinduzi ilipitishwa Azimio la nafasi za Viti Maalum kwa wanawake, Wajumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM kuwa asilimia 20. Kuhusu uwakilishi Bungeni, hivi sasa wanawake ni karibu asilimia 22 katika Bunge la Jamhuri ya Muungano na asilimia 24 katika Baraza la Wawakilishi Zanzibar. *(Makofi)*

**MHE. MZEE NGWALI ZUBEIR:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi hii kuuliza swali moja la nyongeza.

Pamoja na majibu marefu ya Mheshimiwa Naibu Waziri ambayo bado hayajamkomboa mwananchi wa kijijini na hususan mwanamke. Kuweka mikopo kwa wanawake si suala la kumkomboa na umaskini mwanamke wa Kitanzania. Kwa sababu hvi sasa mwanamke wa kijijini anakabiliwa na matatizo mengi ya umaskini hususan miundombinu kama maji, barabara na mambo mengine.

Je, kwa hili Mheshimiwa Naibu Waziri atalizungumzaje wakati ambapo tunataka kumkomboa mwananchi wa kijijini kuhakikisha kuwa anaondokana na huu umaskini uliopo? *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, utoaji wa mikopo unaofanywa na Serikali pamoja na Mashirika yasiyo ya Kiserikali ni sehemu mojawapo tu ya kuweza kuwawezesha wanawake. Mikakati ya kuondoa umaskini ni mikakati ambayo inajumuisha sekta nyingi kama yeye mwenyewe alivyosema. Kama tulivyoshuhudia katika Bunge hili Mawaziri mbalimbali wameeleza mikakati waliyonayo ambayo inalenga katika sekta zao kuondoa umaskini hivyo kuwapa mikopo ni njia mojawapo tu. Lakini yapo mafunzo ya kibiashara, upo uboreshaji wa barabara, huduma za maji zote hizo vinalenga kumkomboa mwanamke na hasa wa kijijini. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ninatazama anayetaka kuuliza mikopo kwa wanaume.

**MHE. JOEL N. BENDERA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kunipatia nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kama alivyojibu Mheshimiwa Waziri, je, Wizara ina habari kwamba Wanawake Vijijini hawapati mikopo hii ambayo wanatolewa. Wanaopata ni wa mijini zaidi. Je, wana mkakati gani wa kuhakikisha kwamba mwanamke wa kijijini hasa angalau anapata hii mikopo kulikoni wengi wa Vijijini? *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, taarifa tulizonazo ambazo nyingi zinatoka Wilayani na Vijijini zinaonyesha kwamba wanawake wa vijijini wanapata mikopo, tutakuwa tayari kutoa jedwali kwa Mheshimiwa Mbunge na Waheshimiwa Wabunge wengine kuonyesha ni kiasi gani cha mikopo kimepatikana.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo hivi sasa tumeboresha utaratibu wa kutoa mikopo ambapo Wizara yetu imeingia Mkataba na Halmashauri mbalimbali ili kuhakikisha kwamba mikopo hiyo inafika vijijini ingawaje bado jitihada zinaendelea za kufanya mkopo huo uenee zaidi. *(Makofi)*

Na. 303

**Barabara ya Kuunganisha Baadhi ya Mikoa**

**MHE. MGANA I. MSINDAI** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali katika tafiti imeona umuhimu wa aina yake wa kuunganisha kwa barabara Mikoa ya Arusha, Kilimanjaro, Tanga na Mkoa wa Mara kupitia Mikoa ya Singida (Iramba Mashariki), Shinyanga (Meatu, Maswa na Bariadi); na kwa kuwa Serikali ilishatoa fedha kwa ajili ya utafiti wa mwanzo; na kwa kuwa Mradi huo utachukua muda mrefu na fedha nyingi kukamilika; na kwa kuwa barabara hiyo ipo na ilianza kutumika tangu mwaka 1920 na hadi sasa inatumika kwa kiasi kikubwa sana nyakati za kiangazi kwa magari makubwa na madogo:-

(a) Je, Serikali haioni kwamba umefika wakati sasa wa kuanza utekelezaji wa mradi huo?

(b) Kwa kuwa kikwazo kikubwa kwa kazi ya utengenezaji wa barabara hiyo kiko kwenye kipande cha barabara chenye urefu wa kilometa 12 kutoka Nyahaa (Iramba Mashariki) na Bukundi (Meatu) ambapo panahitajika pajengwe daraja kwenye Mto Sibiti na kuweka Makalvati.

Je, Serikali itakuwa tayari kutafuta fedha kwa ajili ya kuikamilisha kazi hiyo na kutengeneza mapema eneo ambalo litawezesha barabara hiyo kutumika wakati wote kama ilivyowaahidi wananchi wa maeneo husika juu ya kuunganisha mikoa hiyo kwa njia ya karibu zaidi na kuhimiza maendeleo ya haraka?

**WAZIRI WA UJENZI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mgana Msindai, Mbunge wa Iramba Mashariki, kama ifuatavyo: -

(a) Mheshimiwa Spika, barabara inayohusika na swali hili ni kutoka Makuyuni Mkoani Arusha hadi Lalago Mkoani Shinyanga na Musoma Mkoani Mara ambayo ilijibiwa kupitia swali Na. 122 kwenye Mkutano wa Tisa wa Bunge. Kama nilivyoeleza kwenye jibu la swali hilo, sehemu ya barabara kutoka Makuyuni hadi lango la Hifadhi ya Ngorongoro yenye urefu wa kilomita 77 inajengwa chini ya msaada kutoka Japan na inatarajiwa kukamilika mwezi Agosti, 2005.

Aidha, sehemu ya barabara kati ya Ngorongoro kupitia Oldeani hadi Lalago ilifanyiwa upembuzi yakinifu ambao umekwishakamilika. Pamoja na matokeo ya utafiti kuonyesha kuwa gharama za ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami ni ghali sana, Serikali bado inafuatilia tathmini ya barabara hii na uwezekano wa kupata wafadhili wa kusaidia ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami.

(b) Mheshimiwa Spika,barabara kati ya Nyahaa (Iramba Mashariki) na Bukumbi Wilayani Meatu Mkoani Shinyanga inahudumiwa na Halmashauri za Wilaya husika.

Aidha, ujenzi wa daraja kwenye Mto Kibiti ulifanyiwa utafiti wakati wa upembuzi yakinifu wa barabara ya Ngorongoro - Lalago kama sehemu ya mradi huo na matokeo yake ni kama nilivyokwishaeleza awali.

Hivyo, Wizara inashauri Wananchi waendelee kutumia njia zilizopo na Idara husika zitaendelea kuzifanyia matengenezo ili ziweze kupitika wakati wote wa mwaka.

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili niulize swali la nyongeza.

Kwa kuwa kivuko cha Mto Sibiti kinaunganisha Mikoa ya Shinyanga, Mwanza, Singida, Arusha na Manyara na kwa kuwa ni barabara muhimu sana na kwa vile Serikali sasa hivi inaandaa miradi kwa ajili ya Mikoa kame ili kuomba fedha *ADB.*

Mheshimiwa Spika, je, Waziri atakubaliana nami kwamba hicho kipande cha kilomita 12 kiunganishwe kwenye miradi ambayo inatafutiwa fedha ili iunganishe Wananchi wa Mikoa hiyo na waweze kupita kwa urahisi? *(Makofi)*

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, katika jibu langu la msingi nimeeleza kwamba barabara ya kutoka Makuyuni - Lalago hadi Lamadi katika Mkoa wa Mara yenye jumla ya kilomita 400 imekwishafanyiwa upembuzi yakinifu. Upembuzi yakinifu huo ulipendekeza kwamba barabara husika itengenezwe kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, tatizo lililopo kwa sasa hivi ni upatikanaji wa fedha hizo na sisi Wizara tunaendelea kuangalia ni namna gani tunaweza tukapata fedha ili ziweze kutengeneza sehemu hii ya barabara kwa kiwango cha lami ikiwa ni pamoja na ile sehemu ambayo ameitaja Mheshimiwa Mgana Msindai pamoja na daraja la Sibiti. Kwa hiyo, fedha zikishapatikana sehemu hii pia itahusika katika kutengenezwa kwa kiwango cha lami. *(Makofi)*

**MHE. LAZARO S. NYALANDU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili ya kuuliza swali moja tu la nyongeza.

Kwa kuwa ukitokea Manyoni kuelekea Singida, njia fupi zaidi ni sharti upite Babati - Qatesh - Singida Kaskazini hadi Singida Mjini na kwa kuwa barabara hii ya kutoka Arusha - Minjingu - Babati - Singida - Tabora hadi Kigoma ni barabara muhimu sana katika uchumi wa Taifa hili. Je, Mheshimiwa Waziri atanihakikishia ni lini barabara hiyo itajengwa kwa kiwango cha lami? *(Makofi)*

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba swali la msingi lilizungumzia barabara ya Makuyuni - Lalago hadi Lamadi katika Mkoa wa Mara, swali ambalo ameuliza Mheshimiwa Lazaro Nyalandu ni la kutoka Arusha - Minjingu - Babati - Hanang - Singida na kuelekea kwenye sehemu nyingine.

Napenda kumthibitishia tu kwamba, barabara aliyoitaja ya kutoka Arusha - Minjingu - Babati - Hanang hadi Singida na kuunganika na barabara nyingine alizozitaja, iko kwenye mipango ya kutengenezwa kwa kiwango cha lami na kwa kazi ambazo zinafanyika katika Bajeti ya mwaka huu ni kuanza kufanya *feasibility study* kwenye sehemu ya Singida - Minjingu ambayo tayari Mkandarasi amekwishateuliwa na kazi za *feasibility study* sasa hivi zinafanyika.

Mheshimiwa Spika, baada ya kazi hiyo, kazi itakayofuata ni upatikanaji wa fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara hiyo kwa kiwango cha lami. *(Makofi)*

Na. 304

**Mzunguko katika barabara iendayo Zambia**

**MHE. BENSON M. MPESYA** aliuliza: -

Kwa kuwa mzunguko maarufu wa Mafyati katika barabara kuu iendayo Zambia umekuwa ni chanzo cha ajali na karaha kwa waenda kwa miguu hususan Wananchi wa Iyela au *Airport:*-

(a) Je, nini ufumbuzi wa tatizo hilo?

(b) Je, Serikali iko tayari kupokea ushauri wa kujenga daraja *(Flying way Bridge)* kama lile la Manzese ili kupunguza kero hiyo?

**WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Benson Mpesya, Mbunge wa Mbeya Mjini, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, maeneo yaliyotajwa hayana mzunguko *(round about)* bali ni makutano *(intersection)* ya barabara tatu eneo la Mafyati yanayohusisha barabara kuu iendayo Zambia, barabara iendayo Mjini Mbeya na barabara iendayo Uwanja wa Ndege.

Mheshimiwa Spika, katika barabara hizo kuna alama za barabarani (michoro) zinazotenganisha na kuongoza mwelekeo wa magari. Alama hizo zimeanzia umbali wa mita 300 kabla ya makutano zikitanguliwa pia na alama nyingine za tahadhari.

Aidha, alama hizo pamoja na zile zilizopo makutano ya barabara iendayo Iyela maeneo ya Uyole zitaendelea kuimarishwa kupitia matengenezo ya kawaida ya barabara husika.

Alama za barabarani zimeipa barabara kuu iendayo Zambia kipaumbele cha kupitisha magari kwanza katika makutano hayo yote mawili. Alama hizo kwa eneo la Mafyati pia zinawezesha watembea kwa miguu kuvuka barabara kwa kutumia visiwa vilivyowekwa katikati ya barabara hizo na hivyo kuhakikisha usalama wa makutano hayo.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia idadi ya magari katika barabara hizo, matatizo yasingekuwa makubwa kama watumiaji wa barabara wangekuwa wanazingatia alama za barabarani zinavyoelekeza. Aidha, katika kuboresha zaidi makutano hayo, Wizara itafanya tathmini ya kuweka matuta kupunguza kasi ya magari maeneo husika.

**MHE. BENSON M. MPESYA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

(a) Kwa kuwa lengo la swali langu ilikuwa ni kuokoa mali na maisha ya Wananchi ambao yanapotea kwa sababu ya barabara hiyo, je, Serikali itakuwa tayari kuli-*design* upya eneo hilo?

(b) Je, Serikali itakuwa tayari kumtuma Mtaalam angalau hapa Lusaka Zambia, aone jinsi eneo kama hilo na kwa barabara hiyo jinsi wenzetu walivyojaribu kushughulikia na kuokoa mali na maisha ya watu? *(Makofi)*

(a) Mheshimiwa Spika, nia ya Serikali ni kuhakikisha kwamba inaokoa mali na maisha ya Wananchi kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge alivyozungumza. Lakini katika jibu langu la msingi nimeeleza kwamba, kuna alama za barabarani ambazo zimewekwa kwenye barabara husika, kwa hiyo ni wajibu wa madereva pamoja na Wananchi wenyewe kuzingatia kwanza alama za barabarani.

Aidha, katika jibu langu la msingi pia nimeeleza kwamba, kwa sasa hivi kitakachofanyika ni kwamba tutaangalia ni namna gani tutaweza kuweka matuta ya kupunguza *speed* ya magari yanayopita pale. Kwa hiyo, katika hatua hizi ambazo zitachukuliwa ni kweli kwamba tutaweza kuokoa maisha na mali za Wananchi, lakini ushirikiano mkubwa unahitajika kwa Wananchi wenyewe.

(b) Kuhusu suala la ku-*design* ile sehemu inayohusika, barabara ya kutoka Dar es Salaam - Zambia wakati inatengenezwa ilifanyiwa *feasibility study* na *design* na ndipo ilipofikia hatua ya kutengenezwa, lakini inawezekana baada ya kutengenezwa kuna sehemu ambazo Wananchi wameongezeka zaidi. Kwa hiyo, tutazingatia suala hili wakati tutakapokuwa tunatengeneza matuta kwenye sehemu ambazo Wananchi wanapata ajali kwa wingi.

**MHE. NJELU E. M. KASAKA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Katika sehemu ile ni kweli alama zipo, lakini kwa sababu usiku hakuna taa, alama zile huwa hazionekani! Ufumbuzi katika sehemu ile kama alivyouliza Mheshimiwa Benson Mpesya katika swali la msingi, ni ama kuweka *flyover bridge* ama *round about* ama *traffic lights* au kuweka taa za kawaida ili alama ziweze kuonekana wakati wa usiku. Je, Serikali inachagua lipi katika hayo? *(Makofi)*

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, katika *option* zote ambazo amezizungumzia Mheshimiwa Njelu Kasaka zinahitaji fedha. Kutengeneza daraja la *flyover* gharama zake ni kubwa, kuweka taa barabarani nako kunahitaji gharama na ndiyo maana katika jibu langu la msingi nimesema kwamba kwa hatua za mwanzo katika kuhakikisha tunaokoa maisha na mali za Wananchi walioko pale, kwanza Wananchi wenyewe wana jukumu la kuzingatia alama za barabarani na ninaposema Wananchi maana yake ni pamoja na madreva wanaotumia hiyo barabara.

Lakini pili, Serikali kwa hatua za awali itahakikisha kwamba inaweka matuta kwenye sehemu hizo ili kupunguza *speed* za magari yanayopita kwa kasi. Kuhusu taa za barabarani, suala hilo naliacha kwenye jukumu la Halmashauri ya Mji wa Mbeya, kuona kama wanahitaji kuweka taa pale ili usiku kucha ziwe zinawaka na kuzuia magari yasiwagonge.

Mheshimiwa Spika, lakini kwa ajali zinazotokea pale Mbeya, inadhihirika kwamba ajali nyingine zinatokea hata mchana wakati jua linawaka! Kwa hiyo, jukumu kubwa ni kuzingatia Sheria za barabarani. *(Kicheko)*

Na. 305

**Bei ya Dawa katika Hospitali Binafsi**

**MHE. RUTH B. MSAFIRI** aliuliza:-

Kwa kuwa bei ya dawa itolewayo na hospitali binafsi mara nyingi iko juu kidogo kulinganisha na bei ya dawa katika hospitali za Serikali na kwa kuwa tofauti hii imeanza kulalamikiwa na hivyo kuathiri huduma nzuri ya Bima ya Afya pale ambapo hakuna Hospitali za Serikali:-

(a) Je, Serikali itakuwa tayari kulipa bei ya dawa kama ilivyo katika hospitali binafsi ili kutoa huduma ya Bima ya Afya kwa walengwa wote bila malalamiko?

(b) Ikiwa jibu la (a) ni ndiyo, je, Serikali itakuwa ikipeleka malipo hayo haraka katika hospitali binafsi ili wasianguke mtaji na kuathiri huduma?

(c) Ikiwa majibu ya sehemu (a) na (b) ni hapana, je, Serikali itawahudumiaje wachangiaji wa Bima ya Afya ambao pale walipo hakuna hospitali ya Serikali na iliyo karibu?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ruth Msafiri, Mbunge wa Muleba Kaskazini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo: -

(a) Mheshimiwa Spika, bei za dawa zinazolipwa na Mfuko zimeboreshwa. Kwa sasa vituo vya matibabu vinapata marejesho ya asilimia 25 zaidi ya bei wanazonunua kutoka Bohari Kuu ya Dawa *(MSD)* au katika maduka makubwa ya jumla. Ongezeko hili lililoanza mwezi Agosti, 2002 lililenga katika kuwaongezea uwezo zaidi watoa huduma na kuwafanya wawe na akiba ya kutosha ya dawa muhimu. Aidha, ongezeko hili linaweza kufidia bei kubwa ya dawa toka hospitali binafsi.

Mfuko utaendelea na zoezi la tathmini ya huduma zinazotolewa kwa madhumuni ya kuziboresha. Mbali na ongezeko la bei za dawa, Mfuko umeongeza bei za vipimo kwa wastani wa asilimia 32 pamoja na aina mbalimbali za upasuaji.

(b) Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya ni chanzo imara na cha uhakika cha mapato kwa watoa huduma. Watoa huduma wote waliosajiliwa wanalipwa malipo yao bila usumbufu na kwa haraka iwezekanavyo baada ya kuwasilisha madai yao halali ili kuhakikisha kuwa huduma wanazotoa hazikwami.

(c) Mheshimiwa Spika, kwa kuwa jibu langu katika kipengele (b) ni ndiyo, naomba Mheshimiwa Mbunge azingatie maelezo ya jibu langu sehemu ya (b).

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu niliyoyapokea kutoka kwa Mheshimiwa Naibu Waziri na kwa kuwa kilichonisukuma kuuliza swali hili ni kutokana na mikutano yangu niliyofanya na Walimu mwezi Januari, 2003 na hapa Mheshimiwa Waziri anakiri kwamba marekebisho yameanza tangu Agosti, 2002. Naomba kuuliza kama ifuatavyo: -

Kwa kuwa Walimu walio wengi wanafanyakazi katika maeneo ambayo ni ya Vijijini na kwa kuwa wakati napokea malalamiko haya tayari Serikali ilishasema kwamba imeboresha Mfuko huo. Kwa maana hiyo, walikuwa hawajaona huo ubora ambao Serikali imeuzungumza! Sasa inapotokea Mwalimu akalazimika kwenda katika hospitali za Ndolage au Kagondo katika Jimbo langu ambazo ni za binafsi na akakuta anazuiliwa kupewa huduma kwa sababu tu hii huduma aliyoisema Mheshimiwa Waziri haijafika na akalipa fedha zake mwenyewe...

**SPIKA:** Uliza swali!

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Je, Serikali itakuwa tayari kumrejeshea fedha zake kwa haraka?

Pili, kwa kuwa Serikali baada ya kupokea hoja za matatizo ya huduma za afya katika Jimbo la Muleba Kaskazini ilikubali kuvipa hadhi Vituo vya Afya ambavyo vilikuwa Zahanati ambazo ni Ibuga na Izigo, lakini bado havijapata dawa ...

**SPIKA:** Aaah, usitoe hotuba, uliza swali fupi.

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Spika, ndio swali lenyewe hilo.

**SPIKA:** Basi, kaa chini! Mheshimiwa Naibu Waziri, jibu swali lake la kwanza. *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba niliarifu tu Bunge lako Tukufu kwamba, utaratibu wa utoaji wa huduma kupitia Mfuko wa Bima ya Afya unaendana na Mikataba. Hivyo, hospitali zote ambazo zimeingia mkataba na Mfuko huu bila shaka zimekubaliana katika malipo ya dawa na ninavyosema kwamba bei za dawa hizo zimeongezwa kwa asilimia 25, hiyo ni sahihi na wahusika wamefahamishwa hivyo. Sasa sielewi ni kwa nini mtu anapopewa dawa anatakiwa atoe fedha zake mfukoni, kwa sababu kama kituo kimesajiliwa, basi bila shaka kituo hicho kinapata malipo kutoka Mfuko wa Bima ya Afya!

Mheshimiwa Spika, kama nimelielewa swali la Mheshimiwa Mbunge vizuri ni kwamba, endapo mtu atakuwa ametibiwa katika kituo ambacho hakijasajiliwa hapo atalazimika kulipa mwenyewe, lakini kwa vituo vyote ambavyo vimesajiliwa, bila shaka malipo hufanywa na Mfuko wa Bima ya Afya.

**MHE. DR. BATILDA S. BURIAN:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri katika jibu lake la swali la msingi amezungumzia gharama za dawa na za vipimo, je, anaonaje kuhusu kutoa gharama za vipimo kwa ajili ya ugonjwa wa malaria?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, nilichosema ni kwamba Mfuko wa Bima ya Afya umeongeza malipo katika dawa na umeongeza malipo katika vipimo vinavyofanywa. Sasa kama nimelielewa vizuri swali la Mheshimiwa Dr. Batilda Burian, ni kwamba, hata malaria kama mtu anakwenda kupima ile *Blood Slide (BS)* au kama mtu anatakiwa afanyiwe *Full Blood Picture* na vyenyewe vimeongezewa malipo endapo hospitali au zahanati itafanya vipimo hivyo. Ninachoweza kusema hapa ni kwamba, vipimo vya malaria pamoja na dawa za malaria zote zimepata ongezeko katika malipo yanayotolewa na Mfuko wa Bima ya Afya.

Na. 306

**Kutengeneza Ofisi ya Idara ya Uhamiaji Zanzibar**

**MHE. MZEE NGWALI ZUBEIR (k.n.y. MHE. RAMADHANI NYONJE PANDU)** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali ilikuwa na nia ya kujenga Ofisi ya Idara ya Uhamiaji Zanzibar na kwa kuwa tayari kiwanja kimeshapatikana na kwa kuwa kujenga ofisi hiyo Tanzania Visiwani ni njia moja ya kukuza ushirikiano, utendaji bora na kuimarisha Muungano:-

(a) Je, endapo azma hiyo bado ipo, ni nini kinachokwamisha ujenzi huo ukiacha hali ngumu ya uchumi na ufinyu wa Bajeti?

(b) Kutokana na kiwanja hicho kukaa kwa muda mrefu na kutokana na hali ya uvamizi wa viwanja ulipo Zanzibar, je, kwa nini ujenzi usianze hapo kwa hatua ya msingi tu *(foundation)* ili kuonyesha kuwa nia ya ujenzi ipo na pia kuepuka uvamizi wa kiwanja hicho.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ramadhani Nyonje Pandu, Mbunge wa Baraza la Wawakilishi, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa Ofisi ya Uhamiaji ya Mkoa wa Kusini Unguja ulikwama kwa muda mrefu kutokana na kuchelewa kupimwa kiwanja na kupatikana kwa hatimiliki.

Napenda kuchukua fursa hii kumjulisha Mheshimiwa Mbunge kuwa kiwanja hicho sasa kimeshapimwa na kupewa hatimiliki na Idara ya Uhamiaji imekwishaanza taratibu za kutayarisha michoro ya ujenzi wa ofisi hiyo. Mwaka huu wa fedha 2003/2004, Wizara yangu imetenga shilingi 45,177,736/= kwa mradi huu kwa kuanzia. Aidha, jitihada zimeshaanza kumpata Mkandarasi wa kuanza ujenzi huo. *(Makofi)*

**MHE. BALOZI GETRUDE I. MONGELLA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa swali la msingi limezungumzia Tanzania Visiwani, nami natoka Visiwani, je, Mheshimiwa Waziri atakubaliana nami kwamba wakati umefika wa kuwa na Ofisi ya Uhamiaji katika Wilaya ya Ukerewe ili kuondoa wimbi la wageni walioingia kiholela, wanatamba na kuleta maafa katika maji ya *Lake Victoria? (Kicheko/Makofi)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Getrude Mongella, Mbunge wa Ukerewe, Kisiwa kilichozungukwa na maji baridi kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Getrude Mongella, anatoka kisiwa kilichozungukwa na maji baridi, lakini kisiwa kilichoulizwa hapa kinazungukwa na maji ya chumvi ya Bahari ya Hindi. Lakini pamoja na hayo nakubaliana nae kwamba, wakati umefika wa kuwa na Ofisi ya Uhamiaji kama alivyoitaka, lakini kwa mujibu wa hali yetu ya uchumi na upangaji wetu wa vipaumbele, hadi sasa hivi bado hatujaweza, lakini nia hiyo ipo na tutaendelea kushirikiana kuhakikisha kwamba ofisi inapatikana siku za baadaye. *(Kicheko/Makofi)*

Na. 307

**Kutetereka kwa Mabenki**

**MHE. PHILIP S. MARMO (k.n.y. MHE. SEMINDU K. PAWA)** aliuliza: -

Kwa kuwa Wizara ya Fedha nchini iko makini sana katika kusimamia Vyombo vya Fedha ili kuchangia Pato la Taifa:-

(a) Je, kwa kuwa uzoefu unaonyesha kuwa baadhi ya Mabenki ya kigeni yalienda kombo kama vile *Greenland Bank, Meridian Biao* na *Delphis Bank,* Serikali inajifunza nini juu ya matukio hayo?

(b) Je, Serikali itaimarishaje safu yake ili kudhibiti matukio kama hayo ya kutetereka kwa baadhi ya Benki hizo za kigeni?

(c) Je, ni nini hatma ya wateja wa Mabenki hayo mara inapotokea Benki ikatetereka kama zile tatu katika swali (a)?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. DR. FESTUS B. LIMBU)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Semindu Pawa, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo: -

(a) Kutokana na matukio ya kutetereka kwa Mabenki hususan yale ya kigeni na hata yale ya hapa nchini, Serikali imejifunza jambo moja kubwa nalo ni kwamba biashara ya Mabenki ni ya hatari *(risky)* na kwamba inahitaji uangalifu katika utoaji leseni na usimamizi wa nguvu wa Mabenki hayo baada ya kupewa leseni na kuanza shughuli. Kwa kutambua hilo, Serikali na Benki Kuu zimechukua hatua mbalimbali za kisheria ili kuimarisha shughuli za kibenki na usimamizi imara wa Benki Kuu kwa Mabenki na wa Serikali kupitia Benki Kuu kufanya tathmini ya kutosha kuhakikisha kuwa wale wanaopewa leseni za wanaoanzisha Benki ni watu wenye sifa nzuri, mitaji mikubwa na uwezo wa kuchukua hatua za haraka, pamoja na kuongeza mtaji, mara dalili za matatizo zinapojitokeza.

(b) Mheshimiwa Spika, jukumu la kusimamia shughuli za Mabenki ni la Benki Kuu ya Tanzania. Benki Kuu inafanya kila iwezalo kuimarisha safu yake katika kudhibiti Mabenki hapa nchini. Benki Kuu inayo wataalam wenye uwezo na uzoefu katika shughuli za kusimamia Mabenki na inaendelea kuwapatia mafunzo ya ndani na nje ya nchi kuongeza uwezo wao. Aidha, Sheria zetu za usimamizi wa fedha na Mabenki ni za kiwango cha Kimataifa na zenye kupambana na hali yoyote ya hatari.

(c) Mheshimiwa Spika, hatma ya wateja inapotokea kuwa Benki imetetereka inategemea sana hali ya Benki wakati imetetereka au wakati inawekwa chini ya usimamizi wa Benki Kuu. Wateja hao wanaweza kulipwa fedha zao kulingana na hali ya kifedha ya Benki husika. Hata hivyo, iwapo Benki itafilisiwa, kila mwenye amana atalipwa kikomo cha shilingi 250,000/= kwa mujibu wa Sheria ya *Deposit Insurance Fund.*

Mheshimiwa Spika, ningependa ieleweke kuwa mara zote Serikali kupitia Benki Kuu inafanya kila iwezalo ili kuhakikisha kuwa fedha za Wananchi hazipotei ovyo. Hata hivyo, Wananchi na wateja wa Mabenki na Taasisi za Fedha wanashauriwa kuchukua tahadhari zinazofaa katika kuamua Benki ipi waweke akiba zao.

**MHE. PHILIP S. MARMO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

(a) Kwa mujibu wa Sheria ya Mabenki na Sheria ya Fedha, Benki Kuu ndio ina wajibu wa kufuatilia mienendo ya Mabenki siku hadi siku. Sasa kwa vile wateja wengi wameathirika kwa ajili ya uzembe wa Benki Kuu, je, kwa ajili ya matukio hayo, Benki Kuu pamoja na Gavana wake wamewajibika kwa namna gani?

(b) Kwa vile sifa moja ya uwekezaji katika eneo hili la Mabenki ni kuwa na sifa na tabia nzuri na kwa vile mwekezaji wa *Delphis Bank* anajulikana dunia nzima kwamba ana tabia chafu sana na ameyumbisha hata uchumi wa nchi jirani, je, Benki Kuu haikufahamu tabia chafu na ya ufisadi ya mwekezaji huyu wa *Delphis Bank* ambayo imeathiri Watanzania wengi? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. DR. FESTUS B. LIMBU):** Mheshimiwa Spika, Mabenki ambayo yalitetereka ni pamoja na *Greenland Bank, Meridian Biao* na *Delphis Bank.* Gavana wa Benki Kuu, Benki Kuu yenyewe pamoja na Serikali kwa ujumla ilifuatilia kwa ukaribu sana kupitia kitengo cha Benki Kuu cha *Supervision* ambacho kiligundua hata kabla matatizo makubwa hayajajitokeza. Kwa mfano, matatizo yaliyojitokeza kwenye Makao Makuu ya *Greenland Bank* huko Uganda yalikuwa hayajafika kwetu, lakini kwa sababu ya kutetereka kwa Benki hiyo huko Uganda, Benki Kuu iliamua kusimamisha shughuli zake na kuisimamia. Kwa hiyo, wateja hawakupoteza mali zao kama ambavyo wangepoteza kama kusingekuwa na usimamizi wa karibu.

Mheshimiwa Spika, Benki Kuu imekamata shughuli zote za *Delphis Bank* baada ya kuona kwamba imetetereka na walikuwa wanatakiwa waongeze mtaji ndani ya Benki hiyo. Kusema kwamba mwekezaji ana tabia chafu, hilo hatuna taarifa nalo, alifuata taratibu zote zinazotakiwa katika kuanzisha Benki hiyo.

Na. 308

**Uanzishwaji wa *Freeport* Zanzibar**

**MHE. FATMA SAID ALI** aliuliza: -

Kwa kuwa baadhi ya nchi ndogo huchangia uchumi wa nchi zao kwa kuanzisha Bandari Huru *(Freeport),* je, ni lini Serikali ya Muungano itaisaidia Zanzibar kufanikisha suala la *Freeport* kama chachu ya kuleta maendeleo ya uchumi Zanzibar?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. DR. FESTUS B. LIMBU)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Fatma Said Ali Mchumo, Mbunge wa Mlandege, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Bandari Huru ya Zanzibar *(Zanzibar Free Port Authority - ZFPA)* ilianzishwa mwaka 2000 kwa Sheria namba 9 ya mwaka 1998 iliyopitishwa na Baraza la Wawakilishi la Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Lengo la kuanzisha Bandari Huru ya Zanzibar lilikuwa ni pamoja na kuvutia Makampuni makubwa ya Kimataifa yanayotarajia kufanya biashara katika nchi za ukanda wa Afrika Mashariki, Kati na Kusini.

Mheshimiwa Spika, pia *ZFPA* ilitarajiwa kuweka mazingira mazuri ya biashara ili kuongeza ufanisi kwa Makampuni ambayo yanafanya biashara katika ukanda wa Mashariki, Kati na Kusini mwa Afrika kwa kuwepo kituo cha kusambaza bidhaa zao karibu na masoko.

Mheshimiwa Spika, kulingana na Sheria hiyo, iliyoanzisha Mamlaka ya Bandari Huru ya Zanzibar, umiliki, uendeshaji na uendelezaji wa Bandari Huru Zanzibar uko moja kwa moja chini ya Mamlaka husika ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

Aidha, Mamlaka inayohusika na usimamizi wa Mamlaka ya Bandari kwa upande wa Tanzania Bara yaani Mamlaka ya Bandari Tanzania *(THA)* inashirikiana na Mamlaka husika kwa upande wa Zanzibar katika masuala machache kiutendaji, hususan kwenye kuhakikisha usalama wa Vyombo vya Majini kama meli ziingiazo na kutoka katika Bandari za Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar hajawaeleza kama wana tatizo lolote la kusaidiwa na Serikali ya Muungano katika utekelezaji wa dhana ya Bandari Huru Zanzibar, ni vigumu kusema ni lini Serikali ya Muungano itatoa msaada gani kwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

**MHE. FATMA SAID ALI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Nina swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kuelezea kwamba mpaka sasa hivi Zanzibar haijaelezea kwamba wana nia ya kufanya Bandari Huru. Lakini hata hivyo kwa hatua mbalimbali zinazochukuliwa kunyanyua uchumi na hasa sasa hivi kwa kuanzisha hizi *EPZ;* na kwa kuwa Zanzibar *EPZ* ndiyo tulioanza mwanzo; je, kuna uhusiano gani kati ya *EPZ* ya Zanzibar na *EPZ* ya Tanzania Bara?

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Fatma Said Ali Mchumo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu pamoja na Wizara ya Biashara, Viwanda, Masoko na Utalii ya Zanzibar tumekuwa na utaratibu wa kukutana mara kwa mara. Moja ya mambo ambayo tumekuwa tukizungumza, ni namna gani ya kushirikisha juhudi zetu za pamoja katika kuimarisha uzalishaji hasa katika Sekta ya Viwanda kwa shahaba ya kuimarisha Sekta ya Biashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, *EPZ* ya Zanzibar ambayo kwa kweli imeanza miaka 10 iliyopita, imepiga hatua kubwa zaidi kuliko *EPZ* ya Tanzania Bara. Lakini tunafanya juhudi za kushirikiana ili kuwezesha *EPZ* zote hizi mbili ziimarike na ziweze kuleta matunda yanayofaa kwa jamii yetu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali umekwisha na maswali yamemalizika. Vikao vya Kamati kwa leo, Kamati nne zifuatazo wamepangiwa kukutana.

Kamati ya kwanza, ni Kamati ya Fedha na Uchumi, Mwenyekiti wa Kamati hiyo anaomba Kikao kifanyike saa 5.00 asubuhi, chumba namba 75, Kamati ya Fedha na Uchumi saa 5.00 asubuhi.

Kamati nyingine ni Kamati ya Kilimo na Ardhi, Mwenyekiti wake Mheshimiwa Eliachim Simpasa, anaomba saa 5.00 hiyo hiyo Kamati ya Kilimo na Ardhi ikutane, chumba namba 58. Kamati ya tatu, ni Kamati hii ya Mambo ya Nchi za Nje, Mwenyekiti wake, Mheshimiwa Dr. William Shija, anaomba Kamati ikutane Saa 5.00 hiyo hiyo asubuhi, chumba namba 56. Nne, Kamati ya Huduma za Jamii, Mwenyekiti wake Mheshimiwa Omar Kwaangw', anaomba Wajumbe wake wakutane chumba namba 75, saa 5.00 asubuhi hiyo hiyo. Sijui bado tutakuwa na *quorum* ya kuendelea na shughuli za Bunge. Lakini hizo shughuli za Kamati inahesabiwa kwamba ni sehemu ya shughuli za Bunge kwa hiyo hakuna tatizo.

Kuhusu wachangiaji wa hoja ya leo pengine kwa mwaka ujao tutashauriana na Kamati ya Uongozi tutoe muda zaidi labda wa siku mbili kwa Wizara hii. Inaelekea ambao hawajachangia kabisa ni mmoja, atapata nafasi, waliokwisha kuchangia mara moja ni 17, waliokwisha kuchangia mara mbili ni 18, waliokwisha kuchangia mara tatu ni 10, sasa haitawezekana wote hao kupata nafasi.

**WABUNGE FULANI:** Siku moja haitoshi.

**SPIKA:** Lakini kwa safari hii hatuwezi kutoa siku mbili kwa sababu ratiba imekwishakamilika, naahidi kufanya hivyo kwa Bajeti ijayo. Mwisho wa matangazo.

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2003/2004
### Wizara ya Nishati na Madini

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kutokana na taarifa iliyowasilishwa hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Uwekezaji na Biashara, naomba kutoa hoja kwamba sasa Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Nishati na Madini kwa mwaka wa fedha 2003/2004.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wapya wa CCM na *CUF* kwa ushindi wao katika uchaguzi mdogo

uliofanyika mwezi Mei, 2003. Waheshimiwa hao ni Mheshimiwa Abu Kiwanga, Mbunge wa CCM, Jimbo la Kilombero, Mheshimiwa Nazir Karamagi, Mbunge wa CCM, Jimbo la Bukoba Vijijini, Mheshimiwa Edward Ndeka, Mbunge wa CCM, Jimbo la Kigoma Kusini, Mheshimiwa Sumri Mohamed, Mbunge wa CCM, Jimbo la Mpanda Magharibi, Mheshimiwa Karim Said Othman, Mbunge wa *CUF,* Jimbo la Chambani, Mheshimiwa Masoud Abdalla Salim, Mbunge wa *CUF,* Jimbo la Mtambile na Mheshimiwa Mohamed Juma Khatib, Mbunge wa *CUF,* Jimbo la Chonga.

Wengine ni Mheshimiwa Ali Said Salim, Mbunge wa *CUF,* Jimbo la Ziwani, Mheshimiwa Shoka Khamis Juma, Mbunge wa *CUF,* Jimbo la Micheweni, Mheshimiwa Salim Omar Ali, Mbunge wa *CUF,* Jimbo la Tumbe, Mheshimiwa Mchande Salim Mchande, Mbunge wa *CUF,* Jimbo la Konde, Mheshimiwa Khamis Ali Saleh, Mbunge wa *CUF,* Jimbo la Mgogoni, Mheshimiwa Mohamed Ali Said, Mbunge wa *CUF,* Jimbo la Wingwi, Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, Mbunge wa *CUF,* Jimbo la Gando, Mheshimiwa Khalifa Mohammed Issa, Mbunge wa *CUF,* Jimbo la Mtambwe, Mheshimiwa Bakari Shamis Faki, Mbunge wa *CUF,* Jimbo la Ole, Mheshimiwa Mwadini Abass Jecha, Mbunge wa *CUF,* Jimbo la Utaani, Mheshimiwa Ali Said Juma, Mbunge wa *CUF,* Jimbo la Kojani na Mheshimiwa Omar Juma Omar, Mbunge wa *CUF,* Jimbo la Pandani.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kutoa maelezo ya hoja ya Wizara ya Nishati na Madini, napenda pia kuchukua fursa hii kuwapongeza na kuwashukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu na Waheshimiwa Mawaziri wenzangu walionitangulia kuwasilisha hoja zao kwa hotuba nzuri zenye ufafanuzi wa kina kuhusu maendeleo ya utekelezaji wa sera, kukua kwa uchumi, maendeleo ya jamii na matarajio yetu kwa kipindi kinachokuja cha mwaka 2003/2004. Vile vile napenda niwashukuru Waheshimiwa Wabunge wenzangu waliochangia hoja za sekta zilizotangulia, kwani michango yao imenisaidia kwa kiwango kikubwa katika kuandaa hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, sekta ya nishati ni muhimu katika shughuli za kiuchumi na kijamii. Mwaka 2002 mchango wa Sekta ya Nishati kwenye Pato la Taifa *(GDP)* ulikuwaasilimia 1.5 kama ulivyokuwa mwaka 2001. Pamoja na mchango wake kutoongezeka, ni wazi kuwa sekta hii inachangia katika kuinua mchango wa sekta nyingine kwenye Pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, mwezi Februari, 2003 Serikali ilikamilisha na kuridhia durusu ya Sera ya Nishati iliyoandaliwa kwa kushirikisha wadau mbalimbali wa sekta. Sera hiyo kimsingi inahimiza ushirikishaji wa sekta binafsi katika kuendeleza vyanzo mbalimbali vya nishati vilivyomo nchini. Aidha, inasisitiza umuhimu wa Serikali kuendelea kujishughulisha ipasavyo na usambazaji nishati Vijijini hususan umeme.

Mheshimiwa Spika, chini ya programu ya *Institutional Support* Wizarani kwangu inayofadhiliwa na Serikali ya Sweden utekelezaji wa sera mpya ya nishati umeanza. Wizara inafanya maandalizi ya kuanzisha Wakala wa Nishati Vijijini *(Rural Energy Agency)* pamoja na Mfuko wa Nishati Vijijini *(Rural Energy Fund),* asasi ambazo zitasimamia kwa niaba ya Serikali uendelezaji wa nishati Vijijini. Wizara pia inashughulikia kuundwa kwa kitengo maalum cha kufuatilia athari za matumizi ya nishati katika mazingira, inaweka mfumo bora wa kutunza takwimu na taarifa za nishati *(national data bank)* na imeandaa mpango maalum wa kuongeza uwezo wa watumishi wa Wizara kitaaluma.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2002/2003, Makao Makuu ya Wilaya za Mbarali na Sikonge, Mji mdogo wa Nkinga Mwisi, Shule ya Sekondari ya Chidya na Vijiji zaidi ya 90 nchini ni miongoni mwa maeneo ambayo yalipatiwa umeme. Mradi wa ukarabati wa mifumo ya umeme katika Mikoa ya Tanga, Arusha na Kilimanjaro ili kuboresha huduma ya umeme ulihusisha ujenzi wa vituo vya kupunguza nguvu za umeme katika Miji ya Tanga, Moshi na Arusha chini ya ufadhili wa Mfuko wa Maendeleo wa nchi za Nordic, *Nordic Development Fund (NDF)* umekamilika. Mradi uligharimu jumla ya shilingi bilioni 1.5.

Aidha, miradi ya kupeleka umeme katika Makao Makuu ya Wilaya za Biharamulo na Ngara iliendelea kutekelezwa kwa kukamilisha ujenzi wa nyumba za mitambo ya kuzalisha ujenzi wa nyumba za mitambo ya kuzalisha umeme *(power houses).* Mradi wa kupeleka umeme Biharamulo utagharimu jumla ya shilingi bilioni 5.0 na ule wa Ngara utagharimu jumla ya shilingi bilioni 4.0.

Mheshimiwa Spika, mwaka jana nililieleza Bunge lako kuwa *TANESCO* inatarajia kujenga vituo vya kupunguza nguvu ya umeme ili kukidhi mahitaji ya umeme katika Jiji la Dar es Salaam. Napenda kuliarifu Bunge lako kuwa ujenzi wa kituo cha kupunguza nguvu za umeme wa *Bahari Beach* ulikamilika mwezi Julai, 2002. Kituo hicho kina uwezo wa Megawati 15. Aidha, mkandarasi amekabidhiwa eneo la ujenzi wa kituo cha kupunguza nguvu za umeme cha Tangi Bovu (Mbezi) na matayarisho ya awali kwa ajili ya kukijenga upya kituo hicho kitakachogharimu shilingi milioni 700 yameanza.

Mheshimiwa Spika, *TANESCO* imefanya upimaji na kulipa fidia ya mali kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha kupunguza nguvu ya umeme cha Tandika. Kituo hicho kitakuwa na uwezo wa Megawati 15. Vifaa kwa ajili ya ujenzi tayari vimewasili na taratibu za kupata hati ya kiwanja na kibali cha ujenzi zimeanza.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2000, Wizara imeendelea kusimamia mipango ya kupeleka umeme kwenye Makao makuu ya Wilaya, Miji midogo na Vijiji. Utekelezaji wa miradi ya kupeleka umeme Serengeti na Urambo inayogharimiwa na Serikali pamoja na Serikali ya Sweden kupitia Shirika la Kimataifa la Misaada ya Maendeleo *(SIDA)* unaendelea. Miradi ya Urambo na Serengeti itagharimu Dola za Marekani milioni 5 kila mmoja. Maandalizi ya mradi wa kupeleka umeme Ukerewe yamekamilika na utekelezaji wake utaanza mara baada ya taratibu za kuwapata mshauri na mkandarasi wa mradi zitakapokamilika. Mradi huo utakaogharimu dola za Marekani milioni 8 utahusu upelekaji umeme Nansio ambayo ni Makao Makuu ya Wilaya ya Ukerewe pamoja na Kibara Wilayani Bunda. Mradi huu unagharimiwa na fedha za Serikali pamoja na mkopo kutoka Serikali ya Ufalme wa Hispania. Mkataba wa mkopo ulisainiwa mwezi Novemba, 2002.

Aidha, Serikali ya Sweden kupitia Sida imeonyesha nia ya kufadhili mradi wa kusambaza umeme katika maeneo mengine ya Vijijini katika Wilaya ya Ukerewe hususan yale ambayo hayatagharimiwa na mkopo wa Serikali ya Ufalme wa Hispania. *Project document* imewasilishwa Ubalozi wa Sweden Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, Jedwali Na.1 na Na. 2 zinaonyesha uzalishaji na matumizi ya umeme hapa Tanzania tangu 1995 hadi 2002. Hivi karibuni Wizara yangu kwa kushirikiana na *TANESCO* imefanya tathmini ya bei za umeme katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki. Matokeo ya tathmini hii yanaonyesha kuwa bei za umeme za Tanzania siyo za juu zikilinganishwa na bei za umeme katika nchi za Kenya na Uganda tofauti na ilivyokuwa inaeleweka hapo awali.

Aidha, bei ya umeme kwa watumiaji wa majumbani wanaotumia, kwa mfano, chini ya uniti 200 kwa mwezi, ambao ndiyo wengi katika nchi yetu, iko chini kwa asilimia 20 ikilinganishwa na Kenya na kwa asilimia 22.4 ikilinganishwa na Uganda. Kwa watumiaji wakubwa wa umeme wanaotumia Megawati 5 kwa saa 24 kila siku, bei za umeme zinalingana nchini Tanzania na Kenya na zinazidi bei ya umeme Uganda kwa asilimia 26. Uwiano huu wa bei za umeme, ambao umeonyeshwa katika jedwali Na. 3, 4, 5, 6 na 7 kwa makundi tofauti ya watumiaji wa umeme, unaleta matumaini kwamba Tanzania itaweza kuhimili ushindani kwenye soko la umeme katika nchi za Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, mtambo wa *IPTL* umekuwa ukizalisha umeme kwa mwaka wa pili sasa tangu mgogoro kati yake na *TANESCO* kuamuliwa kwenye Mahakama ya Kimataifa. Napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa pamoja na punguzo la gharama za mradi lililotokana na hukumu ya Mahakama, bado bei ya umeme wa *IPTL* ni ya juu. Kutokana na mazingira hayo, Wizara yangu inawasiliana na Wizara husika huko Malaysia ili mazungumzo yafanyike katika ngazi ya Serikali kwa lengo la kupunguza bei ya umeme wa *IPTL.* Kamati ya Bunge ya Biashara na Uwekezaji ilitoa pendekezo kuwa Serikali iangalie uwezekano wa kununua mtambo wa *IPTL.* Wizara inaangalia kwanza uwezekano wa kushusha bei ya umeme wa *IPTL,* ili ikiwezekana Serikali isiingizwe kwenye kumiliki mtambo huo.

Mheshimiwa Spika, maandalizi ya kurekebisha muundo wa sekta ya umeme, kuigawa *TANESCO* katika kampuni tofauti zinazozalisha na kusambaza umeme na hatimaye kubinafsisha Kampuni hizo kwa awamu, bado yanaendelea chini ya uratibu wa Tume ya Rais ya Kurekebisha Mashirika ya Umma *(PSRC).*

Mshauri aliyeajiriwa na Serikali kuishauri juu ya namna ya kuigawa *TANESCO* amekamilisha awamu ya kwanza ya kazi yake na kuwasilisha mapendekezo ya awali na yanafanyiwa kazi na Serikali.

Aidha, ushauri kuhusu mfumo wa kuuziana umeme *(electricity trading arrangements)* baina ya kampuni zitakazozalisha na zitakazosambaza umeme umetolewa na mshauri mwingine na mapendekezo yake pia yanafanyiwa kazi. Baada ya Serikali kufanya maamuzi juu ya ushauri uliotolewa itaandaa Muswada wa Sheria mpya ya umeme na kuuwasilisha hapa Bungeni kabla ya kufikia hatua ya kuanza ubinafsishaji wa *TANESCO.*

Mheshimiwa Spika, kuhusu sekta ndogo ya petroli na gesi, vita vya Iraq vilileta wasiwasi mkubwa nchini, hususan kutokana na matarajio kuwa bei za mafuta zingepanda sana na kuathiri uchumi wetu. Kabla ya vita vya Iraq kuanza, bei ya mafuta kwenye soko la dunia ilipata Dola za Marekani 25 kwa pipa lakini ilipanda hadi Dola za Marekani 34 kwa pipa kabla ya kuanza kushuka tena. Pamoja na bei kushuka kwenye soko la dunia, hapa nchini ziliendelea kupanda kwa muda. Mazingira ya tofauti hiyo ni matokeo ya kutofuatwa kwa maadili ya biashara huria ambayo iliruhusiwa na Serikali kwa lengo la kuongeza ushindani na ufanisi kwa manufaa ya mteja. Serikali ilikemea vikali na kuagiza wafanyabiashara ya mafuta waache mara moja tabia zinazoashiria kuwepo upangaji wa bei za bidhaa muhimu kama mafuta. Wizara yangu inasisitiza kufuatwa kwa maadili sahihi ya biashara huria ya mafuta. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na *TPDC* na Kampuni za Mafuta ziliendelea kuratibu upatikanaji wa mafuta wakati wa vita vya Iraq. Upatikanaji wa bidhaa zote za mafuta ya petroli nchini ulikuwa wa kuridhisha.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha uliomalizika, idadi ya kampuni zilizosajiliwa kufanya biashara ya mafuta nchini zilikuwa 54 ikilinganishwa na kampuni 52 zilizokuwepo mwaka 2001/2002. Wizara imefuta kampuni za mafuta ambazo hazikuwa na uwezo na zilizokiuka masharti ya biashara ya mafuta na imesajili kampuni mpya. Wakati huo huo Kampuni ya Mobil ilijiondoa katika biashara ya mafuta na kufunga Ofisi zake hapa nchini.

Aidha, ili kuboresha usimamizi wa sekta hii, Wizara imeendelea kushirikiana na *PSRC* katika kuandaa uanzishwaji wa chombo cha kudhibiti na kusimamia Sekta ya Nishati na Maji *(Energy and Water Utilities Regulatory Authority – EWURA). EWURA* hivi sasa inatarajiwa kuanza kazi mwezi Septemba, 2003. Chombo hiki kitasaidia pia kusimamia ubora wa huduma pamoja na masuala ya usalama katika biashara ya mafuta ya petroli nchini. Sambamba na hilo, Wizara imekamilisha rasimu ya Sheria mpya ya mafuta ya petroli *(Petroleum Supply Act)* ambayo imezingatia hali halisi ya mfumo wa soko huria la mafuta ya petroli. Sheria hii itaimarisha usimamizi wa sekta ya petroli kibiashara, kiufundi na kimazingira.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia *PSRC* ina mpango wa kuuza sehemu ya hisa zake katika Kampuni za Mafuta za *Oryx, BP* na *TIPER.* Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi inaendelea kufuatilia kwa karibu hali ya usalama katika sehemu za kupokelea na kuhifadhi mafuta ya petroli nchini. Kamati maalum iliyoundwa mwaka 2001 kudhibiti wizi wa mafuta kutoka kwenye mabomba ya mafuta huko Kurasini, Dar es Salaam inaendelea na kazi hiyo ambapo hatua zimechukuliwa kuboresha na kuhakikisha hali ya usalama katika maeneo husika.

Mheshimiwa Spika, katika juhudi za kutafuta mafuta nchini, Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania *(TPDC)* linaendelea kushirikiana na kampuni zilizowekeza katika utafutaji wa mafuta. Hadi sasa ni Kampuni za Ndovu na *Antrim* tu ambazo zina leseni za kutafuta mafuta katika maeneo ya Nyuni na maeneo ya Unguja na Pemba. Kampuni ya *Maurel and Prom* kutoka Ufaransa imeonyesha nia ya kuwekeza katika maeneo yaliyo karibu na Dar es Salaam na Kimbiji yaliyokuwa yanashughulikiwa na Kampuni ya *Canop* ambayo ilijitoa katika utafutaji mafuta mwaka 2001. Majadiliano ya mkataba kati ya Serikali, *TPDC* na Kampuni ya *Maurel and Prom* yamekamilika na yatawasilishwa Serikalini kupata ridhaa ili mkataba usainiwe na utafutaji mafuta uendelee.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2001 Serikali ikishirikiana na *TPDC* na Kampuni ya *Western Geco* ilitangaza maeneo ya utafutaji mafuta katika kina kirefu cha maji baharini. Kampuni ya *Petrobras* ya Brazil imeonyesha nia ya kuwekeza katika utafutaji mafuta. Majadiliano kati ya Wizara, *TPDC* na Kampuni hii kuhusu mkataba wa kutafuta mafuta katika eneo la Mashariki ya Kisiwa cha Mafia yanaendelea. Maeneo mengine yalitangazwa mwezi Juni, 2002 na Kampuni ya *Shell International*

ikaonyesha nia ya kutafuta mafuta katika maeneo ya kina kirefu cha maji Mashariki ya visiwa vya Zanzibar na Pemba. Majadiliano baina ya Serikali, *TPDC* na kampuni hiyo kuhusu utafutaji wa mafuta katika maeneo hayo yanaendelea.

Mheshimiwa Spika, mkutano wa kwanza wa nchi za Afrika Mashariki kuhusu kutangaza na kuhamasisha wawekezaji kwenye maeneo yanayoonyesha dalili za kuwa na mafuta katika nchi hizo ulifanyika mwezi Machi, 2003 huko Nairobi, Kenya. Mkutano huo ulikuwa na zaidi ya washiriki 200 kutoka katika kampuni za utafutaji wa mafuta duniani, kampuni zinazotoa huduma mbalimbali za utafutaji, Benki za Kimataifa, wafadhili na washiriki kutoka nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki. Nchi yetu ilishiriki kikamilifu kwa kutoa mada zilizoelezea mazingira yetu ya kijiolojia, kisera na Kisheria, vivutio kwa wawekezaji na maeneo yaliyo wazi kwa utafutaji wa mafuta. Ni mategemeo yetu kuwa mada na taarifa zilizotolewa zitashawishi kampuni za utafutaji mafuta kuendelea kuwekeza nchini.

Mheshimiwa Spika, mikataba ya ujenzi wa bomba la kusafirishia gesi asilia ya Songo Songo ilitiwa saini mwezi Agosti, 2002. Maandalizi ya ujenzi yameanza, ujenzi unatarajiwa kuanza mwezi Septemba, 2003 na mradi unatarajiwa kukamilika mwezi Mei, 2004. Kazi nyingine ambazo zitafanyika ni ujenzi wa mtambo wa kusafisha gesi, kuweka mfumo wa mawasiliano, kukarabati mitambo ya kuzalisha umeme iliyoko Ubungo na kuirekebisha ili iweze kutumia gesi na kuvipatia umeme Vijiji na Miji midogo iliyo karibu na mkuza wa bomba la gesi. Umeme huo utazalishwa ama kwa gesi au kwa kutumia mionzi ya jua.

Mheshimiwa Spika, jitihada pia zimeelekezwa katika kuendeleza mradi wa kuzalisha umeme kwa kutumia gesi asilia kutoka *Mnazi Bay.* Majadiliano yanaendelea baina ya Serikali, *TPDC, TANESCO* na Kampuni ya *Artumas Group Inc*. ya Canada kuhusu vipengele vya mikataba ya kutekeleza mradi huo. Aidha, Wizara yangu kwa kuitumia *TANESCO* imefanya uchunguzi wa awali wa gharama za mradi mbadala wa kuzalisha umeme Somanga Funga, Wilayani Kilwa kwa kutumia gesi ya Songo Songo na kusafirisha umeme huo hadi Mikoa ya Lindi na Mtwara. Baada ya matokeo mazuri ya uchunguzi huo, Benki ya Dunia imekubali kutoa fedha kwa ajili ya kuufanyia mradi huo upembuzi yakinifu.

Pamoja na kwamba majadiliano kati ya Serikali na *Artumas Group Inc*. yanakaribia kukamilika, Wizara yangu itaendelea na maandalizi ya mradi wa kuzalisha umeme Somanga Funga. Uamuzi huu unatokana na ukweli kwamba hatutakuwa na uhakika wa kuweza kutumia gesi ya *Mnazi Bay* hadi mwekezaji wa mradi huo atakapokuwa amefanikiwa kufufua kisima cha gesi cha *Mnazi Bay,* kukifanyia majaribio na kuthibitisha kwamba kinaweza kuzalisha gesi ya kutosha kwa gharama inayokubalika, kama walivyofanya wawekezaji wa Mradi wa Gesi ya Songo Songo kwa visima vya Songo Songo. Kuendelea na maandalizi ya mradi wa kuzalisha umeme Somanga Funga kutatuwezesha kuona na kuamua ni mradi upi unaweza kutekelezwa mapema zaidi au kwa bei nafuu ya umeme ili kuondoa kero ya Mikoa ya Mtwara na Lindi ya kutokuwa na umeme wa kuaminika.

Mheshimiwa Spika, kufuatana na mwongozo uliomo katika Mpango Kamambe wa Taifa wa Uendelezaji Umeme *(National Power System Master Plan 2025),* Wizara yangu inaendelea kujadiliana na wawekezaji binafsi kuhusu uzalishaji umeme kwa kutumia makaa ya mawe ya Mchuchuma na maporomoko ya maji ya Mto Ruhudji ili kuweza kukabili ongezeko la mahitaji ya umeme nchini.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania *(TPDC).* Kama nilivyolieleza Bunge lako katika hotuba ya Bajeti ya mwaka uliomalizika, *TPDC* imebaki na majukumu ya kufanya utafiti wa awali wa utafutaji mafuta na gesi, kutangaza maeneo yaliyo wazi kwa wawekezaji na kuendeleza miradi ya gesi ya Songo Songo na *Mnazi Bay* na ya mafuta endapo yatagunduliwa. *TPDC* inaendelea kufanya kazi kulingana na majukumu yake ya sasa, lakini ina tatizo kwamba shughuli zake nyingi zinatekelezwa kwa kutegemea Bajeti ya Serikali ambayo haitoshelezi mahitaji ya majukumu yake ya msingi. Hata hivyo, ni matumaini yangu kuwa tatizo hili litamalizika kuanzia katikati ya mwaka 2004 *TPDC* itakapopata chanzo chake kipya cha mapato yaani mauzo ya gesi ya Songo Songo.

Mheshimiwa Spika, Sekta Ndogo ya Nishati Mbadala. Mwezi Septemba, 2002 nchi yetu ilishiriki katika Mkutano wa *World Summit on Sustainable Development* uliofanyika Johannesburg, Afrika Kusini.

Baadhi ya maeneo muhimu yaliyoamuliwa yawekewe mikakati ya maendeleo yenye misingi ya ushirikiano ni pamoja na uendelezaji wa matumizi ya nishati mbadala na matumizi bora ya nishati.

Mheshimiwa Spika, asilimia 90 ya nishati inayotumika kwa ajili ya kupikia majumbani inatokana na kuni na mkaa, hali ambayo inaleta athari kwa watumiaji kutokana na moshi na kuenea kwa jangwa. Kuna njia mbili kuu za kupunguza kiwango hiki cha matumizi. Njia ya kwanza ni matumizi bora ya nishati kwa kutumia majiko sanifu na ya pili ni kutumia nishati mbadala ambayo ni bora kuliko kuni na mkaa.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imeendelea kushirikiana na asasi husika kuangalia njia za kupunguza gharama za teknolojia ya nishati mbadala kwa ajili ya kupikia. Mpaka sasa mitambo zaidi ya 4,000 ya bayogesi imejengwa sehemu mbalimbali kwa ajili ya nishati ya kupikia na kutoa mwanga. Mikoa ambako teknolojia hii imeenea ni pamoja na Arusha, Kilimanjaro, Mwanza, Shinyanga, Kagera, Iringa, Dar es Salaam na Dodoma.

Mheshimiwa Spika, kuna maeneo mengi ambayo umeme wa gridi ya Taifa hautafika katika kipindi kirefu. Kwa kuzingatia kuwa wananchi wengi Vijijini wanatumia umeme kwa ajili ya nuru na siyo kupikia, Wizara yangu inaendelea na jitihada za kuendeleza nishati mbadala, hususan umemenuru na nguvu ya upepo kwa ajili ya kuzalisha umeme wa kukidhi mahitaji ya aina hiyo. Serikali ya Sweden kupitia Sida imeidhinisha msaada wa kiasi cha Dola za Marekani milioni 2.7 kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa kuwahamasisha wadau na kuondoa vikwazo vinavyozuia upatikanaji na uenezaji wa teknolojia ya umemenuru.

Mheshimiwa Spika, Tanzania inatarajia kunufaika na mradi mwingine chini ya ufadhili wa *GEF/UNDP,* ambao pia una lengo la kuondoa vikwazo katika uenezaji wa teknolojia ya umemenuru. Mradi huo utatekelezwa huko Mwanza. Lengo la mradi ni kuleta mwamko katika matumizi ya teknolojia ya umemenuru. Misaada yote hii inachangia moja kwa moja katika utekelezaji wa *World Solar Programme*, ambayo ilipendekezwa na Mkutano wa *World Solar Summit* uliofanyika Harare, Zimbabwe mwaka 1996. Katika utekelezaji wa programu hii, Tanzania ilipewa fedha kupitia *UNESCO* kwa ajili ya miradi ya maonyesho huko Umbuji, Zanzibar na Mangaka, Mtwara, ambako wananchi wamenufaika na umeme kwa matumizi ya shule, zahanati, kituo cha polisi na nyumba za walimu. Vile vile mwaka uliopita *UNESCO* ikishirikiana na Wizara yangu Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Tume ya Sayansi na Teknolojia *(COSTECH)* ilitoa mafunzo kwa washiriki 30 wakiwemo Watanzania 20 kuhusu umemenuru. Aidha, Serikali ya Denmark kupitia *DANIDA,* ilifadhili mradi wa kukusanya takwimu zitakazotumika kutathmini kasi ya upepo ambazo zitatumika katika kuendeleza nishati ya upepo katika maeneo muafaka nchini.

Mheshimiwa Spika, kwa kipindi kirefu sasa, Wizara yangu imeendelea na uhamasishaji wa matumizi bora ya nishati katika sekta mbalimbali, hususan majumbani na viwandani ambako kiasi kikubwa cha nishati hutumika. Zaidi ya viwanda 180 vimeshiriki kwenye zoezi la kutathmini matumizi ya nishati *(energy audits).* Utafiti unaonyesha kwamba kuna uwezekano wa kupunguza matumizi ya nishati kwa asilimia 20 hadi 30 endapo hatua mbalimbali zitachukuliwa.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imechukua hatua za makusudi za kufanya utafiti wa kupunguza matumizi ya nishati katika majengo ya umma hasa ya Serikali. Lengo kuu ni kuwahamasisha wahusika wajenge tabia ya kutumia nishati kwa ufanisi ili kupunguza matumizi bila kuathiri mahitaji halisi badala ya kulalamika kuhusu bei ya nishati kuwa juu.

Mheshimiwa Spika, uwezekano huu umedhihirishwa na mradi uliokamilika mwaka 2002, kuhusu *energy audits* zilizofanyika katika vituo vitatu vya kusukuma maji ya *DAWASA,* ambazo zilibainisha kwamba hadi asilimia 40 ya umeme unaotumika katika vituo hivyo ungeweza kuokolewa na shilingi bilioni 2.4 kuokolewa kila mwaka kama matumizi bora ya nishati yangezingatiwa. Nina imani kuwa hata majumbani kwa Waheshimiwa Wabunge na wananchi kwa ujumla kuna uwezekano wa kupunguza gharama za umeme kwa asilimia 20 au zaidi kwa kuzingatia matumizi bora ya nishati.

Mheshimiwa Spika, Tanzania ilishiriki kikamilifu katika Mradi wa *SADC Industrial Energy Management*, uliofadhiliwa na *CIDA* ambao ulidumu kwa miaka minane hadi Septemba, 2002. Chini ya

mradi huo zaidi ya Watanzania 100 walipata mafunzo juu ya matumizi bora ya nishati viwandani. Baadhi ya viwanda vyetu vilipatiwa zana za kufanyia tathmini ya matumizi ya nishati na kushauriwa juu ya hatua za kudhibiti upotevu wake.

Aidha, Taasisi mbili yaani Kitivo cha Uhandisi cha Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Taasisi ya Teknolojia ya Dar es Salaam zilipatiwa vitendea kazi muhimu kwa ajili ya kutoa mafunzo kuhusu matumizi bora ya nishati viwandani.

Mheshimiwa Spika, mchango wa sekta ya madini kwenye pato la Taifa ulifikia asilimia 2.7 mwaka 2002 ikilinganishwa na asilimia 2.5 mwaka 2001. Wakati huo huo ukuaji wa sekta hii ulifikia asilimia 15 mwaka 2002 ikilinganishwa na asilimia 13.5 mwaka 2001. Sekta imeendelea kuwa miongoni mwa sekta zinazokua kwa kasi kubwa.

Mheshimiwa Spika, dira ya Wizara yangu katika sekta ya madini ni kushirikisha sekta binafsi katika shughuli za madini kwa lengo la kuhakikisha kuwa madini yanachangia ipasavyo kukuza pato la Taifa na kuongeza maduhuli ya Serikali, ajira kwa Watanzania na mapato ya fedha za kigeni. Katika mwaka wa fedha uliopita Wizara yangu imeendelea na shughuli zake ambazo ni pamoja na kutoa leseni na vibali vya utafutaji, uchimbaji na biashara ya madini; kusimamia shughuli hizo; kukagua migodi, kudhibiti matumizi ya baruti na kutoa huduma kwa wachimbaji wadogo wa madini.

Mheshimiwa Spika, shughuli za utafutaji wa madini nchini zimeendelea kuongezeka hasa kwa madini ya dhahabu, *platinum* na vito. Utafutaji wa madini ya *platinum* unafanyika katika maeneo ya Mikoa ya Kigoma, Rukwa na Mbeya. Utafutaji wa *nickel* umeendelea katika maeneo ya Kabanga Wilayani Ngara ukiwa ni pamoja na kuchoronga miamba na kuichunguza ili kuthibitisha zaidi mashapo ya madini hayo.

Mheshimiwa Spika, ili kuimarisha utafutaji wa madini nchini, chini ya Mradi wa Uendelezaji wa Sekta ya Madini unaofadhiliwa na *Nordic Development Fund (NDF)* Wizara yangu inafanya utafiti na kukusanya takwimu za kijiokemia na kijiofizikia za miamba iliyo katika baadhi ya maeneo ya Mikoa ya Rukwa, Shinyanga, Kagera na Mara; itachora ramani mpya za kijiolojia na itaweka mfumo mpya na wa kisasa wa utoaji na usimamizi wa leseni za madini *(mining cadastre system).* Chini ya utafiti huo, takwimu zitakusanywa ili kutambua maeneo mapya yenye madini. Shughuli hizi ni muhimu katika juhudi zetu za kuendelea kuwavutia wawekezaji wa ndani na nje ya nchi kwa sababu zitawasaidia kutambua maeneo mpya yenye madini na kupata leseni za utafutaji au uzalishaji wa madini bila urasimu.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2002/2003 kulikuwa na ongezeko la uzalishaji wa dhahabu hasa baada ya migodi mipya miwili ya Afrika Mashariki na Buhemba kufunguliwa. Uzalishaji wa dhahabu umeendelea kuongezeka pia kutokana na migodi mingine hapa nchini kuendelea na utafutaji na kugundua mashapo zaidi kwa kufanya utafiti katika maeneo yaliyo karibu ya migodi hiyo. Tanzania sasa ina migodi mikubwa ya dhahabu mitano ambayo iko Geita, Kahama, Nzega, Tarime na Buhemba. Jedwali Na. 9 linaonyesha takwimu za mapato kwa nchi yetu kutokana na shughuli za kampuni mbalimbali zinazozalisha madini na Jedwali Na. 10 linaonyesha viwango vya kodi na mrahaba katika Sekta za Madini za nchi mbalimbali duniani ikiwemo Tanzania.

Mheshimiwa Spika, uzalishaji wa almasi katika mgodi wa Mwadui umekuwa ukiongezeka mwaka hadi mwaka baada ya kuthibitika kuwepo kwa mashapo ya kutosha na mgodi kununua na kufunga mtambo wa pili unaojulikana kama *in-line pressure jig*. Mtambo huo, ambao una uwezo wa kuchambua mchanga wenye almasi kidogo kwa gharama nafuu, ulianza kufanya kazi mwezi Julai, 2002. Inatarajiwa kwamba hadi kufikia mwaka 2005, mgodi utakuwa umeongeza uzalishaji wa almasi maradufu ikilinganishwa na uzalishaji wa sasa wa wastani wa karati 250,000 kwa mwaka.

Mheshimiwa Spika, miradi ya utafutaji na uchimbaji madini inahitaji fedha nyingi na teknolojia ya kisasa. Kwa hiyo, kwa muda mrefu ni kampuni zinazomilikiwa na wageni tu ndizo zilizokuwa mstari wa mbele kwenye Sekta hii. Nafurahi kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa mwaka huu kampuni mbili yaani *Tanzanite Africa Limited* na *El Hillal Minerals Limited* zimepata leseni za kuchimba *Tanzanite* na Almasi. Kampuni hizi zinamilikiwa na Watanzania na zina uwezo wa kutosha kufanya biashara hiyo kwa kiwango

cha kisasa. Aidha, kuna Watanzania ambao wameingia ubia na kampuni kubwa za kigeni kutafuta na kuchimba madini nchini mkakati ambao Serikali inauhamasisha.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuwasaidia wachimbaji wadogo ili waweze kuchimba dhahabu, vito, chumvi na madini ya ujenzi kwa tija zaidi na kwa kuzingatia kanuni za afya, mazingira na usalama. Wizara imekamilisha kituo cha mafunzo ya teknolojia bora na uchenjuaji wa dhahabu huko Matundasi, Wilayani Chunya. Kituo hicho hivi karibuni kitaanza kutoa mafunzo ya uchimbaji, uchenjuaji na kukodisha vifaa vya uchimbaji kwa wachimbaji wadogo.

Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Shirika la *UNIDO* imeendelea na utekelezaji wa mpango wa kutunza mazingira na kuhamasisha utumiaji wa teknolojia rahisi na salama katika uchimbaji na uchenjuaji wa dhahabu na utunzaji wa afya za wachimbaji wadogo wa dhahabu na katika ukanda wa Ziwa Victoria. Katika kutekeleza mpango huo, Dola za Marekani milioni 1.05 zimetolewa na Shirika la Umoja wa Mataifa la Mazingira (*Global Environmental Facility*). Mradi huu ni wa miaka mitatu kuanzia mwezi Machi, 2003 na unalenga kutoa mafunzo kwa wachimbaji wadogo; kuanzisha vituo viwili vya kuonyesha mfano wa teknolojia rahisi isiyotumia zebaki na ambavyo baada ya mradi vitamilikishwa kwa wachimbaji wadogo na kuainisha taratibu za utoaji mikopo kwa wachimbaji wadogo na kufanyiwa majaribio. Katika hatua nyingine, Wizara inaendelea kutoa mafunzo ya utunzaji wa mazingira kwa wachimbaji wadogo hasa wa dhahabu na vito. Mkazo umewekwa zaidi kwenye maeneo yenye mfumuko wa uchimbaji wa dhahabu.

Mheshimiwa Spika, ili kuwawezesha wachimbaji wadogo kuendelea kupata maeneo ya kuchimba madini, Serikali imekuwa ikitenga maeneo maalum kwa ajili ya wachimbaji hao. Maeneo ambayo tayari yametengwa kwa ajili hiyo hadi sasa ni pamoja na eneo lililogunduliwa na wachimbaji wadogo la dhahabu katika Wilaya za Kilindi, Mvomero na Kilosa. Wizara imeanza kugawa viwanja kwa wachimbaji wadogo katika eneo la Tunguli Wilayani Kilindi.

Aidha, taratibu za kutenga maeneo mengine ambayo yaligunduliwa na wachimbaji wadogo na kisha yakawa na mfumuko wa wachimbaji hao kama vile Nyamtukuza Wilayani Kibondo na Melela Wilayani Mvomero zinaendelea. Wizara pia inaendelea kurusha kipindi cha Madini na Maendeleo ambacho hutangazwa kila Jumapili jioni kupitia Redio Tanzania, Dar es Salaam ili kutoa elimu kwa wananchi kuhusu uchimbaji bora na salama.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa muundo wa Wizara yangu ulioidhinishwa mwaka 2001, Kitengo cha Wizara cha *Tanzania Geological Survey (TGS)* kinatakiwa kuundwa kama Wakala wa Serikali. Kuanzia mwaka 2002 Wizara imekuwa ikishirikiana na Idara Kuu ya Utumishi katika maandalizi ya kuifanya *TGS* kuwa Wakala wa Serikali na maandalizi hayo yanatarajiwa kukamilika mwaka 2004/2005. Kama Wakala, *TGS* itakuwa na majukumu ya msingi ya kukusanya, kuchambua na kuhifadhi taarifa za kijiolojia, kuchunguza miamba na madini, kuchora ramani za kijiolojia na kutoa huduma za kijiolojia na maabara kwa wanaohitaji huduma hizo ndani na nje ya Sekta ya Madini. Uuzaji wa madini nje ya nchi umeendelea kukua kwa kasi kutoka Dola za Marekani milioni 312 mwaka 2001 hadi Dola milioni 431 mwaka 2002, ongezeko la takriban asilimia 38. Hivi sasa madini ndiyo chanzo kikubwa cha fedha za kigeni kwa nchi yetu. Takwimu zinazohusika zinaonyeshwa kwenye Jedwali Na. 11 na Na. 12.

Mheshimiwa Spika, uchimbaji wa *Tanzanite* bado unafanywa kwa kiasi kikubwa na wachimbaji wadogo. Katika jitihada za kudhibiti uuzaji na usafirishaji wa *Tanzanite* ili ufanyike kwenye mkondo wa halali, mwezi Agosti, 2002 Serikali ilianzisha utaratibu unaotaka wanaosafirisha *Tanzanite* nje ya nchi wasaini hati maalum iitwayo *Tanzanite Warranty* inayothibitisha kwamba imetoka kwenye chanzo halali. Hati hiyo huambatana na kibali cha kusafirisha madini hayo nje ya nchi. Utaratibu huu unalenga kudhibiti utoroshaji wa madini hayo.

Mheshimiwa Spika, watakumbuka Waheshimiwa Wabunge kwamba Waziri wa Fedha alipokuwa akiwasilisha Bajeti ya Serikali ya mwaka 2003/2004 alisema kwamba Serikali inakusudia kupiga marufuku usafirishaji nje wa *Tanzanite* ghafi na kwamba ningetoa maelezo juu ya utekelezaji wa azma hii ya Serikali. Nachukua fursa hii kuliarifu Bunge lako kuwa Serikali itachukua hatua zifuatazo:-

(a) Itapitia haraka iwezekanavyo Sheria ya Madini ya mwaka 1998, Sheria ya *The Export Tax Act* ya 1974 na Sheria nyingine zinazohusika kuona kama zinahitaji kurekebishwa ili kuzuia uuzaji wa *Tanzanite* ghafi nje ya nchi. Kama ni lazima kuzirekebisha basi mapendekezo ya marekebisho hayo yataletwa Bungeni.

(b) Itawawezesha wafanyabiashara ya *Tanzanite* hasa Watanzania, kuwekeza katika viwanda vya kusanifu *Tanzanite* hapa nchini kwa kuchukua hatua ambazo ni pamoja na kuwapatia mafunzo wakataji, kuweka vivutio muhimu vya kodi na kupunguza urasimu katika utoaji wa leseni zinazohusika katika biashara ya *Tanzanite.*

(c) Itazuia uuzaji wa *Tanzanite* ghafi kwa awamu kulingana na uwezo wa kusanifu madini hayo hapa nchini utakavyoongezeka ili kuepukana na athari mbaya kwa wachimbaji na wauzaji wa *Tanzanite* hapa nchini na kulinda soko la *Tanzanite* nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, ni lengo la Wizara yangu kwamba ifikapo mwisho wa mwaka 2005, *Tanzanite* yote iwe inasanifiwa hapa nchini. Wadau wa *Tanzanite* wa ndani ya nchi wameshirikishwa kikamilifu katika kujadili suala hili kabla ya kufikia maamuzi juu ya suala hili na uchunguzi umefanyika ili kujua uwezo uliopo nchini hivi sasa wa kusanifu *Tanzanite*. Ni muhimu kuzuia uuzaji wa *Tanzanite* ghafi nje ya nchi kwa awamu kutokana na haja ya kupata muda wa kujenga uwezo wa kusanifu *Tanzanite* nchini, kutokuchochea utoroshaji wa *Tanzanite* ambayo itaendelea kuzalishwa, kutowaumiza wachimbaji wadogo hasa wanaotegemea uuzaji wa mawe madogo ya *Tanzanite* yajulikanayo kama upupu na kutokuathiri soko la Kimataifa la *Tanzanite* lenye wateja wakubwa ambao wanaweza kuacha kuinadi *Tanzanite* na kufanya bei yake iporomoke.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imekuwa ikijenga Kituo cha *Arusha Gemstone Centre* tangu mwaka 2002. Kituo hiki kitaanza kutoa mafunzo ya uchongaji wa vinyago kwa kutumia miamba na vito. Wizara yangu tayari imeanza kutoa mafunzo kama hayo na lengo ni kuendeleza mafunzo hayo kwenye kituo hicho kitakapokamilika mwaka huu wa 2003/2004.

Mheshimiwa Spika, ukusanyaji wa kodi zitokanazo na biashara ya madini unaimarishwa. Hatua mojawapo itakayochukuliwa ni kuwawekea wafanyabiashara ya madini viwango vya chini vya mauzo vitakavyotumika kwa ajili ya kuwatoza kodi. Hatua hii inatarajiwa kupunguza idadi ya wafanyabiashara wadanganyifu wa madini ambao huharibu sifa ya wenzao waadilifu.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza maazimio ya Umoja wa Mataifa kuhusu udhibiti wa biashara haramu ya almasi inayochochea vita na ugaidi Mikutano ya Kimataifa imekuwa ikifanyika tangu mwaka 2001 ili kuweka utaratibu ujulikanao kama *Kimberley Process Certification Scheme for Rough Diamonds*. Katika kutekeleza utaratibu huo, Tanzania imeunda kanuni mpya chini ya Sheria ya Madini ya mwaka 1998 ambazo zinalazimu almasi zinazosafirishwa nje ya nchi ziambatane na hati maalum zinazothibitisha zilikotoka.

Mheshimiwa Spika, katika jitihada za kuongeza uwezo wa kusimamia na kukusanya mapato ya Serikali yatokanayo na madini, Wizara yangu imenunua magari mapya 16 na pikipiki kumi kwa ajili ya Ofisi za Madini nchini. Upatikanaji wa usafiri utawawezesha Maofisa wa Madini katika Ofisi hizo kufanya ukaguzi wa mara kwa mara na kuwa na uwezo wa kuwafikia wachimbaji wadogo wengi zaidi ili kuwapa huduma mbalimbali na kufuatilia kodi na ada zitokanazo na shughuli za madini. Aidha, Wizara imeimarisha majengo ya Ofisi za Madini za Bukoba na Shinyanga na inakusudia kujenga Ofisi Geita na Kahama. Vile vile, Wizara inakusudia kuweka kompyuta katika Ofisi zote za Madini nchini na Makao Makuu ya Wizara ili kuimarisha mawasiliano.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na manung'uniko mengi kuwa Serikali haina udhibiti wa kutosha katika kusimamia uchimbaji mkubwa hapa nchini. Naomba kulihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa Serikali ina taratibu za kuhakikisha kuwa wachimbaji wakubwa hawatoroshi madini na kulipotezea Taifa mapato yake.

Hata hivyo, ili kuimarisha udhibiti wa madini, Serikali imeamua kuweka Mkaguzi maalum wa shughuli za uzalishaji dhahabu katika migodi mikubwa. Mkaguzi huyo ajulikanaye kama *Gold Assayer* amekwishaanza kazi chini ya usimamizi wa Benki Kuu ya Tanzania na zaidi ya kukagua uzalishaji wa dhahabu atachunguza pia kama kuna umuhimu wa kupeleka mchanga na sampuli za madini nje ya nchi. Katika hatua nyingine ya kuimarisha usimamizi wa madini, Wizara yangu imeshaanza taratibu za kumpata mtaalam atakayekagua shughuli za Kampuni ya *Williamson Diamonds Limited* na mgodi wake wa Mwadui. Mtaalam huyo atatoa maoni kuhusu uendeshaji na hali ya kifedha ya mgodi huo na atashauri juu ya hatua za kuchukua ili kusimamia shughuli zake kwa karibu zaidi.

Kuhusu usimamizi wa mapato yatokanayo na shughuli za madini, Wizara kwa kushirikiana na *TRA* na kwa msaada wa Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Marekani *(USAID)* imeandaa mafunzo kwa wakadiriaji kodi wa *TRA* ili waweze kukadiria kwa usahihi kodi zinazohusika katika uchimbaji madini nchini. Mafunzo yalianza mwezi Agosti, 2002 kwenye Taasisi ya *ESAMI* Mjini Arusha na mengine yanaandaliwa.

Mheshimiwa Spika, mbali ya masharti yaliyopo kwenye mikataba na leseni za kutafuta na kuchimba madini tunazotoa kwa wawekezaji wakubwa, Serikali pia inataka wawekezaji hao kuhakikisha kuwa wanatimiza mambo muhimu yafuatayo:-

Kwanza, kuajiri Watanzania wengi iwezekanavyo katika ngazi zote ambao wana uwezo unaotakiwa, kuwapa Watanzania mafunzo kazini na vyuoni, kununua vifaa na huduma nyingi iwezekanavyo humu humu nchini, kuchangia kwa hali na mali miradi ya maendeleo katika maeneo ya migodi yao na kutii Sheria zote za nchi zikiwa ni pamoja na za kodi.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imekamilisha kanuni maalum chini ya Sheria ya Madini za kusimamia eneo la Merelani *(Merelani Controlled Area)* na zimeanza kutumika na zoezi la kuwaondoa wazururaji katika machimbo ya Merelani linaendelea. Vile vile, Wizara imeandaa mapendekezo kuhusu marekebisho ya Sheria ya Baruti ambayo yatawasilishwa kwenye Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ambayo inaratibu utekelezaji wa Azimio la nchi za *SADC* kwamba kila nchi iunganishe Sheria zake zinazohusu silaha ndogo ili kuimarisha udhibiti wa ugaidi.

Katika kutekeleza Azimio hilo, Serikali imeamua kwamba Sheria ya Baruti ya mwaka 1963 nayo ihusishwe. Hatua nyingine inayochukuliwa na Wizara yangu hivi sasa ni kupitia Sheria mbalimbali ikiwemo Sheria ya Masonara kwa lengo la kupendekeza namna ya kuirekebisha ili kuimarisha usimamizi wa shughuli zinazoendelea chini ya Sheria hiyo.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea na utaratibu wa kuunda upya Shirika la Madini la Taifa kuwa wakala wa Serikali kwa lengo la kuendeleza utafiti na uchimbaji wa madini ambayo ni malighafi viwandani na yanayotumika katika kilimo na kutoa huduma za ushauri wa kijiolojia na utunzaji wa mazingira kwa wachimbaji wadogo.

Mheshimiwa Spika, Mgodi wa Makaa ya Mawe wa Kiwira Mkoani Mbeya, unaendelea kuzalisha makaa ya mawe kwa kiwango kidogo kutokana na ufinyu wa soko, uchakavu wa mitambo na kukosa mwekezaji mwenye uwezo wa kifedha wa kuingia naye ubia. Mbali ya fedha za kununulia vifaa, kiasi cha Dola za Marekani milioni 2.5 zinahitajika ili kuanzisha eneo jipya la uchimbaji makaa. Kampuni ya Kichina *(CHITEC)* iliyojitokeza mwaka 1999 kuingia ubia katika mgodi imejitoa na hivi sasa juhudi zinaendelea ili kumpata mbia mwingine.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2002/2003 Wizara yangu kwa kushirikiana na Mamlaka mbalimbali iliweza kuajiri watumishi wapya 35. Katika kipindi hicho Wizara iliwapandisha vyeo Watumishi 205 kati ya watumishi 526 wa Wizara. Aidha, watumishi 101 wa kada mbalimbali walipatiwa mafunzo ya muda mfupi na mrefu ndani na nje ya nchi. Watumishi hao walikuwa ni pamoja na Wahandisi Mgodi ambao walishikizwa katika Kampuni za Migodi kwa mafunzo ya vitendo. Katika kipindi hicho utumishi wa watumishi saba ulikoma kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo kufukuzwa kazi na vifo.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2003/2004 Wizara itaendelea kutekeleza mpango wake wa mafunzo na mkazo mkubwa utawekwa katika kuwahamasisha watumishi ili wapambane kikamilifu na rushwa pamoja na janga kubwa la Ukimwi.

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Madini kilichopo Dodoma kinaendelea kutoa mafunzo kwa mafundi sanifu waliopo Wizarani, walioajiriwa kwenye migodi na waliojiajiri katika uchimbaji mdogo. Chuo kina mpango wa kuwafundisha na kuwaendeleza kitaaluma wahitimu wa kidato cha nne watakaopenda kujiajiri wenyewe au kuajiriwa katika sekta ya madini.

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Madini kinaendesha mafunzo ya muda mrefu ya cheti cha ufundi sanifu *(Full Technician Certificate - FTC)* pamoja na ya muda mfupi. Mafunzo yanayotolewa ni ya utafiti, uchimbaji na uchenjuaji wa madini kwa kuzingatia usalama wa wachimbaji wenyewe na mazingira yanamochimbwa. Mafunzo yanaendeshwa darasani na kwa vitendo kwenye migodi mikubwa na midogo.

Aidha, wanafunzi wanapewa mafunzo ya matumizi ya kompyuta katika fani ya madini. Katika mwaka 2002/2003 wanafunzi 30 walisajiliwa na kuanza mafunzo ya muda mrefu. Kati ya hao, 16 walikuwa ni mafundi sanifu kutoka Ofisi za Madini za Kanda na 14 wahitimu wa kidato cha nne. Aidha, katika kipindi hicho, Chuo kiliendesha kozi tatu fupi kwa wahitimu 67 ambapo kati ya hao 57 walikuwa ni mafundi sanifu wa Wizara yangu, wanne mafundi sanifu kutoka kwenye migodi binafsi, watano walikuwa ni wachimbaji wadogo na mmoja alikuwa ni mwandishi wa habari. Katika mwaka 2003/2004 Chuo kinatarajia kusajili wanafunzi 40 kwa ajili ya masomo ya ufundi sanifu na kuendesha mafunzo ya muda mfupi kwa awamu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hatua hii nzuri iliyofikiwa, ujenzi wa miundombinu ya Chuo cha Madini bado haijakamilika. Hivi sasa Chuo kina jengo la Utawala, ukumbi wa mikutano, jiko, bwalo la chakula, bweni la wanafunzi 88 na madarasa matatu. Katika kipindi cha 2003/2004, Wizara inatarajia kujenga maktaba, maabara ya madini, madarasa mengine, nyumba za walimu na viwanja vya michezo.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imeendelea kushirikiana na nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki *(EAC)* na Jumuiya ya Nchi za Kusini mwa Afrika *(SADC)* katika kuendeleza Sekta za nishati na madini. Wizara pia inashirikiana na nchi nyingine wanachama wa Kituo cha Madini *(Southern and Eastern African Mineral Centre - SEAMIC)* kilichopo Kunduchi, Dar es Salaam. Kituo hiki kinaendelea kujishughulisha na utafiti wa uendelezaji wa madini katika nchi wanachama yaani Angola, Comoro, Ethiopia, Msumbiji, Uganda na Tanzania. Hivi sasa kituo kinajaribu kuzishawishi nchi jirani za Malawi, Kenya, Rwanda na Burundi kujiunga kuwa wanachama.

Mheshimiwa Spika, Tanzania imekuwa ikinunua kiasi kidogo cha umeme kutoka Zambia na Uganda kwa miaka kadhaa. Katika kipindi cha miaka michache ijayo tunatarajia kuweza kuiuzia Kenya umeme na hata gesi ya Songo Songo . Wizara yangu inaendelea kuzungumza na Wizara zinazohusika nchini Kenya na Zambia kuhusu ujenzi wa njia kuu za umeme *(interconnectors)* zitakazounganisha gridi za nchi zetu kupitia Arusha hadi Nairobi, Kenya na Mbeya hadi Pensulo, Zambia. Mwaka uliokwisha wa 2002/2003 Tanzania ilichaguliwa kuwa Makao Makuu na mratibu wa mradi mpya wa *Nile Basin Countries Power Trade Power* ambao umezijumuisha nchi zote za Bonde la Mto Nile kwa lengo la kuendeleza ushirikiano wao katika kupanga na kutekeleza na kuendesha miradi ya umeme utokanao na nguvu za maji na vyanzo vingine.

Mheshimiwa Spika, katika kuendeleza sekta ya nishati na madini Wizara yangu imeendelea kushirikiana na Serikali za nchi nyingine na Mashirika ya Kimataifa. Kwa niaba ya Serikali napenda kutoa shukrani kwa Serikali hizo na Mashirika hayo. Naomba nizipongeze kipekee Serikali za Australia, Canada, China, Denmark, Finland, Hispania, Japan, Marekani, Norway, Sweden, Ufaransa, na Ujerumani.

Aidha, natoa pongezi kwa Umoja wa Mataifa na Umoja wa Nchi za Ulaya na kuyashukuru Mashirika ya Kimataifa ambayo ni Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika, Benki ya Raslimali ya Ulaya,

*Global Environmental Facility (GEF), IMF, KfW, NDF, NORAD, SIDA, UNDP, UNESCO, UNIDO* na *USAID.*

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia fursa hii kuwashukuru kwa dhati Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Uwekezaji na Biashara chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa William Shelllukindo, Mbunge wa Jimbo la Bumbuli. Maelekezo na ushauri wa Kamati hiyo umesaidia sana katika maandalizi ya hotuba hii na utazingatiwa na Wizara katika utekelezaji wa majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, pia nawashukuru Mheshimiwa Dr. Ibrahim Msabaha, Mbunge wa Jimbo la Kibaha na Naibu Waziri wa Wizara ya Nishati na Madini na Bwana Patrick Rutabanzibwa, Katibu Mkuu wa Wizara kwa ushirikiano na msaada mkubwa wanaonipa katika kuiongoza Wizara hii.

Pia nawashukuru Wakuu wa Idara na vitengo na watumishi wote wa Wizara pamoja na viongozi wa Mashirika yaliyo chini ya Wizara, kwa ushirikiano wao katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara. Aidha, namshukuru Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali kwa kazi nzuri aliyoifanya katika kukamilisha hotuba hii kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, hotuba yangu imeambatishwa majedwali kadhaa kuanzia ukurasa wa 38. Naomba Waheshimiwa Wabunge warejee majedwali hayo kwa ufafanuzi zaidi wa hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, sasa naliomba Bunge lako likubali na kuidhinisha mapendekezo ya Bajeti ya shilingi 127,457,530,800 kwa ajili ya matumizi ya Wizara na mashirika yake kwa mwaka 2003/2004. Mchanganuo wa bajeti hii ni kama ifuatavyo:-

(i) Bajeti ya maendeleo ni shilingi 102,091,552,300 ambazo kati yake shilingi 5,199,552,300 ni fedha za hapa na shilingi 96,892,000,000 ni fedha za nje na Bajeti ya matumizi ya kawaida ni shilingi 25,365,978,500 ambapo shilingi 855,284,200 ni kwa ajili ya mishahara *(PE)* na shilingi 24,510,694,300 ni matumizi mengineyo *(OC).*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAWASIALIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO – MWENYEKITI WA KAMATI YA UWEKEZAJI NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kuchukua nafasi hii kukushukuru wewe mwenyewe kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuwasilisha maoni ya Kamati ya Bunge ya Uwekezaji na Biashara kuhusu utekelezaji wa malengo ya Wizara ya Nishati na Madini kwa mwaka wa fedha uliopita pamoja na kutoa maoni ya Kamati kuhusu makadirio na matumizi ya Wizara hiyo katika mwaka wa fedha 2003/2004.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kutekeleza masharti ya Kanuni ya 81(1), Toleo la 2003, napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati ya Uwekezaji na Biashara kwa ushirikiano wao na umakini wakati wa kuchambua na kujadili mpango wa bajeti ya Wizara zilizopo kwenye *portfolio* yake.

Naomba niwatambue wajumbe hao kwa sababu ni mara ya kwanza kwa Kamati yangu kuwasilisha taarifa hapa. Wajumbe hao ni Mheshimiwa Salome Mbatia, Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Kassim Mwandoro, Mheshimiwa Dr. Aaron Chiduo, Mheshimiwa Omar Chubi, Mheshimiwa Dr. James Wanyancha, Mheshimiwa Semindu Pawa, Mheshimiwa Herbert Mntangi, Mheshimiwa Stephen Kazi, Mheshimiwa Margareth Bwana, Mheshimiwa Christopher Wegga, Mheshimiwa Freeman Mbowe, Mheshimiwa Aisha Magina, Mheshimiwa Mohamed Abdulaziz, Mheshimiwa Dr. Lucy Nkya, Mheshimiwa Fatma Said Ali, Mheshimiwa Ali Machano Mussa, Mheshimiwa Khamis Abeid Aboud, Mheshimiwa Ismail Iwvatta, Mheshimiwa Nazir Karamagi, Mheshimiwa Abu Kiwanga, Mheshimiwa Mohamed Ali Said na Mheshimiwa Sumri Mohamed. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati, sasa naomba kuwasilisha Taarifa ya utekelezaji wa malengo ya Bajeti kwa mwaka 2002/2003 na kutoa maoni ya Kamati kuhusu makadirio ya Wizara ya Nishati na Madini kwa mwaka wa fedha 2003/2003.

Aidha, ili kutekeleza jukumu hili, Kamati yangu ilizingatia maeneo yafuatayo, Dira, Malengo pamoja na Madhumuni ya Wizara hiyo, Taarifa ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati kwa kipindi cha mwaka 2002/2003, Taarifa kuhusu Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa kipindi cha 2002/2003, Mafanikio na Matatizo yaliyojitokeza wakati wa utekelezaji wa Malengo ya Bajeti ya mwaka 2002/2003, kazi zilizopangwa kufanyika kwa mwaka wa fedha 2003/2004 na maombi ya fedha kwa kazi zilizopangwa kwa mwaka wa fedha 2003/2004.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu kwa ujumla imeridhika na Dira ya Wizara ya Nishati na Madini inayolenga kuwa na nishati ya kutosha na ya gharama nafuu na pia mchango mkubwa kwenye Pato la Taifa hasa kutokana na Sekta ya Madini. Aidha, Kamati imeridhika na madhumuni *(mission)* ya Wizara hiyo ambayo ni kuweka mazingira mazuri ya kisera, kisheria, mikakati na muundo wa Wizara na Taasisi zilizoko chini ya Wizara hii ili kufanikisha malengo ya Dira ya Wizara hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa kuwa katika kutekeleza mpango wa maendeleo na bajeti ya mwaka 2003/2004, Wizara itakuwa na malengo ya msingi yafuatayo. Kuweka mazingira bora ya utoaji huduma kwa umma; kuandaa sera, sheria na taratibu zitakazowezesha wadau kushiriki ipasavyo katika uendelezaji wa sekta ya nishati na madini; kuwezesha upatikanaji wa huduma ya nishati ya kutosha ya bei nafuu na kusimamia shughuli za utafutaji na uchimbaji wa madini; kuhimiza utafiti na matumizi ya teknolojia bora katika kuendeleza sekta ya nishati na madini; kuendelea na kuimarisha ushirikiano kati ya sekta, nchi yetu na Jumuiya za Kimataifa katika Sekta ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Spika, kimsingi, Kamati yangu ya Uwekezaji na Biashara inaafikiana na Wizara hii juu ya malengo yaliyoainishwa hapo juu na kushauri kuwa ili kuleta ufanisi wa kufikia malengo hayo, Wizara sasa iandae programu pamoja na mikakati *(action plans and strategies)* za kuyatekeleza hayo.

Mheshimiwa Spika, katika kikao chake cha tarehe 5 Juni, 2002 iliyokuwa Kamati ya Kisekta ya Biashara ilitoa maoni na ushauri mbalimbali ambao ulihitaji kufanyiwa kazi ili kuboresha ufanisi wa utendaji kazi wa Wizara hiyo. Wizara imeweza kutekeleza na kutoa maelezo ya kina juu ya utekelezaji wa maoni na ushauri uliotolewa na Kamati hiyo. Kwa kiasi kikubwa, Kamati yangu iliridhika na hatua za utekelezaji zilizochukuliwa na Wizara. Hata hivyo, katika kujadili utekelezaji huo, Kamati ilisisitiza umuhimu wa Wizara kuchukua hatua zaidi na za makusudi katika maeneo yafuatayo:-

Kwanza, bei kubwa ya umeme. Hili tutalitolea tena maoni na ushauri kabla ya kumalizia taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, pili, Chuo cha *TANESCO* Kidatu ambacho sasa kimefungwa lakini yako majengo pale, tatu, migogoro katika maeneo ya machimbo ya madini, nne, Elimu ya Ukimwi kwenye maeneo ya machimbo ya madini na tano, tatizo la kukatikatika umeme.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema, tutayatolea maoni zaidi kwa sababu ni mambo ambayo yamejirudia katika Taarifa yetu.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa kuwa katika kipindi cha mwaka 2002/2003 makadirio ya makusanyo ya maduhuli kutoka katika sekta ya madini yalikuwa yawe ni shilingi 12,961,962,573/= ambapo 32% ya mapato hayo yalitengwa kwa ajili ya kuimarisha sekta ya madini pamoja na matumizi mengine ya Wizara hiyo. Aidha, hadi kufikia tarehe 31/3/2003, Wizara ilikuwa imekusanya jumla ya shilingi 11,613,680,500/= ambayo ni sawa na 90% ya lengo ya maduhuli yaliyotakiwa kukusanywa.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa kuwa katika kipindi cha mwaka 2002/2003, Wizara ilipata mafanikio yafuatayo:-

Kuzinduliwa kwa Mgodi mkubwa wa dhahabu wa *North Mara* mwezi Septemba, 2002, *TANESCO* kuendelea kujiimarisha kimapato na hivyo kujenga uwezo ili kupunguza baadhi ya kero za wateja, kukamilika kwa maandalizi muhimu ya ujenzi wa bomba la gesi la Songosongo. Aidha, Kamati ilipokea taarifa kuwa gesi ya Songosongo itafika Ubungo mwezi Mei, 2004, ununuzi wa vifaa vitakavyofungwa kwenye kituo cha kukatia madini Arusha, *Jameson Carving Centre,* kukamilika ujenzi wa kituo cha Matundasi huko Chunya na kupeleka umeme katika Makao Makuu ya Wilaya za Mbarali, Sikonge pamoja na baadhi ya vijiji.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio hayo, Kamati ilielezwa kuwa matatizo yaliyojitokeza ni kama kutotimizwa kwa masharti ya mikataba kwa mfano Mkataba wa *IPTL* pamoja na Mkataba wa Songosongo, kutokamilika kwa baadhi ya miradi ya kupeleka umeme vijijini, ukosefu wa wataalam wa kutosha wa kuweza kupima vitalu vya madini na kukagua wenye leseni hasa Wahandisi wa Jiolojia na Mafundi Sadifu ili kuongeza maduhuli, kutokamilika kwa miundo mbinu muhimu kwa mfano maktaba, maabara, viwanja vya michezo, nyumba za Walimu hasa katika Chuo cha Madini hapa Dodoma na kutokuwa na Ofisi za Madini karibu na maeneo mbalimbali ya uchimbaji wa madini hivyo wachimbaji kukosa utaalam wa mara kwa mara.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu ilielezwa kuwa katika kipindi cha mwaka 2003/2004, Wizara imepanga kutekeleza kazi zifuatazo. Kuimarisha na kuendeleza sekta ya madini; kuendeleza programu ya umeme vijijini, kutangaza na kuendeleza nishati mpya ya kujadidika *(Renewable Energy),* kuimarisha mfumo wa umeme nchini; kuendeleza sekta ndogo ya petrol na utafutaji wa mafuta, kuendeleza gesi asilia ya songosongo, kuboresha mazingira ya kazi ya watumishi na kuwaendeleza na kuimarisha ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali katika sekta ya nishati na madini.

Mheshimiwa Spika, baada ya Kamati yangu kuchambua kwa kina makadirio na matumizi na mapato ya Fungu 58 - Wizara ya Nishati na Madini na kazi zilizopangwa kwa mwaka 2003/2004 Kamati inatoa ushauri ufuatao ili kuboresha utekelezaji wa kazi katika Wizara hiyo.

Mheshimiwa Spika, moja ya kikwazo kikubwa cha uchumi wetu kutokua kwa kasi inayostahili hasa kwa eneo la viwanda ni bei kubwa ya umeme inayotumika viwandani na majumbani. Hali hii husababisha gharama kubwa ya uzalishaji na hivyo kupunguza uwezo wa bidhaa zinazozalishwa na viwanda vyetu kushindana na bidhaa zinazoingizwa nchini na katika soko la dunia kwa jumla. Pamoja na *Management* mpya ya *TANESCO* yaani *Net Group Solutions* kuimarisha ukusanyaji wa mapato bado mafanikio hayo hayajasaidia kupunguza bei ya umeme.

Mheshimiwa Waziri alitoa maelezo ya *comparison* ya *tariffs* za umeme lakini kuna mazingira mengine ambayo pengine yangetazwa zaidi kuliko kuangalia tu hiyo. Nasema hivyo kwa sababu hatuelewi Kenya umeme wao unatoka umbali gani na vile vile mtandao wake umewekwaji na mita zilizopo kule zikoje kuna uwezekano pengine mita tunazotumia zinaongeza matumizi kuliko ilivyo kwa hiyo inaonekana wakati wote bei za umeme katika viwanda vyote ni kubwa. Tulipotembelea maonyesho kule Dar es Salaam, tunamshukuru sana Mheshimiwa Dr. Juma Ngasongwa, Waziri wa Viwanda na Biashara kutuwezesha kutembelea maonyesho. Tumeelezwa waziwazi kwamba katika *calculations* zao umeme ni nyenzo mojawapo ambayo ina bei kubwa sana. Sasa hii *contradiction* tunashindwa kuielewa nadhani itafutiwe ufumbuzi ili tuelewe tatizo ni nini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Dira ya Wizara kuhusu nishati ni kuwa na nishati ya kutosha na ya bei nafuu ipatikane. Kwa mantiki hiyo, Kamati inaishauri Serikali kuchukua hatua za dhati za kupunguza bei ya umeme iwapo inataka nchi yetu ifikie maendeleo ya nchi ya viwanda vya kati *(semi industrialized economy)* ifikapo mwaka 2025.

Mbali ya bei kubwa ya umeme tatizo lingine sugu ni kukatikakatika kwa umeme hali inayosababisha uharibifu wa mali za watu na kuleta hasara kubwa katika viwanda, maofisini na hata majumbani. Ili kutatua tatizo hili, Kamati inashauri Serikali na *TANESCO* kutenga fedha za kutosha ili kuimarisha mfumo wa usambazaji umeme kiufundi na teknolojia. Hata hivyo, Kamati imefurahishwa kupokea taarifa kuwa baada ya kujiimarisha kimapato *Management* mpya ya *Net Group Solutions* imeanza

kushughulikia tatizo hili kupitia timu Maalum ya Ufundi *(Special Maintenance Team)* ambayo hivi sasa imeanza kazi Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, Mkataba wa *IPTL* unagharimu Tanzania shilingi bilioni 2.5 kila mwezi ikiwa ni gharama za kudumu *(fixed costs)* kutokana na mkataba kati ya Serikali na *IPTL.* Hata hivyo, pamoja na gharama hiyo kubwa bado *TANESCO* haitumii kikamilifu umeme wa mitambo hiyo ya *IPTL* ambao una uwezo wa kutoa umeme wa *megawatt* 100.

Kwa mantiki hiyo, Kamati inaona kuwa mkataba huu hausaidii chochote na inaweza kuwa pengine mtego wa kiujanjaujanja wa kuhujumu uchumi wa nchi kuwa na mradi ambao unalipiwa kila siku lakini nguvu zile hazitumiki, sijui tuitee hujuma au ndio utekelezaji bora wa shughuli zetu, nadhani sivyo. Kwa hiyo, Kamati inashauri Serikali ipitie upya mkataba huo na wale wote waliosaini mkataba huo wenye utata wachukuliwe hatua zinazostahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, Kamati inaishauri Serikali na *Management ya TANESCO Network Group Solution* kutekeleza kwa makini mpango wake wa biashara *(business plan)* wa mwaka 2003 – 2007 ili kukidhi mahitaji ya dira ya Wizara kuwa na umeme wa kutosha na wa bei nafuu kwa kutumia vyanzo vingine vya umeme kama gesi ya Songosongo na makaa ya mawe ya Mchuchuma. Hapa Kamati imefurahishwa sana na taarifa kuwa gesi ya Songosongo itafika Ubungo mwezi Mei, 2004.

Mheshimiwa Spika, kwa upande mwingine, Kamati inaishauri Serikali iangalie uwezekano wa kununua mtambo wa *IPTL* ili kuondokana na gharama ya kudumu ya shilingi bilioni 2.5 kwa mwezi. Ijapokuwa taarifa iliyotolewa na Mheshimiwa Waziri kwamba, Serikali isingeweza kuingia katika shughuli hiyo lakini Serikali n*i custodian* kama kuna mradi haujapata mwekezaji yoyote. *Custodian* ni Serikali, hatuwezi kuuacha mradi hivyo hivyo bila uamuzi endelevu.

Mheshimiwa Spika, umeme ni kichocheo kikubwa sana cha maendeleo ya kiuchumi mjini na vijijini. Kutokana na ukweli huo, mnamo mwaka 1998, Serikali ilifanya utafiti wa umeme vijijini *(Rural Electrification Study)* iliyolenga kubaini mahitaji ya umeme kwenye maeneo mbalimbali vijijini na kuweka mkakati wa kupeleka umeme vijijini. Hata hivyo, hadi hivi leo matokeo ya utafiti huo hayajajulikana. Hivi sasa Wizara imeunda Mfuko Maalum wa Nishati Vijiji *(Rural Energy Fund)* utakaosimamiwa na Wakala wa Nishati Vijijini *(Rural Energy Agency).*

Kamati inaishauri Serikali kuweka sera na mikakati endelevu ya kupeleka umeme vijijini badala ya kuwa na mipango ya makaratasi ambayo haieleweki hususan katika kipindi hiki ambacho *TANESCO* iko katika hatua ya awali ya kubinafsishwa. Tunasema hivyo kwa sababu kuna baadhi ya maeneo ambayo yamekubaliwa yapelekewe umeme lakini katika orodha ya maeneo ya kupelekewa umeme hayamo mathalan eneo la Mgwashi kule Bumbuli ambalo lilitengewa shilingi milioni 460 ni mfano halisi lakini zikatumika kwenye kuondoa tatizo la ukame mwaka 1999, Wizara inasema nini? Nadhani tutapata jibu katika hilo. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, mojawapo ya sababu za wateja kukatiwa umeme ni umbali mrefu toka zilipo Ofisi za malipo Wilaya na Mikoa hadi vijijini maeneo yaliyounganishiwa umeme. Kwa mantiki hiyo, Kamati inashauri Wizara na *TANESCO* kuweka vituo na tarehe maalum za wananchi ili waweze kulipia ankara zao bila kufanya safari ndefu ambazo inabidi walipe nauli. Aidha, mita za wateja zifanyiwe uchunguzi wa mara kwa mara ili kuhakikisha usahihi na kuondoa kero kwa wananchi ya kulipia fedha nyingi zisizolingana na matumizi yao halisi.

Mheshimiwa Spika, tatizo la kuchelewesha uunganishaji wa umeme kwa wananchi hususani pale ambapo mteja ameshalipa ada ya kuunganisha umeme na malipo mengine kwa mujibu wa mkataba ni kero. Kamati inashauri kwamba Wizara iiagize *TANESCO i*weke utaratibu mzuri wa kupunguza kwa kiasi kikubwa ucheleweshaji huo.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipokea taarifa kuwa Chuo cha Umeme cha *TANESCO,* Kidatu hivi sasa hakitekelezi majukumu yake kama ilivyokusudiwa. Hivyo Kamati inazidi kuishauri Wizara kukifanya Chuo hicho kiwe Shule ya Sekondari ili majengo hayo yaweze kutumia kwa faida ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na Wizara kuchukua hatua kadhaa ili kudhibiti vurugu kwenye maeneo ya machimbo ya madini siku za hivi karibuni tatizo hilo bado linaendelea kujitokeza kwenye migodi kadhaa hasa Mererani. Kwa kuwa athari za migogoro hiyo ni kubwa na hukumba watu wengi kwa wakati mmoja, Kamati inashauri Wizara iweke utaratibu endelevu wa kisera wa kutatua tatizo hilo. Aidha, sambamba na hilo Serikali ibuni utaratibu wa kuwasaidia zaidi kiteknolojia na kuwalinda wachimbaji wadogo dhidi ya unyonyaji wa wachimbaji wengine ambao ni wakubwa na kutumia nguvu za hawa kujitajirisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Wizara ya Nishati na Madini kwa kuunda Kamati ya Ukimwi Wizarani ijulikanayo kama *Technical AIDS Committee* kwa kushirikiana na Wizara ya Afya ili kutoa elimu kwa watumishi wa Wizara, wachimbaji madini, wananchi waishio karibu na migodi. Hata hivyo, Kamati inazidi kuishauri Wizara kwa kushirikiana na wadau wengine kwamba itekeleze dhamira yake kwa vitendo ya kuanzisha vituo vya hiari vya kupima na kutoa ushauri nasaha kwenye maeneo ya madini.

Mheshimiwa Spika, Tanzania imejaliwa kuwa na rasilimali za madini ya aina mbalimbali lakini matumizi yake hayaonekani kuibua uchumi. Pamoja na ukweli huo, sekta ya madini huchangia kwa asilimia 2.5 tu kwenye Pato la Taifa. Mchango huu ni mdogo sana. Hivyo Kamati inashauri Serikali kupitia Benki Kuu kusimamia kwa karibu zaidi fedha zinazotokana na mauzo ya madini hasa kwa kutumia Sheria ya Fedha za Nje. Nashukuru Mheshimiwa Waziri ameligusia hili katika hotuba yake.

Aidha, Makampuni ya Madini yahamasishwe kujiunga na soko la hisa la Dar es Salaam ili wananchi waweze kununua hisa na hivyo kunufaika na rasilimali hiyo ya madini.

Mheshimiwa Spika, Kamati pia inashauri Serikali ipitie upya mikataba ya madini na kuona kama kuna maeneo ambayo yana utata basi yarekebishwe moja likiwa suala la mrabaha *(royalty). A*idha, utaratibu wa kuwa na Hisa ya Heshima *(Golden Share)* kwenye makampuni ya madini ni jambo zuri ili Serikali iweze kufuatilia mabadiliko ya kisera katika eneo hilo. Hisa hii kwa kawaida haichangiwi na inaweza kuwekewa muda labda kipindi cha miaka mitano wakati Mwekezaji anaanza shughuli zake ili kulinda yale ambayo tunadhani ni muhimu yafanyike kwa mfano kwenye suala la ajira, je, wanatekeleza mikataba ya ajira ipasavyo? Kama hakuna mtu katika bodi kwa kweli na sisi tutakuwa tunanung'unika tu wakati wananchi wanataka tuwape majibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, utafutaji na ufuatiliaji wa mafuta ambao ulianza mwaka 1950 umebaini kuwepo kwa dalili za mafuta nchini. Hata hivyo kasi ya utafutaji rasilimali hiyo imekuwa ndogo kwani toka mwaka 1950 ni visima 25 tu ndivyo vilivyochimbwa wakati nchi nyingine kwa mfano Norway walichimba mpaka visima 100 ndio wakafanikiwa kupata mafuta.

Kwa hiyo, visima hivi vichache haviwezi kutupa uhakika wa mafuta. Kamati yangu inashauri Wizara kwamba ishirikiane na makampuni yenye leseni za utafutaji mafuta ili kuzidisha kasi ya utafuta wa raslimali hii ambayo ni muhimu kwa uchumi wa Taifa.

Mheshimiwa Spika, sambamba na juhudi hizo, Kamati pia inatoa ushauri kwa Serikali kuunadi kwa wawekezaji mradi wa bomba la mafuta kutoka Dar es Salaam kwenda Mwanza kwani umuhimu wa mradi huu kiuchumi bado uko pale pale. *(Makofi)*

Aidha, Serikali ipitie upya Sheria ya Shirika la Mafuta ili iende sambamba na mabadiliko kwenye sekta hiyo. Vile vile Kampuni Tanzu ya *TPDC, COPEC* inayouza mafuta iendelezwe ili iwe ni taasisi mojawapo ya kuisaidia Serikali kuona jinsi biashara ya mafuta inavyokwenda na uwekaji wa bei na ulipaji wa kodi.

Mheshimiwa Spika, suala la kukatiwa umeme Zanzibar lilikuja wakati Kamati yangu imeshaandika taarifa yake. Kwa hiyo, naomba Wajumbe wa Kamati yangu wakubali nitoe ushauri kwa Serikali kwamba Serikali itoe maelezo ya kutosha ili Waheshimiwa Wabunge nao waelewe ni nini kimetokea.

Mheshimiwa Spika, pia nawashauri Waheshimiwa Wabunge wasianze kulaumu mpaka tupate taarifa hiyo kuhusu ni nini kimetokea ili kwa kweli tuwe watoaji wa maoni ambayo kwa kweli yanaongoza vizuri nchi kuliko kutoa maoni ambayo yanazidi kuleta utata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuchukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Daniel Yona, Waziri wa Nishati na Madini pamoja na Mheshimiwa Dr. Ibrahim Msabaha, Naibu Waziri wa Nishati na Madini kwa ushirikiano waliotoa kwa Kamati yangu wakati wa kuchambua Bajeti ya Wizara hii. Aidha, nawashukuru watendaji wa Wizara hii wakiongozwa na Katibu Mkuu, Ndugu Patrick Lutabanzibwa kwa kazi nzuri ya maandalizi ya mpango wa bajeti ya Wizara hii ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee, napenda kuwashukuru wajumbe wa Kamati yangu ya Uwekezaji na Biashara kwa utulivu, uadilifu na ushirikiano waliouonyesha wakati wa kutekeleza jukumu hili zito. Pia napenda kumshukuru sana Katibu wa Bunge, Ndugu Kipenka Mussa na Katibu wa Kamati hii, Ndugu Daniel Eliufoo, kwa kuihudumia Kamati yetu ipasavyo na kuweza kufikia hapa tulipofika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya uchambuzi uliofanyika na ushauri uliotolewa na Kamati, Kamati kwa jumla imekubaliana na mpango na makadirio ya Bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini kwa mwaka 2003/2004 na kuyapitisha bila mabadiliko.

*M*heshimiwa Spika, ila kuna masahihisho ambayo itabidi yaangaliwe katika Kifungu cha 58 kwenye Kitabu cha Pili, *Supply Vote, page 212, figure* inayoonekana kwenye kitabu kile ni shilingi 25,365,980,000/=. Lakini kwenye kitabu cha Mheshimiwa Waziri inaonekana shilingi 25,365,978,500/=.

Mheshimiwa Spika, kwenye kitabu cha Maendeleo wanaomba shilingi 102,091,552,300/= hii inatokana na masahihisho ambayo tumeyapata kutoka Hazina. Kwa hiyo, hii haina utata nakubaliana nayo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Uwekezaji na Biashara na kwa niaba ya Kamati yangu naunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sikuwekewa *glass* ya maji hapa. *(Kicheko)*

**SPIKA:** Ndiyo, kuna Waheshimiwa Wabunge, wamesimama kukuunga mkono lakini kuwasilisha taarifa hakuhitaji kuungwa mkono hii sio hoja. *(Kicheko)*

**MHE. ISAAC M. CHEYO - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii, kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii kutoa kwa niaba ya Kambi ya Upinzani maoni kuhusu Bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini kwa mwaka wa fedha 2003/2004 kwa mujibu wa kifungu cha 43(5b) na (c) cha Kanuni za Bunge Toleo la 2003.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani ingependa kuchangia katika Bajeti hii ya Wizara ya Nishati na Madini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nishati ni nyenzo muhimu katika kuleta maendeleo ya uchumi wa Taifa. Mchango wa matumizi ya nishati unaonyesha kuwa nishati mkaa inachangia asilimia 90 ya nishati yote, bidhaa za mafuta huchangia asilimia tisa na makaa ya mawe asilimia moja.

Mheshimiwa Spika, katika sekta ya nishati, Wizara imependekeza mambo yafuatayo ambayo yatasaidia maendeleo ya sekta hiyo nasi tunakubalina nayo kama ifuatavyo:-

Kuanzisha dira ya nishati ambayo sekta zote za uchumi zitapata nishati ya kutosha, yenye uhakika na yenye gharama nafuu bila kuharibu mazingira, kujiwekea malengo ya kuwezesha upatikanaji wa nishati mbadala Mijini na Vijijini, kwa bei nafuu, kwa kuhamasisha wawekezaji binafsi katika sekta hii, kuweka lengo la kukarabati mitambo ya kuzalisha, kusafirisha na kusambaza umeme Vijijini na Mijini, kujiwekea lengo la kuendeleza na kuhamasisha vyanzo vingine vya nishati, kuwa tayari kuendelea kurekebisha

miundombinu ya sekta ya Nishati na Shirika la Umeme *TANESCO* kuweza kufanikisha utoaji wa bili za umeme kwa kila mwezi, tofauti na hapo nyuma ambapo bili za umeme zilikuwa zinapatikana baada ya miezi miwili, mitatu au zaidi.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaitaka Wizara ya Nishati na Madini kutoa maelezo juu ya matatizo yafuatayo ambayo yanahusiana na sekta ya nishati. Shirika la Umeme Tanzania *(TANESCO)* lina deni kubwa linalowadai wateja wake kati ya deni hilo kubwa asilimia zaidi ya 50% ni deni linalodaiwa Shirika la Umeme Zanzibar, kiasi cha shilingi bilioni 32. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, huko nyuma Wizara hii ilitoa kauli kwamba Serikali ya Muungano wakishirikiana na Serikali ya Mapinduzi wana mpango wa kufuta kabisa deni hilo ambalo mwaka 1999 lilikuwa karibu shilingi bilioni 12. Cha kushangaza deni hili limelimbikizwa hadi kufikia karibu shilingi bilioni 32. Ni kweli Wizara na Idara za Serikali na Shirika la Umeme Zanzibar wanalipa anakara zao za umeme kwa sasa. Kambi ya Upinzani inaona lingekuwa jambo la busara kwa Shirika la Umeme Zanzibar kulipa deni lake hilo. Nguvu ya *TANESCO* kujenga uwezo wa kusambaza umeme inategemea sana uwepo wa fedha na ukusanyaji wa madeni.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Umeme Zanzibar wanakusanya bills kutoka kwa wananchi lakini inafanana kabisa na Halmashauri zetu zinapokata makato ya lazima lakini hayarejeshwi kule na hawa wanakusanya bills za umeme na gharama zake lakini hawalipi. Sasa na wenyewe walipe.

Mheshimiwa Spika, hatutaki Shirika hilo *(TANESCO)* litumie nguvu kudai deni hilo kwa shirika la Umeme Zanzibar. Kama shirika hilo halina uwezo wa kifedha kulipa deni, kwa nini zisitumike njia za Kiserikali kujadiliana namna ya Serikali ya Zanzibar inavyoweza kulisaidia shirika lake kulipa deni, hilo au tunataka *Net Group Solution* watumie nguvu zao za ugeni kuikatia umeme Unguja kama walivyofanya Jumatatu tarehe 21 Julai, 2003 au walivyofanya mwaka jana kwa Wizara na Idara za Serikali, jambo la kiungwana ni kutafuta muafaka wa kulipa deni hilo, bila nguvu ya ziada kutumika. Fedha hiyo *TANESCO* wanahitaji ili kuendeleza miradi ya umeme kwenye Mikoa inayoonekana *disadvantaged* kama vile Mikoa ya Lindi, Mtwara, Ruvuma na hata Pemba ambako umeme kwao ni ndoto.

Mheshimiwa Spika, tunaamini Shirika la *TANESCO* lingelipwa fedha hizo lingeweza kuzitumia kwa kujenga njia za umeme kwenye Miji ya Mtwara na Lindi, ili waondokane na umeme walionao kwa sasa ambao kupatikana kwake ni kwa mashaka. Tunaamini, *TANESCO* kwa kutumia shilingi bilioni 26 wangeweza kuunganisha Mji wa Songea na umeme wa gridi kutokea Makambako kupitia Njombe.

Kambi ya Upinzani ingependa kufahamu hatua zilizofikiwa na Wizara hii katika uendelezaji wa nishati mbadala kama vile micro hydro, nguvu upepo, *bio gas,* mionzi ya jua na makaa ya mawe, kwani upatikanaji wa umeme kwa watu ni tatizo kutokana na bei kuwa kubwa na gharama za kuingiza kwenye makazi au viwanda vidogo vidogo ni kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inataka ufafanuzi wa Serikali, ni jinsi gani *Net Group Solution* inaonyesha umahiri wake katika shughuli za umeme, kwani tangu waingie mwaka jana, mwezi Mei, matatizo ya ukatikaji wa umeme bado yako pale pale, tena kwa kiasi fulani yameongezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wananchi wengi walitegemea kuwa kuingia kazini kwa *Net Group Solution* kungeleta nafuu kubwa kwa wananchi, hasa katika suala la kima cha umeme kulipa kwa unit moja inayotumika. Vile vile gharama za uingizaji umeme kwenye majumba ya kuishi au kwenye viwanda, ingekuwa ndogo na uingizaji wa umeme kuchukua muda mfupi zaidi, lakini mambo hayajawa mazuri mpaka sasa.

Mheshimiwa Spika, hiyo inakwenda kinyume kabisa na zile sifa walizomwagiwa ndani ya Bunge hili, *Net Group Solution* kabla ya kuanza kazi *TANESCO,* Wizara husika ifanye uchunguzi wa kina, kufuatilia kwa karibu sana kwa nini *Net Group Solution,* wameshindwa kuonyesha mambo ambayo wananchi walitegemea kupata katika huduma zitolewazo na Shirika la *TANESCO* kabla ya wao kufika.

Mheshimiwa Spika, Serikali inapata hasara kubwa sana kutokana na Mkataba uliowekwa kati ya *TANESCO* na *IPTL* kwani *TANESCO* wanailipa *IPTL* zaidi ya bilioni 2.5 ambazo zimesemwa sasa hivi kwa mwezi bila sababu ya msingi. Je, wale watumishi na viongozi waliohusika na utiaji sahihi katika Mkataba huu, tulishaambiwa Wabunge watatu na wengine, Serikali imewachukulia hatua gani? Ili hapo baadaye suala kama hilo lisijitokeze tena kwa Taasisi au Asasi yeyote ya Serikali hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani ingependa kuikumbushia Wizara kuwa, siku za nyuma Wizara ilitoa maelezo au matamko kuwa kunafanyika utaratibu wa kupeleka mafuta Mwanza kwa kutumia bomba kama ilivyo kwa bomba la *TAZAMA,* ambalo linapeleka mafuta Zambia, je suala hilo limefikia wapi na vikwazo gani vimejitokeza hata kusababisha utekelezaji wa mradi huo kuwa mgumu?

Mheshimiwa Spika, katika Bajeti ya mwaka 2002/2003, Waziri aliahidi kuwa Wizara imeandaa programu ya kuendeleza Nishati Vijijini, programu ambayo gharama yake ilitegemewa kufikia shilingi bilioni tatu. Je, Wizara ina maelezo yoyote ya utekelezaji wa programm hiyo na mafanikio yapi yameanza kupatikana kutokana na utekelezaji wa program hiyo? Kwani kila siku tunasikia wananchi Vijijini wanalalamikia shida ya kupatiwa umeme ili waende sambamba na mabadiliko ya teknolojia ulimwenguni.

Mheshimiwa Spika, Mikoa ya Mtwara, Lindi na Ruvuma iko kwenye programu ya maendeleo ya Taifa iitwayo *The Mtwara Corridor,* utekelezaji wa programu hiyo utafanikiwa ikiwa masuala muhimu, kama vile umeme yatakuwa hayana matatizo ya kupatikana, lakini hali halisi ya umeme katika Mikoa hiyo bado ni kitendawili, kwani umeme unaopatikana hivi sasa katika Mikoa hiyo ni wakutumia jenereta ambao gharama zake ni kubwa na hauwezi kusambazwa kirahisi.

Je, Serikali kupitia Wizara hii ina mpango gani juu ya upatikanaji wa umeme wenye uhakika katika Mikoa hiyo ili utekelezaji wa *Mtwara Corridor* ufanyike kwa urahisi, ufanisi na haraka. Sisi katika Kambi ya Upinzani kwa kufahamu umuhimu wa *Mtwara Corridor,* tulitegemea kipaumbele kiwe kuweka umeme wa uhakika kwa Mikoa hiyo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2002/2003, Wizara iliahidi kuendeleza upatikanaji wa umeme kwa kutumia mpango wa maendeleo wa mradi wa umeme wa Mchuchuma, je, suala hilo utekelezaji wake umefikia wapi?

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inapata wasiwasi na mwenendo wa nchi katika sekta hii hasa katika upande wa umeme, kwani nchi imejaribu kuongeza kujenga vyanzo vingi vya umeme unaotokana na nguvu za maporomoko ya maji kama vile kule Pangani, Kidatu, Kihansi, Mtera na kadhalika. Lakini cha kusikitisha ni kuona wananchi walio wengi ambao wanaishi jirani au mbali na sehemu hizo hawajapata umeme kwa ajili ya majumbani mwao au uanzishaji wa viwanda vidogo vidogo. Vile vile viwango vya umeme unaotozwa nchini ni vikubwa mno, kuliko nchi yoyote ya Afrika iliyoko Kusini mwa Jangwa la Sahara.

Mheshimiwa Spika, kutokana na upatikanaji finyu wa umeme kwa wananchi, husababisha maendeleo ya nchi na viwanda vidogo vidogo yakwame na hivyo uharibifu wa mazingira kuongezeka kwani wananchi wengi hutumia nishati mkaa kwa shughuli zao mbalimbali. Je, Wizara ina mpango gani wa kurekebisha hali hiyo ambayo inadumaza maendeleo ya nchi na viwanda vidogo vidogo?

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani, ingependa kuishauri Wizara katika sekta hiyo kwa kuzingatia na kutekeleza mambo yafuatayo ambayo yanaweza kuleta mafanikio mazuri siku za usoni katika sekta ya Nishati, Wizara iweke mikakati ya kudumu kuhusu tatizo la upungufu wa maji litokealo kila mwaka katika mabwawa ya Mtera, Kidatu na Nyumba ya Mungu, ukataji wa umeme unaofanywa na *TANESCO* bila kutoa taarifa rasmi na mapema kwa wateja husababisha hasara kubwa kwa wateja kwani mali zao huharibiwa na umeme ukatwao ghafla pasipo taarifa, *TANESCO* ijaribu kupunguza gharama ya kuingiza umeme kwa wateja, vile vile uingizaji umeme kwa wateja uchukue muda mfupi zaidi ili kuwawezesha watu wengi wapate umeme kwa muda mfupi na yatokeapo matatizo ya kiufundi katika njia za umeme, mara wapatapo taarifa hizo wazishughulikie haraka, kwani kutofanya marekebisho mapema na kwa haraka inaleta usumbufu kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, kwa sehemu zile ambazo nguzo kuu za usambazaji umeme zimepita, ni vyema kampuni ya *TANESCO* kutoa motisha fulani kwa Vijiji kwa kuwafanyia mambo muhimu kama vile ujenzi wa Zahanati, Shule, Barabara, maji safi na salama na kadhalika. Kwa kufanya hivyo wananchi hao watakuwa macho kukabiliana na watu ambao wanataka kuziharibu nguzo au kuiba nyaya za umeme na mafuta ya *transformer* katika sehemu hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilikuwa nafikiri kwamba umeme unapopita juu tu angani wananchi wanapata hasira. Kwa hiyo ni afadhali pia kama kuna njia za namna hiyo wanaweza kusaidia katika ulinzi.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wizara yake itenge fedha za kutosha kila mwaka ili zisaidie gharama za usambazaji umeme Vijijini na Mijini. Kwa kufanya hivyo italeta kichocheo kikubwa katika maendeleo ya nchi, hatimaye kuwezesha upunguzaji mkubwa wa tatizo la umaskini ambalo ndiyo tatizo kubwa linaloikabili nchi.

Mheshimiwa Spika, katika sekta ya Madini Kambi ya Upinzani ina haya ya kuchangia.

Serikali kutokuiruhusu *Tanzanite* isiyokatwa kitaalam kuuzwa kwenye masoko ya nje. Hili linahitaji utekelezaji wamakini, kuna maswali mengi ya kujiuliza je, tuna viwanda vya kukata *Tanzanite in piece* kwa sasa. Je, waliokuwa na Mikataba ya kuuza nje *Tanzanite* tuwafanyeje? Haya ni maswali yanayohitaji kujibiwa kabla hatujasitisha uuzaji wa *Tanzanite* nje.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaitaka Wizara itoe maelezo kwa matatizo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba Mikoa inayotoa dhahabu, kuna makampuni ya uchimbaji yanayotoa huduma mbali mbali kwa Vijiji vinavyozunguka machimbo hayo, bado mchango huo unawanufaisha watu wanaokaa karibu na machimbo hayo tu. Jambo hili, linawafanya wananchi ambao wako mbali na machimbo kujiona hawapati huduma sawa na wenzao na hatimaye kuhamia kwenye maeneo ambayo kuna machimbo ili na wao wanufaike na huduma hizo.

Hali hii italeta nguvu kazi kupungua katika maeneo yale ambayo hayana Madini. Hivyo basi lingekuwa ni jambo la msingi kama makapuni hayo yangetumia sehemu ya fedha hiyo kwa kuzipatia Halmashauri za Wilaya ili ziweze kupanga miradi ya maendeleo inayonufaisha wananchi wa Wilaya nzima badala ya kuwanufaisha wale tu wanaozunguka migodi peke yao.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi kumeanza kujitokeza hali ya Makampuni mengi ya madini kuuzwa, baada ya kuanza kuchimba. Makampuni hayo, huuzwa kwenye *Stock Exchange* huko Sydney, Toronto, Turbak na sehemu zingine na hivyo kubadili mmiliki. Kufuatana na kuzwa migodi muuzaji anapata faida, tulitegemea kwamba Serikali ingemtoza kodi kwa njia ya *capital gain.* Suala hili hatuna uhakika kama Serikali imepata chochote kutokana na mauzo hayo.

Mheshimiwa Spika, tunataka Serikali itupatie maelezo nchi imefaidika nini na uuzwaji huo wa makampuni ya Migodi *(Kahama Gold Mine,* kutoka Satorn ikaenda Barek, Ashati imekwenda kwa watu wengine, Samax ikaenda *Resolute* na *East Africa of Recent* na yenyewe imeuzwa, sisi tumepata nini).

Mheshimiwa Spika, katika Bajeti ya Wizara, ya mwaka 2002/2003 imeelezwa kuwa wachimbaji wadogo wadogo watapatiwa mafunzo ya uchimbaji katika Chuo kihusucho uchimbaji kilichoko Matendasi Wilayani Chunya. Kambi ya Upinzani inaona chuo kimoja hakitoshelezi mahitaji ya mafunzo kwa wachimbaji madini wadogo wadogo kwani madini yapo sehemu mbali mbali nchini. Je, Wizara haioni hii haitaleta muafaka kwa wale wachimbaji wadogo wadogo walioko mbali sana na Wilaya ya Chunya kama vile wachimbaji walioko Wilaya ya Tarime, Nyamonko na wengine walio mbali.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani ingependa kutoa ushauri ufuatao kwa Wizara ya Nishati na Madini kuwa Chuo cha Madini kipanuliwe ili kitoe mafunzo kwa wanafunzi wengi zaidi, pia mitaala yake iangaliwe na iwekwe ile inayokidhi hali ya sasa ya soko.

Pia Wizara ihakikishe vurugu kati ya wachimbaji madini wakubwa na wadogo wadogo haitokei, ishirikiane na Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Wizara ya Ushirika na Masoko ili viundwe Vyama vya Ushirika vya Wachimbaji Wadogo Wadogo, iwasiliane na Wizara za Ushirika na Masoko na Viwanda na Biashara kutafuta masoko yenye uhakika kwa wachimbaji madini wadogo wadogo, iunde chombo maalum ambacho kitasimamia shughuli za wachimbaji madini wadogo wadogo na ianzishe Mfuko maalum ambao utatumika kutoa mikopo kwa wachimbaji wadogo wadogo.

Mheshimiwa Spika, pia Wizara isimamie au kukomesha ubaguzi wa ajira ufanywao na baadhi ya makampuni ya Madini na Nishati. Hili hata mwaka jana tulilizungumza, ihakikishe kuwa makampuni makubwa ya nje yanasimamiwa kwa karibu juu ya uzalishaji na uchimbaji wa madini hapa nchini kwetu, Serikali itoe tafiti zote za aina za madini yapatikanayo hapa nchini kwa wananchi na Serikali ipunguze urasimu kwa wananchi kupata viwanja na hati za kumiliki sehemu za machimbo ya madini ya madini.

Mheshimiwa Spika, katika kutazama mwenendo wa bajeti ya maendeleo ya Wizara hiyo kuanzia mwaka 2001/2002, fedha zilizopangwa kwa shughuli za maendeleo zinaonyesha kupungua zaidi. Kwa mfano, katika bajeti ya mwaka 2002/2003, fedha zilizoombwa na Wizara ni shilingi bilioni 132,782/= wakati katika bajeti ya mwaka huu 2003/2004, fedha iliyoombwa na Wizara kwa ajili ya shughuli za maendeleo ni shilingi bilioni 102,092/=. Hivyo kufanya fedha za maendeleo kupungua kwa shilingi bilioni 30.670/= ambazo ni sawa na asilimia 22.8. Je, hali hii ikiachiwa hivyo Wizara itaweza kutekeleza dira na malengo iliyojiwekea?

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali katika bajeti ijayo (2004/2005) fedha za maendeleo kwa Wizara hii ziongezwe zaidi.

Mheshimiwa Spika, *TPDC* ni shirika la Serikali lenye jukumu la kufanya utafiti wa mafuta na lina sura ya Muungano. Jukumu lake la utafiti wa mafuta ni katika mipaka yote ya nchi pamoja na Visiwa vyote vya Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, tunategemea bila kujali umipaka wa Zanzibar *TPDC* inajukumu la kufanya *Exploration and Drilling* kwa maeneo inayoona kuwa kuna dalili za kufanya tafiti hizo. *TPDC* kwa programu zake imeshatoa kibali cha kufanya utafiti kwa mashirika ya nje kama *Shell, Brass, Antrim* na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, Mashirika haya yamekwama kufanya shughuli zake kwenye ufukwe wa Pwani ya Bara na hasa Zanzibar kwa sababu zifuatazo:-

Kwa kusubiri kuletwa Bungeni Muswada wa *Oil exploration* kwa ajili ya marekebisho ili kutoa fursa kwa mashirika hayo kutafiti na kuchimba katika maeneo yaliyotengwa *(Defined Blocks).*

Mheshimiwa Spika, kwa hili, Kambi ya Upinzani inaona sasa ni wakati muafaka kwa Mswada huo kuletwa Bungeni ili sheria hiyo irekebishwe. Kuchelewa kufanya hivyo kutawafanya watafiti hao kuhamia kwingine hasa ikizingatiwa kuwa shughuli za utafiti kama huo pia unaweza ukafanyika Pwani za Kenya kuanzia Lamu hadi Mombasa mpakani na Tanga. (Ukisoma gazeti la juzi la Mtanzania la tarehe 22 Julai, 2003, utaona kichwa cha habari Kenya wahaha na utajiri wa mafuta.)

Mheshimiwa Spika, tunaelewa mashaka yaliyopo kwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kuiruhusu *TPDC* na mashirika inayoyapa kufanya utafiti, kuwa Zanzibar haitafaidika na utafiti na uchimbaji wa mafuta katika maeneo yake. Tungependa kuitoa wasiwasi Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, kwamba shughuli za mafuta ni za Muungano, kwa hiyo hakuna sababu za kufikiria kuwa faida zitakazopatikana zitawanufaisha Wabara na makampuni ya kigeni. Raslimali za nchi kama dhahabu almasi na mafuta, *proceeds* zake ni kwa faida ya nchi na siyo kipande cha nchi. Tunaitaka Wizara na Serikali kwa ujumla kufanya hima na ushawishi wa kutosha kwa Serikali ya Zanzibar ikubali Kampuni ya *Antrim* kutoka Canada kufanya utafiti na uchimbaji wa awali katika Pwani ya Bahari ya Tanzania Zanzibar. Kama tulivyosema hapo awali kuchelewa kutoa maamuzi kuna hasara kubwa kuliko faida ya hofu ya kupoteza raslimali za Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, tukianza kuwa na mawazo kama hayo, raslimali za nchi zitatutelea mgawanyiko. Mwanza, Shinyanga na Mara watasema dhahabu na almasi yao zisichimbwe, Ukerewe na Furu zao watasema zisivuliwe na Kilwa na Songas yao nao watasema isivunwe, mpaka wao wapate uhakika wa mgao.

Mheshimiwa Spika, hali hii ni hatari kwa amani na utulivu tunaojivunia.

Mheshimiwa Spika, kwa kuhitimisha tu niseme Makampuni yote ambayo yanafanya kazi ya uchimbaji pamoja na Wizara hii pia waangalie suala la Ukimwi. Elimu ya Ukimwi itolewe kwa maeneo ya machimbo na makampuni yagharamie elimu hiyo.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. Ahsante sana na Waheshimiwa Wabunge ahsanteni sana kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

**MHE. DR. LUCY S. NKYA:** Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru sana kwa kunipa fursa hii ya kuchangia katika mjadala huu. Awali ya yote ningependa kuwapongeza Waziri na Naibu Waziri wa Nishati na Madini pamoja na watendaji wao wote kwa kuandaa hotuba hii ya Bajeti ambayo imefafanua zaidi shughuli za Wizara yake na nafikiri kwamba wananchi walipoisikiliza leo kuna mambo mengine ambayo yalikuwa yanaleta utata watakuwa wameyaelewa na kutafakari kwa mwelekeo ambao ni tofauti kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, zaidi ningependa kumpongeza Rais Benjamin William Mkapa, pamoja na Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa sera zake nzuri ambazo zimeweka mazingira mazuri ya kuwavutia wawekezaji hususan katika sekta ya nishati na madini.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Nishati na Madini ni nyeti sana katika kuchochea na kuwezesha mikakati ya kuondoa umaskini pamoja na kuongeza Pato la Taifa. Hii ni Wizara ambayo majukumu yake ni magumu sana katika kudhibiti na kufuatilia shughuli za uchimbaji wa madini kwani asilimia kubwa ya wawekezaji wa madini katika nchi hii ni wageni. Hao wageni wengine ni waadilifu na wengine siyo watu wazuri. Hii ni hulka ya binadamu. Kwa mantiki hiyo basi ni dhahiri kwamba Wizara hii inahitaji sana ushirikiano wa karibu kutoka kwa Wizara nyingine, mashirika ya ukusanyaji wa kodi kwa mfano *TRA* na viongozi hususan Waheshimiwa Wabunge pamoja na wananchi ili kuweza kufuatilia nyendo za hawa watu ambao wamewekeza katika nchi yetu tuhakikishe kwamba wanafanya kazi yao ya kuchimba na biashara ya madini kama ilivyoainishwa katika Mikataba na kama walivyokubali kwamba watafuata maadili ya uchimbaji katika nchi hii.

Mheshimiwa Spika, Watanzania walio wengi wanajiuliza kwamba hivi haya madini ni yetu yaani ni raslimali yetu. Kwa hiyo, hiyo ingetosha kabisa kuwa ni mchango wetu katika *Mining Industry,* hivyo basi wanapokuja wawekezaji wanajiuliza sisi kwa nini hatuna hisa katika haya makampuni makubwa makubwa kama haya ya madini wakati haya madini ni yetu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi ningependa kushauri kwamba Wizara inayohusika pamoja na Serikali iangalie namna ambavyo sasa, kama tumeshafanya makosa kwa hawa ambao wapo na sasa hivi wanachimba, basi wanaokuja tunapoingia Mikataba nao tuwaambie kwamba haya madini ni yetu.

Kwa hiyo, huo ndiyo mchango wetu, tunakubaliana kwa kiwango kinachokubalika kabisa kwamba sisi tunakuwa na asilimia fulani ya hisa katika haya makampuni. Zaidi ya hapo kama itashindikana kwamba Serikali itakuwa na hisa basi hawa wawekezaji wakubwa wakubwa kwa sababu sisi tumeshindwa kuwekeza kwa sababu hatuna mtaji na nyenzo waanze sasa ku-*float* hisa zao katika Kampuni ya Hisa ya Dar es Salaam ili Watanzania wenye uwezo waweze kununua hisa na sisi tujisikie kwamba haya madini ambayo ni urithi wetu basi tunafaidi kwa njia moja au nyingine.

Mheshimiwa Spika, mimi naomba Wizara na Serikali iangalie namna ya kuwashauri hawa wawekezaji wakubwa na wao sasa waanze kutuuzia hisa kupitia Kampuni ya Hisa ya Dar es Salaam kama wanavyofanya wawekezaji katika sekta nyingine. Mbona *TBL* inatuuzia hisa, mbona *TTC* inauza hisa, wao wanashindwa namna gani wakati wanazalisha na wanapata fedha? Tunaomba hilo liangaliwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ningependa kulizungumzia ni kuwauliza hawa wawekezaji kwamba unapokaa na unapopatia chakula chako basi ndiko nyumbani kwako na wale ambao wamekukaribisha basi hao ni ndugu zako.

Sasa wao wasiangalie tu kwamba wanatulipa *royalty, royalty* ni haki yetu kwa sababu madini ni yetu, lakini kuwepo hapa wao wanaonyeshaje kiwango cha kuwepo na uzalendo wa ugenini katika kuwasaidia Watanzania kutokana na hii faida kubwa wanayopata kutokana na madini yetu. Mimi naomba kuuliza kwamba wataalam wanasema kuna kitu kinachoitwa *a spill over effect* na hiyo *spill over effect* tunaweza sisi Watanzania tukaifaidi kwa njia kuu tatu.

Mheshimiwa Spika, njia ya kwanza, ni hao wawekezaji wakubwa kupanga mikakati ambayo inaeleweka ya kuwasaidia wachimbaji wadogo wadogo.

Kwanza waweze kuwa na *skills* au *technology* ya kuweza wao kujiendeleza kuchimba madini kwa njia ya usalama, kuchekecha yale madini kwa njia ya usalama zaidi na kuongeza uzalishaji pamoja na kuwasaidia katika kutafuta masoko. Kwa sababu hawa wachimbaji wadogo wadogo pamoja na kwamba wanachimba inafikia mahali ni kwamba kile wanachokipata kinaishia kwenye *black market* kwa sababu hawajui watatafutaje masoko.

Sasa kinapoishia kwenye *black market* ni kwamba hata yeye hapati faida yoyote kubwa na sisi kama Serikali pia hatupati chochote kutokana na hawa wachimbaji wadogo. Mimi nasema kwamba *it is only proper with moral responsibility,* hawa wachimbaji wakubwa wakubwa wakijua kabisa kwamba huu ni urithi wetu tuliopewa na Mungu basi wawasaidie Watanzania kuinua kiwango chao cha kufanya shughuli katika *Mining Industry. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili, ambalo ningependa pia waliangalie na waige mfano wa *TBL, Cocacola Company* na *Baclays Bank*, pamoja na kwamba wanalipa kodi na wanafanya shughuli nyingine. Lakini wameona kwamba wanawajibika kuinua kiwango cha taaluma ya elimu. Wanatoa zawadi *special* kwa ajili ya wanafunzi wa shule wanaofanya vizuri katika masomo yao ya sekondari katika *O-level* na *A-level*. Sasa hawa wenzetu sijawahi kuwasikia kwamba wamekuwa na mpango huo wanaangalie kwamba watusaidiaje kuinua kiwango cha taaluma ya Elimu hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, zaidi ya hapo Watanzania wanaoishi katika maeneo hayo ambapo makampuni makubwa yanachimba dhahabu, *diamond* na vito vingine wamekuwa ni maskini sana na umaskini huo unajidhihirisha katika njia nyingi. Pamoja na kwamba tunasema watoto wasome, mtoto anachaguliwa kujiunga na elimu ya sekondari katika shule ya Sekondari ya Serikali, Mtanzania huyo maskini ambaye Mungu amehakikisha kwamba amezaliwa penye utajiri anashindwa kumsomesha mtoto wake elimu ya sekondari, na huku tunasema kwamba tuna utajiri wa madini pale.

Naomba waangalie kama wanaweza wakatengeneza kitu ambacho tukasema kwamba ni *special scholarship fund* kwenye haya maeneo ili watoto ambao wanatakiwa kujiunga katika elimu ya sekondari na Elimu ya Juu, basi hayo makampuni yachangie kuwapa *sponsorship* wasome. Nafikiri hiyo itaonyesha kwamba na wao wamekuja, lakini wanatutakia mema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ni kwamba tunaangalia katika maeneo yale wao kuwepo pale kunawavutia Watanzania wengi kwenda kufanya shughuli mbalimbali katika hayo maeneo, pamoja na kwamba kuna wale ambao wameajiriwa kama *Labourers* kwao na wale wengine wanaokwenda kwa ajili ya kutoa huduma. Kwa mfano, huduma za mama ntilie, huduma nyingine za maduka, huduma za kuuza maji na sehemu nyingine unakuta hata choo hazipo. Basi tunawauliza wana mipango gani ya kuanzisha Elimu ya Ukimwi na Elimu ya Mazingira katika haya maeneo. Katika maeneo haya wale waliokwenda kufanya shughuli pale wanakufa wanaacha watoto yatima. Sisi tunapenda kuwauliza je, wana mpango gani katika kuchangia kupunguza machungu yanayotokana na athari za Ukimwi, basi tusiseme Tanzania nzima lakini kule ambako wao wanafanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, ningependa sasa nirudi kwa Wizara. Nimeangalia kwenye Kitabu cha hotuba wanasema kwamba wameanzisha Chuo cha Mafunzo ya Uchimbaji, Uchekejaji pamoja na athari nyingine kwenye machimbo. Hiki Chuo kimeanzishwa kule Chunya. Lakini hawajatueleza kwamba wanafunzi wanaochukuliwa katika Chuo kile ni wa aina gani na ni watu gani wanachukuliwa kusoma pale na wana kiwango gani cha elimu na wanatoka wapi.

Tunaomba kuhusu hili katika majumuisho yao watueleze. Lakini ningependa pia kushauri kwamba kama inawezekana Chuo kama hiki kianzishwe kwenye Kanda zote nne za Tanzania kusudi Watanzania walio wengi na wachimbaji wadogo wadogo walio wengi waweze kupata fursa ya kupata hiyo elimu pamoja na kupata fursa ya kuweza kukopa vyombo vya kufanyia kazi. Kwa hilo nawapongeza kwa kuanzisha Chuo basi kisiishie pale Chunya kiende katika maeneo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nizungumzie sasa uharibifu wa mazingira unatokana na shuguli zote za *mining industry*. Mimi kwa uchungu kabisa naomba nizungumzie Mahenge. Mahenge walikuja watu kutoka Thailand wakaanza kuchimba rubi kule, wakamaliza kuzoazoa wakaondoka wameacha mashimo makubwa makubwa tu kule ambayo yanakuwa ni athari kubwa ya mazingira na usalama wa wananchi sijui Wizara imeshafikiria hilo.

La pili, ni uchimbaji wa dhahabu katika chanzo cha mto Ruvu eneo la Matombo. Mimi naomba nitahadharishe kwamba kama hiyo shughuli itaendelea kama ilivyo sasa hivi ni kwamba miaka 10 ijayo ule mto utaanza kuziba na sijui kama Dar es Salaam mtapata maji na Mkoa wa Pwani. Mimi naomba Wizara iliangalie hilo tena kwa makini sana. *(Makofi)*

Mheeshimiwa Spika, jambo lingine ni kuhusu uchimbaji holela. Mimi naomba niulize Wizara je, wana usemi gani au wana tamko gani kuhusu uchimbaji uliofanywa katika maeneo ya *Midu Dam.* Kwa muda wa wiki moja kulikuwa na *very distructive activity* pale kulikuwa hakuna vyoo, watu walikuwa wanajisaidia ovyo, kwa hiyo lile bwawa likawa *contaminated* kwa hali ya juu na kwa sababu hiyo imebidi Mamlaka ya Maji kuingia hasara kubwa kuongeza dawa za ku- *treat* maji.

Mheshimiwa Spika, mimi naomba hivi kwa sababu wamezungumza kwamba wanaanza kupima maeneo katika eneo la Melela na katika maeneo mengine. Sasa kabla hawajapimiwa watu maeneo au wanapopimiwa basi Wizara iangalie namna ambavyo inaweza ikatengeneza mazingira ili wale wanaokwenda pale wasije waka-*cause* tena *environmental degradation* pamoja na *contamination especially* vinyesi vya binadamu. Waangalie kwamba kunakuwepo na vyoo, kunakuwepo na chanzo cha maji na ujenzi holela wa kukata miti na kukata miti mingine kwa ajili ya nishati basi vipungue. Mimi naomba hilo liangaliwe sana.

Mheshimiwa Spika, ningependa kuzungumzia kidogo kuhusu umeme. Mimi ningependa kuiuliza Wizara kwamba ni vigezo gani vinavyotumika katika kupanga *tariffs* za umeme, je ni uzalishaji unakuwa mkubwa au nini? Ninaomba watufafanulie kwa sababu bei kubwa ya umeme inafanya watu maskini wa nchi hii wasiweze wakafaidika na huu umeme, kwa sababu huo umeme unatokana na *natural resources* ambazo tumepewa na Mwenyezi Mungu.

Mheshimiwa Spika, ningependa pia nizungumzie kuhusu wanawake katika *mining industry* na nishati. Ningependa Wizara kama inaweza ikatwambia wanawake wanashiriki namna gani katika *mining industry* na katika ku-*produce* na kuuza nishati. Napenda Wizara itupe mipango iliyo bayana kabisa kwamba watasaidiaje wanawake waweze kushiriki katika *mining industry,* kwa sababu haya madini ni urithi tuliopewa na Mwenyezi Mungu na wanawake tuna haki pia ya kuchangia mapato yanayotokana na hiyo na kushiriki katika uzalishaji ili kuinua kipato chetu na kuinua kipato cha Taifa.

Mheshimiwa Spika, ningependa pia Mheshimiwa Waziri kama inawezekana atueleze kwamba hatma ya Chuo cha *TANESCO* Morogoro ni nini? Kwa sababu sasa haijulikani kile Chuo ni cha nani baada ya ubinafsishaji wa Shirika la *TANESCO.*

Tungependa tujue kuhusu hicho Chuo. Ningependa pia kuuliza kulikuwa na Kiwanda kilichokuwa kinaitwa *TIPPER,* kile kiwanda kipo na mitambo ipo na majengo yapo lakini hakifanyi kazi. Lakini ikumbukwe kwamba zilitumika fedha kwa ajili ya kujenga hiki kiwanda hatma yake ni nini?

Ningependa pia kuuliza kwamba kuna Shirika la *COPEC* tulitarajia kwamba Mheshimiwa Waziri angetueleza kwamba hili Shirika la *COPEC* linafanyaje shughuli na kama limepata faida na lina mwelekeo au dira yake ni nini. Napenda kupata ufafanuzi wake.

Mheshimiwa Spika, ningependa kwa hayo machache, niwatakie kila la kheri Wizara hii ambayo ni nyeti katika kuchangia pato la Taifa na kuondoa umaskini. Lakini wasisahau kwamba ni vizuri tukaweza kuwasaidia Watanzania wakachangia katika kuzalisha nishati na kuuza nishati. Je, Wizara ina mipango gani ya kuwasaidia Watanzania hasa katika maeneo ya vijijini, kuwa na nishati mbadala. Sasa hii nishati mbadala inaweza ikazalishwa na kuuzwa na Mtanzania wa kiwango chochote. Lakini tatizo ni mtaji na *technical know how*.

Naomba wafafanue wao wana mikakati gani ambayo kweli inatekelezeka hasa katika vijiji ambavyo kuanza kufikiria kupeleka umeme wa *TANESCO* itakuwa ni ndoto. Lakini hiyo ndoto itaondolewa tu kama Watanzania wenye ujuzi na elimu ya kuweza kufanyia hiyo shughuli watawezeshwa kuzalisha nishati mbadala na kuiuza kwa wananchi wenzao katika bei iliyo nafuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi ya kwangu yalikuwa ni hayo tu, naomba kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MHE. MWANAMKUU MAKAME KOMBO:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, napenda nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia machache niliyonayo katika Wizara hii ya Nishati na Madini.

Pili, napenda nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini kwa hotuba yake nzuri na kwa kweli tumeielewa. Napenda niseme kabisa kwamba naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakati Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Uwekezaji na Biashara alipokuwa anawasilisha taarifa yake alituambia kwanza tusiendelee kulaumu mambo ya kuzimwa kwa umeme Zanzibar tungojee maelezo.

Mheshimiwa Spika, lakini hata hivyo, mimi ni mmojawapo nitakayeendelea kulaumu. Baadaye kama kulaumu kwetu kumekwishakuwa kwa kiasi kikubwa basi tutaomba radhi.

Mheshimiwa Spika, nikianza mazungumzo yangu napenda niungane na Waheshimiwa Wabunge waliozungumza jana katika Ofisi ya Makamu wa Rais kwa sababu ile Ofisi inabeba mambo ya Muungano wakazungumza hilo la kuzimwa kwa umeme Zanzibar. Kwa hiyo, naomba na mimi niwaungane mkono kulaani kitendo kilichotokea cha kuzimwa umeme kwa muda wa masaa manne kule Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kitendo hicho kilifanywa bila ya kutoa taarifa, na hata kama wangetoa taarifa haiwezekani kuzima umeme Zanzibar nzima. Kitendo kile kwa kweli kilikuwa si cha uungwana mbali ya mambo mengi yaliyoharibika, lakini hata ingeweza kuhatarisha maisha ya binadamu. Kwa hiyo kitendo kile si cha uungwana na lazima tuendelee kukilaani kabisa.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ile ilikuwa ni dhamira yaani ilifanywa kwa makusudi kabisa. Sasa lazima tutaendelea kulaani mpaka Mheshimiwa Waziri atakapokuja kutupa hayo maelezo ndiyo tena tutaelewana. Ingawa jana Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais alisema kwamba haitatokea tena. Lakini na mimi napenda niseme kwamba jambo hili lisitokee tena kwa kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na pengine kwa sababu *management* mpya pale ya *Net Group Solution* hawajui mambo yalivyokuwa huko nyuma. Ingawa Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kazungumzia madeni chungu nzima inayodaiwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, mimi nakubali kwamba tuna madeni.

Lakini hata hivyo, lazima na sisi kwa namna tulivyokaa sisi ni ndugu wa kuzaliwa kwa kweli, siyo ndugu wa kuungana tu, lakini ni ndugu hata wa kuzaliwa. Kwa hiyo, haiwezekani kufanyiana mambo kama yale.

Mheshimiwa Spika, ilivyokuwa umeme kule Zanzibar haukutolewa kama sadaka tu. Zanzibar ilipotaka kuunganishiwa umeme iligharamia miundombinu kwa kutumia zaidi ya paundi milioni 5.7. Sasa fedha hizo kwa wakati ule zilikuwa ni fedha nyingi sana, na baada ya hapo ikagharamia kuendeleza mradi ule kwa zaidi ya shilingi milioni 12 na kwa miaka hiyo fedha hiyo ilikuwa ni fedha nyingi sana. Kwa hiyo, tusitajiane madeni ikawa tena hatukumbuki yaliyopita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi tukiwa kama ndugu lazima kila mmoja amtizame mwenzio kwa matatizo aliyonayo. Kama hiyo haitoshi tulikuwa na majenereta Zanzibar baada ya kuunganishiwa umeme huu, magenereta yale yaliletwa huku Tanzania Bara na yakasambazwa katika Mikoa mbalimbali. Mbali ya hivyo mpaka sasa hivi *TANESCO* pale wanaendelea kutumia vifaa vile vile tulivyovinunua tukaviweka pale kwa ajili ya kupeleka umeme Bagamoyo na wala *TANESCO* haiilipi Zanzibar.

Sasa tusiendelee kutajiana madeni tukatoneshana vidonda. Lazima tuangalie hali halisi ya mambo jinsi yalivyokuwa huko nyuma. Ndiyo maana nikasema umeme Zanzibar hakutolewa kama sadaka isipokuwa na Zanzibar nayo iligharamia huo umeme moja kwa moja kama sehemu nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa kwa yote haya Mheshimiwa Waziri haoni kwamba huu ni unyanyasaji! Hii ilikuwa ni kuinyanyasa Zanzibar na kutaka kuiweka mahali pabaya. Kwa hiyo namuunga mkono Mwenyekiti wa Kamati ya Uwekezaji na Biashara alivyosema kwamba baadaye Mheshimiwa Waziri atoe maelezo na kama lawama zetu ni kupita kiasi basi tutaomba radhi, lakini Mheshimiwa Waziri atoe maelezo.

Vilevile mimi ningeomba Mheshimiwa Waziri aiombe radhi Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar pamoja na wananchi wake, kwa sababu tulipata hasara kwa kweli mbali ya vitu, lakini tulikuwa katika hatari kubwa kwa sababu Zanzibar ni Serikali ile huwezi kuizimia umeme katika sehemu zote mpaka Ikulu na sehemu nyingine muhimu muhimu. Hilo lilikuwa ni jambo la hatari sana. Angalau wangezima umeme katika maofisi. Lakini kuzima umeme katika sehemu zote muhimu kwa kweli kilikuwa ni kitendo kibaya sana. Niishie hapo kuhusu lawama kwa sababu tumeishaambiwa tusilaumu sana lakini kwa kweli ilikuwa haki yetu kulaumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa la pili, nizungumzie habari ya kero zinazojitokeza kule Zanzibar juu ya malipo ya kodi mbalimbali hasa zinazojirudia hasa kodi ya *VAT*. Kule Zanzibar fedha za umeme zinapolipwa lazima kodi ya *VAT* iwepo. Pia wanapokuja huku Tanzania Bara lazima kodi ya *VAT* iwepo, na wananchi vile vile walioko Zanzibar mmoja mmoja wakilipa bili za umeme lazima walipe na kodi ya *VAT.*

Sasa kwa mazoea tuliyozoea Serikali yetu huwa inajitahidi kuondoa kero za wananchi, na kwa kweli Serikali ya CCM inajitahidi isipokuwa penye makosa lazima tuyarekebishe. Kuhusu kodi ya *VAT* lazima Mheshimiwa Waziri atafute namna angalau mambo haya yarekebishwe ili kuwapunguzia kero wananchi wa Zanzibar kule pamoja na Serikali yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda nizugnumzie kuhusu bei ya umeme. Muda mrefu sasa tunaendelea kulalamika juu ya bei kubwa ya umeme. Umeme wa majumbani, umeme unaotumiwa na wafanyabiashara wakubwa pamoja na viwanda. Ingawa baada ya hii *management* ya *Net Group Solution* kuanza kazi Serikali ilijaribu kupunguza kidogo kiwango cha bei ya umeme kwa ajili ya viwanda mpaka kufikia asilimia 16 mpaka 19 na umeme kwa ajili ya majumbani bei zilipanda kufikia asilimia 30. Kwa namna hiyo lazima tuseme kwamba bei ya umeme iko juu sana.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri alipokuwa akisoma hotuba yake ametueleza kwenye majedwali kwamba umeme katika nchi yetu na nchi za jirani kwa kweli haupishani sana pengine kwetu sisi bei iko chini. Lakini bado nasema bei ya umeme iko juu. Ukiangalia zile *graph* alizozitoa utajua

kwamba katika nchi yetu bei za umeme ziko juu. Ukiangalia hali halisi ya wananchi kuongezewa asilimia 30 ya bei ni kubwa sana kutokana na kipato cha wananchi.

Vilevile kwa upande wa viwanda tuliamua kubinafsisha viwanda ili tujipatie kodi kutoka mle mle kwenye viwanda tulivyobinafsisha. Lakini sasa kutokana na gharama za umeme zilivyokuwa kubwa kwa kweli wenye viwanda wanaviendesha katika hali ngumu sana, na ni tabu kukabili ushindani wa biashara. Kwa hiyo kuna haja bei ya umeme ikaangaliwa tena upya na kama Mheshimiwa Waziri alivyosema kwamba atazidi kuiangalia na vilevile itafute njia mbadala ya kupata umeme. Kwa sababu itakapoteremka bei hii ya umeme itakuwa kidogo afadhali na kodi zetu tutazipata kama tulivyokusudia.

Mwisho, Mheshimiwa Spika, ningependa kuzungumzia juu ya suala la utafiti wa mafuta ya petroli. Mimi nakubali kwamba suala hili ni suala la Katiba na tuliliamua. Lakini hata hivyo Katiba si Msahafu. Ukizingatia hasa hali halisi ya uchumi wa Serikali zetu utaona kwamba kwa upande wa huku Tanzania Bara kuna mambo ya biashara mengi tu, kwa mfano upande wa madini, kwa upande wa kilimo na kuna mambo mengine mengi ya biashara.

Sasa hebu tuangalie upande wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar tuna karafuu tu jamani. Sasa kwa sababu tulikubaliana na sisi tunakubali kwamba kweli tulikubaliana na hili ni suala la Katiba. Lakini hata hivyo tutafute namna ya kulifanyia marekebisho suala hili ili utafiti huu wa mambo ya mafuta ya petroli ingawaje hatujawa na uhakika kwamba yapo au hayapo. Lakini suala hili basi lisiwe la Muungano na yatakapopatikana kwa Zanzibar itakuwa pengine ndiyo kitu cha pili, kwa sababu kule hatuna kitu isipokuwa hizo karafuu. Kwa hiyo hili suala tunalikubali kwamba kweli ni la Katiba na tulilikubali katika Mabunge yetu haya, lakini tulifanyie utaratibu ili lisiwe tena la Muungano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niseme naipongeza Wizara, lakini hayo mambo wayaangalie, na kwa kweli kama nilivyosema Mheshimiwa Waziri atakaposimama kuwa- *wind up* basi aweze kuomba radhi kidogo kwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa sababu hasara kwa kweli tulizipata kutokana na kuzimwa kwa umeme.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba niseme naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge kanuni zinaruhusu dakika 15 kwa kila msemaji, lakini kwa tatizo nililonalo leo, ningeomba kama mnaweza kusaidiana kwa kusema chini ya dakika 15 ili kuwasaidia Waheshimiwa Wabunge wengine nao wapate nafasi ya kuchangia. Mheshimiwa James Musalika atafuatiwa na Mheshimiwa Mbaruk Mwandoro na baada yake Mheshimiwa Stephen Kahumbi.

**MHE. JAMES P. MUSALIKA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwanza kwa kunipa nafasi mchana huu nichangie hoja ambayo iko mbele yetu. Lakini kabla sijasema chochote kwa ajili ya *record* za *Hansard,* tarehe 15 Julai, 2003 asubuhi Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini wakati akijibu swali langu la nyongeza alinitambua kama Msabaha Musalika. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, sasa mimi nafahamu mtu hubadilisha jina baada ya kufunga ndoa au kuapa Mahakamani. Kwa kuwa mimi sijapanga kufanya hivyo na Mheshimiwa Naibu Waziri, inawezekana wazazi wangu wameshatoa mahari bila mimi kujua, maana nipo hapa kwa muda wa miezi miwili na bila ridhaa yangu. Lakini ningeshauri Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini, aendelee kunitambua kama James Philipo Musalika. Lile jina lake aliondoe kwanza pale kwenye jina langu. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba sasa nije kwenye hoja ambayo ipo mbele yetu. Nichukue nafasi hii kumpongeza sana kwanza Mheshimiwa Rais Benjamin Mkapa, kwa sera nzuri sana ambazo zimetufikisha hapa kwenye madini. Nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa hotuba nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa yapo masuala machache ambayo ningependa niyachangie. La kwanza, nilikuwa naomba wenzetu wa Wizara ya Nishati na Madini na wenzetu kwenye Serikali wajue kwamba

sisi tuko hapa kuwasaidia katika suala zima la madini. Kwa sababu tumeona kuna mapungufu, sasa wasituelewe vibaya.

Mheshimiwa Spika, zipo Serikali zinawaelewa vibaya baadhi ya wananchi wanapojaribu kuisaidia Serikali. Kuna nchi imewahi kumuua mtu mmoja anaitwa Ken Saro Wiwa, kwa sababu alikuwa anailalamikia Serikali kuhusu masuala ya mazingira yanayosababishwa na wawekezaji.

Sasa mimi tatizo langu liko kwenye mkataba. Kuhusu mikataba ya madini kwanza kuna usiri. Usiri ambao sisi Waheshimiwa Wabunge hatuufahamu na hatuna *information* za kutosha kuhusu mikataba hiyo. Sasa kazi mojawapo ya Bunge ni kuisimamia Serikali kwenye ujumla wake. Sasa utasimamiaje kitu ambacho hujui. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mikataba iliyopo kwa mfano ya madini, *Geita Gold Mine* na Kahama hatujui ni ya miaka mingapi. Kuhusu mikataba hiyo tunalalamikia mapungufu yaliyopo ni kiasi kidogo sana cha fedha inayoachwa kama mrahaba. Kwenye jedwali la Mheshimiwa Waziri ametoa mifano. Nichukue mfano tu wa Namibia na Tanzania, ni kwamba Namibia wao wanatoza mrahaba wa asilimia 5 na sisi hapa ni mrahaba wa asilimia 3. Jedwali linaenda mpaka kuna sehemu ya *VAT,* sisi hatutozi *VAT,* lakini Namibia wanatoza *VAT.* Lakini jedwali hili naona lina mapungufu kidogo tungepata uzoefu wa nchi kama Ghana ambayo ina Kampuni ya Madini inaitwa Ashanti, tungepata uzoefu wa Senegal na tungepata uzoefu wa Nigeria ambazo hazimo kwenye jedwali lake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunasema asilimia 3 ya mrahaba ni kidogo sana. Tuangalie tu kwa mfano *production cost* ya *ounce* moja ya dhahabu kwa takwimu ambazo zipo kwa Tanzania ni *dollar* 156 kwa *ounce* moja. Kwa Afrika ya Kusini ni *dollar* 200. Halafu mrahaba uko pale pale asilimia 3. Ukija kwa mfano kwenye bei ya dhahabu sasa hivi duniani baada ya vita vya Iraq na Marekani na hata baada ya Septemba 11, 2002 dhahabu ilipanda. Wakati wawekezaji hao wanasaini mikataba sina hakika na takwimu vizuri zaidi. Lakini kwa *ounce* moja ilikuwa ni *dollar* za kimarekani 270. Sasa hivi *ounce* moja ya dhahabu inauzwa kwenye soko la dunia kwa *dollar* za Kimarekani 370 mpaka 380. *Production cost* ya Tanzania iko chini na wananchi wako maskini, wakati huo huo sasa hivi kwenye takwimu hizi tumeambiwa Tanzania inapata tani 50 za dhahabu kila mwaka.

Mheshimiwa Spika, wakati haya yanatendeka wananchi wanaozunguka maeneo ambapo migodi ipo ni maskini wa kutupwa. Kuwapo kwa madini hayo kumesababisha watu wengi kwenda huko kutafuta ajira na kufanya biashara. Tumekuwa tukiiambia Serikali hawa wenzetu ambao wamekuja wasaidie basi kutatua matatizo ya jamii ambayo wao wameyasababisha kwa sababu ya biashara yao.

Mheshimiwa Spika, nitoe mfano wa Geita. Geita sasa hivi kuna mfumuko wa watu ambao wako karibu zaidi ya laki moja. Watu hao hawana sehemu ya kukaa, hawana maji ya kunywa na hawana huduma za afya. Wakati hayo yanatendeka maji ya Ziwa Victoria yako kilomita 25 toka Geita Mjini, wawekezaji wameishavuta maji yao na wamepewa maji bure, kwa sababu wana *tax holiday* na kutoka pale *Geita Gold Mine* kuja Geita Mjini ni kilomita 4. Wakati wa masika huwa kuna maji ya mto ambayo yanakwenda kukutana na maji wanayoyavuta kutoka Ziwani na ambao kwao yanakuwa kero hawajui wayafanyie nini.

Mheshimiwa Spika, wakati haya yanatokea pale Geita Mjini ndoo ya maji au lita 20 ni shilingi 100/= maji ambayo si salama na maji ambayo si safi. Wakati hawa wanashangaa haya maji wayafanyie nini na yanawazidi. Wananchi wa Geita wanaugua *Typhoid,* wanaugua amiba na magonjwa ya tumbo, tunawambia watusaidie angalau maji hata kama wakituuzia kama vile wananchi wa Dodoma wanavyouziwa maji. Tupo tayari Geita lakini hilo halifanyiki bado na tunahitaji kwa siku lita milioni 7 ambazo hata kama wangetu-*charge* hata kwa kiasi kidogo sana, baada ya miaka fulani wangeweza kurudisha fedha yao, sasa hilo hawaliangalii. Kuhusu hili ndiyo tunapiga kelele, sera za madini hazieleweki na Serikali tunaiambia haitusikilizi sasa tukamlilie nani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi sijaona mkataba lakini inasemekana kuna sehemu ya mkataba wa *Geita Gold Mine* wanapaswa kulipa kiasi cha 200,000 *USD* kwa mwaka kuilipa Halmashauri ya Wilaya ya Geita.

Kitu ambacho hakipo na kama kipo hapa ningetaka kupata maelezo kutoka kwa Mheshimiwa Waziri. Kinachofanyika kwa hawa wenzetu kuna fedha huwa wanatoa wanapotaka na wanapopenda wanatoa.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, wakitoa mwaka huu, mwaka kesho hawatoi. Hivi kweli ni ustaarabu kwa Halmashauri ambayo ni Serikali ya Tanzania kuwa ombaomba mahali, kama ipo kwenye mkataba tuambiwe, kwamba wanapaswa kutoa wawekezaji kiasi fulani kwa ajili ya maendeleo ya Halmashauri badala ya Mwenyekiti wa Halmashauri na Madiwani wakiwemo Waheshimiwa Wabunge kwenda kugonga hodi kuomba chumvi kwa jirani kila siku ni ustaarabu!

Sasa Mkataba useme wapi unazungumzia kuhusu *Royalty* ambayo wanalipa kwa Serikali Kuu. Kwenye Halmashauri wanapaswa kutupa nini kitu ambacho kipo kwenye sheria badala ya sisi kuwa omba omba. *(Makofi)*

Mimi nilidhani kwamba kwa kuwa Benki ya Dunia na wanatupenda na wametushauri vizuri sana na wametupa fedha nyingi sana mkopo wa MMEM walishindwaji kutupa fedha kwa sababu *capital investment* ya mgodi wa *Geita Gold Mine* ni dola za Kimarekani milioni 400. *Kahama Mine* ni dola za Kimarekani 380. *World Bank* wametupa fedha nyingi sana za MMEM walishindwaje kutushauri kuondokana na kuombaomba wakatukopesha fedha ili tukawa *joint venture* na hawa wawekezaji? Sasa hili nao napenda Serikali ilielewe kwamba tungeweza kuwa na *shares* mle badala ya kutegemea mrahaba ambao kwa sasa hivi unachangia kiasi cha asilimia 2.5 tu ambazo ni kiasi kidogo sana. Tumeanza lakini bado tunaona ni kidogo kwenye Pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, labda nije kwenye suala lingine la kuhusu mazingira. Pale Geita wanafanya uchimbaji ambao wanaita ni *open cast*, hawachimbi chini ya ardhi sio *underground,* wanachimba juu ya ardhi. Sasa wanaacha mashimo na wanahamisha milima, milima inahamishwa ukiingia pale sasa hivi hata kama una shughuli zako unaacha shughuli zao unakuwa mtalii kuangalia mambo yanayofanyika ya ajabu duniani. Milima mikubwa inaporomoshwa kutafuta dhahabu. Je, baada ya hao kumaliza kutafuta dhahabu nini hatima ya milima hiyo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *Kahama Mine* wanachimba na wanapeleka Japan *Mineral concetrates* yaani udongo kuyeyusha kule Japan kwa mwaka wanachukua tani 25,000 baada ya miaka 50 hizo tani zitarudi vipi huku, kule kweli hazina matumizi? Najua Japan wana tatizo la ardhi. Kule kweli huyo haina *value*, huo mchanga hauna thamani kule. Huku unakotoka chini ya ardhi wanaweka nini hapa Tanzania yale mashimo kuirudishia ardhi ilivyokuwa kama alivyoumba Mungu. Haya masuala ndiyo tunapenda tuulize? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ningependa kumalizia swali la maslahi ya wafanyakazi wanaoajiriwa. Waziri ameelezea vizuri sana hapa kwamba katika matarajio yao kwa kuajiri ya Watanzania wengi iwezekanavyo. Lakini kinachofanyika kule kuna ubaguzi wa hali ya juu sana katika maslahi kwa maana ya mishahara. Wakati Watanzania wenye uwezo, elimu na wanaofanya kazi ngumu lakini malipo yao ni madogo sana.

Mheshimiwa Spika, wakati wakitokea wenzetu ambao pengine hawana elimu na uwezo fedha zao inakuwa kwenye dola za kigeni na zinabakia uko nje ya nchi na hapa posho na wengine wanapata posho ya mbwa wao. Sasa hili lazima tuliangalie sana Wizara ya Kazi na Maendeleo ya Vijana. Muangalie kwa sababu wafanyakazi wanalalamika.

Halafu kuhusu heshima ya wafanyakazi wao kuna baadhi yao hawaheshimu Watanzania. Mimi nimewahi kufanya Kampuni fulani ambapo mtu huwezi kuruhusiwa kwenda kutibiwa hospitali au kupata *ED.* Mfanyakazi mmoja siku moja alikuwa na Kisukari na *Blood Pressure* akaanguka, akaumia, akapata majereha. Asubuhi anakuja kwa Meneja kuomba ruhusa aende hospitali yule Meneja mtu kutoka Afrika ya Kusini sipendi kumsema hapa, akamwambia kwamba siamini kama unaumwa inawezekana unafanya mapenzi na simba, akamnyima ruhusa. *(Makofi)*

Kuna mwingine aliugua akamwambia hapana kwa nini hukugua wakati wa likizo. Wanafanya hayo. Sasa vile vyama vya wafanyakazi vinavyojaribu kufanya kazi yake vinaonekana kama ni *Anti Management Movements*. Vinachukiwa na mtu wa kwanza kufukuzwa kazi ni yule anayekubali kuwa

Mwenyekiti wa Chama cha Wafanyakazi katika mgodi au katika wawekezaji. Wizara ya Kazi na Maendeleo ya Vijana hili mnalifahamu?

Sasa Watanzania wetu wanakuwa wana baridi hawana raha. Mara nyingi wanafikiria kugoma sasa wagome lakini pale si kuna ajira, wafanya nini, sio rahisi kukatisha kazi ghafla. Kwa hiyo tulikuwa tunaomba sana na ndio tunasema mapungufu haya Serikali iyafahamu na haiwezi ikayafahamu sisi tunaokaa kule tunayafahamu na ndiyo maana tunawaletea. Tukae pamoja tuboreshe haya si kwamba hatutaki wawekezaji lakini tunataka mazingira yao sisi tufaidike wananchi wetu wafaidike pamoja na wao wafanye biashara zao kwa ajili ya *mature benefit.*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya naomba kushukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. ERNEST G. MABINA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia katika Wizara hii ya Nishati na Madini.

Kwanza kabisa mimi inanichanganya hii Wizara kwa sababu ina sehemu moja nzuri kwangu na sehemu moja mbaya kwangu. Kwa hiyo, nakuwa kama mtu aliyealikwa kwenye harusi halafu nikapata tena msiba. Sasa ni jinsi gani nitakavyoingia lakini nitatumia utaratibu tu kwa sababu zile shughuli zilikuwa karibu karibu sehemu moja kuna harusi na sehemu moja kuna msiba. Lakini walikuwa wanatenganishwa na huwa wa makuti. Kwa hiyo itabidi nipenyeze kichwa sehemu ya msiba nilie sana na sehemu ya sherehe basi nitakuwa nacheza. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, nitaanza sehemu ya kucheza. Nawashukuru sana Wizara hii kwa upande wa *TANESCO* kuweza kutuletea umeme katika mji wetu wa Geita ambao nafikiri tarehe 19 kulikuwa na ufunguzi wa umeme katika Wilaya ya Geita.

Mheshimiwa Makamu wa Rais, tunamshukuru sana alikuwa kule, ameshuhudia tendo la ufunguzi wa umeme katika Wilaya ya Geita ambao lilikuwa ni tatizo sugu kwa wananchi wa Geita. Lakini sasa hivi kumekuwa na faraja sana. Pamoja na ufunguzi huo, nakushukuru lakini nilikuwa naomba yafuatayo. Umeme umeshaingia Geita lakini una matatizo ya kuzimikazimika, umeme ni mdogo sana kwa sababu umefika pale kutoka Sengerema ukiwa na nguvu kidogo.

Kwa hiyo, nilikuwa naomba watuongezee *Transformer* nyingi ambazo sasa hivi hakuna katika Wilaya ya Geita na mji unakua. Watuletee mita na nyaya kwa sababu mahitaji ni makubwa sana nafikiri kuliko mji wowote ambao unaendelea hapa. Nafikiri katika takwimu itaonyesha kwamba mji wa Geita sasa hivi unakuwa kwa *speed* kubwa sana nafikiri katika Afrika Mashariki.

Hilo nilikuwa naliomba tu kwa upande wa *TANESCO* watuletee vifaa hivyo ili wananchi wa Geita waweze kushukuru na kupendezeshwa kwa ujio huu wa umeme katika Wilaya yetu ya Geita. Pili, nilikuwa nashukuru tu kwa sababu kwamba kulikuwa na sehemu ambayo naipigia kelele sana sehemu ya Kasamwa. Sasa hivi Wizara ya Nishati imeweza kutuletea umeme katika eneo hilo na wananchi wanashukuru ila kuna mapungufu kama niliyokuwa nimeyazungumza hapa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo nafikiri sasa hivi nianze kulia. Kilio changu kiko upande wa madini. Unapowasikia Waheshimiwa Wabunge wanalia hapa si kwamba wanaigiza au wanafanya maagizo hiyo ndiyo hali halisi iliyoko katika maeneo ya madini. Naomba tu kwamba Mawaziri na wewe mwenyewe Mheshimiwa Spika, tutakapotoa shilingi leo jioni Wabunge wote tunaomba mtuunge mkono tujue kwamba Serikali hii haiwatendei haki wananchi wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Geita walikuwa na matumaini makubwa sana katika ujio huu wa uchimbaji wa madini. Lakini tofauti yake imekuja kujitokeza badala ya kufurahia wamekuwa na machungu. Nashangaa kuna sheria gani ambayo ni ya ardhi kwa sababu Sheria ya ardhi inasema kwamba unapomhamisha mtu lazima umlipe kwamba fidia. Lakini katika suala la madini ni sheria ipi iliyotumika ambayo imewahamisha watu bila ya kuwafidia. Hapo ndipo unapojiuliza na nataka Serikali inieleze je, hao wananchi wa Geita ambao hawajafidiwa kuanzia mwaka 1999 mpaka leo miaka minne wanategemea fidia

watalipwa lini? Hilo ndilo nililotaka kuliuliza na ninataka labda nitoe ufafanuzi ni kwa nini hawa wananchi wa Geita hawajalipwa?

**MBUNGE FULANI:** *Shame*!!!

**MHE. ERNEST G. MABINA:** Hawajalipwa kwa sababu ya uongozi mbaya wa Serikali ambayo haiwajali wananchi wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, itakumbukwa kwamba wakati Serikali ilipokuwa inataka kuuchukua Mgodi wa Geita iliwaahidi mambo mazuri sana wananchi wa Geita mojawapo ilikuwa ni fidia na kuwajengea majumba na kuwapeleka maeneo mbalimbali kwenda kujionea wenyewe ili hata watakapokuwa katika maeneo yale basi waonekane wanaishi katika bustani ya Eden. Tofauti yake sasa hivi wananchi wale wanapata taabu wengine sasa hivi wamekwishakufa kwa ajili ya kusubiri malipo ambayo hayapo ni sawa sawa na wewe Mheshimiwa Spika utakapokuwa umenyimwa mshahara wa miezi miwili sidhani kama utaweza ukavumilia.

Sasa hawa wamenyimwa miaka minne je, unategemea wataishi vipi? Lakini tatizo lilikuja kwenye Serikali. Wawekezaji walipofanya tathmini ya fidia ya wananchi wa Geita walibaini kwamba wangeweza wakalipa fidia ya shilingi bilioni 1.8.

Mheshimiwa Spika, lakini kwa uroho wa viongozi wa Serikali Ofisi ya *DC,* Ofisi ya Halmashauri na ya Mkoa wakaja wakatathmini wakasema kwamba fidia iwe ni shilingi bilioni 3.8 na bahati nzuri wawekezaji walitoa fedha zote zile sasa nani alaumiwe? Mwenye kulaumiwa ni Serikali kwa sababu imewaweka wafanyakazi ambao wamekula zile fedha na imewaangalia tu mpaka sasa hivi wanazidi kudunda. Sasa utamthamini vipi mwananchi wako. Hii Serikali imeonekana kwamba haiwathamini wananchi ambao wako pale ambao ni wagunduzi wa madini. Kwa mfano, kuna Mzee ambaye amevumbua *Tanzanite,* Mzee Jumanne Ngoma, mpaka leo hii hajalipwa chochote huu ni mfano halisi kwa sababu yule amegundua tangu mwaka 1967 lakini mpaka leo hii hajalipwa. Je, huyu mzee mnamtegemea nini na huyu labda tu kwa sababu ……*(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. ARCADO D. NTAGAZWA):** Mheshimiwa Spika, ili mjadala na mchango wa Mheshimiwa Mbunge, uende sawa, ningependa kutoa taarifa ifuatayo.

Mheshimiwa Spika, wakati mmoja katika Bunge hili hili, nililiarifu Bunge lako Tukufu kwamba wakati nilipokuwa Naibu Waziri wa Fedha huyu Mzee Jumanne Ngoma, mgunduzi wa *Tanzanite,* mimi mwenyewe binafsi nilishughulikia suala la yeye kulipwa fidia. Nilitaka nitoe taarifa hii na alilipwa. *(Makofi)*

**MHE. ERNEST G. MABINA:** Mheshimiwa Spika, hili suala limeoana na wananchi wa Geita mpaka sasa hivi hawajalipwa. Haya sio matatizo ya wananchi, wala sio matatizo ya wawekezaji haya ni matatizo ya Serikali yetu.

Sasa tunachokiomba Serikali si kama iyafunge, nilichokuwa naiomba Serikali ifanye utaratibu wa hali ya juu kuwalipa hao wananchi wa Geita fidia yao ambayo hiyo ni haki yao sidhani kama Serikali inaweza ikakubali kuweza kuwalipa fedha za usumbufu kuanzia mwaka 1999 mpaka leo hii.

Mheshimiwa Spika, kama wananchi wale wangeweka zile fedha katika Mabenki au wangewekeza sehemu fulani basi wangekuwa wanapata *dividend,* wangekuwa wanapata riba je, Serikali labda ninaweza nikaiuliza kwa kiwango kile cha fedha ilichokuwa inataka kuwalipa itawalipa hicho hicho au itakuwa imeongeza kutokana na ongezeko la thamani ya fedha. Hilo lilikuwa ni swali ambalo nilitaka kuliuliza na nataka wakati anajumuisha Waziri ajaribu kuniambia kwa undani zaidi wananchi hawa wa Geita watalipwa lini.

Nafikiri Waziri wakati wa ufunguzi tulikuwa naye pale Geita, wananchi wamekaa kimya si kwamba hawakupenda kuletewa umeme, wamekaa kimya kwa sababu Serikali yao imewadhulumu. Si

kwamba imewatendea haki na mimi niliwasifu wananchi wa Geita kwa kukaa kimya kwa sababu walionyesha uzalendo wao. Walihudhuria watu wengi lakini wakaonyesha kwamba Serikali haijawatendea haki. Kwa hiyo mimi sikutaka nizungumzie mengi zaidi nataka niongee tu kwa hilo na naomba kuunga hoja mkono. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. MBARUK K. MWANDORO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii nami nichangie katika Wizara hii ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Spika, ningependa kuchukua fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Daniel Yona, Naibu Waziri wake Mheshimiwa Dr. Ibrahim Msabaha, pamoja na Katibu Mkuu na viongozi wote wa Wizara na Taasisi zilizoshirikiana na Wizara hii kwa hotuba nzuri hii ambayo wameandaa na kwa kazi nzuri ambayo wamefanya na wanaendelea kufanya. *(Makofi)*

Hali kadhalika ningependa kuchukua fursa hii kumpongeza Mwenyekiti wa Kamati yetu Mheshimiwa William Shellukindo, kwa hotuba nzuri aliyoitoa kwa niaba ya Kamati yetu ya Uwekezaji na Biashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara hii ni Wizara muhimu, nyeti, Wizara ambayo inasimamia sekta muhimu sana Kitaifa. Ina mchango mkubwa kwa maendeleo ya uchumi na maendeleo ya Taifa kwa jumla. Nikianzia na sekta ya madini ni sekta muhimu sana. Sekta ambayo ina maliasili ina raslimali ambayo ni muhimu sana kwa maendeleo ya uchumi wetu kwa wakati wetu wa sasa na kwa siku zijazo.

Ningependa kuipongeza Serikali ya awamu ya tatu kwa sera zake nzuri ambazo zimeweka na ambazo zinaifanya wawekezaji kuja kwa wingi kuendeleza sekta hii. Ni jambo la faraja kubwa kwamba sekta ya madini imeweza kukua kwa haraka sana katika miaka hii ya karibuni na imeweza kuwa ya kwanza katika kuchangia katika fedha za kigeni na mchango wake katika Pato la Taifa umeongezeka kwa kasi kubwa sana. Hata hivyo sekta hii muhimu bado ina nafasi kubwa sana ya kuweza kuchangia zaidi katika maendeleo ya uchumi wetu na Taifa kwa ujumla.

Pamoja na sera nzuri hizo zilizowekwa na kama walivyozungumza Waheshimiwa Wabunge waliotangulia ni kwamba yapo mambo mengi ambayo itabidi tuyatazame upya ili kwamba sekta hii iweze kuchangia na kunufaisha Taifa letu kama inawezekana.

Moja ya kitu ambacho kinatusumbua kutamka wengine wanasema mrahaba, wengine wanasema mrabaha, wengine wanasema Mheshimiwa Dr. Ibrahim Msabaha, sasa hiki ni kitu ambacho kusema kweli hatuna budi kukitazama kwa karibu sana. Pamoja na Mheshimiwa Waziri kutueleza kwamba tuko katika hali nzuri na kutupa mifano ya takwimu za nchi mbalimbali mimi nafikiri bado suala hili linahitaji kutazamwa kwa undani zaidi ili kuweza kutoa fursa kwa sisi kufaidika zaidi.

Mheshimiwa Spika, pili kuna suala la wazalendo kuweza kufaidika zaidi katika sekta hii. Katika masuala ya ajira tumesikia Waheshimiwa Wabunge wengi wakieleza jinsi wanavyonyanyaswa na jinsi ambavyo hawahusishwi.

Mimi ningependa kuungana mkono na Mbunge aliyetangulia kusema kwamba ni vizuri taratibu zikatazamwa, sera ikatazamwa ili baadaye tuweze sekta hii muhimu nayo kuiweka katika soko la mtaji ili wananchi waweze kushiriki na vile vile Serikali ifikirie namna ya kuwahusisha wananchi wadogo wadogo. Wachimbaji wadogo wadogo sasa hivi wameenea nchini kote na wanachimba taratibu ambazo si nzuri hamna njia nzuri za kuwawezesha na kwa hivyo sisi hatufaidiki na sekta hii kama ilivyotakiwa.

Mheshimiwa Spika, moja la suala muhimu ambalo nilipenda kusema hata sisi kule jimboni kwangu Mkinga tuna madini mengi sana. Bahati mbaya ama kwa sababu ya kutokuwa na sera thabiti kuhusu wachimbaji wadogo wadogo au kutokana na jimbo lile kuwa pembezoni bahati mbaya hizi sehemu za pembezoni zina matatizo kidogo halijapewa uzito unaostahili.

Nilieleza Wizarani kwamba kule kuna madini mengi ambayo tungeweza kuyaendelea kwa faida yetu, sehemu za Kirui, Daruni, Malamba zote zina madini ya aina mbalimbali. Vile vile tumesema kule

kuna dalili nzuri ya mafuta kupatikana sehemu za Kigongoi kuna ardhi fulani ambazo zinanukia mafuta ya taa na mafuta ya petroli hivi hivi. Mwambao wa Pwani bahati nzuri jimbo lile la Pwani lina milima.

Mheshimiwa Spika, mwambao wa Pwani una dalili nzuri za mafuta na mimi hapa ningependa kusema kwamba ndugu zangu wa Unguja na Pemba, ndugu zangu wa Zanzibar tusikimbilie kusema kwamba mafuta tuyafanye yasiwe ya Kimuungano. Tunachojaribu kufanya hapa ni kuimarisha Muungano wetu si kuua Muungano wetu. Mafuta yale kwa wale wasiojua labda jimbo langu liko wapi sisi jimbo la Mkinga tunapakana na *Pemba Channel*.

Sasa hayo mafuta tukiyapata tutasema ni ya Pemba au ni ya Mkinga. Kwa hiyo, mimi nafikiri tusianze kugawana mambo haya kabla hali halisi haijajitokeza. Mimi nafikiri tuendelee na uchunguzi halafu hatimaye tuone namna gani nzuri ya kuweza kutumia raslimali yetu vizuri kwa faida ya wananchi wote. Namna gani itakuwa nafikiri tuzungumze baadaye badala ya *constitutes* sasa kuanza kugawana kabla mafuta yenyewe kihalisi hayajapatikana.

Mheshimiwa Spika, ningependa kusema kwamba sekta ya nishati na haya umeme ni kichocheo kikubwa sana cha maendeleo. Muasisi wa nchi ya Kisoviet, Lenin alisema maendeleo yanatokana na kuendeleza vijiji na kupeleka umeme vijijini kote.

Nashukuru kwamba Serikali yetu imelitambua swali hili na kulifanyia kazi inavyostahili na sasa hivi tumeweka mikakati na mbinu mbalimbali za kuweza kufikisha umeme vijijini. Lakini bahati mbaya suala hili la umeme vijijini hatujalifuatilia kisayansi, hatuna mipango iliyo wazi kwamba hii *rural fund* na hicho chombo kinachotengeneza kitakwenda wapi tuna mikakati ya wapi ya kupeleka wapi.

Mheshimiwa Spika, Jimbo langu la Mkinga ni moja ambalo tumekuwa na maombi ya muda mrefu sana, tumezungumzia hapa Bungeni, nimezungumzia na Waheshimiwa Mawaziri na Naibu wake wametoa ahadi ya kufika kwetu jimbo la Mkinga kutazama hali hiyo hata kabla ya Waziri Dr. Abdallah Kigoda na wengine walioko nyuma walitoa ahadi hiyo kwamba watafika watajaribu kuona vipi wataweza kusaidia sekta hii muhimu.

Ningependa nielezee kwamba maendeleo ya sekta mbalimbali kilimo, uvuvi, madini, utalii vyote kusema kweli vinategemea sana kuwepo kwa umeme. Matunda yetu mbalimbali yanaoza, samaki wanaharibika, kule kwetu bahati nzuri tuna fursa ya kila aina ya hewa na kila aina ya chakula na mazao. Lakini yote haya hatuyafaidi na vita ya kupigana na umaskini hatuwezi kushiriki kwa kutosha na wananchi wetu wataendelea kuwa maskini kwa sababu hatuna nishati hii muhimu iliyosemwa.

Mheshimiwa Spika, alikwisha ahidi Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba angetembelea Kata ambazo hazina umeme na kuona nini nifanye zaidi ya mara tatu. Kata hizo zikiwa Daruni, Gombelo, Kigongoi, Kwale, Manza, Mkinga na Mwakyembe. Lakini pamoja na ahadi zote hizo pamoja na kwamba labda zilikuwapo sababu za kutosha za kuwafanya wasifike hawakufika, na wananchi sasa hivi wanachukulia kwamba Serikali yao inawadharau na kuwapa nafasi maadui kusema kwamba nyinyi mnadharauliwa na nyinyi kusema kweli hamstahili kuwa chini ya himaya hii mliyonayo sasa hivi.

Sasa mimi naomba sana Wizara hii sio tu itembelee kule kama alivyoahidi lakini wajitahidi kuondoa hii dosari iliyopo ya kutokuwa na umeme na kuwanyima wananchi wetu nafasi ya maendeleo ambayo tungeweza kuchangia sana katika ukuaji wa uchumi huu.

Kama nilivyosema kule kuna mazao mbalimbali kutoka baharini mpaka milimani kule ambako kuna kila aina ya matunda, kuna kila aina ya viungo, bidhaa yoyote unafikiri ya mifugo, maziwa kila kitu sasa haya hatuwezi kuyaendeleza bila umeme. Wananchi wanategemea sana msaada wenu na ushirikiano wetu katika suala hili. Inawezekana kwamba pengine gharama za kufanya hivi kubwa lakini katika sera zetu za uwezeshaji moja la suala la umuhimu ni kuwapatia wananchi nishati kwa bei nafuu ambayo itaweza kuwasaidia katika suala hili.

Mheshimiwa Spika, katika suala hilo hilo la nishati ni bahati mbaya kwamba hatujatazama sana bado vianzio vingine vya umeme. Tumekuwa mpaka sasa hivi tukijishughulisha zaidi na dizeli, labda gesi

itakuja na sehemu zinazotoa umeme kwa maji makubwa lakini kwa nini tusitoe fursa ya kutumia *mini-hydrous.*

Mheshimiwa Spika, kwa nini tusitumie mionzi ya juu kwa zaidi. Kwa nini tusitumie mambo hayo kwa mfano Mkonge. Mkonge unatoa takataka ambazo zinaweza kutengeneza umeme mwingi sana na kadha wa kadha viko vianzio vingi ambavyo tumeviacha.

Mimi nafikiri hivi tuvichukulie kwa maana tutaweza kupiga hatua kubwa sana. Linalonishanga zaidi ni kwamba siku zote Wabunge tumekuwa tukiuliza kwa nini *Stigler's Gorge* mpaka leo tumeiacha, hatujapata jibu. Tunashauriwa na wataalamu kwamba tutaharibu mazingira na nini na hivi wao kwao wanafanya vitu hivyo hawaharibu mazingira, kwetu sisi ndio tunaambiwa tutaharibu mazingira.

Mheshimiwa Spika, tutaimba wimbo tu kwa umeme mwingi wa kutosha, bei nafuu lakini hatuwezi kuipata hiyo hali kama tutaendelea kufuata haya haya tu tunayoelekezwa na kuacha kutumia raslimali nzuri tulizonazo za kuweza kutupatia umeme mwingi zaidi wa bei nafuu zaidi.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ulitwambia kwamba tubane muda ningekuwa na mengi ya kueleza lakini nashauri kwamba niishie hapa. Mimi ningependa kuiomba Wizara tena itazame maombi yetu ya safari hii wameahidi juu ya umeme hawajafika.Ni matumaini yangu kwamba watafika. Nimewafahamisha kwamba tunayo nafasi nzuri ya kuendeleza madini, tuna nafasi nzuri ya kuweza kupata mafuta kama walivyo ndugu zetu wa Pemba na Unguja pale. Tunawaomba tafadhali mfike ahadi zenu mzitekeleze ama sivyo mtazidi kuangusha imani.

Mheshimiwa Spika, baada ya maneno hayo machache naunga mkono hoja asilimia mia moja. Ahsante.

**MHE. STEPHEN M. KAHUMBI:** Mheshimwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia, sitakuwa na maneno mengi kwa sababu wenzangu wameyasema sana. lakini kabla sijasahau kwanza nimshukuru na kumpongeza Naibu Waziri Msabaha kwa sababu mwaka jana mimi sikuunga mkono hoja yao, lakini alitembelea Wilaya ya Nzega na nikamtembeza kwenye vituo vyote ambavyo nitavigusia leo.

Vile vile nampongeza zaidi kwa kuwa yeye alilala kwenye *Rest House* yetu kinyume cha wengine ambao walilala mgodini. Kulala kwenye *Rest House* yetu kuliwawezesha wapiga kura kumwona na kuzungumza naye badala ya kulala kule mgodini ambako kuna senyenge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Katiba yetu aya ya 63(2) kinasema kuwa kazi ya Wabunge ni kusimamia na kuishauri Serikali ya Jamhuri ya Muungano na vyombo vyake vyote. Lakini mfumo tulionao wa Serikali ambao kuna makundi mawili, kundi moja la Serikali ni Mawaziri ambao wanatokana na watu wa kuchaguliwa hawa wanaapishwa na kukabidhiwa Katiba na ilani ya Uchaguzi.

Mheshimiwa Spika, kuna kundi lingine la Serikali la watendaji wakiongozwa na Makatibu Wakuu ambao ni Maofisa Wahasibu wao kukabidhiwa kasma na usimamizi wote wa matumizi ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, kitu kinachonipa tabu ni kwamba, inapotokea kasoro ya utendaji au ya utekelezaji kwa yale ambayo Bunge limeagiza na pengine kuyapitishia fedha ama mafungu, anayetiwa kitimoto ni Waziri ambaye alipoapishwa alitoka mkononi na Katiba na Ilani ya Uchaguzi! Watekelezaji huwa wanakaa pale kando.

Mheshimiwa Spika, mfano, juzi Mheshimiwa Pascal Degera, alisema hapa Bungeni kwamba: "Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo ilishindwa kujenga chujio la maji ya bwawa la Mwisanga kwa muda wa miaka mingi!"

Sasa, aliyetiwa lawamani ni Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo, lakini tangu wakati mambo yakisomwa kwenye hotuba ya Bajeti, Waziri aliyepo leo, hakuwa Waziri wakati huo, walikuwa ni Mawaziri wengine na waliishaondoka! Makatibu Wakuu wanaweza wakaondoka, lakini wanaacha mafaili

pale ofisini, yapo. Sisi Wanasiasa tukiondoka huwa tunaondoka na mambo yetu, sasa analaumiwa huyu, nadhani hii ni dosari! Au tunamwambia: “Sasa na wewe kamlaumu fulani.” Haijapata kutokea!

Mheshimiwa Spika, binafsi nimeingia katika Bunge hili mwaka 1985 na tangu nilipoingia niliweka lengo moja tu kubwa kwamba, kule kwetu tupate umeme. Kuna mwaka fulani wakati tunafanya mikutano yetu katika ukumbi wa CCM hapa Dodoma, niliingia na kiloba cha mchele Bungeni cha kuwathibitishia Mawaziri kwamba kule Bukene kuna kiwanda kinachokoboa mpunga na kuuza mchele ndani na nje ya nchi. Ndugu zangu Waandishi wa Habari kesho yake waliandika: “Mbunge aja na jipya, aleta kiloba cha mchele Bungeni!” *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, lakini mpaka leo umeme ule haujaja, ndio mwaka jana nikasema: “Aah, naona taabu!” Unawezaje kuunga mkono hoja? Unapokwenda nyumbani kwenu na ukapokelewa, ni lazima wapokee kitu, *you have to deliver beans. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mawaziri na watendaji wao tukimaliza vikao hapa wanafanya na *party* kwa sababu wanacho cha ku-*deliver!* Yule Katibu Mkuu anawaambia na wenzake: “Anzeni kuandika *voucher* pesa tumepata” wame-*deliver*. Sasa, mimi unataka kunifananisha na timu ya *Goss age* ya Zanzibar ambayo ilifungwa mabao. Uganda waliofunga, wali-*deliver* kikombe kwa Gavana wao, timu ya Zanzibar haina cha ku-*deliver!* Lakini wakasema: “Yakhe chenga twawala hawa, twawala chenga!” Sasa, *you can’t deliver* chenga! *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, ninapounga mkono hoja, nikawaambia watu wa Bukene kwamba: “Nimeunga mkono.” Wataniuliza: “Kwa nini, kwani kiwanda chetu kimepata umeme!” Nitawaambia: “Si mlisikia nilivyofoka mle!” Kusikia sio tatizo, ndio nita-*deliver* kusikia! Nashindwa kuunga mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawahurumia hawa Mawaziri kwa sababu tunawaweka kitimoto, lakini hizo fedha hawana! Wana Katiba na Ilani ya Uchaguzi, *that’s all!* Wenye pesa wako kule, wanatutazama tunavyofanya mchezo wa kuigiza! *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wewe na Kanuni za Bunge unasaidia! Mheshimiwa Mbunge mmoja akisema hapa kwamba tutatoa shilingi. Utasaidia, utasema: “Haikuungwa mkono!” Ukienda kwa Waziri unasema: “Unaona, nilikuokoa pale, alikuwa akubane sana Kahumbi.” *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hujamwokoa, kwa sababu wapiga kura wetu kule wanatushangaa!

**MBUNGE FULANI:** Mwambie!

**MHE. STEPHEN M. KAHUMBI:** Wanatushangaa. Pengine iko haja ya kurudisha ile kanuni ya kuchukua Shilingi nikaenda kulala nayo siku tatu! Kwa kufanya hivyo, tutamfanya Waziri ambaye tunamuweka kitimoto akawaweke kitimoto wale …

**MBUNGE FULANI:** Eeeh!

**MHE. STEPHEN M. KAHUMBI:** Wenye makasma, *section* za Sheria na kadhalika *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni mara moja tu Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, alifukuza Makatibu Wakuu. Aliwafukuza na wewe ulikuwepo, walikuwa Makatibu Wakuu nane. Hapo ndio aliwapa na jina la Katibu Mkuu, walikuwa wanaitwa *Permanent Secretary, permanent! (Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, sasa hawa *Permanent Secretaries* tunawafanya nini? *Query* za *auditors* hazifanywi lolote! Tunakaa hapa,Kamati inapitisha ma-*query*, hakuna kinachofanyika! Sisi leo hapa tunazungumza umeme, hakuna kinachofanyika! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *TANESCO* wamekata umeme Zanzibar, Waziri anaambiwa aeleze! Nawaunga mkono Baraza la Wawakilishi wanaosema watashtaki *TANESCO,* siyo Waziri! Kama *TANESCO* walikata umeme bila kuwaarifu *it’s a suicide*, huo ni uhujumu, wamehujumu uchumi! Ni kwa

nini tumtie kitimoto Yona, amefanya nini? Ni kwa nini mwanangu Msabaha alale hoi, amefanya nini? *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Baraza la Wawakilishi wako *right*, kama kweli umeme ulikatwa bila Zanzibar kuarifiwa kwamba saa fulani kama hamjalipa tutakata, wametenda uhujumu, lakini kama waliambiwa ni kitu kingine. *(Kicheko/Makofi)*

Vile vile, nimempeleka Mheshimiwa Msabaha mpaka kwenye kiwanda. Kiwanda hiki kina *horsepower* 280, hicho ni kidogo! Kina *generator* mbili, kila moja ina *kilovolt* 160 na kinatumia lita 348,000 kila siku za dizeli. Tunasema jamani wapelekeeni kwenye kiwanda, hawapeleki! Kutoka pale mpaka kwenye kiwanda ni kilomita 40, lakini hawa wamepeleka kilomita 40 mahali fulani Msabaha anapajua, ili kupeleka kwenye *Secondary School*. Hivi *viability* ya umeme kwenye *Secondary School* na *viability* ya umeme kwenye kiwanda hiki ni sawa? Hebu wafuateni watu wa afya, watu wa afya wamepeleka mradi wa kupasua matende na mabusha Pwani, maana ndipo wapo wagonjwa! *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa napenda kuzungumzia kidogo kuhusu madini. Wabunge wa Geita wameongea sana kuhusu suala hili la madini. Kitu ambacho ninataka kufafanua ni kwamba, watu tunaotoka kwenye mgodi hatuna ugomvi na wenye mgodi, ile asilimia kama ni 3 inayolipwa Serikalini, si mmege kidogo muwape watu wa ile Halmashauri husika? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wale wanaosema: "Mafuta yabaki Zanzibar" wana lao. Kama mafuta yatapatikana kule Zanzibar, mpate *Royalty* kama sisi tunavyoomba au kama watu wa Kilwa watakavyopata *Royalty* ya gesi, kama watapewa! Sisi tumekaa tukasema hatuwezi kuvunja, maana Serikali yetu imesema hivyo, lakini tunaishauri tu.Mbunge mmoja amesema kwamba, Serikali ingefuata mfano wa Ghana. Ghana wana *Commission* ya Madini, *Commission* hiyo ndio inakusanya *Royalty* yote halafu inakasimu sehemu fulani iende Serikali kuu, sehemu fulani iende kwenye *Local Government* na sehemu fulani iende kwenye *stool.* Wanawalipa hata wale Machifu, kwa sababu wenzetu bado wana Machifu. *The Mineral Commission of Ghana* inagawa *Royalty*! Sisi hatusemi ile *three percent* yote ibaki Nzega, aah! Nyingine iende ikatumike Pemba, lakini na sisi tupate kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mgodi uko Geita, sasa wale wa Geita pamoja na kwamba hawana hisa ni maskini, lakini ardhi ni yao! Hata Mjumbe wa Bodi katika ule mgodi ili afahamu kinachoendelea, hamna! Nzega tuna Mjumbe wa Bodi kutoka Dar es Salaam, sasa sijui maana yake nini. Ndio maana Mikataba haieleweki kama alivyosema Mheshimiwa Musalika hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo, hotuba imezungumzia sana Mererani. Yule Mzee aliyegundua madini haya, Waziri anasema, alipokuwa Naibu walimpa fedha, walimpa shilingi 50,000/=.

**MBUNGE FULANI:** Eeeh!

**MHE. STEPHEN M. KAHUMBI:** Shilingi 50,000/=. Je, shilingi 50,000/= ni sawa na ugunduzi huo. Leo hii tunabaki tunagombea: "Ooh, mnatia nembo ya Afrika Kusini." Hii nembo iliyogundua madini hayo, shilingi 50,000/= kweli! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile, hawa watu wanaochimba madini hayo wanapotosha *history!* Hawamtambui yeye, wanamtambua sijui Harijuu sijui Mtujuu, hivi watu wangapi waligundua!

Mheshimiwa Spika, naomba tafadhali Mheshimiwa Arcado Ntagazwa, aje aniambie ni watu wangapi waliogundua. Ni huyu Mzee Jumanne Ngoma au huyu mtu wa juu, wanayemtambua wawekezaji wa Afrika Kusini? Nafikiri ingekuwa ni vizuri tukaweka *history* sahihi, tukamtambua huyu mgunduzi, yupo, tena yupo hapa kwenye viwanja vya Bunge. Pengine labda tungempa mtihani Waziri, je, unaweza kumtambua…*(Kicheko)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria muda wa Mzungumzaji kumalizika)*

**MHE. STEPHEN M. KAHUMBI:** Mheshimiwa Spika, sina cha ku-*deliver*, siungi mkono hoja. *(Kicheko/Makofi)*

**MHE. FRANK M. MUSSATI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya mwisho asubuhi hii kuchangia hoja hii.

Mheshimiwa Spika, umuhimu wa nishati katika maendeleo na hasa nishati ya umeme kama alivyosema Waziri kwenye kitabu chake, ni kichocheo kikubwa cha maendeleo kiuchumi na kijamii. Ninachoshangaa ni kwamba, huo umuhimu unaonekana katika maeneo fulani tu, maeneo mengine umuhimu huo hauonekani! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, labda nikufahamishe tu kwamba, katika Mkoa wa Kigoma miezi ya masika, yaani mwezi wa tatu na wa nne, wavuvi wanavua samaki wengi sana. Lakini kwa sababu hakuna namna ya kuwa-*process* ili wasiharibike na ili bei isiteremke, jioni inabidi yakodiwe malori yawachukue wale samaki kwenda kuwatupa barabara ya Kasulu. Malori kama 10 au 15 hivi yanajazwa samaki kwenda kutupa porini wakati wenzetu wa Tabora ukiendelea mpaka Dar es Salaam wanakula samaki wa kupigwa *brush!* Samaki anakaa gengeni miezi mitatu/minne, lakini ili aonekane kama amefika jana, wanamwagia mawese kidogo na kupiga *brush! (Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, umeme unasaidia kijamii. Katika Wilaya za Kasulu na Kibondo tumejenga nyumba nzuri sana za matofali ya kuchoma. Nadhani Mheshimiwa Waziri Mkuu alipofanya ziara huko aliona. Sasa, fikiria umejenga nyumba yako nzuri hivyo, jioni badala ya kugusa ukuta ili uwashe taa, unakwenda na kibatari na ni nchi hiyo hiyo ambayo unaambiwa sehemu nyingine wanapelekewa umeme Vijijini!

Katika kitabu cha hotuba ya Waziri wameandika kwamba, zaidi ya Vijiji 90 katika kipindi cha mwaka 2002 - 2003 wamepata umeme, lakini katika Wilaya ya Kasulu na hasa Makao Makuu ya Wilaya hiyo iliyoanza mwaka 1920 iko gizani kwa miaka 83 iliyopita! Wilaya ya Kibondo iliyoanza mwaka 1943 iko gizani kwa miaka 60!

**MBUNGE FULANI:** *Ooooooh, it's a shame!*

**MHE. FRANK M. MUSSATI:** Wilaya ya Kigoma ambayo iko Makao Makuu ya Mkoa ina umeme wa mgao. Pamoja na kwamba maji yako mengi, sisi huko bado tunaendelea na mgao kama miaka ile ambapo maji yalipungua! Wilaya ya Kigoma na Mji wa Kigoma wenyewe hauna umeme wa uhakika.

Sasa nauliza, tunaposema Tanzania tunaendelea kwa pamoja, tunaendeleaje! Ni kwa vipande vipande? Yaani wengine wanapelekewa umeme Vijijini, wengine Makao Makuu ya Mkoa hayana umeme wa uhakika, Makao Makuu ya Wilaya ndio kabisa, tunaendeleaje! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilidhania tunaendelea kwa pamoja, kwamba ni Tanzania moja, kabla hatujafikiria kupeleka umeme Vijijini tumalizie kwanza Makao Makuu ya Wilaya yapate umeme. Ni vigezo gani vinatumika kupeleka umeme Makao Makuu ya Wilaya?

Mheshimiwa Spika, Wilaya zilizoanza sasa hivi ndio zinapewa kipaumbele kabla ya Wilaya kongwe kama za Kasulu na Kibondo au tunafanyaje? Napenda Mheshimiwa Waziri katika majumuisho anieleze kwamba Wilaya yangu ya Kasulu ya 1919 kwa nini haina umeme mpaka leo miaka 83 iliyopita? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Kigoma umewekwa kwenye eneo la *Export Processing Zone(EPZ)* tangu mwaka 2001, lakini hiyo *Export Processing* inafanyikaje bila umeme? Tunaambiwa kwamba ni vyema kusafirisha mazao yaliyosindikwa, unayasindikaje? Unayasindika kwa kuyatwanga kwenye kinu au unafanyaje. *(Kicheko/Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Waambie!

**MHE. FRANK M. MUSSATI:** Mheshimiwa Spika, itakuwaje Mkoa huu umeingizwa kwenye *EPZ* wakati hauna umeme? Serikali imechukua hatua gani za kuwavutia wawekezaji kwenda Mkoa wa Kigoma? Utawavutiaje bila kuweka umeme kwanza? Lakini kila siku tunaambiwa tu kwamba Kigoma iko kwenye *Export Processing Zone!* Kivipi, wakati hakuna hatua zozote zinazochukuliwa! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukisoma kitabu hiki cha hotuba ya Mheshimiwa Waziri hakuna hata panapoonyesha kwamba labda Mkoa wa Kigoma utakuwa umeunganishwa na gridi ya Taifa ifikapo mwaka fulani. Afadhali mwaka jana, Waziri alisema mwaka 2004, lakini mwaka huu *to be on the safe side* ameona akae kimya kabisa! *(Kicheko)*

Namwomba Mheshimiwa Waziri katika majumuisho, atwambie *time frame,* Mkoa huu wa Kigoma utaunganishwa na gridi ya Taifa ifikapo mwaka gani?

Pia akumbuke kwamba, Mheshimiwa Rais alivyoenda Kigoma kuomba kura mwaka 2000 alituambia wazi kabisa kwamba mwaka 2005 kwa vyovyote vile na hasa kwa Wilaya ya Kasulu kuwa: “Kabla umeme haujawashwa Masasi, utakuwa umewashwa Kasulu.” Lakini naamini Masasi umeshawashwa, Kasulu hakuna hata mpango, ni miaka 83 ya giza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali kwa kweli ichukue hatua za makusudi. Mkoa wa Kigoma siyo kila mara tu tunapelekewa vitu vibaya, kama kambi za wakimbizi zipo 11. Vitu vizuri kama umeme, tunaambiwa ni gharama kubwa kupeleka umeme Kigoma, lakini vitu vya ovyo ovyo tunaambiwa peleka Kigoma, kwa nini iwe hivyo? *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hizo shilingi bilioni 2.5 zinazolipwa kwa *IPTL* kila mwezi kwa Mkataba wa ovyo ovyo zingeweza zikapeleka umeme katika Mkoa wa Kigoma, kwa mfano katika mwaka mzima ni Shilingi bilioni 30. Kwa Mkoa wa Kigoma sidhani kama tunahitaji fedha nyingi zaidi ya hizo kuunganisha umeme.

Mheshimiwa Spika, umeme sasa utafika Urambo na utafika Kahama. Ni rahisi kuunganisha kutoka Urambo kupeleka Kigoma au kutoka Kahama kwenda Kigoma. Lakini isiwe kila mwaka tunaambiwa tu kwamba, labda mipango, labda mipango, labda mipango. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaomba basi Mkoa wa Kigoma uunganishwe na gridi ya Taifa mapema iwezekanavyo. Kama itashindikana, *TANESCO* walishafanya utafiti wakagundua kwamba umeme unaweza kupatikana kutoka Mto Malagarasi. Serikali ifanye bidii basi kwa kutumia Mto Malagarasi ili Mkoa wa Kigoma tupate umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumekuwa tukiambiwa kwamba tunaweza kupata umeme kutoka Burundi, lakini tunajua wazi kwamba Burundi ni nchi ambayo ina matatizo, kwa hiyo, kupata umeme kutoka huko itakuwa shida. Basi uangaliwe uwezekano wa kupata umeme kutoka nchi nyingine kama Uganda au Zambia kama wenzetu wa Mkoa wa Kagera na Mkoa wa Rukwa walivyopata ili na sisi tufaidi. Jamani hili Taifa tumelitumikia sana, sisi tuna-*host* wakimbizi wengi, kwa takwimu za mpaka tarehe 31 Mei mwaka huu 2003, tuna wakimbizi 560,000 kutoka Burundi na Kongo katika Mkoa wa Kigoma. Tunalipwa nini kwa kuwa-*host* watu wa namna hiyo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata vitu hivi vya kawaida ambavyo ni stahili ya Watanzania na hasa Wananchi wa Mkoa wa Kigoma hatupati mpaka tupige kelele. Kila mahali kuna umeme isipokuwa Mkoa wa Kigoma, kwa nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie kwa kuiomba Serikali itekeleze azma yake ya kuwakopesha wachimbaji wadogo wa madini. Katika Jimbo langu, hatuna madini kama almasi au dhahabu na kadhalika, lakini sisi tunachimba chokaa.

Sasa uchimbaji wetu ni ule ule wa mwaka 1947 tangu walivyokuwa wanachimba kwa kutumia koleo, mpaka leo ni koleo hivyo hivyo. Kwa kweli hawa wachimbaji wanastahili kupewa nyenzo za kisasa,

waweze kupewa mikopo, waweze kusafirisha hii chokaa ili waweze kuyafikia masoko ambayo yataweza kuwasaidia kuondokana na umaskini.

Mheshimiwa Spika, kuunga mkono ni kuunga mkono, naomba kuunga mkono hoja hii ingawa kwa shingo upande. Ahsante sana. *(Kicheko/Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tumefikia mwisho wa kikao cha asubuhi. Katika kuwapanga wachangiaji nilijitahidi kuangalia pande zote mbili za Muungano na jinsia, lakini bado wamebaki wengi, sina la kufanya. Wanne wafuatao ndio watakaochangia mchana mpaka kufikia saa 12.00 jioni, Mheshimiwa Ali Machano Mussa, Mheshimiwa Felix Mrema, Mheshimiwa Getrude Mongella na Mheshimiwa Ismail Iwvatta.

Baada ya hapo, sasa nasitisha Shughuli za Bunge hadi saa 11.00 jioni.

*(Saa 06.54 Mchana Bunge lilifungwa mpaka Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Anne S. Makinda) Alikalia Kiti*

**MHE. ALI MACHANO MUSSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya ya kwanza jioni hii ya kuchangia katika hoja iliyo mbele yetu. Kabla ya kuongea mengi nafikiri kwanza, nimwombe Mwenyezi Mungu, anipe uwezo wa kuwa na busara nzuri za kusema na hekima. Lakini pia baada ya hayo nitangulie kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, pamoja na Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Watendaji wote wa Wizara hii, kwa kukamilisha hotuba nzuri ya Wizara yao, niseme nawapongeza kidogo. *(Makofi)*

Pia kwa sababu mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Uwekezaji na Biashara, sina budi kumpongeza Mwenyekiti wangu, Mheshimiwa William Shellukindo, kwa hotuba yake hii ambayo ameitoa asubuhi na sina budi kusema nakubaliana nayo kwa sababu wakati wa kujadili nilishiriki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri pamoja na kuwapongeza na kukubaliana nao, nisipoteze muda niendelee katika mchango wangu ambao nimeukusudia. Lakini pia kama kawaida yangu, nitajaribu kusema maneno machache ambayo hayatakuwa ya kurudia rudia. Kama itatokea hivyo, naomba unione kuwa nimefanya kosa la kibinadamu na inaweza ikatokea. *(Makofi)*

Kwanza kabisa, mchango wangu napenda kusema kuwa sitazungumzia sana hotuba ya Mheshimiwa Waziri, kwa sababu naona vipengele vyake vingi vinaonekana vimekidhi haja. Lakini pamoja na kukidhi haja, hotuba hii kama wenzangu wanavyosema kwamba mtandao umefanya kazi vizuri sana kuanzia jana, kuna simu nyingi tumezipokea kutoka sehemu kadhaa. Simu hizo ni kutoka Majimboni mwetu. Majimbo yenyewe hasa ya kutoka Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa masikitiko makubwa tu wananchi wa Majimbo ya Zanzibar, wametuambia kwamba, juzi kulikuwa na maandamano ya hapa na pale ya wananchi ambao wamepata matatizo ya kukatiwa umeme. Hili tatizo lipo na hakuna ambaye halijui. Sasa kwanza nitangulie kuwapa pole wananchi wote wa Zanzibar, ambao wamepata tatizo hili, najua kwamba, pamoja na watoto wangu, wapiga kura wangu na wanachama wote wa CCM na wanachama wengine wa vyama vingine. Kwa hiyo, nawapa pole wananchi wa Zanzibar ambao wamepatwa na tatizo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, inaonekana tatizo hili la kukatiwa kwa umeme lipo, nafikiri kama sikosei, niseme kwamba, limeandaliwa. Kwa nini nasema limeandaliwa? Kwa sababu kuna vigezo vinavyoonekana kuwa mazungumzo yalivyo sababu za kukatiwa umeme Zanzibar ni kwamba, kuna deni. Lakini nakataa kwamba hakuna deni kwa kipindi hiki kutokana na makubaliano ambayo yamepitishwa namna ya kulipa deni hili. Lakini kwa masikitiko makubwa ni kwamba, hakuna ambaye hajui kama kulikuwa kuna mgogoro katika baadhi ya benki. *(Makofi)*

Kwa bahati nzuri Shirika la Umeme Zanzibar, limejaribu kulipa deni lake kama walivyokubaliana mnamo tarehe 30 Juni, 2003. Labda niseme tu kwamba, makubaliano yalivyozungumzwa Zanzibar ilipe shilingi milioni mia tano, kwa bahati nzuri Shirika la Umeme Zanzibar linakusanya shilingi milioni 420 na limelipa hizo, *VAT* inalipa mara mbili. Lakini wakati huo huo imehakikisha kwamba, imelipa na nina ushahidi wa kwamba tarehe 30 Juni, 2003 imelipa kwa kutumia *Cheque* Namba 222438 ya shilingi milioni 69,997,000/=, tarehe hiyo hiyo imelipa kwa kutumia *Cheque* Namba 222437 ya shilingi milioni 174,993,000/= vile vile. Tarehe 30 Juni, 2003 hiyo hiyo imelipa kwa kutumia *Cheque* Namba 222436 ya shilingi milioni 174,993,000/=. Tatizo limejitokeza kutokana na matatizo ya mtandao *Cheque* Namba 222436 iliyokuwa na jumla ya shilingi 174,993,000/= ililipwa kwa kutumia *TT* ya tarehe 17 Julai, 2003 ambayo ndiyo imeleta matatizo. *(Makofi)*

Lakini kwa masikitiko makubwa ni kwamba, ilikuwa hili si tatizo la Shirika la Umeme Zanzibar, hili lilikuwa ni tatizo la kibenki. Tukiangalia kwa upande mwingine, kama unadaiwa na unakubali kwamba unadaiwa umeanza kulipa, kwa nini upewe hukumu kama hii? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa masikitiko makubwa ni kwamba, uhusiano uliokuwepo baina ya Tanzania Bara na Tanzania Visiwani, ni uhusiano ambao tunausema hapa wa kindugu. Lakini undugu huu umekuwa siyo undugu wa kufaana. Kwa sababu kama ukiangalia ni kwamba, Tanzania tunadaiwa na Mataifa mbalimbali na hatujasikia kitendo kama hiki cha kukata umeme au kutoa adhabu ya aina yoyote. Ni jambo la kushangaza kwamba, Zanzibar imelipa kiasi kikubwa kilichobakia ni kidogo kabisa kitu ambacho mpaka *cheque* zinaonekana kwamba, tayari zimefika benki, hapakuwa na sababu ya kukatiwa umeme. *(Makofi)*

Leo imetupotezea muda Wabunge wengi tunajadili suala la kukatiwa kwa umeme Zanzibar, kitu ambacho ilikuwa nafasi hii tuitumie kujadili masuala mengine. Sasa tunachangia hili kwa masikitiko makubwa kwa kuona kwamba, Wazanzibari wamedhalilishwa. Nafikiri kwa sauti ndogo kabisa ningemwomba Mheshimiwa Waziri, kabla hatujamaliza kikao hiki aiombe radhi Zanzibar. *(Makofi)*

Tukiangalia ni kwamba, Shirika la *TANESCO* ambalo liko Tanzania Bara na Shirika la Umeme Zanzibar, vyombo hivi vyote vinaongozwa na Chama Tawala, Chama cha Mapinduzi na kinategemea kuingia hapa tena kwa kishindo kwa idadi kubwa ya Wabunge. Hivi unategemea wananchi ambao wamechukia kule Zanzibar kutokana na athari ambazo wamezipata tunajiweka katika nafasi gani? Hili ni tatizo kubwa. Sasa nafikiri si wakati muafaka wa kukaa kwenye Kikao cha Bunge na kujadili masuala ya siasa na siyo wakati mzuri wa kuweza kuangalia makosa yalikuwa ya nani. Lakini haya ya juu juu tu inafaa kuona kwamba, Shirika la Umeme *TANESCO* limeikatia Serikali ya Mapinduzi yote kuanzia hospitali ambako kuna watoto wachanga, kuna wajawazito, kuna walemavu ambao tayari kwa bahati mbaya wanafanyiwa matibabu ambayo ilikuwa yawasaidie lakini yameleta matatizo. *(Makofi)*

Kama hili jambo la kusikitisha na linaonekana kwamba malipo yalikuwa yapo na watu wamepata muda wa kuzungumza ndiyo niliposema kwamba, limeandaliwa kwa makusudi. Mimi nasema kwa mara ya mwisho Mheshimiwa Waziri, ufanye kama inavyowezekana sikuombi, lakini ningekutanabaisha tu kwamba, ili kuyafanya mambo yawe madogo madogo si vibaya anayetenda kosa kukubali kosa na ukaweza kuomba radhi ni suala ambalo la kiungwana kabisa. Haya yalikuwa mawazo yangu binafsi na pia ilikuwa niwasilishe kwa kujua wananchi wa Zanzibar wameathirika kiasi gani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo ni kwamba, hatupendi kuchokonoa mambo, lakini Zanzibar inawategemea ndugu zao na ndugu zao wanawategemea ndugu zao wa Zanzibar. Tusiyakumbushe mambo mengine ambayo yanaweza kuleta matatizo. Kwa hiyo, tufikie mahali tuone kwamba, kuna uwezekano wa mambo haya kuyazungumza na kama inaonekana labda wazungumzaji wanahisi kwamba, hakuna posho au vitu vingine, wachaguliwe watu ambao hawapendi posho na wanao uwezo wa kuyazungumza yakamalizika katika hali ya busara kabisa. Mimi lisifikie mbali kutokana na tatizo hili, limeeleweka hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie suala la *TANESCO,* ambavyo inadhalilisha wananchi. Masuala ya *TANESCO* yanaonekana kwamba, yanadhalilisha wananchi. Ninayo kumbukumbu moja ipo hapa hapa Dodoma, kuna nyumba ambayo imevunjwa. Nyumba hii nikiwaeleza wananchi

wengine wanaweza kuifahamu ipo karibu na Hoteli ya *DM Annex Dodoma.* Nyumba imevunjwa muda wa mwezi mmoja, lakini bado bili ya shilingi 50,000/= inapelekwa. Ni jambo la kujiuliza kama nyumba imevunjwa haipo kabisa lakini bili ya shilingi 50,000/= kila mwezi inapelekwa, je, bili hii inatoka wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi sikupenda nizungumze masuala mengi yanayohusiana na mambo ya *TANESCO,* lakini hata hivyo inaonekana kwamba, kitendo hiki cha kudhalilisha inaonekana kimezoeleka katika shirika hili. Nafikiri imeeleweka. (Makofi)

Suala lingine linalohusiana na mambo ya *TANESCO* ni tatizo la urasimu wakati mtu unaomba kuungiwa umeme. Hili suala silizungumzii kwamba labda liko Zanzibar, nalizungumzia kwa hapa hapa Mjini Dodoma. Ni kwamba kama una nyumba yako ya kuishi au ya kufanyia biashara, wengi wetu mtakubali kwamba, unaweza ukaomba kuungiwa umeme, matokeo yake unaweza ukamaliza miezi mitano au sita bado hujapata huduma hiyo. Hivi kweli Shirika hilo kama linafanya kazi zake vizuri kuna sababu gani kama kuna mteja anahitaji umeme na akachukua muda wote huo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hiyo yote inathibitisha kuwa shirika hili lina matatizo. Kama lina matatizo namwomba Mwenyekiti wangu tufanye mipango ya makusudi baada ya kulitembelea naomba tena turejee tena kulitembelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii lakini naomba marekebisho yafanyike. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. FELIX C. MREMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili na mimi nichangie machache katika hoja hii ya Waziri wa Nishati na Madini. Pili, nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, kwa hotuba yake ya Bajeti nzuri, pamoja na Naibu wake na safu nzima ya uongozi wa Wizara yake. Nimtoe wasiwasi kwamba, naunga mkono hoja yake kwa asilimia mia kwa mia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nitakuwa na machache tu ya kusema na nitayaelekeza kwenye Sekta ya Madini. Sekta hii ya madini ina umuhimu wa pekee katika Jimbo langu, siyo tu kwa wakazi wa Manispaa ya Arusha, bali kwa uchumi wa Manispaa ya Arusha. Uhai wa Merelani ni uhai wa Arusha, kilio chochote Merelani ni kilio chetu Arusha, neema yoyote inayopatikana Mererani, Manispaa ya Arusha inaneemeka pia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kifupi Merelani na Arusha ni kama mapacha. Kwa hiyo, kwetu sisi tuliposikia hotuba ya Mheshimiwa Waziri, akitangaza kusudio la Serikali la kupiga marufuku usafirishaji wa *Tanzanite* ghafi isiyokatwa na kutaka *Tanzanite* yote inayouzwa nje ya nchi iwe imekatwa, sisi pale Arusha tumepokea azma hiyo ya Serikali kwa furaha kubwa kabisa. *(Makofi)*

Lakini pamoja na furaha hiyo ambayo tuliyopokea azma hiyo ya Serikali kuna matatizo. Tatizo moja kubwa ni kwamba, azma hii ya Serikali, imechelewa mno kuja. *Tanzanite* imegundulika kuanzia mwaka 1966, miaka zaidi ya 30 imekwishapita. Katika miaka 30 kazi hii ya usafishaji, ukataji wa vito, ilikuwa inafanyika kwa asilimia 90 siyo Tanzania bali ni India na Thailand. Sisi tunavuna *Tanzanite* lakini uwezo wa kusafisha na kukata ulikuwa unajijenga na kuimarika India na Thailand. Sasa kama uongozi wa zamani ungelikuwa na *foresight* tungelianza kujenga uwezo wetu hapa ndani ya nchi wa kukata na kusafirisha *Tanzanite* toka wakati huo *Tanzanite* ilipogunduliwa kuliko kufanya kazi ya kuvuna na kusafirisha kuwapelekea India na Thailand, kazi hiyo ya ukataji na usafishaji wa *Tanzanite,* lakini hatukufanya hivyo.

Sasa imekuja miaka 35 baadaye, inabidi tujiulize je, kweli hapa tunao uwezo huo wa kuweza kufanya kazi hiyo ambayo inafanywa na miji kama Jaipur kule India, ambayo hivi sasa kuna wafanyakazi zaidi ya 15,000 wanafanya kazi ya kukata na kusafisha vito vinavyotoka Tanzania? Sisi tunao uwezo huo. Naambiwa hapa kwamba, uwezo wa kusafisha na kukata *Tanzanite* sehemu za Arusha tunao watu wasiozidi 250. Sasa niliposoma, nilijaribu kumsikiliza Mheshimiwa Waziri, katika hotuba yake kuangalia ana mikakati gani ya kuhakikisha kwamba, katika miaka hii miwili kama alivyosema yeye mwenyewe kati

ya sasa mpaka 2005, atahakikisha kwamba kazi yote ya ukataji na usafishaji wa vito itakuwa inafanyika hapa Tanzania. Sasa najiuliza hawa watu ambao wanahitaji kufanya kazi hiyo watapatikana kwa namna gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sina wasiwasi hata kidogo kwamba, Watanzania wakipewa maandalizi mazuri, ya uhakika na ya kisayansi, wanaweza kuimudu kazi hiyo bila wasiwasi wowote lakini kubwa kabisa hapa ni yale maandalizi ya kuwaandalia hawa Watanzania kuifanya kazi hiyo. Kazi hiyo, kutoka namba 250 ambao wako hivi sasa ambao hawa watakaoweza kufanya kazi yote ya kusafisha na kukata vito Tanzania ambayo wanahitajika zaidi ya 5,000, lazima mkakati kamambe uwepo wa kuwaandalia Watanzania kufanya hiyo. Sasa mimi nina wasiwasi kwamba, sasa hivi hatuonekani kama tuna mkakati kamambe wa kushughulikia kazi hiyo kubwa ambayo tunaitaka tuibebe sisi hapa. Kwa hiyo, ombi langu kwa Waziri ni kwamba, hiyo azma yake katika miaka miwili ijayo ya kuhakikisha kwamba, tunaweza kubeba hiyo ionekane kweli safari hii siyo maneno tena bali tunaazimia kujiondoa kwenye hii aibu ya kuzalisha na kupeleka India vito vyetu kwa ajili ya kusafisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinachonitia wasiwasi zaidi, niligusia lile suala la *Tanzanite* ilivyogunduliwa mwaka 1966, lakini kuna utata kidogo pale. Waziri aliwahi kutuambia kwamba, *Tanzanite* hiyo iligunduliwa na Mswahili mwenzetu, Ndugu Jumanne Ngoma, mwaka 1966. Lakini nimeona jarida lingine linasema hadithi nyingine. Jarida hili linaitwa *African Legacy* linamilikiwa na hawa wenye Hoteli hizi za *Legacy Resorts and Hotel International,* ambayo moja ya hoteli wanazomiliki ni hii ya *Royal Palm Hotel.* Sasa kuna *article* moja kule ndani wanasema eti aliyegundua *Tanzanite* ni Mgoa mmoja anaitwa Manuel D'Souza mwaka 1967. Yeye aligundua hiyo alifletewa na Mmasai mwenzangu. Sasa sijui kama Mmasai hakugundua hiyo ndiyo huyu Manuel D'Souza amegundua? Anayetambuliwa ndiyo huyu Emmanuel De-Souza, lakini Mmasai mwenzangu anasema ni Mmasai tu mmoja. Huyu Mmasai sisi tunamjua anaitwa Titus Mollel, sasa huyo hapewi nafasi yake. *(Makofi)*

Aanachosema kwenye jarida hilo ni kwamba, huyo aliyegundua kumpelekea *President* wa *Tiffany and Company International.* Hiyo ni *company* kubwa kule Marekani, inayofanya kazi ya kuuza vito pamoja na vitu vingine. Sasa walipoifanyia tathmini wakaona kwamba, lile jiwe lilopelekwa linaitwa *Zoisite*, sasa hawakutaka kulipa jina hilo la *Zoisite,* kwa sababu lilikuwa linafanafana kidogo na *Suicide*. Sasa badala ya kuipa *Zoisite* ambayo inafanana na *Suicide,* wakasema afadhali tuipatie jina la mahali ambapo ilipozaliwa *Tanzanite.* Kwa hiyo, yule *President* wa *Tiffany* ndiyo akalibatiza lile jiwe kwamba hii ni *Tanzanite,* tokea wakati huo jiwe hili likaitwa *Tanzanite* na thamani yake ikaendelea kupanda mpaka hivi sasa.

Sasa hiyo ni historia, ni vizuri tuweke historia yetu iwe sawa. Sasa ni yupi? Ni huyu Jumanne Ngoma, ni huyu Mmasai mwenzangu Titus Mollel, ni huyu Manuel D'Souza. Lakini nafikiri De-Souza hayupo kwenye hiyo, ni kati ya huyo Titus Mollel, Mmasai mwenzangu na Jummane Ngoma. Lakini yote hiyo isitusumbua sana kwa sababu hawa ni Watanzania, la muhimu ni kwamba, huyo Mtanzania ambaye aligundua je, alipewa nini? Naambiwa Jumanne alipewa zawadi ya shilingi 352,000/= mwaka huo, nafikiri Mheshimiwa Arcado Ntagazwa, atatueleza ni wakati gani alipoamua kumpa Mtanzania huyo Jumanne Ngoma zawadi ya shilingi 352,000/= .

**WABUNGE FULANI:** Aliahidiwa kupewa.

**MHE. FELIX C. MREMA:** Naambiwa eti aliahidiwa kupewa, hajapewa mpaka leo. Sasa hebu atufafanulie kama ni kweli. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka kusema ni kwamba, hivi vito vya *Tanzanite* ina mwisho wake. Wanasema pamoja na kwamba tumegundua toka mwaka 1966 miaka karibu 35 imekwishapita sasa, kuna miaka mingine 15 tu, *Tanzanite* itakuwa imepotea kabisa katika dunia hii kwa mwendo wetu huu wa kuvuna kama tunavyovuna hivi sasa wa kuchanganya wakubwa na wadogo kwa pamoja. Sasa kuna umuhimu wakati huu kama ni kweli miaka 15 iliyobaki ya kuvuna *Tanzanite* katika dunia hii, tuwe na mikakati ya kuhakikisha kwamba, hawa wote ambao wanategemea *Tanzanite* hivi sasa wanaweza kuwa na maisha *after this Tanzanite.* Wengi wa hawa ambao wanategemea sasa ni vijana wadogo wanaitwa akina Apolo, wengine Manobeli, wengine Manyoka, ni vijana wa kuanzia miaka 20, 25, 30.

Miaka 15 baadaye watakuwa ni watu wazima wanaodai mengi kutoka kwenye Taifa hili. Sasa tutakuwa tumefanya mikakati ya kuhakikisha huu utajiri unaendelea kukua kwa njia ambayo itawa-*sustain* wao baada ya miaka 15 kupotea kutoka kwenye ardhi ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kurudia kama nilivyosema hapa mwanzo, watu ambao tunawategemea sana pale Arusha ni hawa wachimbaji wadogo wadogo, siyo huyu mkubwa, hawa wadogo wadogo ndiyo ambao tunawategemea pale. Utajiri wao ndiyo ambao unaonekana pale katika Manispaa yetu. Sasa ni imani yetu kwamba, tunavyoangalia miaka 15 iliyobakia, tunaweka nguvu zetu katika kuhakikisha kwamba, hiyo thamani ambayo inazidi kuongezeka na sasa hivi naambiwa thamani ya *Tanzanite* inazidi kuongezeka lakini sababu ambazo zinafanya thamani ya *Tanzanite* izidi kuongezeka moja ya sababu hizo ni kwamba, lile Shirika la *American Gem Trade Association* ilipofika Novemba, 2002 waliamua kuifanya *Tanzanite* iwe *birth stone* ya mwezi wa Desemba. Kitendo hicho ni kitendo kilichofanywa mara ya mwisho vito vimepewa mwezi, ilikuwa mwaka 1912 kwa hiyo, toka mwaka 1912 mpaka mwaka 2002 *Tanzanite* ndiyo ikapata ile heshima ya kuwa *birth stone* ya mwezi wa Desemba. Sasa pamoja na ukweli kwamba, *Tanzanite* inaisha imefanya thamani ya *Tanzanite* kuendelea kuimarika na kuwa kubwa zaidi. *(Makofi)*

Kwa hiyo, ni imani yangu kwamba, jinsi thamani hii inavyozidi kuimarika na kuwa kubwa zaidi, Serikali itakuja na mikakati ya kuhakikisha kwamba, thamani hiyo au sehemu kubwa ya thamani hiyo inakuja hapa Tanzania katika kutengeneza uwezo kuwahudumia Watanzania watakaobaki na magofu haya yanayotokana na haya machimbo ya madini. *(Makofi)*

Baada ya kusema hayo kuhusu *Tanzanite*, nirejee suala la *TANESCO*. Wenzangu wengi wamezungumza vizuri sana mambo ya *TANESCO*. Mimi sitakuwa na mengi ya kusema kwenye *TANESCO*, kuna hili suala la *IPTL* linatusumbua wote. Wanasema *fixed cost* ndio hiyo Dola milioni 2.5 kila mwezi, kwa mwaka itakuwa karibu Dola milioni 36 zinazolipwa kwa *IPTL* bila kutumika na bila kuzalisha umeme. Sasa isije tena ikachukua miaka mingine mitano kabla ya kufanikisha azma ya Serikali ya kununua mtambo huu.

Maana yake kila unavyoungojea ndio jinsi unavyoendelea kulipa na gharama inavyozidi kuwa kubwa. Hakuna sababu ya kuendelea kulipa kwa mwaka milioni 36 inayokwenda kuzama kwa huyu mwekezaji na mtambo unaendelea kuchakaa halafu uje ununue baada ya mtambo wenyewe kuchakaa. Sielewi kwa nini inakuwa ngumu sana kufanya maamuzi haya kwa wakati. Sielewi kwa nini?

Maana matatizo haya ya *IPTL* hayakuanza leo, yameanza muda mrefu kidogo uliopita. Sasa tungekuwa na *foresight* ya kuona kwamba jamani hili litatuletea tatizo, kwa hiyo tuhakikishe kwamba, tunakuwa na mikakati ya kupunguza makali ya matatizo yatakayotokea kuliko kuyangojea mpaka yatokee halafu ndio tunayashughulikia. *(Makofi)*

Mwisho, gharama ya umeme. Waziri katuelezea vizuri kabisa hapa kwamba, takwimu zake zinamwambia kwamba, gharama za umeme zinafanana fanana hapa Afrika Mashariki. Sasa mimi ...

*(Hapa kengele ililia kuashiria muda wa mzungumzaji kumalizika)*

**MHE. FELIX C. MREMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. BALOZI GETRUDE I. MONGELLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii na mimi nichangie katika hotuba ya Waziri wa Nishati na Madini, Mheshimiwa Daniel Yona, akisaidiwa na Mheshimiwa Dr. Ibrahim Msabaha. Bila kupoteza wakati, kwanza naomba niishukuru Serikali ya Tanzania, inayoongozwa na Rais wetu Mheshmiwa Benjamin William Mkapa, kuhakikisha ya kwamba katika kipindi chake Ukerewe inapata umeme. *(Makofi)*

Pia napenda kuwakumbusha wenzangu Wana-CCM ya kwamba, CCM inaposema inaondoa kero ya wananchi, inafanya hivyo bila kubabaisha. Ahadi hii ilitolewa na Mheshimiwa Rais wakati wa kampeni pamoja na kwamba imepita zaidi ya miaka mitano tangu alipotoa hiyo kauli, lakini angalau tumefikia mwisho wa suala hili. Ukerewe ni miongoni mwa Wilaya za zamani kabisa na umeme wa Ukerewe

ulikuwemo katika mpango wa kwanza wa maendeleo wa nchi hii. Lakini kwa hapa na pale mpango huo umekuwa ukibabaishwa mpaka imefikia leo tunapata shilingi bilioni nane. Nataka nisahihishe Kitabu cha Waziri, inasomeka shilingi milioni nane, nadhani ni shilingi bilioni nane kama ilivyo katika Bajeti yenyewe. *(Makofi)*

Ningependa pia niwashukuru Mkurugenzi wa *Rural Rectification,* Mheshimiwa Yona, Mheshimiwa Msabaha, Mheshimiwa Mramba na wengine ambao katika harakati za kufuatilia umeme, nimewabughudhi kwa kiasi kikubwa kwa sababu hii haikuwa ni kazi ndogo na ninadhani tukitoka nje *we can have a glass of wine. (Makofi)*

Lakini napenda kusema kwamba, hili ni fundisho ya kwamba kiasi cha wananchi kutafuta vitu ambavyo ni vya muhimu, haipaswi mtu utembee mpaka umalize soli ya kiatu. Hii ndio kazi ambayo tumeifanya kufikisha jambo hili hapa, lakini linaonyesha tu mapungufu katika utekelezaji ya kwamba, *coordination* kati ya sekta moja na nyingine ni ngumu hata kama nia nzuri inakuwepo. Kwa hiyo, napenda niseme ya kwamba, Waziri ningependa wakati ana-*wind up* anihakikishie ya kwamba, katika ukurasa wa sita amesema mradi huu unagharamiwa na fedha za Serikali, pamoja na mkopo kutoka Serikali ya Ufalme wa Hispania na inaendelea kwamba, Serikali ya Sweden kupitia *SIDA* imeonyesha nia ya kufadhili mradi wa kusambaza umeme katika maeneo mengine ya Vijijini katika Wilaya ya Ukerewe, hususan yale ambayo hayatagharamiwa na mkopo wa Serikali ya Ufalme wa Hispania.

Ninachotaka kuhakikishiwa hasa ni pale ambapo amesema kwamba, mpango wa maandalizi umekamilika, utekelezaji wake utaanza mara baada ya taratibu za kumpata Mshauri. Hii ni *catch-phrase*, tunaweza tena tukatumia miaka mingine 50 kutafuta mshauri. Kwa hiyo, nataka niwe na uhakika ya kwamba, hiki kitatokea *immediately* na hasa baada ya kuzingatia tamko la Waziri, alipokuwa anafungua umeme katika ufunguzi wa umeme wa Geita, ambapo ilisemekana kwamba, umeme huo utapatikana Oktoba, 2004. Utakuwa unawaka katika Wilaya ya Ukerewe na jambo hili likarudiwa na Makamu wa Rais, alipokuwa anatembelea Wilaya ya Ukerewe. Kwa hiyo, nataka tu niwe na uhakika ya kwamba, kuna *scheme of work* ambayo inaonesha hatua kwa hatua ni nini kinafanyika tutakapomaliza Bunge na hatua ya mwisho ya kuwasha umeme huo katika mwezi Oktoba, ili tena tusije tukaambizana, kwa sababu zisizozuilika, ikawa vile ikawa vile. Tumesubiri vya kutosha tangu mwaka 1964 na inaelekea kwamba, hatutaweza kusubiri tena na suala la umeme katika Wilaya ya Ukerewe limekuwa la kisiasa, kuna watu ambao kura zao zimekuwa zikipungua kutokana na suala hili la umeme. Kwa hiyo, naomba hili lichukuliwe *very seriously. (Makofi)*

Baada ya kusema hivyo, ningependa suala la umeme lichukuliwe *serious* pia katika maeneo mengine ambayo hayajapata umeme. Kwa matatizo tuliyoyapata Ukerewe, uchumi wetu umedumaa kutokana na kutokuwa na umeme. Matunda yamekuwa yakioza, samaki tumekuwa tukilanguliwa kwa sababu hatuna njia ya kuhifadhi samaki wala kusindika kwa sababu hakuna umeme. Akina mama wamepoteza maisha yao katika uzazi kwa sababu inakuwa ni vigumu kuwahudumia, kuwafanyi *operation* kwa kibatari. Nimeshaona kwa macho yangu Daktari anatumia kandili kumfanyia *operation* mama ambaye amepata matatizo. Akina mama hao mara nyingi wanaishia katika kupata kitu kinaitwa *VVF,* ambacho ni kitu hatari sana kinachomfanya mama huyu afike mahali apate ulemavu wa kudumu kwa sababu hakuhudumiwa haraka.

Nimemwona kijana mmoja aliyepaswa kukatwa mguu kwa sababu aliangukiwa na mti na hakuweza kuhudumiwa kwa sababu hakuna *X-Ray* Ukerewe kwa kukosekana kwa umeme na jenereta zinapokuwepo haziwezi kutosheleza mahitaji. Mimi najua yapo mengi tu ambayo ningeweza kuyaorodhesha ambayo yameathiri maendeleo ya Wilaya ya Ukerewe na ambayo sio vizuri na Wilaya nyingine ambazo hazijapata umeme kama vile Urambo na mahali pengine, wakakosa kupata umeme wakapitia matatizo tuliyoyapitia sisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa pia nizungumzie suala la *solar energy.* Hili pia kama Wilaya ya Ukerewe tuko kwenye Ikweta, *straight on the equator,* jua lipo wakati wote na ingewezekana kabisa kwa mradi huu wa Mwanza, Ukerewe nayo ikawekwa ili kusaidia ukaushaji wa nafaka na ukaushaji wa samaki kwa sababu itakuwa vigumu kuweza kukidhi mahitaji yote kwa kutumia umeme tu.

Jambo lingine ambalo ningependa nilizungumzie ni kwamba, Sekta nyingine basi, kwa sababu umeme unaingia Ukerewe Oktoba, 2004, zianze kujiandaa kutusaidia kama vile Wizara ya Viwanda kuhakikisha kwamba, wanatusaidia katika kukuza viwanda na tuna eneo dogo la ardhi. Kwa hiyo, ukombozi wetu wa kuondoa umaskini utategemea sana viwanda ambavyo vitatumia mali ghafi kama vile matunda, samaki, mpunga, viazi, kahawa na vitu vingine ambavyo vinapatikana katika Wilaya hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ningependa tu kwa sababu nimeamua kusema kwa kifupi na hasa kwa sababu ya furaha niliyonayo, nimeyasema haya tu kuboresha na kuwaunga mkono hawa wenzetu ambao pamoja na matatizo yote yaliyokuwepo, wamejitahidi kutufikisha hapa ambapo tumefika. Lakini kuna moja ambalo nataka tu nilitolee maoni kama mwanasiasa mkongwe. Hili suala la madini linatupa *pressure.* Tunalizungumza lakini hakuna kitu ambacho kimefanyiwa utaratibu wa kuondoa hii kero. Nadhani kero sio lazima ziwe tu ndani ya wananchi na nje ya Bunge. Suala likishakuwa ni kero ndani ya Bunge linavunja umoja wetu, linadhoofisha hata kwa Chama cha Mapinduzi, tunaposimama kuilalamikia Serikali yao ambayo tumeiweka madarakani sisi wenyewe, linadhoofisha uwezo wetu wa kukijenga Chama na kupambana na ubabaishaji wa watu wengine wasio ndani ya CCM. Kwa hiyo, nadhani kwa kuwa suala hili la madini mradi limelalamikiwa muda mrefu, ni vyema basi Serikali yetu ikalitazama kwa makini. Kwanza, napendekeza kwamba, migodi mipya isimame mpaka tumalize hii kero. *(Makofi)*

Ya pili, tutafute *formula* ya kugawana mali hizi za Taifa. Tatu, tufuate mifano ya nchi nyingine kama Botswana, wenyewe wanagawana *60 percent* na *40 percent* na bado wanaitoza kodi. Kwa nini tusifanye hivyo na sisi tukaondoa umaskini? Kwa hiyo, mahali pa kujifunza ni huko, papo, twende tukajifunze tuangalie. Kama hakuna lingine, *there is no hidden agenda. (Makofi)*

Pia, masuala ya kusomba udongo mpaka na mifupa ya Wasukuma ndani yake inakwenda Japan, lisitishwe kwa sababu udongo huu hauko tu na dhahabu, una mifupa ya babu zetu, wakwe zangu wanabebwa kupelekwa Japan. Lisitishwe mpaka tupate ufumbuzi wa suala hili. *(Makofi)*

Pia, ningeomba ya kwamba, afadhali madini haya tumekaa nayo hayakutuumiza, kama hatuna *formula* basi tukae nayo hivyo hivyo mpaka tutakapopata *formula*. Mimi nimetembelea maeneo haya wakati niko kwenye Idara ya Huduma za Umma ya Chama cha Mapinduzi. Nilikuwa nasikitika, ni heri uwe maskini na madini yako kuliko utakapofika kuwa maskini na madini hatuna na ardhi imeharibiwa. *(Kicheko/Makofi)*

Lakini mwisho napendekeza na hii ni kwa sababu tu nimechelewa nilikuwa kwetu kule *UK* nikachelewa kufika hapa mapema, ningekuwa nimejiandaa zaidi ningelitoa vizuri zaidi. Lakini ukiangalia katika Kanuni zetu, Kanuni ya nne 104 kifungu cha kwanza kinasema: “Kamati Teule yaweza kuundwa na Bunge kwa madhumuni maalum kwa hoja mahususi itakayotolewa kwa ajili hiyo na kuafikiwa.” Mimi nadhani wakati umefika wa kuunda Kamati Teule kuangalia suala hili tulimalize, tuyahusishe mawazo ya Serikali, mawazo ya wananchi, mawazo ya Wabunge, tumalize suala hili tuishi kwa amani.

Hii amani tunayoimba kila siku itakuja kuumizwa kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge mmoja, anakwenda kiongozi watu hawapigi makofi kwa sababu tu ya madini, kwa nini sisi tukae tunachokoana macho?

Kwa hiyo, Kamati Teule ifikiriwe kuundwa, Wabunge waende wakatazame kwa *interest* ya nchi hii tulimalize tufunge hiyo *agenda* tuendelee na mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda tena kusema naunga mkono hoja na ninawapongeza sana na mwezi Oktoba, 2004 wote karibuni Ukerewe, tutawasha umeme usiku na mchana kuhakikisha ya kwamba, kila mtu anajua tuna umeme. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

**MHE. ISMAIL J. R. IWVATTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii ya mwisho ya upendeleo na mimi niweze kuchangia katika hoja hii ya Wizara ya Nishati na Madini. Kwanza, naomba nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, pamoja na watumishi wote walioko katika Wizara hiyo na ninapenda niseme kwamba, naunga mkono hoja hii ya Wizara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili nisije nikaishiwa na muda, mimi nilikuwa nataka nizungumzie masuala ya umeme kidogo katika Wilaya ya Manyoni na hususan katika Jimbo langu la Uchaguzi. Kwanza, naomba nianze kwa kumshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini. Nakumbuka mwaka 2001 na 2002 alitembelea Wilaya ya Manyoni na alitembelea sehemu mbalimbali katika Wilaya yetu ya Manyoni hasa zile ambazo zilikuwa zina mahitaji ya kupelekewa umeme na zile ambazo zilikuwa zinajihusisha na machimbo ya madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, alipofika, tatizo moja tulilomwambia Mheshimiwa Naibu Waziri ni kwamba, umeme katika Wilaya ya Manyoni uliingia mwaka 1999. Lakini bahati mbaya huu umeme ulipokuwa umeletwa, haukukamilishwa katika Vitongoji vyote. Ulijengwa tu katika baadhi ya maeneo. Kwa sababu ya uchache wa vifaa, maeneo mengine hayakuweza kupata umeme. Sasa nitolee mfano kwa upande wa Itigi. Kwa upande wa Itigi, wananchi wa Itigi walitoa mchango wao wa nguvu pamoja na kujichangisha kutoa pesa kwa ajili ya kuchimba mashimo, pamoja na kufyeka njia ya kujenga njia ya umeme kutoka Mkiwa mpaka Itigi na hili lilifanywa na wananchi wa Itigi wote. Lakini wakati unaletwa umeme, umejengwa mpaka maeneo fulani tu.

Sasa watu wanauliza swali na hasa unapokuwa na mkutano, wanakwambia Mheshimiwa Mbunge, wakati wa kuleta umeme ulituhamasisha sisi wote hapa na tulijitolea nguvu zetu tukaenda tukachimba mashimo, wengine tulifyeka na wengine tulitoa fedha zetu kwa ajili ya kulipa wale watu waliokuwa wanachimba mashimo. Lakini mbona huu umeme umefikishwa maeneo fulani tu, wengine hatujafikishiwa? Sasa hilo ndio swali. Mheshimiwa Naibu Waziri, alipokuja tulimweleza na alisema kuwa alikuwa ameagiza hili lishughulikiwe. Lakini napenda kumweleza kwamba, mpaka hivi sasa halijashughulikiwa. *(Makofi)*

Sasa hili limekuwa na tatizo lingine kwamba, kumekuwa na masharti magumu ya watu wa *TANESCO* kama mtu yuko mbali na *line* ilipoishia, anatakiwa achangie gharama ya ujenzi wa nguzo, kama ni nguzo moja ama nguzo mbili na hizi nguzo zina gharama kubwa. Sasa kama gharama ya kuunganisha labda Sh.110,000/=, inamchukua mtu mwaka mmoja kukusanya hiyo fedha kwa ajili ya kuunganishiwa umeme, sembuse hiyo ya kulipia nguzo? Sasa mimi nilikuwa naomba pamoja na kwamba, lengo ni kulifanya hili Shirika lijiendeshe kibiashara, lakini kwa utaratibu huu kwa wananchi wa Vijijini ambao vipato vyao viko chini, itakuwa ni vigumu. Tulikuwa tunaomba hili suala litazamwe upya, ikiwezekana *TANESCO* wapeleke zile nguzo na katika kupeleka nguzo hii inawezesha Shirika kupata wateja wengi. Kwa hiyo, nilikuwa naomba hili liangaliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni kwamba, wananchi wa Mgandu walikuwa wameomba kupelekewa umeme na bahati nzuri Mheshimiwa Naibu Waziri, alifika mpaka kule na juzi juzi hapa nilikuwa nimeulizwa swali Bungeni juu ya Shirika la Umeme kupeleka umeme Mgandu lakini bahati mbaya nilikuwa katika safari nyingine ya kikazi. Lakini jibu lililotolewa ni kwamba, kwa sasa hivi Shirika halina fedha, Serikali itakapopata uwezo itafanya na mimi nakubaliana, sina matatizo. Lakini nilikuwa nashauri kwamba, kama inawezekana kwa nini basi hii kazi isingekuwa inafanywa kidogo kidogo?

Lakini pamoja na kuifanya kidogo kidogo, nina uhakika kabisa wananchi wa Jimboni kwangu wakiweza kushirikishwa, wapo tayari kutoa mchango wao kwa ajili ya kusafisha njia pamoja na kuchimba mashimo na huo unaweza kuwa ni mchango mzuri kwa upande wa Shirika la *TANESCO*.

Lakini katika suala la kupeleka umeme katika Mkoa wa Singida, wakati tunaanza kuomba kuletewa umeme mwaka 1994 kati ya Iramba na Manyoni, Manyoni tuliambiwa kwamba sisi kwetu ilikuwa *economically not viable* kupelekewa umeme. Kwa hiyo, waliona kwanza wapeleke Iramba. Lakini hivi sasa baada ya kupeleka umeme Manyoni Mjini na Itigi, kumekuwa na mapato mengi kuliko Iramba. Lakini mpaka hivi leo tunavyozungumza Iramba bado wanaendelea kupelekewa umeme na huko Iramba kwenyewe unapelekwa upande mmoja wa Magharibi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Msindai kwa upande wake wa Jimbo la Manyoni Mashariki, amekuwa akiuliza na amekuwa akiahidiwa muda mrefu mpaka hivi leo hajapelekewa umeme. Hivi huko Iramba Magharibi kuna nini? Tulikuwa tunaomba huu umeme basi upelekwe na katika Vijiji vingine vya Mkoa wa Singida. Juzi juzi Mheshimiwa Missanga, alikuwa analalamikia upande wa Shule ya Sekondari ya Ihanja na pale ni

karibu sana kutoka Puma. Nafikiri hata kilomita 15 hazifiki. Lakini mpaka leo hawajapelekewa umeme. Sasa tulikuwa tunaomba hili Shirika liangalie uwezekano wa kupeleka umeme katika maeneo mengine pia ya Vijijini ambako umeme unahitajika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia nilikuwa naomba nizungumzie kuhusu Sekta ya Madini. Katika uchimbaji wa madini kumekuwa na tatizo la uharibifu wa mazingira. Nikitolea mfano katika Wilaya ya Manyoni, mwaka 1991 na 1992 tulikuwa na machimbo ya dhahabu katika eneo moja linaitwa Iluma. Hivi leo ukienda Iluma inabidi uwe mwangalifu sana kama unakwenda kutembea kule, kwa sababu wachimbaji wamechimba, wameacha mashimo kama yalivyo na hii inaonyesha ni hatari kwamba, ukienda hovyo unaweza ukapoteza maisha yako.

Lakini vile vile hali kama hii ya kuwa na mashimo ambayo hayajafukiwa, inatufanya tusiwe na matumizi na ardhi ambayo ina mashimo kama haya, huwezi ukaitumia, huwezi ukalima shamba na huwezi ukafanya shughuli nyingine kwa sababu ni hatari. Sasa mimi nilikuwa naomba niulize Wizara ya Madini kwamba, tuna Kanuni ama sheria inayosema kwamba, mtu anayechimba mashimo, baada ya kuchimba anatakiwa ayafukie, lakini mbona haya hayafukiliwi? Hivi hatuna kitengo ambacho kina kazi ya kufuatilia kuona kwamba haya mashimo yanafukiliwa baada ya wachimbaji kumaliza kazi yao? Hao wachimbaji wenyewe wana wajibu gani baada ya kumaliza kuchimba? *(Makofi)*

Mimi nilikuwa nafikiri, kama hii ipo katika taratibu na kanuni, walikuwa na wajibu wa kuhakikisha kwamba, wanafukia haya mashimo, lakini ukienda hayajafukiwa. Hili lipo vile vile hata katika machimbo ya *Gemstone* pale Itigi Mjini. Ukienda pale kuna mashimo watu wamechimba wamechukua *Gemstone* na wameacha mashimo kama yalivyo. Sasa nilikuwa naomba Wizara kama ina kitengo ambacho kinafuatilia kuona haya mashimo yanafukiwa, basi mimi naomba walifanye hilo kuliko kuacha ardhi inabaki na mashimo, hamuwezi mkaitumia, inaleta hatari, inaweza ikahatarisha maisha ya watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ni hili suala mrahaba au mrabaha.

**MBUNGE FULANI:** Mrabaha

**MHE. ISMAIL J. R. IWVATTA:** Lakini nisingependa niseme Msabaha kama yule bwana mwingine aliyesema asubuhi. (Kicheko)

Sasa Mheshimiwa Musalika, alikuwa ametolea mfano hapa juu ya uzalishaji wa dhahabu. Ilionekana kwamba, wenzetu wa Afrika ya Kusini wanazalisha kwa gharama kubwa zaidi ukilinganisha na hapa Tanzania. Sasa kwa utamaduni ambao umekwishajengeka katika nchi hii ya Tanzania hasa kwa usimamizi wa Rais wetu, Mheshimiwa William Benjamin Mkapa, kumekuwa na utaratibu wa kuwahusisha wadau.

Hivi hawa wachimbaji wa dhahabu wakiitwa pamoja na wadau wengine, tukakaa tukajaribu kuzungumzia uwezekano wa kuongeza hii asilimia ya mrabaha, hivi kuna ugumu?

Mimi nafikiri hili linawezekana. Kwa sababu limeshapigiwa kelele kwa muda mrefu, mimi nafikiri haina haja ya kulifumbia macho ama kulizibia masikio. Mimi nilikuwa naiomba Serikali iitishe Mkutano wa hawa wachimbaji na wadau wengine wazungumze na mimi ninaamini kabisa hili halitakuwa na ugumu.

Halitakuwa na ugumu kabisa na kama ikiwezekana basi iongezwe gharama. Kama kuna wengine wanafikia asilimia tano, kwa nini sisi tunakatazwa tusifikie asilimia tano? Mimi nafikiri inawezekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii. Naomba kurudia kusema kwamba, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. MBARUK MWANDORO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi ya yote niliyochangia kwa kauli, ningependa kuongeza kuchangia kama ifuatavyo:-

Kwanza, umeme kukatikatika, hata zile sehemu chache zilizo na umeme katika Jimbo la Mkinga, umeme huu hukatika katika mara nyingi sana, mara nyingine hata kwa muda wa siku tano mfululizo. Zaidi ya kero kwa jumla kwa wananchi, hasara na athari kubwa sana na athari nyingi zinapatikana hasa kwa vile kukatwa huko kunafanyika bila ya taarifa za awali . Hasara nyingi inapatikana kwa mali za wananchi binafsi, shughuli za uzalishaji mali, huduma za afya na kadhalika. Baya zaidi ni kwamba, hamna fidia na wala hakuna dalili za hatua thabiti za kurekebisha dosari hii kubwa.

Pili, zaidi ya kubadili muundo wa *TANESCO,* naamini hatua za kuondoa ukiritimba *(monopoly)* na kuipa ushindani, *TANESCO* inaweza kusaidia kupunguza bei ya umeme na kuboresha huduma. Kwa nini kampuni na wananchi binafsi wanaopenda kujiwekea umeme kwa matumizi yao (hata ya *standby*), wanalazimika kutoa ada kwa *TANESCO?* Nashauri Serikali iondoe ukiritimba huu kwa *TANESCO.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri kwamba, sera ya kusafisha *(Value Addition),* madini kama vile ilivyoamuliwa kwa *Tanzanite,* iendelee kwa madini mengine vile vile ili ajira iongezeke na thamani ya fedha za kigeni tunazopata kwa mauzo ya nje iweze kuongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza kwamba, leseni za machimbo madogo madogo ya madini zisipewe kwa wageni ili kuwapa fursa wananchi kufaidika na shughuli ndogo za uchjimbaji madini ambazo hazihitaji mtaji mkubwa, teknolojia nzito na utaalam wa hali ya juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Serikali iendeleze shughuli zake za uhimili kwa wananchi kwa kuongeza huduma za ugani, mafunzo, taarifa za masoko na ama kuunda Mfuko wa kuwaendeleza wawekezaji wadogo wadogo katika sekta hii au kuwatafutia nafuu za kibenki katika kuendeleza na kukuza uchimbaji na biashara ya madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutazama upya mikataba na wawekezaji, pawepo na hatua za makusudi za kuhakikisha kwamba, nchi (Wananchi na Serikali) wanafaidika zaidi katika kugawana mapato na wawekezaji kama vile ilivyo kwa nchi zinazozalisha mafuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mara nyingine tena naunga mkono hoja asilimia 100 na kuitakia Wizara mafanikio mema.

**MHE. EDGAR D. MAOKOLA-MAJOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini. Pamoja na hayo ninaomba Mheshimiwa Waziri, anieleze Mradi wa Umeme wa Nachingwea Mjini - Nkonjela hadi Mnero Misheni Hospitali utaanza lini. Mradi huo uliwekwa kwenye Bajeti ya Shirika la *TANESCO* mwaka wa fedha 2001/2002.

Zaidi ya maelezo ninaiomba Wizara ifuatilie Mradi huu ili uweze kuanza bila kuchelewa.

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Maoni yangu ni yafuatayo:-

Kwenye Fungu la Sita ukurasa wa tatu wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri (ya Bajeti 2003/2004), amesema kuwa Wizara yake inafanya maandalizi ya kuanzisha *Rural Energy Agency* na *Rural Energy Fund.* Sawa, lakini ni muda sasa wanatueleza habari ya maandalizi. Tunataka Bajeti ijayo vyombo hivyo viwili viwe vimeanza kazi. Ili usambazaji umeme vijijini sasa ufanyike kikweli kweli.

Katika Wilaya ya Kongwa tuna mahitaji makubwa ya usambazaji umeme ambayo tumeyasemea sana na naomba niyasemee tena na naomba majibu ya Wizara kimaandishi.

(i) Tunaomba Vijiji vya Chae, Hogoro, Songambele, Mkoka, Matongolo na Norini, vipewe *line* moja ya umeme kutokea pale *NARCO* Kongwa, urefu wa *line* hii hauzidi km 20. *Consumption* ya umeme ya vijiji hivi itazidi *consumption* ya Makao Makuu ya Wilaya nyingi tu hapa nchini. Itakapoanza programu ya umeme vijijini katika Mkoa wa Dodoma, eneo hili lipewe kipaumbele kwa vile linao wananchi wakulima wazuri, wenye *tractors*, malori, shule za sekondari na kadhalika.

(ii) Kupeleka *line* ya umeme Kongwa Sekondari, eneo la Ugogoni pale Kongwa Mjini na maeneo mengine ya Mji wa Kongwa. Ofisi ya *TANESCO* Kongwa ni mpya (kutokea Mpwapwa) bado haipewi mafungu ya kufanya kazi tajwa hapo juu, kwa nini? Kazi hii ni ya ndani ya Shirika *(TANESCO),* haihitajhi fedha nyingi, kwa nini haifanyiki ndilo jambo tunaloshangaa.

(iii) Kulikuwa na mradi uliokuwa kwenye *advanced stage* wa kupeleka umeme Hemba Hemba kutokea kutoka Pandambili. Mradi huo umesimama kwa sasa, kwa nini? Tunaomba mradi huu uendelezwe.

(iv) Kijiji cha Ndurugumi (km 8 kutoka Kibaigwa) wanayo *generator* kubwa ambayo haijawahi kutumika *for years*. Mashine hiyo walipewa na Serikali ya Awamu ya Kwanza na nguzo na Nyaya zikasambazwa kijiji kizima na zipo hadi leo hii. Wananchi wanaomba kuunganishwa na umeme wa Gridi na *TANESCO* wachukue ile *generator* wapeleke watakako. Naomba Meneja *TANESCO* Mkoa, aende huko Ndurugumi kuona jambo hili tunaloliongelea na waniandikie *reaction* yao ili nami niwasiliane na wananchi juu ya *position* ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja na nawatakia kazi njema.

**MHE. REMIDIUS E. KISSASSI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kusema kuwa naiunga mkono hoja hii. Pamoja na hayo napenda kuchangia machache kama ifuatavyo:-

(i) Pamoja na maelezo mazuri ya Mheshimiwa Waziri kuhusu gharama za umeme wa *TANESCO*, bado kila mtumiaji anasema gharama za umeme Tanzania ni kubwa. Nashauri utafiti wa kutosha ufanywe ili gharama hizi ziwe nafuu zaidi na hasa kupunguza kodi.

(ii) Mfuko wa kusambaza umeme vijijini bado haujawa *very effective.* Nashauri mfuko huu uimarishwe maalum kama vile mfuko wa barabara na usambae Tanzania Bara na Zanzibar, hivi sasa umeme ni muhimu sio anasa tena.

(iii) Suala la umeme mbadala hasa *Solar Energy* ni la muhimu sana hasa katika yale maeneo ya vijiji ambavyo umeme wa gridi utachelewa. Tatizo kubwa ni kodi kubwa kwa vifaa hivi vya kuzalisha na kusambazia umeme wa njia. Hii inafanya bei ya vyombo/zana hizi kuwa kubwa mno.

(iv) Kukatiwa umeme Zanzibar, pamoja na yote yaliyosemwa napenda kumtanabaisha Mheshimiwa Waziri kuwa, sio watu wengi wanapenda Muungano wetu, hivyo wapo ambao wangependa kuuchokonoa ili kuutia kasoro. Hivyo, namshauri Mheshimiwa Waziri, awe mwangalifu sana na viongozi wanaosimamia masuala haya ya umeme na mengineyo ili busara zaidi zitumike kwa pande zote mbili za Muungano.

Baada ya kusema hayo, napenda kuunga tena mkono hoja hii . Ahsante.

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Nzega ilipata umeme wa *generator* kutoka Shinyanga 1981. Iliunganishwa na Gridi ya Taifa miaka ya 1985/86. Lakini kutokana na Sera ni vijiji vitatu tu kati ya 142 vilivyopata nishati hiyo. Kwa nini *TANESCO* isiwe inajenga umeme wenye moto wa kawaida wakati wa Gridi ya Taifa inapita?

Ni lini vijiji vilivyo katika Wilaya zenye umeme vitapata umeme kwa mfano, Bukene, Mwangoye, Ndala, Puge na Mwamala?

Ndala kuna *TTC*, Hospitali na ni *center* ya Tarafa ya Puge. Kwa sasa wanachuo na Hospital wanatumia *generator*. Je, Wizara ipo tayari kuungana nao ili itumike kwa wananchi wote?

Tumejaliwa Tanzania kuwa na raslimali ya madini kwa mfano, dhahabu, almasi, vito vya thamani na kadhalika. Ukilinganisha mrahaba tunaotoza Tanzania na nchi za Kiafrika mfano *South Africa,* Namibia, Botswana na kadhalika, 3% kwa *gold* na 5% kwa *diamond.* Mbona sisi tupo chini kuliko wenzetu? Kodi gani zingine tunazotoza? *Tax Holiday* katika nchi zingine zinatofauti gani? Ni fedha kiasi gani zinazopatikana kwa kusafirisha mchanga?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na Serikali kuwa na kigugumizi juu ya *Royalties* naomba tutoe *retention* kwenye Halmashauri husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, madini na mafuta ni mambo ya Muungano. Watanzania tumesikitishwa na tamko la SMZ, juu ya mafuta ya Zanzibar. Hapa Mheshimiwa Waziri, utoe taarifa rasmi kufafanua hili mbona sisi mnatubana kila kitu tunakitumia wote? Ni wapi Wizara ya Nishati na Madini imeweka akiba ya madini kwa ajili ya kizazi kijacho?

**MHE. IRENEUS N. NGWATURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja iliyo mbele ya Bunge lako Tukufu.

Awali ya yote naomba nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, pamoja na Watendaji ambao wameshiriki katika kuandaa hotuba hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sitaunga mkono hoja hadi nitakapopata maelezo yanayoeleweka kwa wananchi wa Mbinga kuhusu suala la umeme wa Mbinga hususan Mji wa Mbinga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mji wa Mbinga umekuwa Makao Makuu ya Wilaya zaidi ya miaka arobaini, Mji huo una viwanda vikubwa vitatu, viwili vya kukoboa kahawa na kusaga ngano,vyote vinatumia *generator* za dizeli, yapo mabenki, hospitali mashule, viwanda vidogo vidogo, kila asasi hutumia *generator* yake. Hali hii imefanya uzalishaji kuwa wa gharama kubwa sana, kwa mfano, gharama ya kukoboa kilo moja ya kahawa ni Sh. 64/= ukilinganisha na Kiwanda cha Moshi, Mkoa Kilimanjaro ni Sh.22/= kwa kilo. Tofauti hii inatokana na gharama za umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ieleweke kuwa watu wa Mbinga hawahitaji umeme kwa ajili ya starehe, wanahitaji umeme kwa ajili ya uzalishaji. Wananchi wa Mbinga wanasikitishwa sana na Wizara yako kwa kutotilia maanani juhudi zao, wanashangaa kwa nini wilaya zilizoanzishwa juzi na hata vijiji ambavyo havina hata nyumba za kudumu vinapewa vipaumbele badala ya kuweka vipaumbele katika maeneo yenye *potential* ya kuchangia Pato la Taifa.

Moja ya mambo yanayowafanya watu wa Mbinga wakose imani na Wizara hii ni tendo linalojirudia kuwa Mji wa Mbinga una umeme wa ushirika pamoja na Wilaya ya Urambo, sasa inakuwaje Mji wa Urambo unapata umeme wa gridi na kuuacha Mji Mkongwe wa Mbinga.

Naamini Wizara yako inapendelea baadhi ya sehemu na kuwa-*marginalised* wananchi wa Mbinga. Naamini hali hii inajitokeza kwa sababu Watendaji wako hawatembelei na kuona hali ilivyo. Pamoja na hayo namshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kutembelea Mji wa Mbinga na kuona hali halisi. Vile vile Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kutembelea na kuhakikisha kuwa Mji wa Mbinga hauna umeme. Lakini jambo la kushangaza ni pale ilipotolewa taarifa kwenye Mkutano Mkuu wa CCM uliofanyika mwaka 2002 kuwa Wilaya ya Mbinga ina umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya mambo ninayoiomba Wizara hii ni kusema ukweli katika Bunge lako Tukufu kuwa, Mbinga hakuna umeme na wananchi wajue hatua zinazochukuliwa.

**MHE. HEZEKIAH N. CHIBULUNJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana juhudi zinazofanywa na Wizara katika zoezi la usambazaji umeme nchini.- Wananchi wa Vijiji vya Buigiri, Chinangali II na *Wilunze Camp* vilivyoko kwenye Jimbo langu, wanashukuru sana kwa kupatiwa umeme kwenye vijiji hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wananchi wa Vijiji vya Manchali na Chalinze ambavyo viko kwenye njia panda ya barabara iendayo Mpwapwa, wanaomba Wizara itazame ukamilishaji wa mpango wa kupatiwa umeme. Vijiji hivi viwili ndivyo vikubwa kwa eneo na kwa wingi wa watu. Pia ndiko kwenye shule za msingi na eneo la *Mission* ya *Roman Catholic.* Makisio yalikwishaandaliwa na *TANESCO* Mkoa na hivi sasa wananchi wanasubiri kwa hamu kubwa sana kupatiwa umeme kwenye vijiji hivi ambavyo viko njiani kwenda njia ya umeme uendao Mpwapwa na Kongwa.

Kwa ujumla tuna imani kubwa kuwa endapo vijiji hivi viwili vitapatiwa umeme, maisha ya wananchi yataboreka zaidi kiuchumi. Kwenye eneo la vijiji hivi ndiko kuna mradi wa umwagiliaji kwenye Bwawa la Chalinze (Ikowa).

Naomba kuwasilisha ombi hili kwa niaba ya wananchi hao na niombe iwapo Mheshimiwa Waziri, utapata muda utembelee eneo la vijiji hivi, ili wananchi wapate fursa ya kubadilishana nawe mawazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja 100%.

**MHE. OMAR S. KWAANGW':** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa *Electricity Four Babati,* ambao sasa unapaswa kuwa kwenye awamu ya pili unatazamiwa kupeleka umeme kutoka Magugu (Babati) hadi Minjingu, ambapo kuna Kiwanda cha *Phosphate (MIPCO).* Kwa kuwa katika utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya 2000 na ile ya 1995, Serikali imekuwa ikitoa ahadi kuwa vijiji vyote vitakavyopitiwa na njia ya miradi ya umeme vitapatiwa umeme. Hivyo basi, nakumbushia kuwa vijiji vya Mwada (Mbuyu wa Jerumani) na Vilima Vitatu (Mdori) na Kijiji cha Minjingu ambako *MIPCO* ipo vipatiwe umeme wakati wa utekelezaji wa mradi huo. Maelezo yanayohusu vijiji hivyo niliyawakilisha *TANESCO* kwa Meneja wa Umeme Vijijini, Ndugu Massawe. Ni imani yangu kuwa maombi haya yatazingatiwa ili kuharakisha maendeleo Wilayani Babati.

Katika hotuba ya Waziri, kwa kawaida huonyeshwa katika majedwali, vijiji ambavyo vinapaswa kupatiwa umeme. Lakini safari hii inaonyesha wazi kuwa Serikali sasa haitilii mkazo suala la umeme vijijini. Jambo hili ni tatizo kubwa sana katika utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi. Kwenye hotuba ya Waziri (uk. 4 fungu la 7), imeonyeshwa tu kwamba, vijiji 90 vimepatiwa umeme mwaka 2002/2003, lakini hakuna maelezo yoyote ya vijiji vipi vitapatiwa 2003/2004. Aidha, kwenye hotuba ya Kamati ya Uwekezaji na Biashara, imeelezwa kuwa utafiti wa umeme vijijini umefanywa lakini matokeo ya utafiti hayajulikani na kwamba Wizara imeunda Mfuko Maalum wa Nishati Vijijini *(Rural Energy Fund).* Naomba kufahamu matokeo ya utafiti huu na mipango ya Serikali ya kupeleka umeme vijijini.

Pamoja na maelezo hayo, naunga mkono hoja na kwamba nitapenda kufahamu jinsi ambavyo vijiji nilivyovitaja chini ya *Electricity Four* vitakavyopatiwa umeme.

**MHE. HALIMENSHI K. R. MAYONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja. Tatizo letu kwa Mkoa wa Kigoma halina ufumbuzi na mwelekeo wa kupata umeme wa gridi. Jambo hili linaleta kero kubwa sana kwa wananchi wa Mkoa huo. Je, Wizara ina mpango wa kupata umeme wa gridi kutoka wapi au tutaendelea na majenereta?

Viongozi wakuu wa Selrikali, wote katika ziara zao Mkoani Kigoma, hiyo ndiyo sala ya wananchi. Mpaka sasa hakuna jibu sahihi. Mawaziri wote tangu mimi nimechaguliwa kuwa Mbunge wao 1990 mpaka leo 2003, hakuna Waziri wala Naibu Waziri aliyewahi kufika Mkoani Kigoma. Jambo hili siyo zuri hata kidogo. Mkoa wa Kigoma hauwezi kuondokana na umaskini kama suala hili litaendelea kuachwa bila ya kupata umeme wa haraka. Tunaomba umeme Kigoma, ili tuweze kuondokana na umaskini wa muda mrefu.

**MHE. YUSSUF KOMBO JUMA:** Nashukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia katika Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa masikitiko makubwa, napenda kutoa malalamiko yangu kwa Wizara hii kutokana na suala la Zanzibar kukatiwa umeme. Ninachotaka kusema ni kwamba, Zanzibar ni nchi na ina Serikali kamili, itakuwaje mnyonge kama kijiji au Wizara miongoni mwa Wizara za nchi yenu

(Tanzania Bara)? Namwomba Waziri hiki atueleze kwa umakini sana vinginevyo litazidisha yale matatizo ambayo tumekuwa tukisema siku zote lakini huwa hamuyasikii.

Kuhusu umeme ni Serikali ndio iliyokubaliana na Serikali ya Zanzibar inakuwaje Makaburu waliikatia umeme Serikali? Je, ingelikuwa nyie mngekubali au kwa kuwa mmetenda nyinyi mnasema sio suala kubwa na halina tatizo?

Mimi naona ni tatizo kubwa na sio kwenye umeme tu, bali hata kwenye muungano wetu.

Kuhusu malipo ya umeme kwa nini Zanzibar inalipa *VAT* mara mbili? Kwa sababu tunapolipa kwenye gridi huwa tunalipa *VAT* na tunapoleta malipo kutoka kwa wateja pia tunalipa *VAT,* je, huu sio udhaifu kwenye masuala ya Muungano na kuhusu tatizo hilo tumekuwa tukizungumza mara kwa mara lakini inaonekana kuna dharau na inaonesha kuwa ni lengo maalum ili tushindwe kupata huduma hii kutoka upande mmoja wa Muungano.

Napenda kusema kuwa suala la *petrolium* ni suala amabalo ni la nyongeza kwenye mambo ya msingi ya Muungano na kuna wasiwasi kuwa limeingizwa kinyemela hivyo, nashauri kwanza turudi kwa wananchi tupate ridhaa yao vinginevyo italeta matatizo makubwa. Zanzibar ni nchi ambayo haina vyanzo vya kutosha vya kujiwezesha kiuchumi na sasa inafikiriwa labda kuna mafuta, sasa nafikiri ni vyama tufike mahali tuwe na imani ya kuona kwamba nao Zanzibar wanajiwezesha kiuchumi. Kwa sababu Tanzania Bara kuna vyanzo vingi sana vya kiuchumi na ndio maana Zanzibar kwa sasa haina hata maamuzi ya kujipangia mambo madodo madogo na kufikia mizozo ya mara kwa mara, ambayo husababishwa na njaa, ukosefu wa ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, nashauri Waziri muhusika, ashauriane na Mawaziri wenziwe, Katiba yetu irudishwe kwa wananchi ili tuifanyie mabadiliko kwa maslahi ya Watanzania wote wapenda Muungano.

**MHE. HENRY D. SHEKIFFU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba hii ni nzuri na maelezo yametolewa kwa ufasaha sana, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia yafuatayo: Kwa kuwa suala la uchimbaji madini ni nyeti na mikataba iliyowekwa inaashiria matatizo kwa vizazi vijavyo; je, Serikali imeanza utaratibu wa kuangalia upya mikataba iliyowekwa? Mfano ni tatizo la upelekaji mchanga Japan hivi Serikali inajibu vipi masuala ya wananchi kama vile ujazaji wa mahandaki yatakayo achwa baada ya kuuza mchanga nje ya nchi? Je, vizazi vijavyo havitapata shida ya mahandaki hayo kudidimia na mazingira kuwa ya kutisha sana? Nashauri Serikali iangalie utaratibu wa kujaza mahandaki hayo kabla ya wawekezaji kuondoka. Kama kuna makubaliano yoyote ya kulinda mazingira, basi wananchi waelemishwe.

Je, Serikali inatamka nini juu ya umeme vijijini? *TANESCO* kwa sasa haionyeshi umaskini katika kusambaza umeme vijijini. Hoja ya Wizara kuanzisha kitengo au shirika la umeme vijijini, ni muhimu lakini ifanyiwe tathmini ya kutosha hususan kipindi hiki cha mpito. Kwa kuwa ipo miradi mingi ambayo *TANESCO* ilikwisha anzisha vijijini, Serikali itoe tamko ni hatua gani zitachukuliwa kuhakikisha miradi iliyokwisha anzishwa haisimami katika kipindi cha mpito.

Naomba miradi ya kupeleka umeme Vijiji vya Ubiri, Miegeo, Boheloi, Gare, Mlola, Ngwelo, Kwembago na kadhalika katika Jimbo langu la Lushoto, vipewe kipaumbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru.

**HON. ANTHONY M. DIALLO:** Mr. Chairman, when you look at the figures of your budget book (page 44) there's a production surge of gemstone in 1997 then a sudden drop for the rest of the proceeding years! What could be the reason behind this synergy?

Page 45, the average price of gold during 2002 was USD 330 - 345 per trolley ounce as per the gold bullion market data. The income of USD 387.2 million is far below actual sales figures for 2002. What could be the reason for this under reporting?

The contribution of the mining sector to the Community Projects is less than 4% of the taxes paid to Government and Agencies! What could be the scenerio after their Tax Holidays is over? Wouldn't be that this contribution will significantly be reduced in lieu of taxes?

Under the present tax laws and TIC Act, an investor is entitled to renew the incentives in an event a new investment/modernisation/expansion made. Though there's always a possibility that for every new investment cost is portioned separate from the existing when calculating or computing the tax returns, chances are minimal for the tax regime to capture (seperately) the actual differences between previous and new investments at the production level. This is due to the complication existing where the old and new plant/equipment are merged or intergrated into one production unit. Now with this possibility in place, do you envisage a time these investors falling into the full taxable enterprise where incentives under the TIC, the Mining Act and Tax Law are clearly favourable to the situation?

**MHE. PASCAL C. DEGERA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nichangie hotuba ya Waziri wa Nishati na Madini.

Ninachukua nafasi hii kumpongeza Waziri kwa hotuba yake nzuri, hata hivyo, ninaomba nichangie maeneo machache yafuatayo:-

(i) Ninaipongeza Wizara na Serikali kwa ujumla kwa kutekeleza Mradi wa *Electricity IV*, kwa ufanisi mkubwa. Chini ya mradi huu vijiji vinane Wilayani Kondoa vilipatiwa umeme vikiwemo Vijiji vya Mondo, Kelema Maziwani, Goima, Songolo, Chandama, Mrijo Juu, Mrijo Chini na Olboroti. Usambazaji huu umekuwa ni changamoto kubwa kwa maendeleo katika vijiji hivi, ujenzi wa nyumba bora umeshamiri katika vijiji vyote. Aidha, viwanda vidogo vidogo vinavyotumia umeme vimeanzishwa. Kwa ujumla umeme umekuwa ni changamoto kubwa kwa maendeleo katika vijiji hivi.

(ii) Baada ya Mradi wa *Electricity IV* kukamilika, ilikuwa ni mategemeo ya vijiji vilivyo jirani na njia ya umeme, usambazwe umeme lakini tangu mradi huu ukamilike hakuna usambazaji uliofanyika. Kwa mfano, Kijiji cha Soya Wilayani Kondoa, kilikuwa kikiahidiwa umeme lakini mpaka sasa hakijapatiwa umeme. Aidha, vijiji vifuatavyo vimeomba vipatiwe umeme, navyo ni Jenjeluse, Kelema Balai, Pongai, Waida, Sori, Mirambo, Makamaka, Hamai, Madaha, Mapango, Nkulari, Magasa, Isusumya na Songambele. Ninaomba vijiji hivi vipatiwe umeme haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kwa makusudi kabisa, itenge fedha ya kugharamia usambazaji wa umeme vijijini badala ya kutegemea uwezo wa Shirika la Umeme *(TANESCO)* peke yake. Baada ya mchango wangu huu mdogo, ninatamka kuwa ninaunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini.

**MHE. EMMANUEL E. KIPOLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mgodi wa *Kahama Mining Corporation Limited* kusafirisha mchanga kwa kutumia malori makubwa kutoka Bulyanhulu kwenda *Isaka Dry Port* si tu ni kinyume cha Sheria ya Madini Namba 5 ya mwaka 1998 na Sheria ya Barabara inayotaka matumizi ya barabara yasiwe kwa magari zaidi ya tani kumi, bali suala hili limekuwa kero kubwa kwa wananchi wanaoishi kando kando ya barabara ya Busoka - Bulyanhulu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shughuli zote zinazohusiana na madini kwa kawaida hutakiwa kabla ya kupatiwa leseni ya aina hiyo kuambatisha mpango kamambe wa kuzuia uharibifu wa mazingira na hivyo ndivyo ilivyofanyika kwa Mgodi wa *Kahama Mining Corporation Limited.* Nitumie fursa hii kuipongeza *Kahama Mining Corporation Limited,* kwa kutunza mazingira katika eneo la mgodi na ku-*observe safety regulations* zote kama vile, *Helmet, Gumboots, Reflective Jackets, Dust Masks* na kadhalika. Kwa sasa shughuli nzima ya kuchimba au ku-*process* madini hayo imekuwa *extended* kwa kusafirisha madini hayo kupitia barabara niliyoitaja hapo juu. Ni dhahiri suala zima la mazingira ni lazima lifanyiwe kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kwa fursa hii kuleta Serikalini malalamiko ya wananchi juu ya kero kubwa ya vumbi linalowakabili wakati wa shughuli ya usafirishaji wa madini hayo kati ya Bulyanhulu na Busoka umbali wa km 76. Wananchi wa Vijiji vya Kakola, Bugarama, Ilogi, Lunguya, Shilela, Segese, Masabi, Ntobo, Kalagwa, Izengwabahala, Nyambula na Busoka, wamenituma niiambie Serikali kwamba, shughuli ya kusafirisha madini kwa kutumia malori inasababisha kero kubwa ya vumbi na inatishia afya zao. Hivyo, wanataka mambo yafuatayo yafanyike: Kwanza, Serikali iikataze mara moja kampuni ya *Kahama Mining Corporation Limited,* kufanya shughuli hiyo mpaka pale tahadhari zote za kudhibiti mavumbi zitakapofanyika, kama vile kuweka lami barabara hiyo.

Pili, Serikali itoe ufafanuzi wa kina wa kifungu cha sheria kinachoruhusu biashara ya aina hiyo hapa nchini.

Tatu, Sheria ya Barabara Vijijini inayotaka uzito wa magari yanayozitumia usizidi tani 10 isimamiwe vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa haya machache, naomba tupatiwe majibu ya kina kabisa na ya kuridhisha ili hapo baadaye tuweze kuunga mkono hoja. Naomba kuwasilisha.

**MHE. PROF. HENRY R. MGOMBELO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kumpongeza Waziri wa Nishati na Madini, kwa hotuba nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mitambo ya *IPTL* inagharimu *TANESCO* fedha nyingi. Mimi nashauri kuwa Serikali ikubali pendekezo la Kamati ya Bunge ya Biashara na Uwekezaji la kununua mitambo hiyo, maana itakuwa vigumu kupunguza bei ya umeme huo wa *IPTL.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu inaweza kunufaika sana kama juhudi za makusudi zinaweza kufanywa katika kuendeleza umeme, nishati ambayo ni nyingi nchini kwetu. Nashauri Wizara hii ifanye kila linalowezekana ili kusambaza nishati hii nchini kwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa *Stigler's Gorge* chini ya *RUBADA* kama ungeendelezwa, tusingekuwa na matatizo ya uhaba wa umeme hivi sasa. Kwa kweli tungeweza kuuza nishati hii pia kwa nchi jirani kama vile Kenya, Uganda na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Waziri atueleze, ni lini Serikali itaufufua mradi huu? Sisi Wana-Tabora tunaishukuru Serikali ya CCM kwa kutuletea umeme Wilaya za Sikonge na Urambo. Kwa upande wa Urambo tunaomba Serikali ikamilishe mradi huo mapema iwezekanavyo maana wananchi wanasubiri umeme wa gridi kwa hamu sana. Naunga mkono hoja hii.

**MHE. NAZIR M. KARAMAGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kumshukuru Waziri, Mheshimiwa Daniel Yona, Naibu Waziri, Mheshimiwa Dr. Ibrahim Msabaha, Bwana Patrick Rutabanzibwa, Katibu Mkuu na Watendaji wote walio chini ya Wizara, kwa kazi yao nzito ya kuongoza Wizara yenye Sekta nyeti za Nishati na Madini kwa Taifa.

Mchango wangu utahusu umeme Vijijini. Jimbo la Bukoba Vijijini kwa kuanza na historia, suala la umeme Bukoba Vijijini lilianza miaka ya 1990. Katika mwaka wa uchaguzi wa 2000 watu wa Bukoba Vijijini maeneo ya *Ikimba Area* yenye wakazi wapatao 150,000 ndani ya Kata 13 waliahidiwa nishati ya umeme. Watekelezaji wa *TANESCO* walitumwa kwenye maeneo husika na kuanza kuorodhesha kaya ambazo zingeweza kufanya mradi uonekane unafaa. Kitendo hiki kiliwapa matumaini wananchi na wakaunga mkono Serikali kwa asilimia kubwa katika kila sera zilizotungwa. Hili suala liliendelea kufuatiliwa na Marehemu Mheshimiwa Kinyondo na kuwa *supported* na Wizara. Jinsi muda uliavyopita, watu wakaanza kuona wenzao Wilaya za jirani zikikumbwa angalau kwa kiasi fulani.

Mwaka huu wa 2003, Watendaji wa *TANESCO* wamepitia tena kwa kufanya makadirio ya gharama ya kuweka umeme kwenye maeneo hayo, *code named Katoro Project* kama ifuatavyo: Kanazi - Kafunjo Sh. 257,060,791.07/=, Kafunjo - Izimbya Sh. 286,496,460.31/= na Kafunjo - Katoro Sh. 261,201,034.77/=, jumla Sh. 794,758,286.15/=.

Jambo hili limewapa matumaini tena wananchi wa sehemu hizi lakini wako *skeptical,* kama halikuwa mbinu ya kuwahadaa. Wanachotegemea kuona ni kuwa Serikali inaweka ahadi hizo kwa vitendo. Kwa niaba ya wananchi hao, naomba Wizara itafute kokote kule ili Mradi huu uanze kutekelezwa kabla ya mwaka 2005, kipindi ambacho wanakitegemea sana kufuatia Serikali ya Mheshimiwa Benjamin William Mkapa kuwa na *reputation* ya kutimiza ahadi zake.

Nategemea kupata kwa maandishi mpango wa Serikali juu ya tatizo hili. Baada ya hayo napenda kusema, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. ABDULA S. LUTAVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie kwa kusema kwamba, tunalo tatizo la msingi katika suala zima la nishati ya umeme kwamba, umeme ni chachu muhimu kwa maendeleo ya nchi, inaelezeka vizuri tu. Lakini nashangaa sana maswali mengi hapa Bungeni yanayohusu kukatikakatika kwa umeme yanajibiwa mara zote kwa maelezo ya uchakavu wa mitambo na mfumo mzima wa usambazaji wa umeme nchini. Ajabu, kama hoja hii inafahamika tangu awali, ilikuwaje basi tukali-*address* tatizo la umeme kwa kuajiri *Management* ghali ya kigeni badala ya kushughulikia tatizo la msingi kwanza? Tunaambiwa *nonfood inflation* ilipanda mwaka 2001 kutoka asilimia 1.2 hadi 6.3 kwa maelezo ya *electricity tariff*. Kwa hiyo, mchango wa umeme katika maendeleo ya uchumi wetu ni muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kiwango kikubwa maelezo ya kusimama kwa viwanda vya korosho katika Mikoa ya Lindi na Mtwara ni gharama kubwa itokanayo na umeme usiotabirika. Kama haja ya kuboresha thamani ya mauzo yetu ya korosho nchi za nje ipo, basi dawa ni kuvifanya viwanda hivi vibangue korosho na kama tunataka kwa dhati maeneo ya Kusini yazinduke, basi na yaandaliwe mazingira yatakayovutia uwekezaji katika eneo hilo. Moja ya vivutio vikuu ni upatikanaji wa umeme unaotabirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kelele nyingi juu ya uamuzi wa awali wa Serikali kuandaa mradi wa gesi ya songosongo kwa dhamira ya kuisafirisha kuipeleka Dar es Salaam, bila kuzingatia uwezekano wa gesi hii kuzalisha umeme kutokea Kilwa kwa ajili ya Mikoa ya Kusini, leo Mheshimiwa Waziri, anataja mpango wa kutafiti uwezekano huo. Hiki ni kiini macho tu inavyoonekana. Kwa nini Serikali haikuona haja ya kukiweka kipengele hiki kwenye mkataba wa *project* hii inayosainiwa Septemba, 2003? Tumehoji jambo hili bila majibu tena katika kipindi ambacho mpango huu ungewezekana zaidi kuliko sasa. Je, hiyo *feasibility study* inayoelezwa na Waziri ikisema mradi huo sasa utakuwa ghali zaidi, Serikali ipo tayari kuendelea nao ikipuuzia ushauri huo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, inaonekana maamuzi ya Serikali yetu kuhusu utaratibu wa kusambaza nishati hii muhimu, hayazingatii kwa dhati maslahi ya Taifa hili kwa maana ya kuweka uwiano unaokubalika wa maendeleo baina ya maeneo mbalimbali nchini. Inawezekanaje umeme sasa umeshafika hadi Vijijini tena kwenye Wilaya zilizoanza juzi tu wakati maeneo mengine hata Makao Makuu ya Wilaya hayajapata huduma hiyo? Hivi umeme wa Gridi ya Taifa umeshafika hadi Musoma ikashindikana umeme huo kufika hata Lindi tu! Maelezo yake ni nini? Jambo hili pamoja na mengine yanayoonyesha ulemavu wa maamuzi katika mgao wa raslimali za Taifa yatatugawa nchi hii na maelezo ya kila siku ya ufinyu wa Bajeti yanakosa uzito. Serikali hii iwe angalifu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la madini hasa dhahabu lisipopatiwa ufumbuzi wa haraka tutalaaniwa na kizazi kijacho. Hoja hii isidhoofishwe kwa madai ya kuongezwa viwango vya mrabaha na kuugawa mrabaha huo kwenye maeneo yanakochimbwa madini hayo. Hoja ya msingi siyo hiyo, maana kama ingekuwa ni hivyo tungesema vile vile mapato yatokanayo na Bandari ya Dar es Salaam yaunufaishe Mkoa huo kwanza. Tuzungumze kwamba pawepo na mpango ndani ya Mikataba hiyo unaohusu *production sharing,* mpango ambao utatuhakikishia kuwa kila ikichimbwa, basi Tanzania itachuikua *share* yake kwanza ya dhahabu hiyo na Serikali itaendelea kutoa kodi na aina nyingine za ushuru kwa kiasi kile *(share)* anachobaki nacho mwekezaji. Hivi ndivyo ilivyo mahali pengi.

Kwa bahati mbaya, jedwali Na.10 analotuelekeza Mheshimiwa Waziri, tulisome kwenye hotuba yake liko *deceptive* kwa sababu *element* ya *production sharing* haijalinganishwa hapa. Mheshimiwa Waziri haonekani kutaka wasomaji tulifahamu na hili pia. Kuna mapungufu makubwa yanayotukosesha

(Taifa) mapato ambayo yangeharakisha jitihada za nchi hii kupambana na umaskini. Mikataba hii hasa ya dhahabu lazima ifanyiwe mapitio upya.

**MHE. KHALID S. SURU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru wewe kwa kunipa fursa hii ya kuchangia hoja hii ya Waziri wa Nishati na Madini. Pia namshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, Naibu wake, Katibu wake na Wasaidizi wake kwa maandalizi mazuri ya hoja hii. Baada ya hapo, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umeme sio mwanga tu, umeme ni maendeleo ya mara moja, maendeleo ya kilimo, viwanda, biashara, elimu, sayansi, mawasiliano, kuondoa umaskini na kadhalika. Umeme ni haki ya wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule Kondoa, umeme wa gridi uliingia mwaka 1998/99 ukitokea Babati. Kondoa ndiko ilikojengwa *substation* kwa ajili ya kusambaza umeme Kondoa Mjini na Kibaya (Kiteto). Katika njia hiyo, umeme huo umepita (nyaya) katikati ya Vijiji vifuatavyo bila kupewa umeme: Kijiji cha Puhi, Mji wa Bereko, Kijiji cha Salanka, Kijiji cha Masawi, Kijiji cha Bukulu, Kijiji cha Humai, Kijiji cha Kwadino, Kijiji cha Kolo na Kijiji cha Choka/Gubali, Wanavijiji wote hao wanalilia umeme. Wananchi hao wanasema wataendelea kuwa walinzi wa nyaya hizo mpaka lini? Wao sio binadamu? Serikali itapata dhambi kubwa kama jamii hii ya Vijiji hivyo havitapata umeme. Wapeni, ni haki yao! Kabla sijaleta dosari ya kuondoa Shilingi, Waziri anihakikishie kuvipa Vijiji hivyo umeme mwaka 2004/2005.

Mheshimiwa Mwenyekiti, njia ya kuvipatia umeme ni kurudisha umeme toka Kondoa au Bonga Babati au Galapo Babati.

Ili kuharakisha umeme Vijijini, tuongeze mbinu zaidi, tutumie mitambo midogo midogo ya umeme wa *solar*. Nasikia *solar* moja inaweza kutumiwa na kaya 300 na bei ni rahisi. Sambazeni umeme huu pia.

Mwisho, nashauri watu walipwe fidia kutokana na mimea yao wakati wa ujenzi wa njia za umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. ISSA MOHAMED SULEIMAN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wizara ijielimishe zaidi mahusiano ya asili kuhusu umeme kati ya Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar. Ukweli ni kwamba, ingawa tumebadilisha utawala, lakini utu na ubinadamu haujabadilika, ni sasa tunalazimishwa kuubadilisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Zanzibar yafuatayo yamefanyika: Miundombinu yote imegharamiwa na Zanzibar kwa 5.7 *pounds,* Zanzibar imetoa majenereta yote waliyonayo kabla ya kumaliza mradi wao na kuipa *TANESCO,* Zanzibar imeikubalia *TANESCO* kutumia miundombinu yake na kupeleka umeme katika baadhi ya maeneo ya Mkoa wa Pwani, mfano Bagamoyo, vile vile Zanzibar imestahimili kukatwa *VAT* mara mbili na hilo Wizara hii na *TANESCO* wanajua na pia Zanzibar haijapiga kelele mbali na kukatwa *VAT* mara mbili na wakati huo huo Taasisi za Muungano hazilipi *VAT* hiyo. Pamoja na hayo yote, Wizara hii ikakubali Zanzibar yote ikatiwe umeme wa deni la Shilingi milioni 174. Nasema Wizara imekubali kukatwa umeme huo, kwani imepewa taarifa na *TANESCO* wiki moja kabla kama watakata umeme na bila ya kujali utu au ubinadamu, Waziri hakumjulisha Waziri mwenzake wa Zanzibar kufanyika kwa kitendo hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani hapa ipo kasoro ya kutojali kama Zanzibar kuna Waziri na pia kutojali kama Zanzibar mahitaji ya umeme yanahitajika kwa maji, hospitali na kadhalika. Hali hii ya sasa ya kuwa na nyumba isiyo na maelewano, ni hatari. Tafadhali tueleze Zanzibar italipwa madai yake ya Shilingi milioni 62.6?

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuongelea kuhusu mafuta. Utafutaji wa mafuta ni suala la Muungano na mafuta yenyewe yanaelezwa na Katiba kama ni ya Muungano. Nilipochangia hoja ya Ofisi

ya Makamu wa Rais na kutaka suala la mafuta lisiwe la Muungano na kuna haja ya kubadilisha kwa hilo, Mheshimiwa Ntagazwa alisema: "Mabadiliko kama hayo yana utaratibu wake". Kwa kauli hiyo naomba ukubali kwamba, ipo haja ya kupeleka tamko hilo Serikalini ili huo utaratibu ufanywe. Suala hili kubaki kama lilivyo haliimarishi Muungano. Hata hivyo, Zanzibar nayo inahitaji kuwa na kilicho chake kama Bara walivyokuwa na vyao. Tanzania Bara wana madini ya aina mbalimbali ambayo ni yao peke yao.

Mwisho, suala la kupakana maeneo sio tatizo, Uarabuni wamepakana na kila mmoja anachimba mafuta yake.

**MHE. JEREMIAH J. MULYAMBATTE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Wake, Katibu Mkuu na *Management* yote kwa kupanga vizuri Bajeti ya mwaka huu wa 2003. Nasema hongera sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu ni kwamba, gharama za umeme za *IPTL* ziko juu mno kiasi kwamba, Tanzania imekuwa nchi mojawapo ya kushangaza kana kwamba tunayo mashindano ya kuzidiana, gharama za umeme ndio maendeleo ya nchi. Kumbe umeme ni nyenzo muhimu ya kuleta maendeleo katika utoaji huduma kwa jamii. Hivyo basi, gharama za umeme bora zilingane na uzalishaji wake. Hivyo hivyo, bidhaa zitokanazo na nguvu za umeme zitakuwa na bei nafuu kwa walaji. Serikali ifanye hima kuwa na mazungumzo ya namna ya kupunguza gharama za umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kupata taarifa ya mapato ya kila mgodi kwa mwaka wa fedha 2002/2003. Hii itanipa imani kuwa mali yetu ya madini inachangia Pato la Taifa letu kiasi gani. Madini yetu Tanzania ni mali ya Taifa. Mali hii hatuitumiwi vizuri ili kutuletea maendeleo hapa nchini.

Aidha, Serikali kwa suala hili haiko wazi kabisa. Kwa mfano, machimbo sita hayawahusishi Waheshimiwa Wabunge walioko kwenye maeneo ya Machimbo husika. Bulyanhulu, Bodi yake Waheshimiwa Wabunge hawakuwekwa kabisa. Nao ni Mheshimiwa Mlolwa, Mheshimiwa Kipole na Mheshimiwa Mashalla. Hawajui kinachoendelea wala faida inayotokana na machimbo hayo. Mgodi wa Lusu - Nzega Waheshimiwa Selelii na Mheshimiwa Kahumbi. Machimbo ya Geita, Waheshimiwa Wabunge watatu, Mheshimiwa Musalika, Mheshimiwa Mabina na Mheshimiwa Rwilomba, akaletwa Mjumbe nje ya Mgodi huo kuwa *Board Member.*

Machimbo ya Mara, Waheshimiwa Wabunge walizuiliwa kuingia kwenye uzinduzi wa machimbo hayo. Haya yanatia mashaka kazi ya machimbo kwani kuna usiri sana kati ya Makampuni na Serikali.

Naishauri Serikali kuwa, iundwe Tume ya kuangalia upya mikataba yote ya madini iliyosainiwa na Serikali yetu ili kuona yale mapungufu yanayojitokeza katika uendeshaji wake. Taarifa ya Tume iletwe katika Bunge ili kuonesha uwazi wake. Tume hii iwahusishe Waheshimiwa Wabunge watokao katika machimbo hayo.

Wasombaji/usombaji mchanga wetu udhibitiwe na Serikali ili *sampling* iwe ya mchanga mchache kuliko ilivyo sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama sikujibiwa hayo, mimi nasita kuunga mkono hoja hii mpaka kwanza nitakapopata maelezo ya kuridhisha. Ahsante.

**MHE. ALI SAIDI SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ilifanya Mkataba na *IPTL* kwa nia safi kabisa, lakini inaonekana kuwa azma nzima ya Serikali katika Mkataba huu imekwama. Hivyo nashauri, Serikali iangalie upya na ikibidi ivunje kabisa Mkataba huu wa *IPTL.* Serikali iwachukulie hatua za nidhamu wale wote waliohusika kwa njia moja ama nyingine kuweka saini Mkataba huu ili iwe funzo kwa wengine.

Umeme ni kitu muhimu katika maisha ya kila siku na hasa katika wakati huu wa sayansi na teknolojia. Hivyo basi, naishauri Serikali ichukue hatua za dharura katika kukabiliana na tatizo la umeme Vijijini ili wananchi wa Vijijini wao wawe na umeme wa uhakika. Kwa tatizola kuchelewesha

kuunganishiwa umeme hata baada ya kulipia, naishauri Serikali kuliagiza Shirika la *TANESCO* nchini kurekebisha tatizo hili ili wananchi waodokane na kero hii.

Pia naishauri Serikali kuliagiza Shirika la Umeme kupunguza gharama za kuunga umeme majumbani ili wananchi wengi waweze kupata umeme kwa urahisi na kwa idadi kubwa.

**MHE. SHAMSA S. MWANGUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa hongera kwa Mheshimiwa Waziri na Naibu wake, pamoja na watumishi wa Wizara yake, kwa hotuba yake nzuri ya maelezo ya kina ambayo imeniwezesha kuelewa Bajeti ya Wizara yake na ninaiunga mkono hoja hii. Napenda kuchangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeshuhudia mwenyewe jinsi wananchi wa Vijiji mbalimbali vya Tukuyu wakinufaika na matumizi ya *Biogas* kwa kuwasha taa (karabai) na pia kupikia. Hii ni teknolojia nyepesi na rahisi. Je, kwa nini Wizara haitilii maanani teknolojia hii na kusambaza aina hii ya nishati kwenye Vijiji vya wafugaji wasiohama hama kama vile wafugaji wa Mikoa ya Dodoma, Mwanza, Mbeya na kadhalika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kupongeza teknolojia hii ya kulipa umeme kadiri unavyotumia. Hii ni nzuri, haina bughudha kati ya mtumiaji na wafanyakazi (wasoma mita) wa *TANESCO,* ambao walikuwa ni kero kwa wananchi. Pia, inamsaidia mtumiaji kubana matumizi na kutumia umeme kwa uangalifu. Kwa hiyo basi, kwa nini Wizara isichukue jitihada za makusudi za kusambaza mita hizi za LUKU nchi nzima na hususan kwenye Miji Mikuu? Hii itaiokolea Shirika pesa kwa kupunguza watumishi na pia itaongeza ufanisi wa *TANESCO.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi leo hii *solar energy* bado inazungumziwa kinadharia tu. Teknolojia hii tumeanza kuisikia tangu miaka ya 1980 lakini kwa nini Serikali inakuwa ikisita kujitosa kikamilifu katika kuisambaza? Kwa wachache walionazo zikiwemo Hoteli Maarufu za Kitalii Mkoani Arusha, ni teknolojia rahisi na isiyohitaji uwekezaji mkubwa. Pia, malighafi yake ni jua ambalo liko, ni *abundant*. Ningeshauri na kutoa wito kwa Serikali ijaribu teknolojia hii kwa wananchi wetu Vijijini kwani kila mwananchi inaweza ikamfikia bila gharama kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii kuwapongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watumishi wote wa Wizara ya Nishati na Madini, kwa kazi nzuri ya usimamizi wa umeme na madini yetu Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii ilileta sera ya kuwa kila Vijiji na Wilaya, umeme utawekwa. Ni kweli gharama za uunganishaji wa umeme ni ghali lakini ningeomba umeme uwekewe utaratibu mzuri kwa awamu kuliko kusubiri fedha zote zipatikane ndipo wananchi wapewe umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi *Net Group* wanakusanya vizuri ankara za watumiaji umeme. Ni nini sasa kinasababisha umeme kukatikakatika? Hivyo basi *TANESCO* iweke fungu la kufidia wananchi wanaoharibikiwa na vifaa vya nyumbani, kwa uzembe wa *TANESCO.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, imekuwa sasa ni kitu cha kawaida vitu kuungua ovyo kwa uzembe wao. Hii kuzidi kuwaongezea umaskini kwa wale waliowekeza miradi yao kwa kutumia umeme kama friji kwa ajili ya kuuza *ice cream*, soda, vinywaji baridi, madawa kwa binadamu na wanyama, kifaa kinapoungua hakuna fidia yoyote na ni uzembe wa *TANESCO.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, umeme ni njia mojawapo ya kuwapatia Watanzania maendeleo yao, kwa kupevuka kwa kutumia *TVs,* kuona nchi zingine zinafanyaje. Bila umeme hawawezi kuona vitu hivyo. Hivyo, Wizara ifanye haraka kutekeleza mikakati waliyojiwekea kuwa ifikapo mwaka 2005 Wilaya zote ziwe na umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa Serikali ilione hili kuwa ni malalamiko kwa Watanzania wengi kutonufaika na madini yao. Je, haiwezekani sasa mitambo ya kuchekecha mchanga ikaletwa Tanzania ili tuwe na uhakika na madini yetu yanayopelekwa nje yakiwa ndani ya mchanga yasiyofahamika. Kama Serikali itawahamisha wawekezaji watatuelewa na watafanya hivyo.

Hivi sasa imekuwa ni kero kwa maeneo wanayochimba madini. Hivi wanapochimba mashimo hawawezi kufukia? Mfano pale Maganzo Shinyanga, mashimo ni mengi na ni hatari hata majambazi yanaweza kutumia kama mahali pa kujificha. Suala hili lifanyiwe kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudia tena kuunga mkono hotuba hii asilimia mia kwa mia na kuwapongeza kwa kazi nzuri wanazofanya na wapewe fedha zote walizoomba.

**MHE. SIJAMINI MOHAMMED SHAAME:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nina heshima kubwa kuchukua fursa hii ya kutoa mchango wangu kwa maandishi. Naanza kwa kuunga mkono Bajeti hii kwa asilimia mia moja.

Aidha, nataka nichukue fursa hii kumshukuru sana Waziri na wasaidizi wake wakuu, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu nawashukuru wao kwa kuandaa hotuba hii nzuri ambayo imetoa uchambuzi mzuri unaofahamika kwa kila mtu ambaye anapenda kuyaona maendeleo ya nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimeshawishika sana na namna ambavyo *TANESCO* inavyosambaza umeme wake hapa Tanzania Bara na kuwa ni Shirika pekee ambalo linauza umeme wake huko Unguja kwa muda mrefu kwa ufanisi bila ya dosari, kitendo ambacho kwa hakika kimekuwa kinaleta manufaa na maslahi yake kifedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haikutarajiwa hata siku moja kwa viongozi wa nchi hii, waliokwishafika mbele ya haki na walioko hai kuwa *TANESCO* ingeliwaza kufanya kitendo cha kudhalilishana au kuleta kiburi kwa viongozi wa Serikali zetu mbili, tukio ambalo kwa hakika lingeweza kuleta dosari kubwa katika uhai wa Muungano wa Jamhuri yetu ya Tanzania na ni lazima Serikali yetu ya Muungano kuwa macho na kutambua chanzo cha kitendo hiki ambacho kimeashiria ubabe na kuonesha kudhalilishana ndugu wawili ambao wana haki sawa ya kuishi maisha ya udugu ambao ni wa asili ya tangu na tangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuishauri Wizara hii sasa kuona umuhimu wake kwa suala la umeme unaotegemewa kutoka *TANESCO,* ambao unaendesha uhai wa uchumi kwa Zanzibar na ni vyema kuangalia hata miundombinu ya njia ya umeme uliopita baharini kwa muda maalum *(Life Span),* ambayo kwa sasa nadhani umeshakaribia kupita kama haujapita. Si vibaya kuliangalia suala hili kwa kuepusha matatizo ambayo hayatapendeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwetu Zanzibar tunalazimika kuliona suala ambalo ni budi kulieleza kwa kina zaidi kwa kutotoa *agenda* kwa wakorofi na wapinga maendeleo na wale wasiotutakia heri kwa Muungano wetu utakaodumu kwa maisha yetu yote ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuishauri Wizara hii kuanza utaratibu wa kuwafunza hawa viongozi wa *Management* ya *TANESCO,* historia na maudhui ya Muungano wa Zanzibar na Tanzania Bara pamoja na taathira inayoweza kutokea kwa kuwadhoofisha wenzetu wa Zanzibar kuonekana dhaifu na Tanzania Bara kuonekana ni wenye kumiliki na upande mwingine wa Muungano kuwa na wanunuzi tu. Si busara hata kidogo kukatiwa umeme kule Zanzibar hata kama kuna madeni ya muda wowote, kwani kule Zanzibar kuna Taasisi ambazo zinalipiwa deni la umeme na Serikali ya Muungano. Mfano Mambo ya Ulinzi, JWTZ, Polisi, Usalama wa Taifa na kadhalika. Sasa vigezo gani vimechukuliwa hata umeme huu ukakatwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaelekea wapi? Kwa kuwa suala hili Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, kwa maneno yake aliyosema kuwaeleza viongozi wa *Management* ya *TANESCO* kuwakataza wasikate umeme kwa Zanzibar na kauli yake kudharauliwa, mimi naona hiki ni kitendo cha dharau na ufedhuli ambao unaonyesha kudhoofisha uongozi wa Serikali ya Muungano wa Tanzania. Aidha, kwa

kitendo hiki, naomba Wizara ichukue hatua ya makusudi ya kutoa maelezo ya kutoka kwa *Management* ya *TANESCO* kwa nini isihusike na gharama za uharibifu uliotokea huko Zanzibar?

Mheshimiwa Mwenyekiti, si vyema kuwafanya watu wa Zanzibar kuwa na masononeko kutoka *Net Group Solution* kuwepo kwake hapa nchini, ni vyema busara ikawa ni chombo cha kuimarisha na kuinua uchumi wa Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa ukamilifu.

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hongera kwa Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri wa Wizara hii kwa mashirikiano mazuri na utendaji mzuri wa kazi. Napenda pia kupongeza wafanyakazi na wataalamu wa Wizarani kwa ufuatiliaji katika kazi zao. Kwa kuwa hotuba ni nzuri sana na ina mwelekeo wa kuwakomboa wananchi wake, napenda kuunga mkono hoja hii asilimia mia moja.

Napenda kuchangia kabisa suala la umeme Zanzibar (Deni la umeme Zanzibar). Napenda kuiomba Wizara ilifuatilie kwa kina na kwa uhakika suala la uzimwaji wa umeme Zanzibar na kulipatia ufumbuzi. Kwa kuwa nchi yetu ni ya Muungano, basi kufanyike mazungumzo ya mara kwa mara pale litokeapo tatizo la kutokulipwa kwa madeni ya umeme Zanzibar. Mimi naamini kuwa penye maelewano na ushirikiano, basi hapataharibika kitu. Ni vizuri viongozi kulifuatilia tatizo hili kwa kina ili kulipatia ufumbuzi wa haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muungano daima, ushirikiano daima. Naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. DR. THADEUS M. LUOGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, wataalamu na wafanyakazi wote wa Wizara kwa kukamilisha hotuba hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumefanya mazungumzo kadhaa na Mheshimiwa Waziri juu ya mradi wa kupeleka umeme wa Gridi Mkoa wa Ruvuma kutoka Makambako kupitia Njombe ili Tunduru, Namtumbo na Mbinga, wapate huduma hii muhimu katika shughuli za kiuchumi na kijamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri, hakuna chochote kilichosemwa juu ya mradi wa kupeleka umeme wa Gridi Songea. Mawazo hayo mazuri kwa wananchi wa Mkoa wa Ruvuma yamefia wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Mbinga, Mji wake hadi hii leo hauna umeme. Mimi pamoja na wananchi wa Mbinga, tunaamini Serikali haitaki kabisa kupeleka umeme Mbinga kwa sababu hakuna haki kwa kuwa Wilaya ya Mbinga ni Wilaya pekee nchini iko katika orodha isiyotakiwa kupata umeme. Kwa nini tumewekwa katika orodha hiyo, sisi wananchi wa Mbinga hatujui, bali Serikali inajua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tuambiwe kwa nini tunatendewa hivyo kwa kunyimwa huduma hii muhimu kwa maendeleo? Ahsante sana.

**MHE. OSCAR T. MLOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda nitoe pongezi nyingi sana kwa hotuba nzuri ya Waziri wa Nishati na Madini. Mikakati aliyoiainisha imenifanya niridhike kabisa na hoja iliyo mbele yetu. Hivyo, natangulia kusema kuwa, naunga mkono makadirio ya Wizara hii mia kwa mia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyoeleza wakati nachangia hoja ya Bajeti ya Serikali kuwa katika Jimbo langu la Morogoro Mjini, wananchi katika kuhangaika na maisha wamegundua uwepo wa madini ya dhahabu kwenye Kijiji cha Mindu na tayari walishaanza kuyachimba na kuboresha hali zao kwa kiwango cha juu sana. Bahati mbaya ugunduzi huo unakwazwa na miundombinu ya Kitaifa iliyo kwenye eneo hilo kama vile njia ya Gridi ya Taifa ya Umeme kutoka Kidatu kwenda Dar es Salaam, Barabara kuu

ya Tanzania Zambia, Bomba Kuu la Mafuta la *TAZAMA* na Bwawa la Mindu linalolisha asilimia 75 ya Wakazi wa Mji wa Morogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mara nyingine natoa ombi rasmi kwa Wizara hii kutuma watalaamu wake waje kufanya utafiti wa kina kuona mwelekeo wa mkondo huo ili dhahabu hiyo iweze kuchimbwa kwenye uelekeo ambao hautaathiri miundombinu hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Bunge lako hili nilijibiwa swali la umeme kwa Vijiji vya Konga na Bigwa. Napenda kutoa shukrani kuwa tayari Kijiji cha Bigwa umeme wa msongo wa kati umepelekwa, bado *transformer* ya kuuteremsha kufikia kiwango cha kutumika majumbani. Kwa Kijiji cha Konga ambacho kina Zahanati, muhimu sana, umeme wa msongo wa kati (33 kv) umepita kuelekea Mzumbe bila kuwanufaisha wananchi wa eneo hili. Naomba Wizara itazame kwa uzito mkubwa kabisa kuweka *transformer* pale Konga ili Zahanati na wananchi wa hapo wafaidike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hali ya kawaida, si vizuri mimi kama Mbunge, kulalamika, lakini nalazimika kuliarifu Bunge lako kuwa *transformer* inayoleta umeme nyumbani kwangu ina hitilafu ya siku nyingi. Nilishaunguliwa na vyombo mbalimbali pamoja na wakazi wenzangu wa eneo zima la *Kola 'A'* mara kadhaa. Ni ajabu kuona kuwa hata baada ya kunikatia umeme kwa makosa, lakini umeme umepita kwenye waya wa *neutral* na kuunguza dari ya nyumba yangu na *computer*. Suala hili Meneja wa *TANESCO* Mkoa wa Morogoro analifahamu na ameahidi kuibadilisha *transformer* ile.

Sikuona madai ya kufidiwa hasara niliyoipata kutokana na nafasi yangu kama kiongozi, lakini nimeumia. Hivyo, kupitia kwako ningemwomba Waziri mhusika, alishughulikie hili kwani nimevumilia vya kutosha ikiwa ni pamoja na kuwataka radhi wananchi ninaowawakilisha wasilishtaki Shirika, kwani nimeahidi kulishughulikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo machache, napenda kurudia tena kuwa, naiunga mkono hoja ya Bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini mia kwa mia.

**MHE. DR. JAMES M. WANYANCHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia. Pia, napenda kumpongeza Mheshimiwa Daniel Yona, Waziri wa Nishati na Madini, kwa hotuba yake nzuri. Vile vile, napenda kumpongeza Waziri wa Nishati na Madini, Naibu Waziri wa Nishati na Madini na wafanyakazi wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri walioifanya katika mwaka 2002/2003. Napenda kusema kwamba, naunga mkono hoja hii asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa kutoa maoni yangu kuhusu masuala yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu Bajeti ya mwaka 2001/2002, 2002/2003 na hata Bajeti ya mwaka huu 2003/2004, mradi wa kupeleka umeme Wilayani Serengeti umekuwa ukiwekwa katika Bajeti hizi ili utekelezwe. Pia Shirika la *SIDA* lilishatoa pesa za kugharamia mradi wa kupeleka umeme katika Wilaya ya Serengeti katika mwezi Februari, 2002. Ingawa mradi umekuwa unaingizwa kwenye Bajeti tangu mwaka 2001/2002 na *SIDA* ilishatoa pesa ya kusambaza au kupeleka umeme Wilayani Serengeti, haijaanza. Tunaomba Wizara ya Nishati na Madini itilie mkazo wa kuharakisha kupeleka umeme katika Wilaya ya Serengeti mapema iwezekanavyo. Naomba Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, anihakikishie kuwa kazi hiyo itaanza lini na kukamilika lini wakati atakapokuwa anatoa majumuisho ya hotuba yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka sasa Kituo cha *IPTL* hakitumiki kikamilifu kama inavyotakiwa. Katika kutembelea Kituo hicho tuliambiwa kuwa kuna miezi mingi tu ambapo Kituo hicho hakitumiki kutoa umeme na wakati huo huo Serikali inalipa Shilingi bilioni tatu kila mwezi. Hii ina maana kuwa kila Mtanzania hulipa Sh.1,000/= kwa mwezi kwa umeme ambao hakutumia. Hivyo, kwa mwaka kila mtu hapa nchini hulipa Sh.12,000/= kwa umeme ambao hakuutumia. Hii ina maana kuwa katika miaka 20 kila mtu atalipa 240,000/= kwa umeme ambao hakutumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali hii ya watu kulipia umeme wa *IPTL* bila ya kutumia ni kitu kisichokubalika. Tunaomba Serikali ilitafutie jibu suala hili na mchezo wa wananchi kulipia umeme

ambao hawautumii ukome.  Pia hatua zichukuliwe kuwawajibisha wale wote waliotia saini Mkataba huu, Serikali iwawajibishe kwani kitendo walichofanya ni kuihujumu nchi.  Vile vile, Serikali iangalie uwezekano wa kununua mtambo wa *IPTL* ili kukomesha uhujumu uchumi wa Kitaifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuvitembelea viwanda vingi hapa nchini, wamilikaji wa viwanda hivyo walilalamikia bei kubwa ya umeme.  Viwanda vingi haviwezi kuuza bidhaa zake nje ya nchi kwa sababu ya gharama kubwa ya umeme.  Tunaomba Serikali ifanye utafiti namna ya kupunguza bei za umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi ipo migodi mingi ya dhahabu hapa nchini.  Kinachoshangaza huchimbwa na kuuzwa nje na pesa zote kupelekwa nje.  Tunaomba sana tena sana Mheshimiwa Waziri, alitolee suala hili maelezo, imekuwaje Serikali yetu imeyaruhusu Mashirika ya nje na kuacha Watanzania wakifa na umaskini? Tunaomba Serikali isitishe mchezo wa kuruhusu Makampuni ya nje kuanzisha mgodi mwingine zaidi wakati Watanzania hawanufaiki nayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natumaini Mheshimiwa Waziri atayatolea maelezo masuala niliyoyasema humu wakati anatoa majumuisho ya hotuba yake leo jioni.

**MHE. MCHANDE SALIM MCHANDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza natoa shukurani zangu za dhati kwako na pili napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, kwa hotuba yake nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa nguvu ya Shirika la Umeme la *TANESCO* kujenga uwezo wa kusambaza umeme unategemea sana kuwepo fedha za ukusanyaji wa madeni ili Shirika hilo liweze kuendeleza shughuli zake vizuri.  Pia, ni vizuri kuwahamasisha wateja wao kulipa bili zao mapema ili Shirika liweze kufanya shughuli zake kwa ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninasikitishwa sana na Shirika la Umeme la *TANESCO* kulikatia umeme Shirika la Umeme la Zanzibar.  Aidha, Shirika hilo hutumia nguvu za kudai deni lake kwa Shirika la Umeme la Zanzibar, si vizuri, bali Shirika hilo litumie njia za Kiserikali kujadiliana namna Serikali ya Zanzibar inavyoweza kusaidia Shirika lake kulipa deni lake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunategemea kuwa kitendo cha kulikatia Shirika la Umeme la Zanzibar kilichofanywa na *TANESCO* hakitatokea tena.  Ahsante.

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote ikiwa ni pamoja na Watendaji wa Mashirika yaliyo chini ya Wizara hii kwa kushirikiana kuandaa na kuiwasilisha hotuba hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaelekeza mchango wangu katika maeneo yafuatayo:-

Gharama za umeme wa *IPTL,* kwa kuwa *IPTL* italazimika kubadilisha mfumo wake ili kutumia gesi mwaka 2004, Serikali ipitie upya Mkataba huo na kuelekeza nguvu katika kubadilisha maeneo yafuatayo ya Mkataba:-

(a) Kurekebisha bei za mafuta ya *DPK* zilizokubaliwa katika Mkataba ili bei hizo ziendane na bei sahihi za Soko la Dunia kwa mafuta hayo yanayotumika kuendesha mtambo huo wa umeme.

(b) Ili kuepuka bei kubwa zisizo na kikomo, Serikali iangalie ndani ya Mkataba uwezekano wa kununua *IPTL*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya Kampuni ya *BP (T) Limited* kuanza kutumia *petrol* aina ya *Unladed*, Wizara ishauri Serikali kutumia mafuta hayo kikamilifu kwa Makampuni yote ya Mafuta na kwa nchi nzima katika Soko la Dunia.  Mafuta hayo ya *Unladed* ni ya bei nafuu kuliko ya *Laded Petrol.*  Hivyo,

Makampuni yote yakitakiwa kusambaza mafuta hayo bei itashuka kutokana na kuongezeka kwa uagizaji wa shehena kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna gharama kubwa zitakazohitajika kubadilisha mfumo huo. Jambo la msingi kwa Serikali kuzingatia ni kutoa muda wa kuendelea kutumia mafuta ya *Laded Petrol* kwa muda, kwa ajili ya magari chakavu yaliyopo kwa sasa nchini na wakati huo huo kusimamisha uingizaji wa magari chakavu yaliyotengenezwa kabla ya mwaka 1993 (zaidi ya miaka kumi). Madhara ya kuendelea kutumia *Laded Petrol* ni makubwa sana hasa kwa afya ya watoto na uharibifu wa mazingira kwa moshi unaotokana na matumizi ya mafuta hayo kwa magari yetu.

Wizara ya Nishati na Madini na *TANESCO* wamekuwa wakilalamikiwa Bungeni kuhusu kutokamilishwa kwa miradi mingi Vijijini. Ni vizuri Wizara ikatoa orodha ya miradi ya aina hiyo na kuandaa utaratibu wa kuikamilisha ili kupunguza kero za wananchi. Mfano katika Wilaya ya Muheza, mradi wa kupeleka umeme toka Muheza kwenda Bombani - Tongwe na Kiwanda ulioanza zaidi ya miaka sita iliyopita hadi sasa umesimama baada ya kutekelezwa kwa asilimia karibu 50 tu hadi Kijiji cha kilomita saba na haujafika Bombani - Tongwe na Kiwanda ambako kipo Chuo cha Ufundi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sio sahihi kuacha mradi katikati hata kama fedha zilizotengwa hazikutosha. Kinachotakiwa ni kutenga fungu la nyongeza na kukamilisha mradi badala ya kuacha viporo na kero.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasikitisha pia kwa Wizara kueleza katika Bajeti na kutengewa fedha kupeleka umeme katika Vijiji (Bajeti ya Wizara hii 2000/2001), ilikuwa ipeleke umeme Vijiji vifuatavyo Wilaya ya Muheza, Kilulu, Kibanda na Sakale, lakini hadi leo 2003 Vijiji hivyo havijapelekewa umeme. Licha ya tofauti hiyo, Wizara wala *TANESCO* hazikuingiza Vijiji hivyo katika Bajeti zao za 2001/2002 wala 2002/2003 wala katika Bajeti hii ya 2003/2004.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ombi la kupatiwa umeme Shule ya Sekondari ya Songa iliyopo karibu na Kituo cha Umeme Hale, ombi ambalo lilijibiwa katika swali ndani ya Bunge mwaka 2002, pia halipo kwenye mpango wowote wa Wizara. Iwapo fedha zilizokuwa zimetengwa kwa miradi hiyo huko nyuma zilitumiwa sehemu nyingine, nashauri Wizara iweke Vijiji hivyo katika mpango wa *TANESCO* mwaka huu 2003.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Taifa linayo nia na mpango wa dhati wa kusambaza umeme Vijijini, basi ichukue hatua ya awali ya makusudi ya kupunguza gharama za kuweka *Service Line* kwa maeneo ya Vijijini kutoka Sh.105,000/= hadi Sh.55,000/=. Ni dhahiri kabisa uwezo wa Wanavijiji ni mdogo na wengi wameshindwa licha ya kuwa na uwezo wa kulipia ankara za mwezi za wastani wa Sh.3,000/= - 4,000/= kwa mwezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naunga mkono hoja.

**MHE. PARSEKO V. KONE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, kwa niaba ya wananchi wa Wilaya ya Simanjiro na hasa wanaohusika na *Tanzanite* naipongeza Serikali kwa uamuzi wa kutouza nje ya nchi *Tanzanite* isiyosanifiwa.

Nashauri kwamba utekelezaji wa uamuzi huo siyo suala la kufumba na kufumbua. Pia mtakubali kuwa ni suala nyeti. Serikali ikutane na wadau ili kupanga utekelezaji wa uamuzi huo. Aidha, Wizara ya Nishati na Madini ikutane na Wizara ya Fedha, ili kuondoa mgongano uliopo sasa wa Wizara ya Nishati na Madini kutoa kibali cha kuuza nje Tanzanite isiyosanifiwa na Wizara ya Fedha kuzuia.

Pili, kuhusu kodi za *Tanzanite* ni nyingi. Kuna kodi nyingi za *Tanzanite* zinawakatisha tamaa wadau wa *Tanzanite*. Nashauri mamlaka zote zinazohusika na kodi hizo zikae na wadau ili kupunguza kodi hizo. Tatu, madini ya vito *(Gemstones)* ikiwepo *Tanzanite* yachimbwe na Watanzania tu.

Tatu, mgogoro wa *Block C and B* kuhusu mipaka itatuliwe haraka kama ilivyopendekezwa na Tume ya Jenerali Mboma. Taarifa ya Tume iliyoongozwa na Jenerali Mboma ni muhimu sana

kufahamika kwa wadau wote na wadau wote kukaa na kupanga utekelezaji wake. Je, ni kwa nini Wizara ya Nishati na Madini haijatekeleza taarifa hiyo? Kama imetekelezwa ni yapi yametekelezwa na yapi bado? Je, wadau wote wanaijua hiyo taarifa na utekelezaji wake? Serikali inaweza kunieleza ni kwa sababu gani sikupata taarifa ya Tume ya Jenerali Mboma? Kwa sababu gani sikushirikishwa kwenye Mkutano wa *TUSCON.* Mimi ni mwakilishi wa watu wa Mererani, mimi ni wa kwanza wananchi kunitaka kutoa maelezo au kunitupia matope. Ni haki yangu kushirikishwa kikamilifu kwa niaba ya wananchi wa Mererani. Naomba kupata ratiba ya uanzishwaji wa *EPZ* Mererani.

Nne, Makao Makuu ya Wilaya ya Simanjiro haina umeme, tumeahidiwa mara nyingi . Taarifa niliyopewa na Wizara tupo mwaka 2004. Naomba nithibitishiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeomba kuchangia kwa kuzungumza na kwa bahati mbaya sana sikupata nafasi. Mheshimiwa Waziri, naomba nijibiwe hoja zangu nilizoziandika, vinginevyo utawajibika kutoa maelezo wakati wa Kamati kwenye vifungu.

**MHE. SALAMA KHAMIS ISLAM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa pongezi zangu kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na uongozi wote wa Wizara ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kuchangia kwenye hoja hii kuhusu ukatwaji wa umeme Zanzibar, ni wengi wamezungumzia suala hili na mimi pia nimo miongoni mwao. Kitendo cha ukataji umeme ni kitendo cha unyanyasaji na udhalilishaji kwa sababu sisi wote ni Watanzania na tunasaidiana kwa mambo mengi sana, hili la kudaiwa isiwe ni sababu ya Zanzibar kukatiwa umeme kwa sababu Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ina lengo la kulipa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ningependa kuzungumzia kuhusu upandaji wa bei ya mafuta ya petroli, pamoja na kwamba kuna biashara huria, ni vyema Serikali ikaingilia kati suala hili, bei ilipanda kabla ya vita vya Iraq na sasa imekuwa kama mtindo kwa wafanyabiashara kupandisha bei kama wanavyotaka wao kwa sababu hakuna chombo chochote kinachodhibiti bei hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri ni haya mawili tu yanatosha na naunga mkono hoja hii.

**MHE. ABU T. KIWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, Naibu Waziri wake, Katibu Mkuu, pamoja na watendaji wote wa Wizara yake. Bila kusahau pia kuipongeza Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji na Biashara, Kamati ambayo mimi pia ni Mjumbe, kwa kupitia Bajeti ya Wizara hii na kushauri ipasavyo na hatimaye kuiwasilishwa kwa ufasaha hotuba ya Waziri, Mheshimiwa Danie Yona, hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kero ya Wizara hii hususan Jimboni kwangu Kilombero, ambako kuna migodi miwili ya Kidatu na Kihansi ni kushindwa kuwapatia vijiji vyenye migodi hiyo umeme kwa matumizi ya wananchi. Ningeomba Mheshimiwa Waziri, aweke kipaumbele suala hili kwa umahiri wote unaostahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa taratibu za *TANESCO, TANESCO* inapaswa kulipa *Services Fee* kwenye Wilaya zenye migodi hiyo. Nasikitika Jimbo langu la Kilombero, zaidi ya kuliandikia Shirika halijajibu wala kulipa hiyo *Services Fee* stahiki kwa Jimbo langu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningemwomba Mheshimiwa Waziri, alishughulikia suala hili na kuilipa Halmashauri ya Kilombero hizo fedha ili iweze kuboresha huduma nyingine za kijamii, bila kusahau, kuweka mikakati muafaka ya usambazaji umeme kwenye vijiji ambako umeme wa migodi hiyo ya Kidatu na Kihansi unafuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maoni haya, naomba kuunga mkono hoja ya Wizara ya Nishati na Madini kwa asilimia mia moja.

**MHE. PAUL E. NTWINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri Daniel Yona na Naibu wake kwa kazi nzuri sana wanayoifanya katika Wizara hii ikiwa ni pamoja na Katibu Mkuu na wafanyakazi wote wa Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Daniel Yona, ametumika kama kiraka kuziba Wizara hii baada ya kwenda mrama na ni kweli wakisaidiana na Naibu wake, Mheshimiwa Dr. Ibrahim Msabaha, wanajaribu sana kutekeleza azma ya kupeleka umeme kwenye wilaya zote nchini, ni kazi ngumu na bila fedha za kutosha wanazopewa na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niishukuru sana Wizara na Shirika la Umeme, *TANESCO,* kuwezesha kupeleka umeme katika Jimbo la Songwe na sasa umeme umeahidiwa kwenda Vijiji vya Kanga na Galula, wananchi wanaungoja umeme huo kwa hali na mali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, nawapongeza na naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. JACKSON M. MAKWETTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba *TANESCO* itekeleze ombi la zaidi ya miaka 10 la kushusha umeme katika Vijiji vya Kiumba, Ikelu na Itunduma, vilivyoko kati ya Miji ya Njombe na Makambako. Nyaya za umeme kutoka Njombe zinapita juu ya vijiji hivi. Maombi yao ni ya zaidi ya miaka 10. Sasa ni suala la kisiasa na mimi Mbunge napata taabu sana kuelezea sababu za kutoshusha umeme katika vijiji hivi wakati maombi ya nyuma yanasikilizwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. ANNE S. MAKINDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri na watalaam wake, kwa kuiendesha Wizara vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni yangu ni kuwa shughuli za kuuza nje mali iliyotengenezwa hapa hapa nchini ni muhimu sana kwani tutaongeza ajira hapa ndani. Vijana wengi hawana kazi, eneo la madini linaweza kuchangia sehemu kubwa ya ajira. Hivyo, pamoja na *Tanzanite* basi madini mengine pia yatafutiwe utaratibu wa kukatwa na kutengeneza mali zake hapa hapa badala ya kuuza ghafi.

Ningependa kupata maelezo ya Serikali kuhusu maelezo yanayotolewa na Mheshimiwa Augustino Mrema, Mwenyekiti wa *TLP,* kuwa ataweza kusambaza umeme vijijini kwa kutumia mashine ndogo ndogo. Maelezo hayo anasema amepata mfadhili kutoka nje ya nchi kama ni kweli Serikali ilishindwa nini kufanya hayo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii.

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri, kwa kazi nzuri wanayoifanya. Aidha, nampongeza Katibu Mkuu, pamoja na watendaji wengine.

Pili, nampongeza sana Naibu Waziri, Mheshimiwa Dr. Ibrahim Msabaha, kwa kutambelea Singida na hata Jimbo langu mara mbili.

Tatu, napenda kuikumbusha Wizara kuhusu tatizo la umeme Ihanja, wananchi wanalalamikia sana kukosa umeme wakati nguzo za umeme zimewekwa au zimepelekwa huko Ihanja miaka 5 iliyopita . Hii ni hatari kwa Serikali ya CCM, ambayo iliahidi mara kadhaa kupeleka umeme Ihanja. Ahadi ya mwisho ilikuwa ndani ya Bunge hili Februari, 2001. Matokeo yake sio mazuri. Naomba sana tena sana, suala hili lipewe kipaumbele. Wafadhili toka Amerika, ambao wapo tayari kusaidia shule ya Sekondari ya Ufundi ya Ihanja wanashindwa kuelewa vipi shule hiyo inakosa umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudia kusisitiza kuhusu umeme Ihanja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii.

**MHE. FATMA SAID ALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii. Kwanza, kuhusu *TANESCO* kukata umeme Zanzibar, kwa nini wasitoe taarifa mapema kwa wananchi wa Zanzibar? Je, ile hasara kubwa iliyosababishwa na kukatwa kwa umeme na *TANESCO* watalipa nani? Zanzibar si imejitahidi kulipa umeme ili kupunguza deni lao? Huo udugu wa Muungano uko wapi? Mbona hatuoneani huruma? Hivi kweli ndugu wawili wanaweza kuuana bila chanzo cha kugombana? Je, Wizara itakaa kimya kuhusu swali hili?

Pili, kuhusu mikopo kwa uchimbaji wa madini. Wizara itoe mikopo maalum kwa wachimbaji wanawake wadogo wadogo wa madini ili waweze kushiriki kikamilifu katika uchimbaji na uuzaji wa madini huko nje.

Tatu, kuhusu utafiti wa mafuta Zanzibar. Naunga mkono kwa wale Waheshimiwa Wabunge, waliotaka Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ikubali Kampuni ya *ANTIM* kutoka Canada kufanya utafifi wa uchimbaji wa awali katika Pwani ya Bahari ya Tanzania Zanzibar. Mheshimiwa Waziri, tukifanikiwa kwenye suala hili si ndiyo tutaumaliza umaskini.

Mwisho, nampongeza Mheshimiwa Daniel Yona, Waziri wa Nishati na Madini, pamoja na Mheshimiwa Dr. Ibrahim Msabaha, Naibu Waziri, kwa jitihada kubwa wanayoifanya kutatua matatizo ya Wizara hii.

**MHE. DR. LAWRENCE M. GAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Nina masikitiko makubwa sana kusema kwamba, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri hakutaja chochote kuhusu maendeleo ya kuupatia Mkoa wa Ruvuma na Mji wa Songea umeme. Mradi wa Mchuchuma ulifikia hatua ya kuwekewa saini mbele ya Waheshimiwa Wabunge wa Mikoa ya Kusini hapa hapa Bungeni miaka miwili iliyopita. Sasa hatupati taarifa yoyote ya utekelezaji wa mradi huu. Je, kweli kuna kinachofanyika tangu saini iwekwe, kama kweli kazi zinafanyika basi tupate taarifa. Mradi wa *NAKATUKA* wa kuipatia Wilaya ya Songea umeme ulikuwa karibu ukamilike kama Wizara ingeweza kumpata mfadhili wa kumsaidia Mjerumani *(KWF),* ambaye alikubali kuifanya kazi hiyo kwa maandishi. Mjerumani alingojea kwa miaka miwili na baada ya hapo akajitoa kwa hasira. Wizara haijatamka nini kinafanyika badala yake?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mazungumzo ya Mheshimiwa Waziri na sisi Waheshimiwa Wabunge wa kutoka Mikoa ya Kusini, Aprili, 2003 hayakuzaa matunda. Sina uhakika kama washauri wako wameamua kukusaidia. Nasikitika kusema hayo kwa sababu Wizara hii haifanyi chochote katika kusaidia kero sugu. Ahsante.

**MHE. PHILIP S. MARMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na sera na mipango tuliyokubaliana ya kupeleka umeme katika Makao Makuu ya Wilaya zote ifikapo 2005, lakini hii haina maana kwamba, usambazaji wa umeme katika maeneo mengine umesimamishwa, kila Mkoa huwa na miradi ya kusambaza umeme. Sisi Mbulu tunapata shida kufikiwa na umeme hasa kwa maeneo yaliyokuwa karibu na Makao Makuu ya Wilaya. Tafadhali Meneja wa *TANESCO* Arusha, atufahamishe katika mipango yake kwa Mkoa wa Arusha na Manyara, Miradi ya Umeme Mbulu - Dongobesh na Mbulu Daudi itaanza lini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Meneja wa *TANESCO* Singida, ambaye ana majukumu ya kusambaza umeme upande wa Magharibi mwa Wilaya ya Mbulu, kwa vile kwa miaka zaidi ya 20 hajalipangia eneo hilo ambalo haliko katika Mkoa wa Singida mradi wowote. Je, haoni kuwa sasa wakati wa kufikisha umeme katika vituo vya biashara vya Maghang, Labay na Maretadu katika Wilaya ya Mbulu umewadia?

Pili, mapendekezo ya miradi midogo mipya ya umeme kuanzia katika *RCC* au *RDC* ya zamani na kwa vile *RCC* Mkoa wa Singida haiwajibiki kushughulikia miradi ya umeme ya Mkoa wa Manyara hivyo, *RCC* ya Mkoa wa Arusha haiwajibiki wala haina haja ya kuishughulikia miradi ya Mkoa wa Manyara. Kwa maoni yangu ni lazima haraka iwezekanavyo, kwa Mkoa wa Manyara uwe na Meneja wake. Kwa muda Meneja wa *TANESCO* aliyeko Babati aweza kukaimu kama Meneja wa Mkoa.

**MHE. MOSSY SULEIMAN MUSSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naunga mono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wa mwanzo nauelekeza katika nishati na madini, ningependa kuishauri Serikali kutupia macho katika maliasili hii ambayo ndiyo chanzo cha kuondoa umaskini kwa kuyashughulikia madini hayo, kimiundombinu hasa kule Mchuchuma kwa sababu mbalimbali Serikali ingetumia nguvu zake zote hasa za kitaalam kuona kwamba hili linatekelezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kuchangia katika suala la ushirikishwaji wa wananchi katika uchimbaji wa madini, pamoja na Serikali kuingia mikataba mikubwa na makampuni ya nje na kutuingizia mapato, lakini ingekuwa busara pia wachimbaji wadogo wadogo wangepewa kipaumbele katika maeneo maalum. Aidha na wao wakafaidika na maliasili yao hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa tahadhari kwa Shirika la hili nyeti, hivi sasa upo mtindo wa kutojali nyaya. Aidha, kwa kujenga chini ya nyaya kuu za umeme au nyaya za umeme kuzagaa kiholela bila mpango maalum, hatimaye wataalam kuziangalia kwa kutokujali hatma yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la *Management* ya *Net Group Solution,* labda ningeipongeza kwa ukusanyaji mapato katika kiwango kizuri. Lakini cha kuzingatia ni kwamba, lazima Serikali itoe maelekezo nini Watanzania wanataka kwani zipo sehemu nyingi kuna tatizo la umeme. Hivyo, huduma hii ifike kwa maendeleo ya watu wetu. Lakini pia utafiti ufanywe kwa nini umeme umeendelea kukatika bila utaratibu .

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la Zanzibar kukatiwa umeme lazima nilieleze wazi kwamba, suala hili lisitiwe katika siasa kwani hii ni biashara, hivyo Viongozi wa *TANESCO* na *Zanzibar State Fuel,* lazima wawe na uhusiano wa karibu ili kuepusha utata usio wa lazima kwa maslahi ya nchi zetu. Lakini pia tumeelezwa kwamba, *PBZ* ilitoa hundi bandia, tungependa ifafanuliwe kwamba, suala hili lina ukweli kiasi gani.

Mwisho, Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga tena mkono hoja na kuitakia mema Wizara hii, kwa kuchukulia umeme ni maendeleo na si anasa.

**MHE. BEATUS R. MAGAYANE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ugunduzi na uchimbaji wa madini umekuwa ukifanywa na wachimbaji wadogo wadogo mpaka siku za karibuni ambapo makampuni makubwa yameingia. Hata hivyo, makampuni hayo yamekwenda mara nyingi katika maeneo hayo hayo waliko wachimbaji wadogo wadogo na hii mara nyingi imesababisha migogoro kati ya wachimbaji wadogo na makampuni hayo. Ni vema wachimbaji hao wadogo waheshimiwe kama waanzilishi wa maeneo yanayogunduliwa madini na wachimbaji wadogo wadogo, kama ilivyo Nyamutukuza Jimbo la Buyungu, yatangazwe mapema maeneo maalum ili Kamati za kugawa vitalu ziundwe mapema kuondoa migogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vibali vya kutafuta madini ndani ya hifadhi za wanyama *(Game Reserves),* vitolewe kwa uangalifu sana kwani zoezi zima ni *Counter Productive.* Mara nyingi Makampuni hayo au wanafanyakazi wao wamegeuka majangili. Kama hatuna uhakika na madini angalau tuna uhakika na tembo tulionao, ambapo tembo mmoja ukimuwinda kisheria, huliingizia Taifa si chini ya Sh. 25,000,000/=! Ikiwezekana zitumike taarifa za utafiti za awali au tuache kabisa kufanya utafiti unaoleta uharibifu ndani ya hifadhi!

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vizuri kuwa vijiji vingi sasa vipatiwe umeme. Lakini si jambo zuri sana kuzungumzia kupeleka umeme kwenye vijiji viwili vilivyosalia katika Wilaya fulani wakati Makao Makuu ya Mkoa wa Kigoma hayana umeme wa uhakika! Wilaya ya Kasulu ilianzishwa mwaka 1913 lakini haina umeme na Kibondo. Ni lini zitapatiwa umeme ili ionekane Serikali inajali wakazi wake? Wakati *Net Group Solution* wanaingia *TANESCO,* wote tulitegemea kupungua, kama siyo kwisha kabisa tatizo la kukatikakati umeme. Lakini hali si hivyo kukatika kwa umeme kumeharibu sana vyombo vya ofisini na majumbani, lakini imekuwa tatizo sana kupata fidia. Ni vyema *TANESCO* wakawa na

utaratibu wa *surveillance* na kukatika umeme ili watu wakilalamikia kuhusu vifaa vyao, wasiwaone kuwa ni waongo tu na waweze kuwafidia ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge lako Tukufu lilishangilia sana wakati Mheshimiwa Waziri wa Fedha alipowasilisha Bajeti ya Serikali ya kutosafirisha *Tanzanite* ghafi nje. Dhamira ya Serikali kutekeleza jambo hili haiko dhahiri katika hotuba ya Mheshimiwa Waizri wa Nishati na Madini. Kipengele cha (a) kifungu 43 ukurasa wa 25: "kama ni lazima kuzirekebisha...." haionyeshi hata kidogo *commitment* ya Serikali, ni vema hizo awamu zinazozungumziwa kifungu 44 zikaainishwa vizuri!

Mheshimiwa Mwenyekiti, Madini ya *Tanzanite* yamegunduliwa na mtu mmoja aitwaye Jumanne Ngoma, lakini mara nyingi wamekuwa wakitajwa wengine kama wagunduzi. Kwa nini Serikali isiweke rekodi sahihi kuhusu huyu mgunduzi na ili kulinda haki yake, kwa nini asipewe *Intellectual Parent Right* yake?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mrahaba unaotolewa na Makampuni ya madini bado ni kidogo sana. Utaratibu ufanywe ili kiwango hicho kipande hasa kwa wachimbaji wapya watakaokuja kuwekeza. Pia wachimbaji hao wakubwa wafanye *Environmental Impact Assesment (EIA),* kabla ya kuanza kazi ili kuhakikisha mazingira yetu yanalindwa na siyo kuacha mashimo tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii.

**MHE. KIDAWA HAMID SALEH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kupata nafasi ili nami niweze kuchangia katika hoja hii iliyoko mezani sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii mimi nitaelekeza mchango wangu katika eneo moja tu la umeme unaozalishwa na Shirika la *TANESCO.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaelewa umeme ni nishati muhimu katika maendeleo ya nchi. Kila nchi inajaribu kuboresha vianzio vyake vya umeme ili kuwekeza kupata umeme wa uhakika

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika nchi yetu umeme ni uchumi, umeme ni siasa na ni siasa kwa sababu unagusa jamii yote, kwa maana hiyo masuala yanayohusiana na ukosekanaji wa umeme ni lazima yashughulikiwe kwa tahadhari kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiwa kama Mtanzania, nimepata uchungu mkubwa mno kwa kitendo kilichofanywa na *TANESCO* tarehe 21 Julai, 2003 cha kuikatia umeme Zanzibar, ikiwa inaeleweka kuwa Zanzibar haina kianzio chohote kingine cha umeme angalau cha kujihami ikitokea hali kama hii ya kukatiwa umeme kwa tafsiri yangu binafsi, kitendo hiki ni cha kibabe na kimefanywa makusudi kuidhalilisha Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na watu wake.

Serikali nyingi duniani hata zile zilizoendelea, zina madeni ya ndani na utaratibu wa kiustaarabu huandaliwa wa kuyafanya madeni hayo yalipike na wala hawatumii ubabe wala kukomoana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania tukiongozwa na viongozi wetu mahiri wanaotokana na Chama Tawala (CCM) tumekuwa mara zote tukijadili mambo na matatizo yetu na kufikia makubaliano muafaka bila ya kudhalilishana, leo kimezidi nini mpaka *TANESCO* iikatie umeme Zanzibar, ingawa makubaliano yapo na madeni yamekuwa yakilipwa kama yalivyo makubaliano isipokuwa katika kipindi cha miezi iliyopita kutokana na matatizo ya kibenki yaliyojitokeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maoni yangu ingawa *TANESCO* ni *business entity* na inatakiwa ijiendeshe kibiashara, hakukuwa na sababu za kutosha za kuikatia umeme Zanzibar. Aidha, ninapenda kukumbusha kwamba, Zanzibar sio kiwanda kimoja au Wizara moja ambapo ikikataiwa umeme haitaathiri sana jamii, lakini Zanzibar ni nchi inayojitegemea kiuchumi na kwa maana hiyo inazo sekta zote za kijamii na kiuchumi, hivyo kukatwa kwa umeme kibabe tu kunaweza kusababisha madhara makubwa makubwa sana ya jamii na uchumi wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachukulia tukio hili ni *early warning signal* kwa Serikali ya Zanzibar na kama hatua muafaka hazikuchukuliwa, matatizo makubwa yanaweza yakatokea hapo baadaye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaishauri Serikali iandae *team* ya watafiti wakafanye tathmini kuona ni athari gani za kiuchumi, kijamii, kisiasa na kisaikolojia zilizopatikana kutokana na tukio hili. Athari hizo ziwekwe i*n money terms* na zilinganishwe na deni la *TANESCO* lililosababisha waikatie umeme Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti na kama gharama zitajitokeza kuwa ni kubwa zaidi, Serikali iitake *TANESCO* itoe fidia kwa Zanzibar. Serikali pia itoe onyo kwa *TANESCO* kuwa kitendo hiki kisitokee tena hapa Tanzania kwani kinavuruga baada ya kujenga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya mchango huo, ninaunga mkono hoja. Ahsante.

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wengine wote wa Wizara hii. Naanza kuchangia kwa kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niikumbushe Wizara juu ya kuvuta umeme toka Mtingo, Singida Kaskazini kwenda Iramba Mashariki. Ahadi ambayo Wizara imekuwa inatoa kwa wananchi wa Iramba Mashariki toka mwaka 2000, lakini hadi leo bado hatujapewa umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi namwomba sana Mheshimiwa Waziri mwaka huu wa Fedha tupewe umeme. Nafahamu kabisa ya kwamba, kunaweza kukawa na upungufu wa fedha, lakini hata hivyo, naomba umeme mwaka huu uvutwe toka Mtinko hadi Hospitali ya Nkungi, inayotoa huduma kwa wananchi wa Iramba Mashariki , Hanang na Singida Kaskazini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Iramba Mashariki wanapata taabu sana kufuata matibabu Wilaya za Mbulu au Hanang (Katesh), Singida, ambako maeneo yote haya yana umbali wa wastani wa kilomita 70. Wananchi wetu hasa akinamama na watoto wanapata taabu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Baba Askofu wa KKKT Dayosisi ya Kati, alitafuta wafadhili wa kufanya kazi zifuatazo:-

(a) Kupanua Hospitali ya Nkungi iwe ya kisasa, vifaa vyote vilishaletwa vinasubiri umeme vifungwe, miundombinu ya kutengeneza njia za kuweka nyaya ilifungwa toka mwaka 2000 kwa thamani ya Tanzania shilingi 11,000,000/=.

(b) Wafadhili toka Marekani wameshafika lakini wameshindwa kuanza kazi kutokana na kukosekana kwa umeme.

(c) Wafadhali hawa wanatujengea Chuo cha Uganga mpaka kwa kiwango cha *Diploma.*

(d) Kujenga Chuo cha Maendeleo kitakachotoa Elimu ya Ufundi kwa vijana wetu.

(e) Kupanua na kuifanya Shule ya Sekondari ya Iambi kuwa ya kisasa kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nimepata wafadhili watakaofunga mtambo mkubwa na wa kisasa wa kukamua mafuta ya alizeti. Tumepata fedha za kutosha kwa ajili ya maji ambapo mitambo inayotumia umeme inahitajika ili kuvuta na kusukuma maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Nkungi ni eneo ambalo lina wakazi wengi sana na tayari walishatayarisha nyumba zao kwa ajili ya kupokea umeme. Nakuhakikishia ya kwamba, Shirika la Umeme Tanzania lilitakiwa liwe linapata kipato kikubwa toka kwa wananchi wa eneo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juu ya Shirika kukata umeme Zanzibar, mimi naipongeza hatua hii kwa sababu enzi hizi ni za ukweli ni lazima kila mtu Shirika na Serikali na kadhalika kulipia kile anachotumia. Narudia kuipongeza sana *Management* ya *TANESCO* waendelee kukata mpaka hapo watakapolipa. Nafahamu ya kwamba, wao Zanzibar wanalipia kwa mtindo wa kiwango maalum na pia wanafahamu ya kwamba, wanatakiwa walipie kwa sababu nafahamu semina mbalimbali zilishafanywa na Wizara/Shirika huko Visiwani. Hatua hii ya kukata umeme itafanya Muungano ukomee zaidi maana hakuna atakayemnyonya mwenzake.

**MHE. OMAR JUMA OMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uingiaji wa makampuni ni vizuri sana hasa ukilinganisha na uwezo wa Serikali kushindwa uwezo wa kuendesha makampuni hayo lakini uuzwaji huu wa hayo makampuni haumaanishi kuuzwa kwani wamekubaliana na Serikali na kwa kuwa Serikali inauza sehemu tu za sera zake na hata hivyo wanunuzi hawalipi hizo sera ambazo ni mali ya Serikali na Serikali kuwa wazito wa kufuatilia. Vilevile lengo la kuuza Makampuni ni Serikali kupata mapato zaidi na wananchi kupatiwa ajira na uzalishaji uweze kuongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu nishati inayotokana na miti kwa wakati huu imepitwa na wakati kwani husababisha uharibifu wa mazingira na vilevile huletea nchi jangwa kwa ajili ya ukataji wa miti. Naishauri Serikali iboreshe zaidi njia ya usambazaji wa umeme na gesi ili wananchi waweze kutumia nishati hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la umeme kwa Visiwa vya Zanzibar, bado haitoshi na jaribio la kukata umeme bila ya kutoa taarifa ni dharau na kutojali watu wa Unguja kwani kitendo cha kukata umeme bila kutoa taarifa ni sawa na kujaribu kufanya uhalifu. Kuhusu kisiwa cha Pemba bado inaonekana kwamba, wao hawastahiki kupatiwa huduma hiyo kwa sababu hadi leo Pemba hakuna umeme wa uhakika kwani mpaka sasa wanategemea umeme wa majenereta ambao hutegemea mafuta ya dizeli na mafuta ambayo kwa Pemba huwa ni adimu. Kwa sababu ya ukosefu wa mafuta na hata hayo mafuta yakiwepo umeme huo unapatikana kwa mgao. Kwa hiyo, tunaishauri Serikali itupatie umeme kutoka Tanzania Bara kupitia Tanga ili na Wapemba waweze kufaidika na matumizi ya umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la utafiti wa mafuta ya uchimbaji Zanzibar tunahisi kwamba, ipo haja ya kufanyiwa marekebisho kwani Zanzibar kama nchi na Tanganyika kama nchi zilizoungana kwa makubaliano yake, kuna mali za uchumi wa nchi ambazo kwa mtazamo wa kina ukiingiza kuwa iwe ni Muungano inaathiri upande mmoja kama mafuta ambayo yasemekana yapo Zanzibar ukifanya ya Muungano itakufa Zanzibar kiuchumi kwani tegemeo la Zanzibar sasa ni mafuta badala ya karafuu ambazo zimekosa soko na vilevile ikiwa mafuta yatakuwa ya Muungano basi Zanzibar haitofaidika na chochote kwani mfano hai ni ule wa misaada ya nje ambayo Zanzibar hupewa gawio la asilimia 4.5 kiasi ambacho hakitoshi hata kununua madawa ya hospitali kwa mwezi mmoja. Kwa hiyo, tunaishauri Serikali ya Muungano, suala la mafuta liachiwe Wazanzibari kwani mafuta yalianza kufanyiwa utafiti kabla ya Mapinduzi ya Zanzibar. Kwa hiyo, hii ni haki ya Wazanzibar sio haki ya Muungano kama vile dhahabu kwa Tanzania Bara na madini mengine kama almasi, *Tanzanite*, gesi na vinginevyo.

**MHE. GWASSA A. SEBABILI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika hoja ya Wizara hii. Suala la umeme katika Wilaya ya Ngara, Mradi Na. 3138 na *Vote* 38 unatokana na ahadi ya Mheshimiwa Rais Benjamini William Mkapa, alipokuwa katika kampeni za Uchaguzi Mkuu wa 1995. Baada ya ufuatiliaji wa muda mrefu sana, Mradi ulianza 2002 mwishoni na nyumba ya kuweka jenereta imekamilika. Mpango wa usambazaji ni Makao Makuu ya Wilaya na Miji Midogo ya Kabanga na Rulenge. Ukubwa uliokubalika na kutangazwa kwa wananchi wa Ngara na Serikali ya Mkoa wa Kagera ni *KV* 35.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi huu uliendelea kughubikwa na mizengwe mingi baada ya ule wa kuchelewa kuanza uliochukua miaka sita. Mnamo Machi, 2003, Wizara kupitia kwa Meneja wa Mkoa wa *TANESCO,* ilieleza haitatekeleza kutokana na uhaba wa fedha za kufidia mashamba ya wakulima kwa kuwa hakuna mashamba ya kufidiwa na bado uongozi ulilishughulikia hili lilikamilika. Baadaye likaletwa wazo la kukataa kupeleka umeme Mji wa Rulenge. Sababu zilifichwa, mnamo Mei ikajulikana kuwa Wizara ilibadili *KV* 35 kuwa *KV* 11. Aidha, ilibadili majenereta ya Ngara badala ya kutoka Babati, Arusha, wakaamua kuleta machakavu na madogo kutoka Kondoa!

Mheshimiwa Mwenyekiti, ufuatiliaji uliofanywa na Mbunge wa Ngara, Mkuu wa Mkoa wa Kagera, Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Kagera na kadhalika, ukabaini uzushi mwingine kwamba, Mji wa Rulenge, hauwezi kulipia gharama za umeme! Hisia hiyo isiyo na msingi niliombea ziara kwa uchunguzi kutoka Wizarani bila mafanikio. Rulenge ni Mji mkubwa wa zamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hiyo haitoshi sasa Wizara inaweka kisingizio cha mbali, eti Rulenge ni kilomita 60 badala ya kilomita 40 kutokea Njia Panda ya kupeleka umeme Kabanga. Kwa yote hayo wananchi wa Ngara wanaiona Wizara hii inahujumu Wilaya ya Ngara hasa pale ushahidi wa Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini, alipozindua umeme wa Biharamulo tarehe 23 Mei, 2003 akapuuzia kufika Ngara, licha ya wito wa Mkuu wa Mkoa wa Kagera, kwa barua na *KGR/T/46/Vol X/57* ya tarehe 14 Mei, 2003.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa iliwezekana kupeleka umeme Chato, kilomita 80 toka Biharamulo, inawezekana pia kupeleka umeme Mjini Rulenge kilomita 40.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Ngara wanasema kuwa, Wizara iwaeleze kama Mheshimiwa Rais, alibadili ahadi yake ya 1995 na wamenituma kuwa niondoe shilingi moja ikiwa Wizara haitatoa umeme kwa Ngara kutekeleza ahadi ya Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matatizo ya Wizara hii kuhusu umeme wa Ngara yamedhihirika kuwa wa kuionea kwa sababu Miradi ya Ngara na Biharamulo ilianza pamoja na yote ni ahadi ya Mheshimiwa Rais. Inashangaza kuwa Bajeti ya 2003/2004, Biharamulo imetengewa Sh. 5,309,620,000/= lakini Ngara ikapewa Sh.400,000,000/= tu!

Hata baada ya kukutana na Mheshimiwa Waziri na Naibu wake pia kuwasiliana kwa barua kadhaa, sipati jibu lolote bali kunikwepa kila mara. Wizara imezidi kujichanganya pale Bajeti yake ya Maendekeo ya usambazaji umeme, *Vote 58, Project 3113* - Biharamulo imetengewa Sh. 5,309,620,000/= na *Project 3183* - Ngara imetengewa Sh.400,000,000/=. Hotuba ya Mheshimiwa Waziri, Ibara ya 7 ukurasa wa 4 amesema kwamba, Ngara imetengewa shilingi 4,000,000,000/=.

Tofauti hizi zikiunganishwa na visingizio vingi vilivyotangulia inaonyesha wasiwasi wa kama kweli mradi huu unatekelezwa kwa misingi ya uwazi na unaweza kutolewa maelezo yanayoeleweka na kutosheleza kwa wakazi wa Ngara, ambao wanaishi katika mateso makubwa kwa miaka mingi ya wakimbizi wa Rwanda na Burundi na hivi karibuni wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaunga mkono hoja hii baada ya kuhakikishiwa kuwa kauli ya Mkuu wa Nchi itaheshimiwa na umeme kusambazwa katika Wilaya na Mji wa Ngara, Rulenge na Kabanga na kuwashwa mwaka 2003 kama ilivyopangwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Nickel* Wilayani utafiti wake ulianza miaka 10 iliyopita. Kila mwezi kwa muda wote huo tani nyingi za udongo/mchanga hupelekwa nje ya nchi kuchambauliwa. Inashangaza kwamba, Serikali haijapata kutaja kiasi cha *Nickel* iliyopatikana kutokana na mchanga huo wala pato lake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Nickel/Cobalt* imeshindikana kuchambua kwa sababu ya ukosefu wa umeme na barabara/reli kusomba madini hayo. Huu ni wakati wa kusaidia Ngara yenye shida nyingi kwa kufungua mgodi huo kwa ajili ya kupunguza umaskini. Iwapo nitapata maelezo ya maana, basi nitaiunga mkono hoja hii.

**MHE. MWADINI ABASS JECHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kuchangia suala la nishati hasa uchimbaji wa mafuta. Kumekuwa na maneno na malumbano ya aina nyingi kuhusiana na suala la kuwepo au kutokuwepo kwa mafuta katika Visiwa vya Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa tunasikia kupitia vyombo vya habari kwamba, Kampuni ya *Antrim* imepewa jukumu la kutafuta mafuta katika Pwani ya Zanzibar, jambo ambalo Serikali ya Zanzibar ilikuwa inakanusha vikali sana. Tunashukuru kwamba, suala hili sasa liko wazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maliasili ya mafuta hii ni miongoni mwa mambo ambayo yameongezwa katika orodha ya asili ya mambo ya Muungano. Nani kaliingiza au namna lilivyoingizwa suala la mafuta ndani ya orodha ya mambo ya Muungano limeanza kuzua utata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni katika kikao cha Baraza la Wawakilishi kinachoendelea Zanzibar, Mheshimiwa Waziri Kiongozi amesema kwamba, Serikali ya Zanzibar inatafuta namna ya kuliondoa suala la mafuta kwenye orodha ya mambo ya Muungano. Hii inadhihirisha wazi kwamba, suala hili ni tete limeingizwa katika orodha hiyo kinyemela. Mheshimiwa Waziri, ameeleza katika hotuba yake kwamba, majadiliano yanaendelea baina ya Serikali, *TPDC* na Kampuni ya *Shell International,* kuhusu kutafuta mafuta katika maeneo ya kina kirefu cha Bahari, Mashariki ya Visiwa vya Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kusikitisha hapa ni kuwa pamoja na kwamba shughuli hii ya utafutaji mafuta inahusu maeneo ya Zanzibar, lakini Serikali ya Zanzibar haionekani kushirikishwa katika mazungumzo haya ya awali. Mbaya zaidi ni kuwa *TPDC,* ambayo ndio inapewa mamlaka ya suala la mafuta, si kampuni ya Muungano. Je, inakuwaje *TPDC* kupewa mamlaka ya shughuli za mafuta katika Visiwa vya Zanzibar?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninaishauri Serikali isichukulie suala la mafuta katika maeneo ya Zanzibar kuwa ni jepesi. Ni suala zito sana na linaweza kuleta migongano baina ya Zanzibar na Tanzania Bara kama busara haikutumika.

**MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kuniruhusu kuchangia katika hoja. Kwanza, napenda kumwomba Waziri wa Nishati na Madini, atoe ufafanuzi wa kutolewa hadharani Taarifa ya Tume ya Jenerali Mboma huko Melerani kuhusu madini ya *Tanzanite*. Je, itatolewa hadharani?

Pili, wananchi wengi wa Tanzania wanapenda na wanaezeka nyumba zao kwa makuti, je, kwa nini Serikali ya Tanzania haitilii maanani uchimbaji wa madini ya bati *(Tin)* huko Kyerwa katika Jimbo la Kyerwa Wilaya ya Karagwe?

Tatu, Wizara inaweza kujibu ni sehemu gani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kunachimbwa madini ya bati kiasi kwamba madini hayo toka Kyerwa hayahitajiki?

Nne, Je, Serikali inajibu nini kuhusu malighali ya bati inatoka wapi katika viwanda vyetu vya kutengeneza mabati?

**MHE. EMMANUEL E. KIPOLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *TANESCO* naipongeza Serikali kwa kudhani kwamba, *Management Contractor* angefanya kazi nzuri sana kuliko mameneja wetu waliosomeshwa kwa kodi ya wananchi wa Taifa hili.

Katika kipindi cha *Net Group Solution* tumeona yale ambayo hatukuwahi kuyaona huko nyuma kama vile Taasisi za kijeshi kulipa malimbikizo ya madeni yao, taasisi za Kiserikali kulipa malimbikizo yao na nzuri zaidi juzi Serikali tukufu ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) kukatiwa umeme. Tumeyaona haya yakifanywa na *Net Group Solution* katika mazingira ambayo menejimenti yetu ya nywele nyeusi, haikuruhusiwa kufanya hayo yote. Kibaya zaidi ni pamoja na kufanya hayo yote matatizo ya *TANESCO* Mikoani na Wilayani yamebakia pale pale. Kwa mfano, katika Wilaya yangu ya Kahama matatizo ya mita, wire, nguzo za umeme sasa yamekomaa mara dufu kiasi kwamba, hata watoto wadogo wa miaka kati ya 4 - 5 wanaweza kusimama hapa na kuyaelezea.

Hivi *Net Group Solution* zaidi ya kudai madeni ni tofauti gani nyingine wameleta katika kipindi tulichowapa kazi hii?

Hivi ni kwa nini menejimenti yetu isirejeshwe na *Net Group Solution* wakabakia kama wakala wa kudai madeni, kazi ambayo inaonekana wanao uzoefu mkubwa? Hivi Serikali kwa vitendo vyake vya

kutothamini kazi zinazofanywa na Wazalendo, haioni kwamba wataalam wetu Wazalendo wanavunjika moyo wa kufanya kazi ikiwa ni pamoja na walimu wao waliowafundisha katika vyuo mbalimbali?

Hivi kwa harakati ya kudai madeni tu, inayofanywa na *Net Group Solution* bila kujikita katika utandazaji wa mfumo wa umeme mijini na vijijini inatosha? Ukiondoa mipango mizuri kama ya kupeleka umeme Ngara, Biharamuro, Serengeti na kadhalika, ambayo imefanywa na menejimenti ya Wazalendo iliyoipitisha *Net Group Solution*, ni mazuri yapi menejimenti mpya inafanya?

**MHE. DAMAS P. NAKEI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Daniel Yona, Waziri wa Nishati na Madini, pamoja na Mheshimiwa Dr. Ibrahim Msabaha, Naibu Waziri, kwa hotuba nzuri na kwa kazi nzuri wanazofanya katika Wizara hii. Baada ya pongezi hizo, naunga mkono hoja hii moja kwa moja.

Mwaka 2001 Serikali iliahidi kufikisha umeme sehemu ya Riroda na Bonga, ambapo kazi hii ingekamilika ifikapo June, 2002. Naomba ahadi hii iliyotolewa kwenye Bajeti ya 2001/2002 itimizwe, naamini *Net Group Solution* wanakusanya mapato ya kutosha kutimiza ahadi hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kazi nzuri inayoendelea katika kusambaza umeme hadi vijijini. Naomba nifahamishwe *latest development* ya Mradi wa *Electricity IV* kwa upande wa Wilaya yetu ya Babati hususan Jimbo langu la Babati Magharibi, Mji wa Bashanet, watafikiwa lini na Mradi huu wa Umeme?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ina mpango gani au inahusikaje na *solar energy* pale ambapo umeme wa kawaida wa *TANESCO* unashindwa au ni vigumu kufika? Je, kuna mpango gani wa *nuclear energy* ili kutoegemea tu kwenye *hydropower* inayotegemea mvua?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati umeme unapelekwa Kondoa kutokea Babati, baadhi ya wananchi wa maeneo waliopitiwa na njia ya umeme walilipwa fidia. Lakini bado kuna baadhi yao wanalalamika kwamba, hawakuridhika na zoezi hili. Je, kuna maelezo yoyote? Naomba niwasilishe maombi yangu machache kwa Serikali ili iyafikirie katika mwaka huu wa fedha. Naomba transfoma eneo la Bermi km 1.5 kutoka *Dareda Mission* kuna umeme, naomba umeme ufikishwe Dareda Kati - Darajani pamekwisha pimwa ni kama km 1.5 kutoka uliko umeme hivi sasa. Pia naomba uwezekano wa kufikisha umeme Dohom kutokea ama Dareda Kati au Kiru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla sehemu nilizotaja hapo juu zinahitaji *little extensions* kwa nguzo chache na transfoma kwani ni umbali usiozidi km 2 ukiacha Riroda ambayo inafika km 7.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo machache naunga mkono hoja hii.

**MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nawapongeza Mheshimiwa Daniel D. Yona, Waziri wa Madini na Nishati, Mheshimiwa Dr. Ibrahim S. R. Msabaha, Naibu Waziri, Ndugu Patrick Rutabanzibwa, Katibu Mkuu, Wakuu wote wa Idara na Asasi zilizopo chini ya Wizara hii, kwa hotuba nzuri ya Bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, kumekuwa na juhudi za dhati za kuwapatia wananchi wa Mwanga umeme. Hata hivyo, wananchi zaidi ya 200 ambao wametayarisha nyumba zao kuwekewa umeme wakalilipa Shirika la *TANESCO* tangu 1994 - 2000, lakini kwa upande wake Shirika bado halijawafungia umeme. Hatua za hivi karibuni za Mheshimiwa Dr. Ibrahim Msabaha, Naibu Waziri wa Nishati na Madini, zinatia moyo na msukumo huu ukiendelea, ninayo hakika ya wananchi hawa kupata umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, pamoja na wananchi hawa 200 niliowataja hapo juu, Vijiji vya Kituri, Mbambau, Kiverenge na Mgagao, vimeahidiwa umeme, nguzo zimepelekwa kule na wananchi wamezichimbia chini, lakini nyaya zimekuwa ni tatizo kubwa. Taarifa tulizonazo ni kuwa zaidi ya *drums* 4 za nyaya za *50mm* zilizotumwa Mwanga tangu Januari ni *drums* 2 tu ambazo zimefika Mwanga. Kumekuwa na hali isiyoeleweka kuwa ni kwa nini *drums* za nyaya kwa ajili ya Wilaya yangu hazifiki,

zinaishia Moshi? Rai yangu ni kuwa Serikali kuhakikisha kuwa miradi hii inakamilika mara moja. Hii ni kwa sababu kama vifaa vinavyopelekwa Mwanga vingefika, miradi hii ingekuwa imekamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne, napenda pia niikumbushe Serikali kuhusu ahadi zake za kuwapatia wananchi wanaokaa katika Vijiji kando kando ya Bwawa la Nyumba ya Mungu. Tangu mwaka 1972 bwawa lilipofunguliwa mpaka leo, wananchi na Vijiji vya Kiti cha Mungu eneo la Shauri Moyo na *National* njia panda, Kiwanja na Handeni, wamepewa ahadi nyingi kuwa watapatiwa umeme lakini mpaka leo bado.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tano, miradi yote niliyotaja katika vifungu 2, 3 na 4 inagharimu shilingi za Tanzania milioni 150. Kama Waheshimiwa Mawaziri, wenye dhamana, watasukuma kikamilifu, miradi hii itaisha mwaka huu. Naomba matamshi rasmi kuhusu hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sita, *TANESCO* ina ujeuri ambao hauna uungwana lakini pia inafanya kazi kama vile mwenyewe sio Serikali. Wizara inaonekana kama haina usimamizi ulio juu ya Shirika hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kisima cha maji cha Kijiji cha Kifaru kimekatiwa umeme tangu mapema mwaka huu. Nikamwomba, Mheshimiwa Waziri kwa unyenyekevu kuwa eneo hilo linaweza kuvamiwa na ugonjwa wa kipindupindu hivyo waturudishie umeme kwa kuwa Halmashauri yetu imepanga katika Bajeti yake shilingi milioni 37 ili kulipa deni hili kama fedha hizi zitakavyokuwa zinatolewa na Serikali na pia Halmashauri yetu imeahidi kulipa matumizi yatakayoanza baada ya kufunguliwa umeme kila itakapopata deni la mwezi.

Baada ya kufuata taratibu zote, Ofisa wa *TANESCO* Mkoa amemkatalia Waziri kata kata kufungulia kijiji kisima cha Maji. Hivi hili shirika ni mali ya nani? Kwa hili, naomba ahadi ya dhati kuwa umeme wa kisima cha Kifaru utarudishwa lini? Ahsante sana.

**MHE. KILONTSI M. MPOROGOMYI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, kwa hotuba yake nzuri. Naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nitoe mchango wangu. Kwanza, tatizo la umeme katika Wilaya na Mikoa ambayo mpaka hivi sasa haijapata umeme. Je, Mheshimiwa Waziri, anayo mipango ya uhakika ya kuzipatia umeme Wilaya kama Kasulu na zingine ambazo maendeleo yake yako mashakani na shughuli nyingi haziwezi kufanyika.

Pili, hivi sasa *supply* ya umeme chini ya *Net Group Solution* ni *erratic* kwa nini hali hii inatokea?

Tatu, *Net Group Solution* walisema wataleta watalaam wanne na hivi sasa wameongezeka. *Qualifications* za hawa watalaam hazifahamiki. Je, Serikali imefanya uchunguzi gani kuona kuna watalaam hawa ni wa lazima kuletwa kufanya kazi hapa nchini?

Nne, hivi karibuni *Net Group Solution* walitangaza kwamba wataagiza nguzo kutoka *South Africa* na wasambazaji pia wangetoka huko. Hapa nchini tuna mbao nyingi na hapa nchini tunao uzoefu wa kusambaza nguzo. Je, hatua hizi zilizochukuliwa na *Net Group Solution* ni za lazima na hatuoni kwamba zina madhara kwa uchumi wa nchi yetu?

Tano, Mkataba wa *Net Group Solution* na Serikali kwa nini *Board* ya *TANESCO* haikushirikishwa? Kwenye Mkataba huo *Net Group Solution* hawakusamehewa kodi na zipo habari kwamba *Board* pia haikuidhinisha jambo hili. Ni nani alitoa idhini hiyo ya kusamehe kodi? Tangazo la kuwafutia kodi lipo.

Sita, watumishi wa *Net Group Solution* walikuja mwaka 2002 na Aprili, 2003 walijilipa *success fee* eti kwa sababu wamekusanya madini na wakapata sifa kem kem na Serikali. Walijipa shilingi 1.4 bilioni. Naomba maelezo ni kazi gani walizozifanya?

Saba, kulikuwa na pendekezo la Serikali kusambaza umeme vijijini kutumia kampuni tofauti kwa ajili ya *rural electrification*. Je, kampuni hii itaanza lini?

Nane, kwa nini Serikali haitaki kufufua mradi wa *Stiegler's Gorge,* ambao *potential* yake ya kuzalisha umeme wa kutosheleza nchi nzima. Kama *Stiegler's Gorge* ingefufuliwa, tungeweza kuuza umeme nchi nyingine kama vile Malawi, Kenya na kadhalika.

Tisa, Je, Serikali itakuwa tayari kutoa maelezo kwa nini haitaki kutoa taarifa juu ya jinsi gani Serikali ilijiingiza katika Mkataba wa *IPTL* na tumekubali kuingia hasara ya Shilingi bilioni 3 kila mwezi, uwajibikaji ukoje?

Kumi, kwa nini Serikali haitaki kumlipa haki zozote Bwana Jumanne Ngoma, aliyegundua Madini ya *Tanzanite*?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali itoe tamko kuhusu kumlipa mzee huyu, aliyefanya kazi ya heshima kubwa kwa Taifa hili.

**MHE. ABDILLAHI O. NAMKULALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa naunga mkono hoja hii. Lakini ningependa kujua ahadi ya kupeleka jenerata ya umeme Mtwara imefikia wapi na Serikali inajua tunavyoteseka kwa kukosa huduma hii?

Pili, Waziri wa Nishati na Madini, aliwaahidi wakazi wa Mji Mdogo wa Nanyumbu kuwa Wilaya Mpya ya Tandahimba, ikipata tu umeme basi Nanyamba itapata pia (Nanyamba iko Mtwara Vijijini) na *Survey* imefanywa na *TANESCO* pia iliwaelezwa wanakijiji hao kuwa wawe tayari kutofidiwa mimea na nyumba zao, wamekubali, lakini baada ya kuja *Management* mpya ya *TANESCO,* suala hili limesimama na hakuna dalili ya kupatiwa umeme na alama zote za *survey* zilizowekwa zinapotea *Management* na Serikali inatuelezaje juu ya hili?

**MHE. RAPHAEL N. MLOLWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Daniel N. Yona, Waziri wa Nishati na Madini kama ifuatavyo:-

Sheria ya Madini ya mwaka 1998 budi irekebishwe, kwani ndiyo kiini cha migogoro mingi iliyopo katika suala zima la madini nchini. Miaka 5 ya utekelezaji tayari imetupa uzoefu wa kutosha kupelekea kuifanyia mapitio upya. Kwanza, Sheria hii inampendelea sana mwekezaji wa nje dhidi ya mmiliki ardhi ya kimila. Haiwezekani kuendelea na mtindo huu, kwani ardhi ndiyo mtaji wa kipekee wa maskini ambao ndiyo wananchi walio wengi. Haiwezekani ardhi ambayo Watanzania maskini wameikalia miaka nenda rudi, ardhi ambayo ndiyo msingi wa maisha yao ya kila siku, ikachukuliwa kirahisi rahisi tu, eti kwa sababu dhahabu imepatikana pale, pasipo kuwafikiria kwa makini warithi wa ardhi hiyo. Tumeshuhudia mara nyingi kwa mfano, katika Kijiji cha Mwambomba, Kata ya Idahina, Wilaya ya Kahama, ambapo mara madini yanapogunduliwa, wamiliki wa kimila wa eneo husika hufukuzwa kana kwamba siyo raia walio na haki ya msingi juu ya ardhi hiyo.

Pili, utaratibu uliowekwa wa kuwekeana mikataba kati ya mwekezaji wa nje na mmiliki ardhi kimila katika ardhi iliyogunduliwa madini haufai hata kidogo ni kumwacha mwananchi kupambana na Mabepari ya Kimataifa. Iweje kuelekeza kwamba mmiliki wa ardhi ya kimila atakiwe aelewane na mwekezaji wa nje wakati mmiliki huyu hajui sheria za biashara za Kimataifa licha ya kufahamu namna ya kuendesha majadiliano ya kibiashara na mwekezaji wa nje? Itatendekaje haki kwa mwananchi, mmiliki huyu wa ardhi kimila, kupambanishwa na Mabepari ya Kimataifa, ambayo yamebobea katika mikakati yenye lengo moja tu, *to maximise profit at any cost.* Lazima Wizara itoe mwongozo wa uhakika katika suala hili na usimamie utekelezaji wake ili kuhakikisha haki, inatendeka kwa pande zote mbili.

Tatu, utaratibu wa sasa unamwezesha mwekezaji wa nje kufikia hatma ya eneo lililoainishwa kwa uchimbaji madini pasipo kuzishirikisha Serikali za Mikoa, Wilaya na wawakilishi wa wananchi. Baya zaidi ni pale ambapo uchunguzi wa madini unafanywa kwa kutumia ndege pasipo kutoa taarifa zozote kwa wananchi walioko kwenye maeneo unakofanyika uchunguzi huo. Mazoezi kama haya, moja lilifanyika

mwishoni mwa Juni au mwanzoni mwa Julai, 2003 huko Kahama. Mazoezi haya huleta hofu na mitafaruku isiyo ya lazima kwa wananchi. Tunaelewa ardhi yote ya nchi hii iko chini ya Rais.

Hata hivyo, huku ni kuendesha mambo kiubabe ubabe. Haifai kuendeshwa katika Taifa huru, Taifa linaloheshimu haki za msingi za raia wake.

Nne, hata pale ambapo wawekezaji wa nje wanapotakiwa kuchangia maendeleo ya maeneo ya machimbo, misaada yao hutolewa kwa mitindo ya fadhila, siyo haki ambayo wananchi katika maeneo haya wanastahiki kuipata, tena kuipata kwa wakati, kwa uhakika na mara kwa mara. Uhusiano kati ya wananchi katika maeneo ya machimbo ya madini na wawekezaji budi uwe rasmi tena wa kiungwana.

Tano, asilimia ya mrahaba budi iongezwe na wananchi katika maeneo ya uchimbaji madini budi wabakishiwe sehemu ya mrahaba huu kufidia uharibifu wa mazingira na kuchangia kwa uhakika maendeleo yao. Vinginevyo haileti mantiki kuendelea kung'ang'ania na msimamo wa sasa. Kama kweli kama Taifa limedhamiria kuyachimba madini hayo sasa, wala siyo kesho, kwa sababu za kutaka kuharakisha maendeleo ya Watanzania, basi mgao kwa Taifa wa mapato yatokanayo na madini hayo, lazima uwe mkubwa wa kutosha. Marehemu Baba wa Taifa, alijua fika kuwepo kwa madini haya. Lakini kwa makusudi kabisa, aliahirisha uchimbaji wake mpaka pale mazingira yangekuwa muafaka kwa madini haya kuwanufaisha Watanzania.

Mwisho, ni wasiwasi mkubwa uliopo katika mazoezi yanayoendelea ya kutafiti madini katika misitu ya hifadhi zetu za Kitaifa. Mfano halisi ni msitu wa Hifadhi wa Kigosi, ambao takriban asilimia 50 ya eneo lake lote imegawanywa na wawekezaji wapatao 4 - 5 kwa ajili ya kutafiti dhahabu. Licha ya kuanzisha uchimbaji wa dhahabu wa chini chini na licha ya kufanya uwindaji haramu wa wanyapori katika hifadhi hii, suala la msingi sana hapa ni tishio la hatma nzima ya misitu ya Hifadhi ya Taifa.

*Honorable Chairman, is it true and have we really come to the point whereby in the pursuit of the dollar, we are prepared to risk everything in terms of destroying the National Forest Reserves and their ecosystems, the priceless herritage which nature has bequeathed to us and only to us, we Tanzanians and to our posterity!* Mimi nakataa!

Mheshimiwa Mwenyekiti, naungana na Wabunge, kuiomba Serikali ifikirie kumtambua vizuri zaidi Mzee Jumanne M. Ngoma, mgunduzi wa madini ya *Tanzanite.* Mzee Ngoma, anastahili tuzo ya *intellectual property right,* ambayo pamoja na mambo mengine, awe anapata asilimia fulani ya mapato yanayotokana na mauzo ya *Tanzanite* kila mwaka. Hii ni haki yake ya msingi katika mazingira ya sasa ya uchumi wa soko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja iliyo mbele yetu.

**MHE. DR. AARON D. CHIDUO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu katika hoja ya Waziri wa Nishati na Madini, nauelekeza zaidi kwenye umeme wa Gairo na Madini ya vito katika Milima ya Ukaguru na madini kwa ujumla.

Naishukuru sana Serikali kwa kutupatia umeme kwenye Mji Mdogo wa Gairo lakini umeishia kwenye Mji Mdogo wa Gairo tu, vijiji vinavyozunguka Mji Modogo havijafaidika na umeme. Ili kuwapata wateja wengi zaidi na kuinua uchumi wa Vijiji hivyo ambavyo ni Chakarale, Kiedya, Ngiloli, Ibutu, Msingisi, Rubeho, Ukuramani, Kisituri, naishauri na kuiomba Wizara kufikiria kuvipatia vijiji hivyo umeme. Vijiji hivyo vyote viko umbali wa *radius* ya kilometa 5 na hasa Kituo cha Misitu cha Msingisi chenye shughuli kubwa ya upandaji miti, utafiti wa aina mbalimbali ya miti unaofanywa na Chuo Kikuu cha Sokoine na kinatumiwa kama *seminar centre,* kinastahili kupatiwa huduma ya umeme. Kituo hicho kipo umbali wa kilometa 4 tu kutoka Gairo.

Milima ya Ukaguru ina utajiri mkubwa wa madini ya vito na hivi karibuni katika Mto Tame na maeneo yanayozunguka Vijiji vya Makwambe na Nguyami, kuligundulika dhahabu. Ningeshukuru kama Idara ya Madini ingechukua hatua ya kuwaelimisha wachimbaji wadogo wadogo katika Tarafa za Nongwe na Gairo katika Wilaya ya Kilosa, jinsi wanavyoweza kupata msaada wa kuelewa utaratibu wa kuweza

kupata hati za kumiliki maeneo ya uchimbaji wa madini na vile vile kuwaelimisha jinsi wanavyoweza kupata soko kwa madini wanayoyapata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi naunga hoja ya Waziri wa Nishati na Madini kwa asilimia mia moja.

**MHE. FRANK M. MUSSATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naunga mkono hoja hii. Ninaomba kumpongeza Mheshimiwa Daniel Yona, Waziri wa Nishati na Madini, Mheshimiwa Dr. Ibrahim Msabaha, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watumishi wote wa Wizara hii, kwa kutekeleza majukumu yao vyema mwaka 2002/2003. Ninawaomba waongeze jitihada katika mwaka 2003/2004. Hata hivyo, ninayo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Kigoma ni miongoni mwa Mikoa michache ambayo haina umeme wa kuaminika kutokana na kutounganishwa na gridi ya Taifa ya umeme. Aidha, Mkoa huu una Wilaya za Kongwe za Kasulu ya 1920 na Kibondo 1943, ambazo hazina umeme licha ya umri huo. Je, ni vigezo gani ambavyo Serikali inavifuata kupeleka umeme kwenye Wilaya mpya na hata vijijini wakati Makao Makuu ya Wilaya Kongwe kwa mfano, Kasulu na Kibondo, hakuna mpango wa kupelekea umeme?

Mkoa huu upo kisheria katika utaratibu wa *EPZ,* kama Bunge hili Tukufu lilivyokwisha pitisha. Kwa mradi huu Mkoa ungeweza ku-*export* mazao ya bidhaa mbalimbali katika nchi za *DRC*, Rwanda, Burundi, Zambia na Malawi, lakini hayo mazao na bidhaa yataweza kuwa *processed* na kusindikwa bila umeme? Aidha, Serikali inategemea kwamba, kuna mtu ataweza kwenda kuwekeza katika eneo ambalo halina umeme; ni maandalizi gani Serikali inafanya kuvutia wawekezaji kwenda kuwekeza Mkoani Kigoma?

Wakazi wa Mkoa wa Kigoma nao wanastahili kupata umeme wa gridi kwa ajili ya maendeleo kiuchumi na kijamii ili waweze kuendesha viwanda vidogo vidogo na vikubwa kwa lengo la kupambana za umaskini. Kwa hiyo basi, Serikali inatakiwa kufanya yafuatayo haraka iwezekanavyo:-

(a) Kuunganisha Mkoa wa Kigoma na Gridi ya Taifa.

(b) Kuangalia uwezekano wa kuanza kutekeleza mradi wa kutengeneza umeme kwa kutumia maji ya Mto Malagarasi.

(c) Kuangalia uwezekano wa kuupatia Mkoa wa Kigoma umeme toka nchi jirani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mikopo kwa wachimbaji wadogo wa madini kama chokaa, Serikali itekeleze azma yake ya kuwasaidia wachimbaji wadogo hasa wale wa chokaa wa Tarafa ya Makere, Bukoro na Kasulu, ili waweze kupata vifaa vya kisasa vya kutengenezea chokaa na kuisafirisha kwenda kwenye masoko. Wananchi hao wanaendelea kutengeneza chokaa kwa mtindo ule wa babu zetu miaka 100 iliyopita. Serikali iwasaidie ili wapambane na umaskini kiuhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii.

**MHE. JUMA S. KIDUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuipongeza Wizara hii ya Nishati na Madini, kwa juhudi kubwa inazozifanya katika kusambaza umeme nchini, chini ya Uongozi safi wa Waziri Yona na Mheshimiwa Dr. Ibrahim Msabaha, pamoja na timu ya wataalam ikiongozwa na Katibu Mkuu, Ndugu Rutabanzibwa, naomba nitoe kero kubwa katika Jimbo langu la Kilindi kama ifuatavyo:-

Mradi wa kupeleka umeme Makao Makuu ya Wilaya Mpya ya Songe kwa awamu kuanzia ile awamu ya Handeni hadi Kwediboma ambayo ilitakiwa kukamilika miaka mitatu iliyopita ni kero kubwa. Wananchi wanashukuru kuwa Meneja wa *TANESCO* wa Handeni, ndiye anayekwamisha mradi huu, kwa sababu za kisiasa dhidi ya Wilaya Mpya ya Kilindi. Naomba hoja hii ifuatiliwe maana inaimarisha ubovu wa mahusiano yaliyopo kati ya Wilaya ya Handeni na Wilaya Mpya ya Kilindi. Tunaomba mtusaidie katika kutatua kero hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wizara iainishe mpango mahsusi kwa ajili ya kufikisha umeme katika Mji Mdogo wa Songe, Makao Makuu ya Wilaya Mpya Kilindi mapema kutoka Handeni ili nishati hii itusaidie katika ujenzi wa Makao Makuu yenye huduma muhimu za kibiashara na kiuchumi kama viwanda na taasisi nyeti kama Hospitali, vyuo na mashule. Huduma zote hizi tunazipanua haraka sana kwa kuwa mahitaji ni makubwa sana na yanaendelea kupanuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii ili Wizara ipate fedha za kutatua kero nilizoorodhesha.

**MHE. SHOKA KHAMIS JUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, namshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kutujaalia tena kukutana leo, kwa mara nyingine tukiwa wazima na salama. Pili, napenda kumshukuru mtoa hoja, yaani Waziri wa Nishati na Madini.

Kwa kuanza kuchangia kwenye mada yenyewe, mimi nitaanzia kwenye nishati ya umeme. Umeme ndiyo chanzo cha maendeleo bila ya umeme hakuna maendeleo kwani hakuna kitu chochote cha kimaendeleo kisilichokuwa hakitumii umeme. Kwa hiyo, kutokana na umuhimu wa umeme, napenda kumwuliza Mheshimiwa Waziri kutokana na umuhimu nilioueleza, je, ni lini Serikali za Tanzania zitapeleka umeme wa kudumu katika Kisiwa cha Pemba, badala ya huu wa jenereta ambao si wa kudumu? Umeme ambao unakatikakatika mara kwa mara na kusababisha uharibifu wa vifaa vya raia maskini.

Siku za nyuma tulisikia kuwa kuna mpango wa kupeleka umeme Pemba kutoka Tanga, je, mpango huu Mheshimiwa Waziri ulifikia wapi? Naona kwenye hotuba yako jambo hili halimo wala halina ishara ya kuwemo karibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Wapemba tunategemea umeme wa jenereta sasa linapoharibika inakuwa ni giza Pemba nzima na maji nayo vile vile hatupati kwani maji hayaendi bila ya nguvu za umeme. Kwa hiyo, tunaomba na sisi mtuangalie, msituangalie kwa kupeleka kampuni za kutafuta mafuta tu kwani Serikali zetu zinaitambua Pemba kwa kutafuta faida tu lakini kwa kupeleka maendeleo Pemba haitajwi, ingawa tukisema hivyo Serikali mnakuwa wakali. Kuna sababu gani ya msingi mpaka leo umeme wa kudumu haujafika Pemba? Mbona sehemu mnakotaka mnapeleka?

Kuhusu suala la umeme uliokatwa Ungujam mimi napendekeza umeme ulipwe kwa sababu wananchi wanalipa sasa Serikali nayo ilipe, bila ya kulipa huo umeme utapatikana wapi? Ila napendekeza wasikatiwe lakini muelewane ili msikatishe maisha ya watu kwani umeme ukizimwa pengine wengine wanakuwa kwenye *operation* kwa hiyo, umeme ukizimwa inakuwa hatari.

Kuhusu suala la mafuta, napendekeza Mheshimiwa Waziri, mtuachie angalau na sisi tuweze kunyanyua uchumi wetu kidogo, hatuna vyanzo vya fedha Wanzabari, kwa hiyo, hili jambo lisiwe la Muungano.

**MHE. HAMZA A. MWENEGOHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kuwapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Wataalam wake wote, kwa matayarisho mazuri sana ya hotuba ya Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza ambalo nataka kulizungumzia hapa ni umuhimu wa nishati ya umeme katika Jimbo la Morogoro Kusini. Ninaomba nikiri hapa kuwa, nilikwishaiandikia Wizara ya Nishati ya Madini na kujibiwa kuwa gharama ya kupeleka umeme Jimboni mwangu, hatua ya kwanza umeme ukitokea Morogoro hadi Mkuyu ni jumla ya shilingi bilioni mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama umeme utakuwa umefikishwa Mkuyuni basi hapo hautafika Jimboni kwangu, kutabakia km 90 kufikishwa Jimboni kwangu. Kwa jinsi watu wa Jimbo langu wanavyohitaji Nishati hii tumefanya utafiti sisi wenyewe tukisaidiana na Uongozi wa *Seleous Game Reserve* na kugundua yafuatayo:-

(i) Umeme rahisi kwa Jimbo la Morogoro Kusini ni ule wa kutoka Kilombero - Mikumi.

(ii) Umeme hapa utapelekwa *Kisaki Station Village (Seleous Game Reserve),* inakutana na *Mikumi National Park* katika Jimbo la Morogoro Kusini.

(iii) Katika moyo wa kushirikiana na *Seleous Game Reserve,* wao wamesema watasaidia gharama za kueneza umeme toka Kisaki hadi Kijiji cha Mvuha, hapa watakuwa wamefikia vijij 22 ambavyo *Seleous Game Reserve* wenyewe watasaidia pia kusambaza umeme kwenye Kambi ya Matambwe na Hoteli ya Sebo. Vile vile kusambaza umeme kwenye Sekondari za Milengwelengwe na Selembala. *Seleous Game Reserve* wameahidi kusaidia huduma za umeme katika Kituo cha Afya Duthumi, Zahanati za Gomero, *Kisaki Station*, Mngazi, Sesenga, Kituo cha Afya Duthumi na Mvuha. Tafadhali tunaomba huduma ya nishati ya umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ni kuhusu uchimbaji madini ya dhahabu kiholela katika Tarafa ya Matombo. Tarafa hii imebahatika kuwa na madini mengi, yakiwemo na dhahabu. Inaonyesha wazi kuwa wachimbaji madini haya hawadhibitiwi na wanaingia kiholela. Je, ni msaada gani unaoweza kupatikana ili Serikali ipate haki zake na wachimbaji wadogo wadogo wafaidike? Tunaomba msaada.

**MHE. KABUZI F. RWILOMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuanza kwa masikitiko makubwa kueleza tatizo la fidia kwa wananchi waliohamishwa Mtakuja na fidia ya barabara ya Geita kwenda Ilogi Kahama. Ni zaidi ya miaka 4 wananchi hawa wanasubiri. Hivi sasa Wabunge wa Geita tunakabiliwa na hali ngumu kama fidia ya Mtakuja na barabara ya Geita Ilogi haitalipwa. Naomba yafuatayo yatekelezwe:-

Kwanza, fidia ya Mtakuja na barabara ya Geita Ilogi ilipwe na waliosababisha hujuma hizo washtakiwe kwani hali inaeleweka wazi.

Pili, barabara zilizopindishwa za Geita zirekebishwe kwa mfano, barabara za kupitia Ngankumbu irekebishwe ipitie Samina, Magena hadi *Cop Cot* mpaka Geita. Ngankumbu ni mbali sana na wananchi wanateseka. Mimi nimezunguka na wawekezaji ikaonekana inawezekana kwani haiingii Mgodini. Nilishafanya vikao na wananchi wa Magema wakakubali kutoa maeneo bila fidia. *GGM* haijatekeleza inapiga chenga. Tafadhali njia hii itipitishwe, namwomba Waziri amwagize Mr. Peter Turner, *Chief Executive Director* wa *GGM* akafungue njia hiyo, anaielewa vizuri.

Tatu, naomba wachimbaji wadogo wadogo waangaliwe upya. Kuna wachimbaji wengi wa dhahabu maeneo ya Rwangara, Nyarugusu, Nyakagwe, Bukoli na *Tembo Mine* (Meremeta). Naibu Waziri wa Nishati na Madini alipitia njia hiyo na kuona jinsi wanavyofanya kazi. Tatizo lao kubwa ni umeme. Tafadhali upelekwe umeme ili waweze kuzalisha dhahabu zaidi badala ya kuwaachia wageni.

Nne, tunaomba misaada inayotolewa na *GGM* iwe *formalized* kwa sababu haieleweki. Wanachelewa kutimiza ahadi zao na wakati mwingine haitolewi na hukwamisha maendeleo. Kwa mfano, mwaka 2002 tumeshindwa kufungua baadhi ya shule kwa mfano, Shule ya Sekondari Katoro kwa sababu ya ahadi zisizotimilika haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naomba Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, atueleze Wabunge wa Geita twende na jibu gani kuhusu fidia ya Mtakuja na Barabara ya Ilogi, kufupisha barabara ya kupitia Nyankumbu badala yake ipitie Samina- Magema *Cop Cot* hadi Geita. Wananchi wa Tarafa ya Butundwe na Busanda wanateseka sana. Naomba mumshirikishe Mr. Peter Turner katika hili analifahamu.

Wananchi wako tayari kutoa ardhi kwa ajili ya kupitisha barabara bila fidia kwani Mheshimiwa Mabina, Diwani wa eneo hilo, wamekwisha kutana na wananchi wakakubali kupitisha barabara. *GGM* tunaomba isipigwe chenga. Umeme uanze kusambazwa vijijini siyo uishie Mjini Geita tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaunga mkono hoja zangu zikijibiwa.

**MHE. KHADIJA SALEH NGOZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana nami nianze kuchangia Wizara hii ya Nishati na Madini kwa kumpongeza Waziri, kwa hotuba yake iliyojaa hekima na busara. Naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichangie kuhusu suala la umeme ukweli ni kwamba, ukataji wa umeme kwa muda wa saa Zanzibar haukuwa wa kiungwana japo *TANESCO* siyo Shirika la Muungano. Ilikuwa ni vema kabisa kabla hatua haijachukuliwa ya ukataji umeme Zanzibar, basi watendaji wa pande zote mbili, wangekaa pamoja, wajadiliane na wakubaliane ndipo uamuzi au hatua yoyote ichukuliwe baada ya maamuzi ya pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uamuzi ulifanywa wa kukatiwa umeme siyo tu umeathiri kwa upande wa Zanzibar, ambapo tumeathirika zaidi kisiasa na pia kwa upande wa Jamhuri ya Muungano, pia imeleta sura siyo nzuri huku ukizingatia kuwa Zanzibar ndiyo wanunuzi wakuu wa umeme. Uamuzi uliochukuliwa kwa upande mmoja wa nchi moja, lugha moja, siyo wa kufurahisha hata kama kulikuwa na haja ya kufanya hivyo. Mazungumzo ya pamoja ni muhimu zaidi hasa ukizingatia kuwa umeme unagusa au unahusisha maisha ya wananchi wetu kwa namna moja au nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. PAUL P. KIMITI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimshukuru Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, pamoja na Naibu wake na Katibu Mkuu, anayeongoza watumishi wote wa Wizara hii, kwa jitihada wanazoendelea kujenga heshima ya maliasili ya nchi hii, naunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri, atazame kwa undani masuala yafuatayo:-

Upatikanaji wa nishati vijijini hauwezekani kama sote tutabaki tukisubiri kuunganishwa na gridi ya Taifa. Yapo maeneo mengi yenye maporomoko ya maji, ambayo yangeweza kutoa umeme wa kutosheleza baadhi ya maeneo huko vijijini. Natoa mfano wa maporomoko ya *Kalambo Falls,* ambayo yako mpakani na Rukwa na nchi jirani ya Zambia. Maporomoko hayo ni muhimu kuanza kutumika kwa ajili ya nishati, lakini pia kama eneo la utalii.

Matumizi ya *Solar Energy* na pia ujenzi wa *Biogas* katika maeneo mengi ya wafugaji, ingekuwa ni kichocheo cha maendeleo katika maeneo husika.

Je, si ingekuwa kazi muhimu kwa sasa Wizara ikaondoa *programes* maalum katika kuwakomboa akina mama wa vijijini na kuhakikisha kila Wilaya inakuwa na mpango kamambe wa nishati vijijini?

Matumizi ya mkaa wa mawe, upate msukumo maalum kwa kutengeneza *brickets* za kupikia na la ziada ni kwa ajii ya kuchomea tofali. Tunaomba hili liwe la kufa na kupona ili mkaa wa mawe uliopo Namwele Sumbawanga, uanze kutumika vizuri. Wachimbaji wa mkaa wa mawe wasitakiwe kulipia kodi yoyote ile ili wavutiwe kuifanya kazi hiyo kwa nguvu zote. Huo utakuwa ukombozi kwa wananchi katika maeneo yote yasiyo na kuni.

Madini katika Mkoa wa Rukwa ni mengi na tungeomba Wizara itueleze yako wapi na ni ya aina gani na hata mafuta ya petroli yanasemekana kuwa yapo. Je, utafiti wa mafuta katika Bonde la Rukwa umefikia wapi. Eneo la *Chala Mission* Sumbawanga, linasemekana lina mafuta na madini mengi. Tumeambiwa kuwa eneo hili pia lina *Burma Rubby.* Je, ni kweli na kama yapo madini haya ambayo yana thamani nyingi sana, tunaiomba Serikali iutangaze Mkoa wa Rukwa kuhusu madini yaliyomo.

Ninashauri kuwa Mradi wa *IPTL* ununuliwe na Serikali kwa kushirikiana na *TANESCO*. Ni vizuri sana tukafanya hilo kuliko kusubiri tukaja kulazimika kufanya hivyo. Bado hali ya upatikanaji wa maji ya uhakika kwa kujaza mabwawa yote ya maji ya umeme siyo ya kutegemea. Lazima tuwe na *source* ya mbadala katika dharura ya aina yoyote ile. Kuendelea kusita kuamua hatma ya *IPTL* inaweza kutugharimu zaidi huko mbele. Tunaomba pia wachimbaji wadogo wa madini wakopeshwe vifaa vya kuchimbia madini.

Hili limekuwa likizungumzwa bila mafanikio. Ni vizuri kikawepo kifungu cha fedha za madini zitumike kwa kununulia mitambo kama hiyo kwa wachimbaji wadogo. Pia wachimbaji washauriwe wawe

na chama chao cha pamoja Kitaifa. Hii itakuwa ni nafasi yao ya kuweza kupambana na uonevu wowote utakaojitokeza. Umoja wao utawaendeleza vizuri katika kufanikisha azma hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii ya Wizara na kuwatakia mafanikio ya mpango wao kamambe wa kuendeleza Sekta ya Nishati na Madini.

**MHE. ANATORY K. CHOYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote naunga mkono hoja iliyopo mbele yetu. Pamoja na kazi nzuri inayofanywa na Wizara naomba kuchangia yafuatayo. Katika hotuba ya Waziri ukurasa wa 4 ibara ya 7 gharama ya kupeleka umeme Wilaya ya Biharamulo - Chato ni shilingi bilioni 5 na wakati huo huo katika kitabu cha 4 (Makadirio ya Fedha za Serikali (Sehemu A) kitabu ukurasa 158 *Project 3118 Electrification Biharamulo* inaeleza kuwa *Total Project* ni shilingi 4,700,620,000/= na maelezo yaliyotolewa katika *An Addendum on Development Projects Vote 58* imeonyesha ni shilingi 200,000,000/=. Kwa maelezo haya kama mtu haelewi mpangilio huu kwa kumbukumbu ya Bunge sahihi. Usahihi uko wapi na maelezo yasiyo na utata ni yapi.

Naomba maelezo ya kina. Vile vile uwazi wa maelezo haya utakuwa ni wa manufaa kwa wananchi wa Biharamulo. Vile vile katika maelezo ya hotuba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Uwekezaji na Biashara ukurasa wa 15 kuna maelezo ya uundaji wa Mfuko Maalum wa Nishati Vijijini *(Rural Energy Fund).* Je, mfuko huo uko wapi katika vitabu vya Serikali na kwa sasa una kiasi gani na matumizi yake yatakuwaje.

**MHE. CAPT. THEODOS J. KASAPIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ukurasa 5 sehemu ya 10 Wizara imeeleza utaratibu wa kuendelea kupeleka utaratibu wa kuendelea kupeleka umeme Makao Makuu ya Wilaya. Kwa masikitiko makubwa sisi Wilaya ya Mahenge/Ulanga umeme tayari umefika Wilayani Makao Makuu. Lakini umeme huo, huzimika mara nne (4) au mara tano (5) kwa wiki. Waziri Mkuu mwaka huu 2003 alipofika Mahenge na kulala Mahenge Mjini, umeme ulizimika mbele yake kwa saa saba (7).

Toka jana hadi leo Mahenge hakuna umeme kutoka Kidatu. Mkuu wa Mkoa ameshindwa kuwasiliana na Mahenge toka jana 23 Julai, 2003 hadi leo 24 Julai 2003 upasuaji wa wagonjwa Hospitali ya Wilaya umesimama, nyama zinaoza kwenye mafriji. Na hakuna yoyote anayeshughulikia suala hili. *TANESCO* naomba kupata majibu kwenye majumuisho ya Waziri. Iwapo mafundi watatumwa Mahenge kushughulikia suala hili kabla ya Bunge hili kumaliza kikao chake.

Pili, naomba Wizara iunganishe umeme wa Mahenge na umeme toka Kihansi/Kilombero/Mahenge. Badala kutoka Kidatu/Ifakara/Mahenge. Nitaunga mkono hoja baada ya kupata majibu. Vinginevyo nitatoa shilingi.

**MHE. RAYNALD A. MROPE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Mheshimiwa Daniel Yona, Waziri na Mheshimiwa Dr. Ibrahim Msabaha, Naibu Waziri, Ndugu Patrick Rutabanzibwa, Katibu Mkuu na wataalam wa Wizara yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna baadhi ya mambo katika Wizara hii ambayo sina budi niyazungumzie kwa lengo la kuboresha dira *(vision)* na mwelekeo wa Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza na *IPTL* kwa kirefu *Independent Power Tanzania Ltd.* Mkataba wake ulitiwa saini Juni, 1995 kati ya *IPTL* na *TANESCO* chini ya usimamizi wa Wizara ya Nishati. Utekelezaji wa Mkataba huu umegubikwa na mizengwe mingi kiasi kwamba leo hii Tanzania inajikuta ikiilipa *IPTL* shilingi 3.6 bilioni kwa mwezi na tutafanya hivyo kwa miaka 20 ijayo! Nchi kama Tanzania haiwezi kumudu gharama za aina hii ambazo kimsingi zimegubikwa na mienendo mingi ya rushwa kutoka kwa watumishi na viongozi waliokuwemo wakati huo na wengi wao bado wapo Serikalini hivi leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *IPTL* ilijiingiza kwa mkono wa rushwa na hivyo kupelekea kutotiwa saini Mkataba wa kutumia gesi ya Songosongo - *SONGAS.* Mwaka 1997 Benki ya Dunia ilikuwa tayari kutoa *USD 200* milioni kati ya *USD 350* milioni ambazo ndizo zilihitajika katika kutekeleza mradi huo.

Cha kushangaza *IPTL* ilipata haraka haraka *Government Agreement, Tax Exemptions* na mambo mengine ambapo *SONGAS* haikupata upendeleo wa aina hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama *IPTL* haingepitishwa kwa mizengwe mingi, umeme kwa kutumia gesi ya Songosongo ingeanza kutumika miaka 7 iliyopita na hivyo kunusuru hasara tuliyopata ya kutokuwa na umeme kutokana na ukame wa 1994 na pia mwaka 1997, kwa hiyo mradi ukafa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili la *IPTL* limeshughulikiwa na nguzo ya Mahakama hadi *International Centre for the Settlement of Investment Disputes* huko *London,* na nguzo ya pili *The Executive* ilifikisha suala hili *PCB* na *CID* ili washughulikie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nguzo ya tatu, Bunge halijajihusisha hata kidogo. Kuna masuala ya uwajibikaji kisiasa ambayo yanahusu viongozi wa siasa. Hatuwezi kukaa kimya na kuona nchi hii ikilipa fedha kiasi cha *trilion* moja katika miaka 20 ijayo, fedha za wavuja jasho wa Tanzania bila uwajibikaji wa kisiasa *(Political Responsibility).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati umefika wa kuunda Tume ya Bunge kuchunguza kwa kina skandali hii na kuwaadhibu viongozi wa kisiasa watakaobainika kuwa waliohusika kwa namna moja au nyingine. Tume hiyo iundwe wakati wa kikao hiki cha Bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba wakati huo huo nimpongeze ndugu Patrick Rutabanzibwa, Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati na Madini kwa uadilifu na kusimamia imara katika suala la *IPTL.* Bila yeye, nchi hii ingemalizwa vibaya sana na wajanja wachache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho nashindwa kuelewa kwa nini mradi wa umeme wa kuunganisha kati ya Masasi na Nyangao ili kuvipatia vijiji vya Chikukwe, Chigugu, Chikundi Mwema, Nangao na Nanganga umeme haijakamilika kwa zaidi ya miaka 15 sasa. Kinachotakiwa ni *step-down transformers* tano, waya na nguzo za kuunganisha Ndanda na Nangao km 8, na Nangao-Nanganga km. 10. mradi huu hauwezi kuzidi shilingi 200 milioni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati *TANESCO* inalipa shilingi 3.6 bilioni kwa mwezi kutokana na ulaji rushwa wanashindwa kuikamilisha mradi wa shs 200 milioni walioanzisha wenyewe *TANESCO* miaka 15 iliyopita. Wananchi wa Kusini waeleweje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Kamati ya Matumizi ya Bajeti hii, suala hili lisipopatiwa ufumbuzi, nitalileta tena. Kama mwana-CCM imara naunga hoja ya Wizara lakini siridhiki na sikubaliani na uongozi wa Wizara hasa kwa jinsi wanavyotunyima huduma za umeme katika jimbo langu.

**MHE. BAHATI ALI ABEID:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nianze kwa *TANESCO* kuikatia umeme Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Serikali zetu mbili ndizo zilizowekeana Mkataba wa juu ya umeme na wala siyo *TANESCO,* sasa imekuwaje Zanzibar imekatiwa umeme? Je, huu si udhalilishaji na unyanyasaji na kutiana hasara kwa makusudi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ni malipo mbona Zanzibar inalipa hivi ukimdai mtu akichelewa kidogo kukulipa unapaswa kumhujumu au kumpeleka panapohusika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nende kwenye gesi, Serikali ya Muungano inafanya matayarisho ya kuanza kuitumia gesi je, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar imeshirikishwaje angalau kwa mazungumzo ya gesi hiyo? Na ni viongozi gani walioshiriki kwenye mazungumzo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamwomba Mheshimiwa Waziri anijibu. Baada ya kuchangia machache ninaomba niunge mkono hoja hii. Ahsante.

**MHE. JACOB D. SHIBILITI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa nafasi hii ili nami nichangie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wengine wa Wizara kwa hotuba nzuri inayoeleweka.

Mheshimiwa Mwenyekiti nianze mchango wangu kwa kuishukuru Serikali kwa kazi nzuri na ngumu ya kugawa umeme kwa nchi yetu ya Tanzania. Si rahisi kumaliza matatizo yote lakini ukweli Wizara imefanya kazi nzuri. Ninaipongeza Serikali kwa niaba ya wananchi wa Misungwi kwa kuwapatia umeme wananchi wa vijiji vya (1) Mabuki hali iko katika hatua za mwisho (2) Inonelwa nguzo na vifaa vipo bado kuikamilisha (3) Shule ya Sekondari Misasi vifaa vipo bado kuikamilisha kuwasha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Misungwi wanaomba vijiji vifuatavyo viwekwe kwenye mpango wa kupelekewa umeme:-

1. Buhingo Seeke na Busongo Sekondari umbali wa kilomita 5 toka nguzo zilipoishia.

2. Koromije, Kanyerere na Kijima.

3. Kijiji cha Fella hapa ni muhimu kwani (a) ni *station* ya garimoshi mizigo mingi hupaswa kuteremshwa wakati wote na kuna mpango wa kuwa Bandari ya nchi kavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona nitoe umuhimu kwa vijiji vichache kwa kujua si rahisi kukamilisha vijiji vyote vya Tanzania kwa Misungwi naomba vijiji hivyo vipewe umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu madini Wilaya ya Misungwi inayo madini ya aina ya Almas sehemu ya Mabuki na Mwamanga. Pia dhahabu inasemekana katika eneo la Mwamazengo, Buhunda Kabale na Shilalo ipo ya kutosha. Wawekezaji wanakaribishwa ili pato la Taifa liweze kuongezeka hivyo Serikali itapata pesa nyingi na kupunguza kero kwa wananchi wake kwa kuwapa huduma bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukweli wananchi wengi wamekuwa na wasi wasi na wawekezaji juu ya kuchukua mchanga na kuupeleka Ulaya hivyo nchi au eneo husika kubaki wazi hali hii inaharibu mazingira ni vyema Serikali ikaboresha sera ya madini ili kuondoa utata uliopo ambao huenda ukaleta tafsiri mbaya isiposhughulikiwa mapema. Vile vile ni vyema ukaangaliwa utaratibu wa kuvipatia Mrahaba vijiji au Halmashauri za Wilaya ili kukidhi shughuli za awali wakati mgao wa jumla unasubiriwa toka Serikalini kama ilivyo kwa Hifadhi za Taifa *(TANAPA).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina ugomvi na Wizara hii naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja naomba wapewe pesa wakafanye kazi. Ahsante sana.

**MHE. MOHAMED A. ABDULAZIZ:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la umeme wa Mikoa ya Kusini Lindi, Mtwara na Ruvuma nataka maelezo ni kwa nini Serikali haipo tayari kutupatia umeme wa uhakika kutoka *Songosongo Gas.* Gesi ya *Mnazibay* ni kiini macho kwani fedha zilizotolewa na *World Bank* shilingi 15,000,000,000/= ziliazimwa na kupelekwa kusaidia kuondoa tatizo la umeme Dar es Salaam miaka saba (7) iliyopita. Hadi leo fedha hizo hazijarejeshwa na wala Serikali haizitaji katika hotuba. Nitaomba maelezo kabla ya kukubali kifungu.

*World Bank* imetoa fedha shs. bilioni 174 lakini gharama halisi za Mradi ni bilioni 114 tu. Hivyo Shs. 60,000,000,000/= zinabaki *World Bank* na Serikali inatakiwa iandae mradi mwingine wa kutumia fedha hizo. Kwa nini Serikali isitumie shilingi bilioni 60 hizo kupeleka umeme wa Songo Songo katika mikoa ya Lindi na Mtwara? Naomba maelezo ya Waziri kwa nini fedha hizo zisitumike kupeleka umeme Lindi. Hali ya umaskini katika Mikoa ya Lindi na Mtwara inachangiwa na ukosefu wa umeme wa uhakika.

Niliuliza kwenye hotuba ya Waziri Mkuu hivi ni kama wapi ambapo kuna raslimali kama hii ya gesi ya Songosongo lakini wenye mkoa huo hawafaidiki. Huu ni uonevu. Nitaunga mkono hoja hii baada ya maelezo ya Waziri na si vinginevyo.

**MHE. KHAMIS SALUM ALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri naomba nipate maelezo ya kwa nini Serikali haijakemea kitendo cha hivi karibuni cha *TANESCO,* kudhibiti kuikatia umeme Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa muda wa masaa matatu. Mheshimiwa Waziri tunaelewa kuwa Wizara yako inahusika moja kwa moja katika kutekeleza na kusimamia Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2000 kuhusu swali hili la kuimarisha umeme sehemu zote nchini na hii haliwahusu Menejimenti ya *TANESCO* (Ilani).

Mheshimiwa Waziri kwa nini *TANESCO* inataka kutuharibia Umoja wetu wa SMT na SMZ kudhubutu kuikatia umeme Serikali kwa ghafla. Iwapo Serikali haitomkemea Meneja wa *TANESCO* anaweza kutuweka pahali pabaya kwa upande mmoja wa Muungano kutokwa na imani kwa hilo. Suala ambalo limefanywa na *TANESCO* limetuharibia sana tena sana siasa Zanzibar. Tunaowajibika kwa hili ni mimi na wewe ni maana ya viongozi wa SMT na SMZ kwa kulinda chama chetu. Pia lingine ukatwaji wa umeme siku hiyo umezua tatizo kwa wawekezaji nchi nzima Zanzibar, wananchi na huduma mbalimbali kwa masaa hayo. Imani inapungua kwa suala hiilo.

Mwisho kwa swali hili, nakuomba Mheshimiwa Waziri iwapo unakubaliana na mawazo yangu, suala hili litolee kauli nzito na kumkemea Meneja hapa hapa Bungeni ajue kuwa kitendo alichokifanya sio kizuri kwa nchi yetu Tanzania ambayo ni nchi ya Muungano. Swali la Utafutaji wa Mafuta Nchini

Nakuomba Mheshimiwa Waziri suala hili liendelee vizuri kwa majadiliano ya pamoja baina ya SMT na SMZ na hapo itapoamulika kutendwa kazi hiyo kuwe hakuna matata. Napenda nitamke wazi kuunga mkono hoja ya Wizara yako. Lakini zingatia kwa vizuri maswali yangu hayo mawili yaani *TANESCO* na utafutaji mafuta.

**MHE. MUDHIHIR MOHAMED MUDHIHIR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Kwa miaka minane sasa nimekuwa nikiomba bila ya mafanikio, kupatiwa umeme katika vijiji vya Mchinga na Ng'apa. Wananchi wa Vijiji hivi jimboni Mchinga, Wilayani Lindi wamekata tamaa. Kijiji cha Mchinga ni Makao Makuu ya jimbo, ipo Mahakama ya Mwanzo, Ofisi ya Katibu Tarafa na Kata, Zahanati, Shule za Msingi mbili na shule moja ya Sekondari. Ipo Misikiti ya Ijumaa mitatu. Robo tatu ya samaki wanaoliwa mjini Lindi huvuliwa Mchinga hivyo kuhitajika huduma za umeme kwa ajili ya kuhifadhi samaki.

Kijiji cha Ng'apa ambacho ni Makao Makuu ya Tarafa na Kata, kina Mahakama ya Mwanzo na Shule mbili za msingi. Ni Kijiji kinachotegemea biashara ya nazi na mafuta ya nazi. Pangekuwa na umeme ukamuaji wa mafuta ungeinua kipato cha wananchi. Nimefikisha kilio hiki kwa Mawaziri wa Wizara hii na nimeandika barua kuhusu suala hili. Nimekuwa nikipewa ahadi ambazo hazitekelezwi.

Mwaka 2001 *TANESCO* walipeleka wataalam wa Mchinga na kuwapa matumaini makubwa wananchi. Makisio wakati huo yalifikia shilingi milioni mia moja na ishirini (milioni 120). Sasa ni miaka miwili hatujaona sini wala nuni.

Namwomba Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini leo atutamkie wananchi wa Mchinga na Ng'apa iwapo na sisi tunayo haki ya kutumia umeme kama walivyo wenzetu wenye huduma hii. Aidha, Waziri atuambie ni lini tutapatiwa huduma hii. Namwomba Mwenyezi Mungu amuongoze Mheshimiwa Waziri na awaongoze wasaidizi wake katika kupokea kilio chetu hiki na kutupatia suluhisho. Halipo linalomshinda Mwenyezi Mungu na inshallah hili litafumbuka. *Amin.*

**MHE. PROF DAIMON M. MWAGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza hotuba ya Mheshimiwa Waziri na ninaiunga mkono mia kwa mia.

Ningependa kusema kuwa inasikitisha sana kuona Mheshimiwa Waziri katika ibara 22 anazungumzia juu ya umeme wa makaa ya mawe ya Mchuchuma kwa kupita tu!! Mradi wa umeme kwa kutumia makaa ya mawe kwa taarifa zilizopo umefikia hatua ya juu ya umepata wawekezaji.

Tatizo lililopo ni ugumu wa kugeuza mtazamo wa Wizara kuhusu mradi huu. Bado Wizara na *TANESCO* yenyewe haiamini kuwa mradi huu utachangia katika utoaji wa umeme nchini kwa bei nafuu. Naomba sana kuwe na "change of mind" kwa Wizara na *TANESCO* kuhusu mradi wa umeme wa makaa ya mawe wa Mchuchuma.

Pili naomba kukumbushia mradi wa umeme kutoka Iyenge kwenda Pwaga ambao utatekelezwa kwa fedha za *TANESCO* kwa sababu ni mradi ambao umo chini ya uwezo wa Shirika. Kila kitu kimekamilika isipokuwa taratibu za kupata fedha ili mradi uanze. Naomba sasa taratibu hizo ziharakishwe kwa sababu wananchi wa Pwaga wamekuwa wakisubiri kwa hamu kubwa.

**MHE. SHAIBU AHAMADA AMEIR:** Mheshimiwa Mwenyekiti na mimi nitaanza kujiunga na wenzangu kuchangia hotuba hii ya Waziri wa Nishati na Madini ambayo imesomwa leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti kwanza nianze kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri na inayotia tamaa ya kuleta maendeleo kama itatumiwa kama ilivyopangwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na bei kubwa ya umeme, wananchi wengi wanashindwa kutumia nishati ya umeme kutokana na hali zao kuwa duni kimapato. Kwa hivyo wananchi wengi hutumia mafuta ya kerosene kwa matumizi ya kila siku majumbani. Pia hata wananchi wenye kipato cha chini pia hawamudu kutumia nishati ya umeme kwa kupikia, hivyo basi nishati ya mkaa hutumika. Pamekuwa na ongezeko kubwa la matumizi ya nishati ya mkaa kuliko matumizi ya majiko ya umeme. Hii inadhihirisha wazi bei ya umeme ni kubwa, na umekuwa kwa matumizi ya wenye uwezo tu. Umeme wetu pia una matatizo ya kukatika mara kwa mara bila ya kutaarifiwa watumiaji wa maeneo yatakayokatika hapo kabla. Baadhi ya wakati usumbufu huu husababisha uharibifu wa vyombo vya majumbani na kusababisha hasara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule Zanzibar suala la kukatika umeme mara kwa mara husababisha kukatika maji jambo ambalo pia ni kero. Kitendo cha kukatwa umeme Zanzibar kuanzia saa 7 mchana hadi saa 11 jioni siku ya Jumatatu ni kitendo cha kusikitisha sana kwani Zanzibar ni sehemu ya Muungano. Na Muungano huu ni wa kidugu kabisa maana sasa tumekwishachanganya damu. Panapotokea tatizo sehemu moja ya Muungano wetu ni budi lazima busara ipite ili pande zote ziridhiane, ili upande mmoja wa Muungano usimlaumu mwenzake. Tokea hilo tokeo kupita mpaka sasa hakuna kiongozi yeyote aliyetoa tamko angalau la kutuliza zogo hili wanalolalamika Wabunge kutoka Zanzibar kwa hisia ya Serikali ya Zanzibar kudhalilishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa leo sina zaidi na mimi naiunga mkono mia kwa mia.

**MHE. ROBER K. MASHALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie nafasi hii kuchangia hotuba hii ya Waziri wa Nishati na Madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti umeme ni maendeleo ili tuweze kufanikiwa kwenye suala zima la kupunguza umaskini lazima tuimarishe huduma za umeme kwenye maeneo ambayo hayana umeme na hasa Makao Makuu ya Wilaya zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakulima wetu wamekuwa wakizalisha mazao mengi lakini wanakosa bei ya uhakika kwa vile mazao hayo hayana ubora unaotakiwa na hayajasindikwa hivyo yanakuwa na bei ya chini lakini tukiimarisha huduma hii mazao ya wakulima yatasindikwa na yatanunuliwa kwa bei nzuri na mkulima wetu tutamwondolea umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile tukiimarisha huduma hii vijana wetu wataanzisha viwanda vidogo hivyo kujiajiri na wengine kuajiriwa na viwanda vikubwa hivyo tutapunguza tatizo la ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nichangie kwenye eneo la Madini. Madini yanachangia kwa kiwango kikubwa katika pato la Taifa lakini athari zinazotokana na uchimbaji wa madini ni mkubwa sana na hazizibiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasikitisha Serikali inapoamua kuruhusu wachimbaji wakubwa wenye vifaa vya kisasa kuingia kwenye eneo la hifadhi na kufanya utafiti wa kuchimba madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hifadhi zilizotengwa zimetengwa kwa ajili ya kuhifadhi rasilimali zilizomo kwenye eneo hilo ikiwa pamoja na wanyama, misitu, mito na ardhi vile vile kwa manufaa ya vizazi vyetu unaporuhusu uchimbaji ufanyike kwenye eneo hili ina maana misitu yote itateketea, wanyama, wataisha, vianzo vya maji vitakauka, na ardhi itaharibiwa. Hivyo Taifa halitakuwa na eneo kwa ajili ya vizazi vijavyo. Nashauri Serikali ihakikishe maeneo ya hifadhi yasimilikishwe kwa wachimbaji na badala yake yaangaliwe maeneo ya wazi wapewe kwa ajili ya uchimbaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie suala la wachimbaji wadogo. Wachimbaji wadogo wamekuwa hawana haki ndani ya nchi yao hauna sera inayowalinda wachimbaji wadogo wanapogundua madini badala yake wanafukuzwa na wanaletwa wachimbaji wakubwa. Nashauri Serikali iandae sera itakayowapa haki wachimbaji wadogo kumiliki eneo la madini walilogundua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suingi mkono hoja hii mpaka Mheshimiwa Waziri atoe ufafanuzi juu ya kauli aliyoitoa wakati wa kufungua Mradi wa Umeme Geita kuwa Wilaya 16 za Tanzania Bara kupata umeme kabla ya mwaka 2004. Kauli hii ingeaminika kama ingekuwemo kwenye Mpango wa Serikali, kwenye hotuba hii ambayo Mheshimiwa Waziri amewasilisha. Hivyo naomba ufafanuzi ili nishawishike kuunga mkono.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. Ahsante.

**MHE. CHARLES H. KAGONJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Waziri Daniel Yona. Naibu wake Mheshimiwa Ibrahim Msabaha kwa kazi nzuri wanayoifanya. Zaidi ya hayo nampongeza pamoja na wafanyakazi wote wa Wizara hiyo Katibu Mkuu Bwana Patrick Rutabanzibwa kwa kufanya kazi nzuri.

Kwa vile jimbo langu ni la vijijini na kero yangu kubwa kwa Wizara hii ni umeme vijijini basi nitaendelea kuzungumzia jambo hilo. Kwanza sina hakika kwamba suala la kueneza umeme bado lipo au vipi? Kama ni kweli bado mpango huo upo basi ni vema Wizara ikaonyesha wazi wazi kwa kutaja majina ya vijiji badala ya maelezo ya jumla tu. Kama nilivyouliza swali jana Na. 291 bado ninaomba Wizara ya Nishati na Madini kufanya kila iwezalo kupeleka umeme katika vijiji hivyo vya Mlesa, Dule, Ngazi, Zaizo na Mhelo. Kama nilivyosema vijiji hivyo vilikuwa katika mradi wa umeme Mlalo na kwa bahati mbaya havikupata umeme wakati mradi huo ulipokamilika.

Licha tu kwamba vijiji hivyo vilichangia gharama mbalimbali miongoni mwa gharama za mradi huo, gharama ya sasa ya kuvipelekea umeme vijiji hivyo kama kweli ni shilingi 200,000,000/= kutokana na majibu ya swali langu basi hicho ni kiasi kidogo sana kwa miradi ya umeme. Naomba fedha hizo zitafutwe na vijiji hivyo vipatiwe umeme.

Kama kweli mpango wa umeme vijijini bado upo naomba Wizara hii na Shirika la Umeme *(TANESCO)* Tanzania kuangalia yale maeneo ya nchi yetu ambayo wananchi wamefikia kiwango cha juu katika vita ya kupambana na umaskini wawezeshwe kuruka mbele zaidi kwa kupelekewa umeme badala ya kuvutwa shati nyuma.

Kwa hili nasemea hasa mahitaji ya umeme Kata ya Rangwi, Sunga, Mtae, Mizazi pamoja na vijiji vya Gologolo na Mamolo. Kwa kweli nimesema hapa Bungeni mara kadhaa kuhusu vigezo vyote muhimu kwa maeneo hayo kupatiwa umeme. Pili, mradi wa umeme Mlalo hautakuwa na faida zaidi kwa Shirika kama maeneo hayo niliyotaja hayapewi umeme.

Mradi wa Umeme Mlalo una umeme wenye nguvu sana. Una nguvu ya *KV 33* hivyo ukiendelea kubaki katika maeneo yale yale tu ni hasara kubwa kwa Serikali. Nasema kwa dhati kabisa maeneo hayo yanastahili kupelekwa umeme. Naomba sana jambo hili liangaliwe kwa makini. Kuhusu sekta ya madini ningependa nitilie mkazo eneo la usanifu wa madini. Suala la kusanifu Tanzanite hapa nchini lina

umuhimu mkubwa sana. Kwa sababu hiyo jambo la kuhimiza uwekezaji na ujenzi wa Kiwanda cha Kusanifu hayo madini ya Tanzanite.

Taarifa na ramani za madini ni zile za zamani sana. Nina hakika yapo maeneo mapya ambayo yanaweza kupatikana madini hivyo ni vema tukapewa ramani ya maeneo mapya ya madini.

Napenda kuchukua nafasi, hii kumpongeza Naibu Waziri wa Nishati na Madini kwa kutembelea Wilaya yetu ya Lushoto pamoja na jimbo langu la Mlalo. Namshukuru sana sana kwa kufika na kuona mwenyewe pamoja na wataalamu wa Wizara. Naunga hoja mkono.

**MHE. ARIDI M. ULEDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kupata nafasi hii ili niweze kuchangia hoja ya Waziri wa Nishati na Madini, Mheshimiwa Daniel Yona. Kwanza nampongeza Waziri kwa mawasilisho mazuri ya hotuba yake ya Bajeti. Vile vile nitumie nafasi hii kumpongeza Naibu Waziri Mheshimiwa Dr. Ibrahim Msabaha kwa kazi nzuri ya kumsaidia Waziri katika kuandaa Bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini. Aidha, nitumie nafasi hii vile vile kuwapongeza kuanzia Katibu Mkuu, Wakurugenzi na wafanyakazi wote wa Wizara ya Nishati na Madini kwa maandalizi mazuri ya Bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu unaanzia kwenye bili za umeme. Tumezoea kupata bili za umeme ambazo ni za makadirio tu *(estimates)* ambazo mara nyingi huwa ni za juu sana kuliko matumizi halisi. Hali hii huwafanya wateja walipe zaidi kwa sababu tunajua kuwa jinsi matumizi yanavyokuwa makubwa ndivyo mteja anapolipa zaidi. Naomba tabia hii ya kukadiria matumizi ya umeme ikomeshwe kwani inaleta usumbufu mkubwa sana kwa wateja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nizungumzie umeme wa *LUKU.* Wateja wa umeme wa *LUKU* hawana uhakika juu ya kupata umeme kiasi gani kwa fedha zile zile wanazolipa. Mfano ukienda na shilingi 5,000/= leo, kiasi cha umeme utakachopata hailingani na kila utakachopata kwa fedha hiyo hiyo ya shilingi 5,000/= wiki moja au mbili zijazo. Je, ni sababu gani zinafanya hali hiyo itokee? Naomba maelezo yakatolewa juu ya kutotabirika gharama za umeme wa *LUKU.*

Naomba sasa nizungumzie hali ya kukosekana umeme kwenye jimbo langu la Nanyumbu. Jimbo la Nanyumbu halina umeme licha ya kuwa Wilaya ya Masasi inazalisha umeme wa kuaminika na kutosha ukilinganisha miji mingine ya Mkoa wa Mtwara na Lindi. Umeme wa Masasi umesambazwa hadi Wilaya za Newala, Tandahimba, Nachingwea na Ruangwa. Kitu gani kinafanya umeme wa Masasi usifike Mangaka ambayo ni Makao Makuu ya jimbo la Nanyumbu ambapo ni kilomita 50 tu kutoka Masasi Mjini unapozalishwa umeme huo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mangaka licha ya kuwa Makao Makuu ya jimbo vile vile ni Makao Makuu ya Kata ya Nangomba. Aidha, kuna Taasisi kadhaa kama Shule ya Sekondari ya Mangaka, Shule za Msingi za Mangaka, Kilimahewa, Ngalinje, Nachiwa, Mwambani, Ndwika, vile vile kuna kituo cha afya Mangaka, Misheni, Makanisa, Misikiti, Maduka, Vituo vya Petroli, Kituo cha kuendeleza zao la Korosho, Nyumba za Kulala wageni, Mahoteli, Mabaa, Masoko, Vyama vya Ushirika na Mashine za Kusaga Nafaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutoka Masasi kupelekea Mangaka kuna Taasisi muhimu sana ambazo zinakosa umeme kama Shamba la Mifugo la Nangaramo, Ofisi ya Kata ya Mikangaula, Kijiji maarufu cha Nangomba, Shule za Msingi za Namatumbusi, Kilosa, Mihangaula, Nangaramo, Nangomba, vile vile Kijiji njiani kuwa na mashine kadhaa za kusaga nafaka. Lakini vile vile jirani na Mji wa Mangaka kuna vituo vya afya vya Nanyumbu na Michiga kila kimoja umbali wa kilomita 25 kutoka Mangaka. Hivyo vyote vimekosa umeme. Naomba Serikali ipeleke umeme wa Masasi kwenye jimbo la Nanyumbu ili kuondoa kero ya kukosa nishati hii muhimu sana katika kuleta maendeleo ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jimbo la Nanyumbu vile vile linayo madini hasa ndani ya hifadhi ya Lukwika - Lumesule lakini wananchi ambao zamani walikuwa wanachimba hapo waliondolewa wakati wa kuanzisha hifadhi hiyo. Kitendo hicho kimewakosesha wananchi hao kipato kwani kila wakijaribu kulima mazao yanashambuliwa na wanyama kutoka kwenye hifadhi hiyo. Naomba Serikali ikawaruhusu wananchi kuanza kutumia madini tena katika maeneo ambayo waliondolewa ili waondokane na umaskini walionao sasa. Sehemu hiyo ni Lumesule chini ambayo kwa sasa ni sehemu ya hifadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo nitamke kuwa naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Mwisho nashukuru tena kwa nafasi hii. Ahsante sana.

**MHE. PROF. PIUS P. MBAWALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naiunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Hata hivyo ningependa kujua hatma ya upatikanaji wa umeme wa *Grid* toka Makambako hadi Namtumbo kupitia Njombe na Songea.

Waziri wa Fedha yuko *sympathetic* na azma hiyo maana umeme huu wa *Grid* utaweza kufika pia Mbinga kushughulikia kiwanda cha kahawa cha Songea kiwanda cha Tumbaku. Kilio cha wananchi kuhitaji *Grid Electricity* toka Makambako kimemfikia pia Mheshimiwa Waziri Mkuu akiwa Wizarani Mkoani Ruvuma wakati wa Mei/Juni 2003.

Mheshimiwa Basil Pesambili Mramba, anangoja barua toka Waziri wa Nishati na Madini kusudi pafanyike *feasibility study* wakati wa 2003/2004. Barua hii upatikanaji wake unangojwa kwa hamu sana toka kwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati na Madini. Ahadi zimekuwa nyingi lakini utekelezaji wake umekuwa mgumu sana sana. Tafadhali sana suala hili lipewe uzito unaotegemewa ili *feasibility study* hiyo ya utakaji umeme Makambako-Njombe-Songea hadi Namtumbo na Mbinga ukamilike.

Tayari Sweden inagharamia ufungaji wa umeme Makambako *Grid Line* hadi Njombe. Hivyo *feasibility study* ni kati ya Njombe hadi Namtumbo na Mbinga kupitia Songea. Waziri wa Fedha Mheshimiwa Mramba (Mb.) yupo tayari kutoa fedha hizo za f*easibility study.* Tafadhali sana tunaomba hiyo itekelezwe maana Waziri wa Fedha hawezi kutoa fedha hizo kabla ya kupokea barua toka kwa Wizara hii ya Nishati na Madini. Ahadi zipo lakini utekelezaji wake ni kama umesimama kulikoni?

Vile vile *Grid Lines* zikifika Namtumbo Sweden imeahidi kushughulikia *Distribution* vijijini, Wilayani Namtumbo. Barua kuhusu suala hili ninayo. Chonde wana-Ruvuma tunasubiri sana kwa hamu, barua kwenda Wizara ya Fedha kufanyia *feasibility study.* Kwa *spirit* hiyo naomba tena kuunga hoja mkono na matumaini sana ahadi zilizotolewa na Waziri Mheshimiwa Yona (Mb.) kwangu za mara kwa mara.

**MHE. ALHAJI SHAWEJI ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuanza kwa kuunga mkono hoja ya Bajeti ya Waziri wa Nishati na Madini.

Mchango wangu unahusu kupatiwa umeme kwa Hospitali ya Berega, Shule ya Mfano wa Mgugu, Magubike na Maguha.

Nafurahi kueleza kuwa Naibu Waziri Mheshimiwa Dr. Ibrahim S. R. Msabaha (Mb.) alifika na kutembelea vijiji hivyo nilivyovitaja juu kufuatia maelekezo ya Ikulu yaliyotolewa Wizarani na Mheshimiwa Benjami William Mkapa, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano alipotembelea alitoa ahadi ambazo zilikuwa binafsi. Amechangia T.Shs. 3,000,000 kwa kuendeleza ujenzi wa Sekondari ya Mfano ya Mgugu, alieleza angemuomba Mama Anna Mkapa achangie utoaji wa madawa katika Hospitali ya Berega inayotoa huduma za matibabu kwa Mikoa minne ya Mkoa wa Manyara, Tanga, Dodoma na Morogoro.

Nafurahi kukujulisha kuwa Mama Anna Mkapa alitoa msaada wa madawa kwa Hospitali ya Berega kwa jumla ya Tshs. 1,000,000 (shilingi milioni moja). Pamoja na kutoa michango yake binafsi Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, pia alitoa ahadi ya kutoa magodoro mia mbili (220) kwa ajili ya wanafunzi wa Shule ya Mfano ya Mgugu. Na pia alieleza atakuwa anatembelea Shule ya Mgugu na Hospitali ya Berega bila kutoa taarifa rasmi Kiserikali. Mheshimiwa Waziri nafurahi kukujulisha ziara ya aina hiyo tayari Mheshimiwa Benjamin William Mkapa ameshafanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafurahi kukujulisha Mheshimiwa Benjamin William Mkapa ametimiza ahadi zake zote hizo. Hata ya maombi ya kupatiwa umeme ametimiza kwa kuiambia Wizara ya Nishati na Madini kupeleka umeme. Uthibitisho huo unadhihirika pale Wizara ya Nishati na Madini walipoagiza *Regional Manager* wa Mkoa wa Morogoro apeleke makisio ya gharama za kupeleka umeme

katika sehemu nilizozitaja *Regional Manager* wa Mkoa wa Morogoro amefanya hayo makisio na kusema mradi huo wa kupeleka umeme ni *viable* kiuchumi.

Pamoja na maelezo hayo ya *Regional Manager,* pia Naibu Waziri wa Nishati na Madini alithibitisha kupata maagizo hayo ya Ikulu na kwamba kutembelea kwako ilikuwa kujiridhisha yeye mwenyewe binafsi na akafika kuwaambia wananchi katika sehemu hizo kuwa suala la kuleta umeme sasa ni lake yeye na Wizara ya Nishati na Madini, halipo tena kwenye mabega ya Mheshimiwa Mbunge wa jimbo la Kilosa Alhaji Shaweji Abdallah.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa katika hotuba ya Waziri wa Nishati na Madini ametamka chini ya *programme* ya institutional support mpango unaofadhiliwa na Serikali ya Sweden utekelezaji wa sera mpya ya nishati umeanza. Amesema katika hotuba Wizara inafanya maandalizi ya kuanzisha Wakala wa Nishati Vijijini *(Rural Energy Agency)* na Mfuko wa Nishati Vijijini *(Rural Energy Fund)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia kuwa Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Naibu Waziri, Dr. Ibrahim S. R. Msabaha (Mb.) wamethibitisha kupokea maagizo ya Rais ya kupeleka umeme katika maeneo niliyoyataja na kwa kuwa ripoti ya *Regional Manager* wa *TANESCO* Mkoa wa Morogoro amethibitisha makisio ya kujenga mradi huo kuwa kiuchumi upo viable na kwa kuwa Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, alitoa ahadi ya kupeleka umeme katika maeneo hayo na kwa kuwa Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ametamka atakuwa anafanya safari binafsi kutembelea maendeleo ya Berega Hospitali na *Mgugu Secondary School.* Naomba kuishauri maeneo haya yawemo katika *programme ya Institutional support,* na yawemo katika mipango ya itakayosimamiwa na *(Rural Energy Agency)* Wakala wa Nishati Vijijini na pia naomba Mfuko wa Nishati Vijijini *(Rural Energy Fund)* ujumlishe vijiji vya maeneo hayo ili isije ikatokea aibu ya kutotekeleza ahadi ya Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, atakapoulizwa endapo atafanya ziara binafsi kama mwenyewe alivyosema na alivyokwishaanza kufanya ziara za aina hiyo za kibinafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namuomba Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini anipe majibu ya hoja zangu hizi kwa maandishi ili nikiwa Mbunge wa maeneo haya niwe na majibu ya kuwapa wananchi wa maeneo haya. Naunga mkono hoja.

**MHE. JOHN E. SINGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Wakurugenzi na watendaji wa Wizara ya Nishati na Madini kwa kazi ngumu wanayofanya ya maendeleo ya nishati na madini nchini. Nawapongeza kwa sababu nishati na madini ni nyenzo muhimu kwa maendeleo ya uchumi ya nchi yetu; na miundombinu ya maendeleo hayo ni duni kwa nchi maskini kama Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu katika hoja ya nishati na madini umelenga katika maeneo matatu: Umeme vijijini, nishati mbadala na utafiti wa madini nchini. Kwa kuanza naiomba Wizara iweke juhudi kubwa kumaliza viporo vya kupeleka umeme mahali pote ambapo njia za umeme umepita. Hakuna maana yoyote kuendelea na usambazaji wa umeme maeneo mapya ikiwa maeneo ya zamani umepita tu bila kuhudumia watu waliopo. Mfano mzuri ni kule katika Wilaya yangu ya Same ambapo yapo maeneo yalipitishwa na njia ya umeme bila kupewa huduma wala wananchi waishio hapo kupewa sababu za kunyimwa umeme.

Maeneo hayo ni Ijinyu (line ya Same - kisiwani/Mbaga), Bangalala, Mkanyeni, Mgwasi (*line* ya Mwembe -Makanya - Hedaru), Majengo mapya na mabilioni (*line* ya Hedaru-Mabilioni). Maeneo haya yako yaliyokuwa yamelengwa kupatiwa umeme katika njia za miradi ya umeme niliyotaja. Je, kumetokea nini maeneo hayo yakakosa umeme iwapo Wizara iliyaweka katika mpango wake wa kupeleka umeme vijijini? Inasemekana kuwa mipango mizuri ipo lakini inaharibiwa na maagizo ya baadhi ya viongozi kuhamisha vifaa vya umeme vilivyokusudiwa mahali fulani na kupelekwa mahali pengine. Naiomba, Wizara na ilisahihishe hili ili kuepuka athari za kufanya kazi kama Zimamoto!

Pia naomba Wizara kwa juhudi za makusudi iwawekee umeme wananchi wa maeneo niliyoyataja ambayo yanapitiwa na njia za umeme. Jambo la pili kuhusu umeme vijijini ni vigezo vinavyotumika kupeleka umeme maeneo mapya nchini. Ni jambo la kusikitisha kuwa yapo maeneo katika Wilaya ya Same ambayo hayana umeme wakati njia kuu na ndogo ya umeme inapita sio zaidi ya km. 10 kutoka maeneo hayo. Maeneo hayo ni Kata za: Mhezi, Mshewa (Manka), Msindo, Mtii, Didokwamomo, Vumari na Tarafa nzima ya Mamba-Vinta.

Wananchi wanahoji walichoikosea Serikali ya CCM wakati wameichagua kwa asilimia mia moja. Wanahoji kukosa miundombinu yote ya uchumi kama; barabara, simu na sasa umeme! Katika maeneo hayo barabara hazipitiki kwa magari makubwa bali kwa madogo ya *4X4 drive.* Hivyo watu bado karne hii ya 21 wanatembea kwa miguu! Hakuna simu wala umeme, naiomba Serikali sasa ipeleke umeme maeneo haya ya milimani ambapo ndipo 80% ya wananchi wa Wilaya ya Same wanaishi. Vinginevyo Serikali kuwa imewafikisha wananchi wa Same katika mazingira mabaya kisiasa na kimaendeleo. Sasa tunataka jibu kujua maeneo haya yatapata umeme lini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu wa pili unahusu nishati mbadala. Hivi mazingira na misitu ya nchi yetu yameharibika mno kwa sababu ya matumizi ya nishati ya kuni na mkaa katika kupikia. Kuni na mkaa ndio nishati kubwa na inayotumika sana nchini Tanzania.

Naishauri Wizara hii kwa kushirikiana na Wizara ya Maliasili na Utalii, na Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira, na kuondoa umaskini waweke mikakati ya matumizi ya nishati mbadala ya kupikia kwa makaa ya mawe, kukatisha tamaa matumizi ya kupikia kwa mkaa au kuni na pia nishati mbadala ya umeme wa jua na upepo vijijini.

Hatima ya kuharibika kwa mazingira yetu, mazingira kame na tishio la jangwa ni vigezo tosha vya umaskini uliokithiti kwa vizazi vyetu vijavyo. Ipo haja pia kwa Wizara kurekebisha *tariff* za umeme kwa matumizi ya nyumbani ili wananchi waliopo maeneo ya mijini na huduma ya umeme ilipo waweze kutumia nishati ya umeme kupikia kwa sababu itakuwa *affordable and available.* Inasemakana kuwa Jiji la Dar es Salaam pekee linatumia tani 20 za mkaa siku. Je mkaa huo utakuwa umeharibu ukubwa gani wa mazingira yetu? Naiomba Wizara iliangalie hili na kulitolea majibu hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu wa tatu ni utafiti na ugunduzi wa madini nchini. Wizara haina sehemu yoyote inayotaja kuwekeza katika utafiti na ugunduzi wa madini. Raslimali ya madini inapatikana chini ya ardhi ambapo haionekani.

Sasa madini yatapatikanaje kama hayafanyiwi utafiti na ugunduzi. Katika ukurasa 51 wa mauzo ya mazao ya nchi yetu, jedwali linaonyesha kuwa madini yanachangia 38.9% ya pato la Taifa na ni zao kiongozi katika pato la Taifa. Naishauri Wizara iwekeze katika utafiti na ugunduzi ili iweze kupata mavuno maradufu katika pato la Taifa.

Pia nashauri Wizara ihamasishe ugunduzi wa madini kwa kuwalipa wagunduzi wa madini *royalty.*

Ndugu Jumanne Ngoma aliyegundua madini ya *Tanzanite* anaishi maisha ya kimaskini sana na Serikali inadai ilishamlipa. Hivi madai ya Serikali kwa nini ni ya mkato? Mgunduzi gani duniani anaishi maisha hohehahe?

Je, Serikali imetumia kipimo/vigezo gani vya kumlipa? Kama ni Kitaifa kwa sheria ipi? Na iwapo ni Kimataifa sheria inasema nini? Mimi naishauri Serikali iwe wazi juu ya madai ya mgunduzi wa *Tanzanite* wa Ndugu Jumamne Ngoma badala ya kumfumbia mgunduzi wetu wa *Tanzanite* na Bunge letu. Haitoshi tu kusema: "Alishalipwa kama Msemaji mmoja wa Serikali alivyosema".

Je, sheria ya *Intellectual Property Right* haihusu ugunduzi wake. Tunaiomba Serikali itoe maelezo ya wazi kuhusu madai ya mgunduzi huyu. Mimi nadhani Serikali ilimpatia tunzo ya ugunduzi na sio malipo yake ya ugunduzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho wa mchango wangu huu naunga hoja ya Wizara ya Nishati na Madini asilimia mia moja. Ahsante.

**MHE. MARIA D. WATONDOHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, katika ukurasa wa 13 wa hotuba ya Waziri anadai kuwa Serikali imefanya uchunguzi wa awali wa kupeleka umeme toka Somanga Funga kwenda Lindi na Mtwara, kwa kutumia gesi ya Songosongo. Wananchi wa Mikoa ya Kusini wamekuwa wakihoji miaka nenda rudi ni kwanini gesi itolewe Songosongo kuja kuongeza nguvu kuliko na umeme wa gridi wakati Mkoa wenye gesi hauna umeme wa uhakika? Maelezo yaliyoko ukurasa wa 13 hayaridhishi na wala hayajibu hoja, maana kama kawaida Serikali imekuwa katika mpango wa upembuzi yakinifu, hivyo utekelezaji unaweza kuanza miaka 10 ijayo. Miaka 40 ya uhuru hatuna umeme wa uhakika! Wakati Mikoa mingine wawekezaji wakipigana vikumbo, Lindi hakuna hata anayeulizia! Hali hii ni ya kudhalilisha sana na kuwadharau Wananchi ambao ni sehemu ya Tanzania na mafao yao yanachangia Mfuko wa Taifa

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ni kuhusu nishati mbadala. Tanzania iko katika hatari ya kugeuka jangwa! Hii yote ni kwa sababu nishati mbadala Mijini ni mkaa. Hivyo, kila kukicha Wanavijiji wanakazana kukata miti na kutengeneza mkaa ili wauze Mijini. Iwapo *TANESCO* hawatapunguza gharama za umeme, Tanzania itageuka jangwa. Historia itailaumu Serikali ya CCM iliyoko madarakani. Hivi Serikali haioni kasi ya ukataji wa miti? Kwa nini gharama zinapanda kiasi hicho wakati sehemu kubwa ya umeme ni na nguvu ya maji?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati umefika kwa Serikali kuandaa nishati mbadala hasa katika Mikoa ambayo haina mifuko. Nishati kubwa na rahisi ni umemenuru, maana Tanzania kwa jua tumejaliwa. Umemenuru ndio ukombozi wa Vijijini maana umeme wa gridi hautafika leo Vijijini. Tatizo lililopo ni kwamba, vifaa vya umemenuru ni ghali hasa kwa vile 35% ya bei ni kodi. Je, Serikali haioni hiyo ni kurudisha maendeleo nyuma? Nashauri Serikali ichunguze hili na kuondoa kodi katika vifaa vya umemenuru ili tusogeze nishati hii Vijijini. Iwapo Vijiji vitapata umemenuru idadi ya vijana hasa wanaokimbilia Mijini itapungua. Serikali sasa iandae mpango wa kuondoa kodi hizi za vifaa vya umemenuru ili Tanzania nayo ipige hatua na ijikomboe kiuchumi. Hizo fedha za misaada zinazotolewa kama ilivyoainishwa ukurasa wa 16, zingeweza kusaidia kusambaza huduma hii Vijijini badala ya kutumika ofisini kufanya semina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *Net Group,* nasikitika kuona Serikali inathamini Wazungu kuliko Watanzania! Wakati wa Menejimenti ya Kitanzania, Serikali na Idara yake zilikuwa hazilipi bili za umeme. Zanzibar ndio kabisa, sasa wanakatiwa umeme wanalipa! Hivi menejimenti ilipokuwa chini ya Mzawa kwa nini Serikali ilikuwa haishtuki kulipa, leo Mzungu kila mtu anamshtuka! Serikali inasifia kumbe wanadai tu madeni ambayo Tanzania ilitakiwa kulipwa.

Je, huu sio ukoloni mamboleo kwa Serikali kuthamini Mzungu kuliko Mtanzania? Kwa nini mnataka kuuza nchi yetu kirahisi rahisi hivi! Hebu sasa tuamke na tuonyeshe uzalendo, hakuna anayeweza kuthamini nchi yetu zaidi ya sisi wenyewe na tusiipeleke nchi ikatawaliwe na Wazungu! Maskini Nyerere, tuombee huko uliko, nchi inauzwa ovyo! Watanzania 1,200 wanatakiwa waachishwe kazi *TANESCO,* waende wapi? Ole wetu!

Mheshimiwa Mwenyekiti, siwezi kuunga mkono hoja hii mpaka nihakikishiwe ukoloni mamboleo unakomeshwa.

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutumia nafasi hii kumpongeza mtoa hoja, Mheshimiwa Daniel Yona, Waziri wa Nishati na Madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Wizara kwa jitihada inazofanya kujaribu kuondoa kero ya umeme nchini. Nami napenda nitaje kazi nzuri inayofanyika katika Jimbo langu. Hata hivyo, yako maeneo ambayo ni muhimu, lakini bado hayajapatiwa umeme ulio karibu. Maeneo hayo yako karibu na nguzo za mwisho zilipo. Maeneo hayo ni Kata na Kijiji cha Kagoma, mahali ambapo pia tunatarajia kufungua Shule ya Sekondari hivi karibuni. Hapa tuna vituo vya mafuta na pia mwalo wa Ziwa Victoria

unaboreshwa kutoka Kagoma. Kwa hiyo, tuna matarajio hata ya kuwa na viwanda vya kusindika samaki hapo baadaye. Hili ni eneo endelevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, napenda kuishauri Wizara itilie nguvu matumizi ya mita za *LUKU,* badala ya kuendelea kutumia mita za kupeleka wasomaji ambazo mara nyingi matumizi yake yanaonekana kutoridhisha wateja. Nashauri *LUKU* ziwepo nchi nzima kwani matumizi ya nishati ni mazuri na ni kichocheo cha ukuaji wa uchumi wa maendeleo ya jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mita za *LUKU* zinapunguza matumizi kwa sababu kunajengeka tabia ya kujali matumizi ya lazima. Mtumiaji hawezi kulalamika isipokuwa kama mita ina hitilafu. Haipendezi wateja kulalamikia huduma wanazopata tena kwa malipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuwa na utaratibu mpya wa kuagiza vifaa *(Procurement Act)* kumekuwepo na ucheleweshaji mkubwa wa kazi ya umeme, hasa matatizo makubwa ya kukosekana kwa vifaa vya *Service Line.* Hii ni kero, nashauri wafanyakazi wasomeshwe ili wajue namna ya kukadiria matumizi na utaratibu wa kumpata Mkandarasi mwenye uwezo wa kutoa huduma ya vifaa endelefu uandaliwe. Hivi sasa kila panapofika umeme Wananchi wako mstari wa mbele kuomba *Service Line,* lakini kuna ucheleweshaji mrefu hadi kufikia mafanikio. *(Makofi)*

**MHE. ZAHOR JUMA KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la madini limetajwa katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ibara ya 15. Hata hivyo, kifungu hicho kina mapungufu makubwa sana. Kama ni madini, basi ilikuwa madini yote yanayopatikana nchini yatajwe katika ibara hiyo. Nashauri ibara hii ifanyiwe marekebisho haraka ili ijumuishe madini yote yanayopatikana Tanzania au vinginevyo ibara hii ifutwe kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu umeme, hatua ya kuikatia umeme Zanzibar hakikuwa kitendo cha kiungwana, ustaarabu wala ubinadamu. Si kweli kwamba Zanzibar walikuwa hawajalipa! Kauli ya *TANESCO* kuwa wanadai Sh.174,000,000/= ni uthibitisho kuwa sehemu ya malipo walikwishapokea. Malipo kwa mwezi wanayolipwa *TANESCO* na Zanzibar ni Sh.420,000,000/= kwa mwezi. Hilo deni linaloelezwa lililipwa kwa *T.T. tokea* tarehe 17/07/2003. Lakini pamoja na *TANESCO* kuelezwa bado waliamua kukatia umeme Zanzibar!

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vile *TANESCO* walieleza kuwa azma yao hii walimuandikia Mheshimiwa Waziri na Katibu Mkuu, lakini walikaa kimya! Aidha, Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Mheshimiwa Waziri Mkuu walisoma taarifa hizo kwenye magazeti, kuangalia kwenye *television* na redio pia zilitangaza azma hii, lakini hawakuchukua hatua yoyote! Ili kusafisha jina zuri la nchi yetu na heshima ya Serikali zetu mbili, Mheshimiwa Waziri awaombe radhi Watanzania wa Zanzibar kutokana na udhalilishaji uliofanyika, aidha atoe ahadi kuwa tatizo kama hili halitarudiwa tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siungi mkono hoja mpaka baada ya kupata majibu ya Mheshimiwa Waziri.

**MHE. MOHAMMED RAJAB SOUD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Mkurugenzi pamoja na wataalam wao kwa pamoja kwa kuandaa hotuba hii ya Bajeti ya Wizara yao. Wizara hii ni muhimu sana katika nchi yetu kwa kuwa ni Wizara inayowagusa Wananchi wengi katika masuala ya kijamii. Suala la umeme lililojitokeza hivi karibuni kwa kukatwa kwa umeme Zanzibar ni jambo ambalo haliwezi kusahaulika kwa Wazanzibari kwa kuweza kudharauliwa kiasi ambacho heshima na utu wa Wazanzibari umepotea kwa kitendo kilichofanywa kwa makusudi na baadhi ya watu fulani kwa malengo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali mbili zilikaa na kutiliana Mkataba kuhusu kupelekwa Zanzibar umeme kwa pamoja na *TANESCO* na wakakubaliana na hivi juzi tu Mheshimiwa Waziri alijibu swali la Mheshimiwa Mwaka Abrahman Ramadhan; Mbunge wa Viti Maalum, kuhusu kukodishwa au kubinafsishwa kwa *TANESCO* na Mheshimiwa Naibu Waziri alijibu kuwa *TANESCO* haijabinafsishwa wala haijakodishwa ila management ndio iliyobadilishwa. Kama ni hivyo, maana yake mkono wa Serikali bado upo na kama upo maana yake Serikali ya Muungano imeshiriki katika ukataji wa umeme Zanzibar.

Kama hivyo sivyo, mbona mpaka hii leo hatujasikia Serikali ya Muungano kutoa karipio lolote kwa *Net Group?* Kwa maana hiyo, walivyofanya ni sahihi, kuidhalilisha Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zilipoanza fununu tu za *NBC* kugoma, Serikali ilimwondoa Mheshimiwa Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo aende Dar es salaam kushughulikia tatizo hilo na kwa bahati nzuri akafanikiwa. Leo kweli tumeshindwa kufanya aina yoyote ya mazungumzo isipokuwa kuwatia adabu ya kuwakatia umeme Wazanzibari! Je, huo ndio usuluhisho sahihi wa matatizo yetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo machache, napenda kupata tamko la Serikali kuwa kati yao na *Net Group* ni nani mwenye nguvu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii kwa masikitiko.

**MHE. ANNE K. KILANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri wa Nishati na Madini kwa hotuba nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, naunga mkono hoja. Jambo ambalo naomba Serikali ituhakikishie leo na itoe kauli ya mwisho ni kwamba. Je, ni nani mgunduzi hasa hasa wa madini ya tanzanite? Je, *Tanzanite* imegunduliwa mwaka gani? Je, aliyegundua *Tanzanite* amelipwa kwa ugunduzi wake?

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mgunduzi wa *Tanzanite* limezua utata sana. Ni madini ambayo yanapatikana Tanzania tu, tungeomba historia yake ieleweke vyema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, tunapendelea liandikwe jedwali maalum kuhusu madini haya lisambazwe ulimwengu wote kuhusu ugunduzi wa madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. JOHN L. MWAKIPESILE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu ni mfupi sana. Kwanza napenda kumpongeza Waziri Daniel Yona kwa hotuba yake nzuri, kwa kweli uongozi mzima wa Wizara unastahili kupongezwa kwa kazi nzuri, Naibu Waziri wa Wizara hii anafanya kazi yake vizuri sana na anajibu maswali ya Waheshimiwa Wabunge kwa ufafanuzi mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa njia ya pekee kabisa, napenda kuwapa pongezi/hongera Shirika la Umeme *TANESCO* kwa kazi nzuri wanayofanya. Uongozi wa *TANESCO* umeongeza makusanyo ya fedha kutoka kwa wateja wake ambao huko nyuma walikuwa hawalipi umeme waliokuwa wanatumia. Serikali zote mbili na Taasisi zake walikuwa jeuri na sugu na *TANESCO* ilikuwa ikipata tabu kuendesha shughuli zake. Kitendo cha *TANESCO* kuikatia umeme Zanzibar ni sawa kabisa kwani wateja wasipolipa kazi ya kusambaza umeme Vijijini inakwama. *TANESCO* waendeleze kazi yao nzuri bila kutishwa!

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri anieleze juu ya ombi langu la siku nyingi la kupeleka umeme *Matema Beach* kutoka Mji mdogo wa Ipinda. Kata zitakazohudumiwa na line hii ya umeme ni Ipinda, Makwale, Lusungo na Matema. Ni Kata tajiri kwa zao la cocoa na Wananchi wamejiandaa kikamilifu na wanajenga nyumba za kisasa na kufanya wiring.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru Serikali kwa kufikisha umeme katika Vijiji vifuatavyo: Ibanda, Busale, Lewa, Kasumulu, Itunge, Kafundo na Nkuyu. Kuna haja sasa ya kuunganisha umeme toka Ntaba (Rungwe Mashariki) na Ipanda (Kyela) kilomita 5. Naomba majibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. DR. BATILDA S. BURIAN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa sikuweza kupata nafasi ya kuchangia kwa kuzungumza Bungeni, napenda kuchangia kwa maandishi hotuba hii ya bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Daniel Yona, Naibu Waziri wake, Dr. Ibrahim Msabaha, Katibu Mkuu, Bwana Rutabanzibwa na wataalam wote wa Wizara hii kwa jitihada kubwa ya kuendeleza Sekta hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu ni katika maeneo yafuatayo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, ni kuhusu umeme. Gharama za umeme bado ni kubwa sana, Wizara hii imekuwa ikitoa ahadi ya kupunguza gharama hizo tangu mwaka 2000. Mheshimiwa Dr. Kigoda katika hotuba yake ya Bajeti ya mwaka 2000 alitamka humu Bungeni msimamo wa Wizara yake wa kushusha gharama za umeme. Lakini cha kushangaza zaidi hili halikufanyika na matokeo yake gharama zimepanda!

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ni kuhusu nishati inayotumia mionzi ya jua *(solar power).* Pamoja na ukweli kwamba nishati hii ina umuhimu mkubwa hasa kwa wakazi wa Vijijini, bado kwa kiwango kikubwa teknolojia hii imebakia ni nadharia tu! Naomba Serikali iongeze jitihada ili kuhakikisha kwamba teknolojia hii inawafikia Wananchi wa Vijijini na kwa gharama nafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu ni kuhusu Sekta ya Madini.

(a) Nafurahi kuona kwamba Wizara imepanga mikakati thabiti ya kuendeleza Sekta hii. Hata hivyo, naomba Serikali ihakikishe kwamba inaendelea na mikakati ya makusudi kusaidia wachimbaji wazalendo hususan wachimbaji wadogo wadogo.

(b) Pia, utaratibu wa kutenga sehemu ya Mererani kama *controlled area* ni mzuri. Hata hivyo, Wizara hii iwe na mpango wa kimkakati *(strategic plan).* Ni vizuri kukawa na mpango wa kutenganisha maeneo ya uchimbaji hasa maeneo yote ya uchimbaji wa vito na siyo tu tufanye utaratibu mara panapotokea maafa! Hivyo, maeneo kama ya Mahenge kwenye uchimbaji wa ruby na kadhalika na yenyewe yawekewe utaratibu mzuri na siyo kusubiri tu eneo lifikiwe na maafa.

(c) Uamuzi wa Serikali kusitisha uuzaji wa tanzanite ghafi kusema kweli utasaidia kuongeza ubora wa *Tanzanite* zetu *(to add value)*, pia, utasaidia nchi yetu kupata mapato zaidi, utaongeza ajira na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo yangu ni kama ifuatavyo:

* Ni vizuri kukawa na muda maalum ambao utatengwa ili kuruhusu watakaoshughulikia masuala hayo ya utekelezaji na usafirishaji *(lapidary)* wa *Tanzanite* kupata uzoefu. Muda huu ni lazima utamkwe hapa Bungeni na siyo tu uachwe hivi hivi *regularly.*

* Wizara isaidie akina mama watakaokuwa na interest ya kufanya shughuli hizo za faceting na lapidary. Maeneo mengi ya duniani Wanawake wanashughulika na shughuli hizo za utengenezaji wa *jewelers* kwa vile wao pia ndio watumiaji wakubwa wa bidhaa hizo.

* Ni vizuri ikaeleweka kwamba utaalam huu wa *lapidary* siyo mgumu kama mtu akifundishwa. Mimi mwenyewe niliishafanya kazi hii Uingereza, siku moja tu nilipata utaalam mkubwa. Hivyo, naomba Wizara itoe mkopo na mafunzo ili kuwawezesha Wanawake na vijana wazalendo kuingia katika biashara/shughuli hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. ABDALLAH KHAMIS FERUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Wizara ya Nishati na Madini kwa hotuba yake nzuri pamoja na wataalam wake wote walioandaa hotuba hiyo. Suala la *TANESCO* kuikatia umeme Zanzibar bila ya taarifa ni kitendo ambacho si cha kiungwana hata kidogo kwani kuikatia umeme Zanzibar ni kuidhalilisha Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na ni kitendo ambacho kimeleta tafsiri nyingi kwa Wananchi wa Zanzibar na hata kwa wageni waliokuwepo kwa wakati huo!

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri anijibu maswali yafuatayo: -

Wakati Serikali inatafuta mwekezaji wa Shirika la umeme *TANESCO:* Je, iliwahi kuwasiliana na wenzao wa SMZ? Kama waliwasiliana, sawa, lakini kama hawakuwasiliana, kwa nini ilifanya hivyo wakati Zanzibar ni mteja wake mkubwa wa umeme?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitendo cha *TANESCO* kuidhalilisha SMZ ni kibaya sana kisiasa na kijamii. Kwa hiyo, napendekeza Mheshimiwa Waziri aombe radhi kwa kitendo kilichotokea.

Mheshimiwa Spika, ipo haja ya Serikali kufuatilia suala hili la ukataji wa umeme. Je, nani aliyetoa ruksa ya kukata umeme SMZ? Pia, ni nani aliyechukua hatua ya kukata umeme bila hata ya kutoa taarifa kwanza? Napendekeza anayehusika na tatizo hilo ikiwa ni Meneja au yoyote, basi awajibike kwa kitendo cha kudhalilisha Serikali. Suala hilo ni nyeti, hivyo Serikali izingatie ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mafuta ni la kikatiba. Suala hili haliwezi kuzungumzwa ovyo ovyo tu isipokuwa ni lazima vikao vinavyohusika vikae pamoja na kukubaliana kwa utaratibu wetu wa kiuongozi ulivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na hali ya uchumi ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilivyo, hivi sasa kutegemea zao moja tu la karafuu si sahihi. Ipo haja ya suala hili kuangaliwa na kuzingatiwa ipasavyo katika vikao vinavyohusika kisheria na kikatiba ili kuiwezesha Zanzibar kumiliki mafuta yatakayochimbwa Visiwani humo, hivyo itasaidia kuboresha uchumi wa SMZ na kusaidia sana kuondoa kero nyingi za Wananchi wa SMZ.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hotuba hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nimpongeze Mheshimiwa Waziri pamoja na timu yake yote kwa jinsi walivyoweza kuchambua vizuri bajeti ya Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba ya Wizara hii umeme Vijijini haukupewa kipaumbele kabisa! Inaashiria kuwa Wizara hii haioni umuhimu wa utunzaji wa mazingira katika utunzaji wa miti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, Wizara hii imeshindwa kabisa kuzungumza habari ya umeme katika Wilaya mpya kama vile Kilolo. Ikumbukwe kuwa Wilaya hii mpya ndio yenye vyanzo vingi vinavyopeleka maji yanayozalisha umeme. Mfano katika Bwawa la Mtera, kiasi kikubwa cha maji kinatoka katika Mto wa Matitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Bwawa la Kihansi maji yote yanatoka katika Wilaya ya Kilolo kwenye Kata ya Bomang'ombe. Hivyo, kutopeleka umeme katika Wilaya hii itakuwa ni kutowatendea haki Wananchi hao na itasababisha kuvunjika moyo katika utunzaji wa misitu, kitu ambacho kitaleta athari kubwa katika vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaomba Mheshimiwa Waziri atoe ufafanuzi katika suala hili leo hii ili Wananchi wa Wilaya ya Kilolo wapate majibu ya Serikali yao kwa sababu suala hili ni kero kubwa sana kwa Wilaya yetu.

**MHE. ESHA H. STIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nampongeza Mheshimiwa Daniel Yona, Waziri wa Nishati na Madini, Naibu wake, Mheshimiwa Dr. Msabaha na watendaji wa Wizara hiyo kwa kazi nzuri wanazozifanya bila kujali manung'uniko wayapatayo kutoka kwa baadhi ya Wananchi kwa mapungufu ya kutopatikana kwa umeme katika maeneo mengi Vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba hii ya 2003/2004 imetupa faraja kwa jinsi malengo yaliyoainishwa. Kwa hiyo, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, Wanawake wengi wa nchi hii ndio wanatumia nishati ya kuni na mkaa. Katika ukurasa wa 15 wa hotuba hii ya Wizara ya Nishati na Madini imetajwa kwamba, Mkoa wa Shinyanga umefungiwa mitambo ya kutumia biogas. Nasema ahsante kwa kazi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiwa Kiongozi wa Wanawake (Mbunge) Mkoani Shinyanga, naomba nipatiwe taarifa ni familia gani zinatumia nishati ya *biogas* Mkoa mzima (Kiwilaya) ili niweze kuwaelimisha Wanawake umuhimu wa matumizi ya nishati hiyo kwa maeneo ambayo bado hawajaanza kutumia. Matumizi ya biogas yatawaepusha Wanawake kuwa na macho mekundu kwani wataacha kuni na kinyesi cha ng'ombe na kutumia *biogas.*

Kwa misingi hiyo, naiomba Wizara ya Nishati na Madini itenge fedha kwa ajili ya kuja Shinyanga kutoa semina kwa Wanawake ambao wakielewa umuhimu wake watawashawishi Waume zao na hivyo nishati hii itaenea Vijijini na kupunguza kero za upatikanaji wa umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, ni kuhusu kero ya upatikanaji wa nguzo za umeme Mkoani Shinyanga. Ni muda mrefu baadhi ya wakazi wa Shinyanga Mjini tunanyanyasika kwa ukosefu wa nguzo za umeme na hii imesababisha wafanyabiashara wenye vibanda vya biashara kupata hasara eneo la kiwanja karibu na *SHYCOM* kwa sababu wanashindwa kufanya kazi zao walizokusudia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namuomba Mheshimiwa Waziri anipe majibu ni lini kero hii itakwisha? Meneja wa *TANESCO* Mkoa wa Shinyanga ana maneno mengi ya kupoza watu, lakini hana utekelezaji. Mara aseme kuwa hawana fedha, mara Bajeti imepita wataanza hivi karibuni na kadhalika! Kwa kweli tunachoka na maneno matupu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namalizia kwa kusema naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. ELIZABETH N. BATENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri pamoja na watendaji wote wa Wizara hii kwa maandalizi na hotuba iliyowasilishwa mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya za Ngara na Biharamulo ni miongoni mwa Wilaya chache kongwe ambazo hazina umeme. Suala la kuzipelekea Wilaya hizi umeme limekuwa la kusuasua na ahadi nyingi zisizotekelezwa na kwa muda mrefu! Mwaka 2001/2002 na 2002/2003 Serikali imekuwa ikitenga fedha kwa ajili ya kujenga nyumba za kufungia mashine/jenereta. Nyumba hizo zimejengwa na Waziri katika kujibu swali langu mwezi Februari, 2003 alisema umeme katika Wilaya hizo utawaka mwezi Septemba mwaka huu, 2003. Je, itawezekana?

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kitabu cha nne cha *Vote 58, Sub vote 3001, Project 3113, Electrification of Biharamulo,* jumla ya Sh.5,309,620,000/= *Vote* na *Sub Vote* hiyo hiyo *Project 3083, Electrification of Ngara* ni Sh.4,000,000/= tu zimetengwa! Je, fedha hizo zitatosha kumaliza kazi zote zilizobaki ili umeme uwake mwezi Septemba?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo katika hotuba ya Waziri ukurasa wa 4, ibara ya 7 inaonekana kuwa Biharamulo itahitaji Sh.5,000,000,000/= na Ngara Sh.4,000,000,000/= wala haelezi fedha hizo zitatoka wapi! Mbona kwa umeme (ukarabati) wa Tanga, Arusha na Moshi ameeleza kuwa fedha zitatoka *NDF?* Mbona kwa umeme wa Serengeti na Ukerewe ameelezea?

Sasa kwa Ngara na Biharamulo hasemi zitatoka wapi! Kwa nini kuna maelezo na tarakimu zisizofanana? Marekebisho aliyoleta kuhusu *Rural Electrification* hayaonyeshi kama zipo dalili za umeme kuwaka katika Wilaya hizi kwa ahadi ya Septemba mwaka huu!

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vyovyote vile, Wilaya hizo kongwe zilizoko pembezoni na zinazopakana na nchi nyingine bila kusahau ziko mbali sana na Makao Makuu ya nchi yetu, hazijaweza kuona umeme! Kwa kuzingatia wakati huu tulionao, wakati ambao tunasema tunapambana na umaskini. Je, ni halali au ni busara, au Serikali inaonyesha umakini katika kufanya kazi zake kwa kupanga na kuwapelekea Wananchi wa Wilaya hizo umeme wa jenereta?

Binafsi nasema jenereta hizo ni mbovu, kwani kama jenereta hizo zimeishatumika nani ana hakika kuwa ni nzima? Kwa nini Serikali isitumie busara ikakusanya fedha za kutosha Wilaya ili hiyo ikaunganishiwa kwenye umeme wa gridi au umeme wa Uganda ambao unaishia Muleba na Karagwe?

Hivi Rais Mkapa alipowaahidi Wananchi wa Ngara na Biharamulo kupata umeme alimaanisha umeme wa jenereta? Hizo ni Wilaya maskini, lakini kuna madini mengi kama dhahabu, *nickel* na kadhalika. Ni siku nyingi tunasubiri uchimbaji wa *nickel* ya Kabanga (Ngara) bila umeme wa uhakika uchimbaji wa *nickel* utaendelea kuwa ndoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namuomba Mheshimiwa Waziri atakapojibu atueleze yafuatayo: -

(i) Gharama za kuvuta umeme kutoka Muleba/Karagwe kwenda Ngara na Biharamulo ni kiasi gani na ingechukua miaka mingapi kupata hizo fedha?

(ii) Kwa nini jenereta hizo zilifunguliwa Babati na Kondoa na ikaamuliwa zipelekwe Ngara na Biharamulo? Hii si ni dalili inayoonyesha kuwa kuna Wananchi bora na wengine duni?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitashukuru kupata majibu, naunga mkono hoja.

**MHE. IBRAHIM W. MARWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijielekeze kwenye eneo la nishati. Upatikanaji wa umeme kwa watumiaji wapya limekuwa tatizo sugu kwenye Mji wa Musoma Mjini. Mji wetu ambao unaendelea kukua kwa kasi kubwa kwa ujenzi wa nyumba nyingi za kisasa ambazo zimeshindwa kupatiwa umeme kwa muda mrefu sasa. Maelezo yanayotolewa na ofisi ya *TANESCO* mara ni kwamba maombi mapya ni budi yapate kibali kutoka Makao Makuu Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa yapo maombi yanayofikia au kuzidi 1,000 (elfu moja) ambayo ni ya muda mrefu na hakuna dalili ya kuyashughulikia katika muda mfupi! Gharama ya kuweza kushughulikia maombi hayo inakadiliwa kufikia Shilingi bilioni 1 au pungufu. Mapato ya Mkoa wa Mara kwa mwezi ni takriban Shilingi bilioni 2 ambazo zingeweza kabisa kuondoa kero ya kuunganisha umeme kwa wateja wapya ambao endapo watapata umeme wataongeza wigo wa mapato ya Shirika. Lakini fedha hizo ni lazima ziwasilishwe Makao Makuu ambao wao ndio wenye maamuzi ya mwisho ya matumizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namuomba Mheshimiwa Waziri anihakikishie kuwa maombi haya yatashughulikiwa ili wakazi wa Musoma hususan wakazi wa Kata za Kigera, Bweri, Buhare na Makoko waweze kupatiwa umeme katika makazi yao. Nitaunga hoja hii mara baada ya Waziri wa Nishati na Madini kunihakikishia kuwa maombi haya yatashughulikiwa katika kipindi cha fedha cha 2003/2004. Naomba kuwasilisha.

**MHE. BAKARI SHAMIS FAKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uwezo wa kuchangia hoja hii ya Wizara ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili nchi yoyote ile ipate maendeleo ni lazima iwe ina nyenzo muhimu ambazo zitailetea nchi husika maendeleo. Umeme ni moja kati ya nyenzo na kichocheo kikubwa cha maendeleo katika nchi, iwe ni Mijini au Vijijini. Kwa hali hiyo basi, Serikali kupitia Wizara ya Nishati na Madini ni lazima ifanye juhudi za makusudi ii isambaze umeme sio tu Mijini, bali hata Vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tunavyojua kwamba umeme ndio unaotumika katika kuviendesha viwanda ambavyo ndilo tegemeo mojawapo la kutuletea maendeleo ya kiuchumi nchini, lakini kutokana na bei kubwa ya umeme gharama za uzalishaji viwandani zimepanda sana hivyo kupunguza uzalishaji wa bidhaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili basi tuweze kuzalisha vizuri kukuza uchumi wetu kupitia viwandani, tunashauri Serikali ifikirie upya kupunguza bei ya umeme. Kama tunavyojua, umeme sio tu kwamba unatumiwa viwandani na maofisini, bali na hata majumbani, kwa hiyo, suala la kukatika kwa umeme

kunawaathiri sana wateja wa nishati hiyo. Umeme unapokatikakatika huleta uharibifu mkubwa sana wa mali za watu, vifaa vya ofisini na hata vya viwandani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuliepusha hilo, lazima Serikali iandae mikakati ya makusudi kuboresha mfumo wa usambazaji wa umeme. Tunashukuru kwamba *TANESCO* inajaribu kulishughulikia tatizo hili kwa kuliundia Tume maalum ya ufundi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba Wizara inayo juhudi kubwa ya kuelimisha watumishi wake juu ya janga la UKIMWI, lakini kwa kuwa UKIMWI umekuwa ni gonjwa sugu na kwa kuwa binadamu na wao wamekuwa sugu, tunaishauri Wizara isikomee hapo tu, iendelee na juhudi zake za kuelimisha tukizingatia kwamba UKIMWI unatumaliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi zilizoendelea kama vile Marekani, Ujerumani na kadhalika, zina raslimali nyingi zikiwekmo bidhaa za viwanda, mafuta, madini na kadhalika. Vile vile, nchi yetu imepata neema ya madini, gesi na kadhalika, bado mambo haya hayajaleta maendeleo ya kutosha kiuchumi, lakini ni chanzo kizuri cha kufikia tulikokusudia. Jambo tunaloshauri hapa ni kudhibiti matumizi ya madini haya ipasavyo ili tufikie lengo.Tatizo la mgogoro katika maeneo ya machimbo ya madini sasa limekuwa ni suala sugu. Hili si jambo la kuchukulia kirahisi vinginevyo nchi itajikuta katika balaa kubwa! Tunashauri Serikali kupitia Wizara hii ipange mipango madhubuti ya kuzuia kutokea migogoro kama hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkataba wa *IPTL* kwa kweli umekuwa mzigo mkubwa kwa Serikali, umegharimu mabilioni ya fedha kwa mwezi, tena gharama zenyewe za kudumu. Kwa hiyo, inashauriwa kwamba Serikali ipitie upya mkataba huo ili isiendelee kubeba gharama kubwa kama hizo. Baada ya kusema hayo, napenda kuwasilisha. Ahsante sana.

**MHE. PHILIP A. MAGANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja na kumpongeza Waziri Yona na wasaidizi wake kwa kazi nzuri wanayoifanya katika mazingira magumu ya ufinyu wa miundombinu

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mradi wa *Mnazi Bay,* utekelezaji wake bado unasuasua kutokana na ucheleweshwaji wa maamuzii ya kuridhia *MOU* ambayo walikubaliana na mwekezaji. Wakati haya yanaendelea, Wananchi wa Mtwara na Lindi wanaendelea kuathirika kwa ukosefu wa huduma ya umeme. Ukarabati wa mitambo *(generators)* iliyotoka Kihansi hairidhishi kwani mpaka sasa uzalishaji wa umeme bado hauna uhakika! Ninatoa rai kwa Serikali kuhakikisha kuridhia *MOU* na mwekezaji wa *Mnazi Bay Gas-Electricity Project* aendelee ili umeme wa kutosha upatikane. Umeme huu unahitajika sana kwa ajili ya kuendesha viwanda vya korosho vilivyopo Mtwara, Lindi, Newala Masasi, Mtama na Nachingwea.

Kuhusu mradi wa Mchuchuma, ni vyema sasa Serikali itoe maamuzi ya mwisho na ya haraka ili uzalishaji wa umeme kutokana na nishati hii mbadala, makaa ya mawe uanze. Tumeshaona athari ya kutegemea kianzio kimoja cha nishati hii yaani hydropower hususan wakati huu wa mabadiliko ya hali ya hewa ya haraka haraka yanayosababisha kutokea kwa hali ya ukame. Taifa liachane na tabia ya kuendeleza mlolongo wa feasibility studies. *Studies* ambazo zimeshafanywa ziwekwe bayana ili wadau mbalimbali watoe michango yao ambayo labda inaweza kuisaidia Serikali kutoa maamuzi muafaka. Ikumbukwe kuwa baadhi ya studies hizi zimefanywa wakihusisha Shirika la Maendeleo la Taifa *(NDC)* ambalo ni Shirika la Serikali. Je, hata maoni ya Shirika hili letu wenyewe hatuyathamini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *Stigler's Gorge Hydropower Project,* mradi huu usitelekezwe na Serikali kwa kuwa umeme utakaozalishwa hapa ni mwingi wa kutosheleza mahitaji ya Taifa letu pamoja na ziada ambayo tungeweza kuwauzia majirani zetu hususan Kenya ambao siku zote wameonyesha nia yao ya kununua umeme kutoka Tanzania. Rai yangu ni kuwa Serikali iwaalike wawekezaji kwa mtindo wa *BoT.*

**MHE. ALLY A. KARAVINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata fursa hii angalau kuchangia kwa maandishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuishukuru Serikali yetu ya CCM kwa kuikumbuka Wilaya yangu ya Urambo kwa kutupatia umeme. Shukrani hizi pia ziwaendee Ubalozi wa Sweden kwa kufadhili mradi wa umeme wa Urambo na Serengeti. Jambo muhimu sasa ni kwa Waziri kuwaeleza Wananchi wa Urambo kupitia hotuba yake hii na wajibu kwamba ni lini umeme utaenda Urambo? Ujenzi unaanza lini na Mkandarasi ni nani na kwa sasa yuko hatua gani? Gharama za umeme ziko juu sana, sidhani kama kweli nishati hii itaweza kuchangia kuondoa umaskini na kulinda mazingira ya nchi yetu kama vile misitu na uoto mwingine wa asili. Naomba Mheshimiwa Waziri anihakikishie kama umeme uliopo hautoshi na umefikia kikomo! Naomba uhakika huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vinginevyo, ni kwa nini tusipunguze bei ili kupanua soko na kupata fedha zaidi pamoja na multiplier effect yake kwa upande wa kupunguza gharama inayotokana na uharibifu wa mazingira? Ninaomba Mheshimiwa Waziri alieleze Bunge hatua ya Kampuni ya Canada iliyokuwa tayari kujenga mtambo wa kuzalisha umeme kutokana na gesi ya *Mnazi bay* kwenye mpango wao ilikuwa ifikapo 2004 ili Wananchi wa Lindi na Mtwara na sehemu nyingine za Kusini wawe tayari wamefaidika na umeme huu. Sababu zilizotolewa kuchelewesha uzalishaji huu ni za Wizara ya Nishati yenyewe, je, kwa sasa mfadhili huyu yuko wapi?

Je, hajakata tamaa na amelipwa fidia gani? Tatizo lilikuwa ni mfadhili, je, kwa nini Wizara hii inamkataa mwekezaji huyu? Naomba Mheshimiwa Waziri anieleze kwa nini Mikataba ya Madini hailetwi Bungeni na kuwekwa bayana kwa Wabunge ili tujionee wenyewe?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niishauri Serikali kwamba uchimbaji wa madini hususan dhahabu, migodi mipya isitishwe mpaka formula mpya itakapopatikana ambayo Wananchi wataridhika kwamba ina manufaa kwao na kwa Taifa. Kwa nini hatufuati mfano wa Botswana, kulikoni? Naomba majibu.

**MHE. EMMANUEL E. KIPOLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayo malalamiko ya muda mrefu dhidi ya matatizo yanayotukabili katika Kijiji chetu cha Kakola kilichomo katika eneo la leseni ya *K.M.C.L.* Msingi wa malalamiko yenyewe ni Wananchi wa Kakola kunyimwa haki yao ya kikatiba ya kumiliki mali na kujiendeleza kiuchumi kama vile kujenga majumba mazuri, kupimiwa viwanja vyao na kupatiwa hati za kumiliki maeneo yao. Kwa mujibu wa Sheria ya madini Na. 5 ya mwaka 1998, Sheria inawatambua wakazi wa Kakola kama *lawful occupier of land* ambao kwa msingi wa Sheria hiyo anazo haki zake za msingi kama vile kufidiwa *promptly and accurately* mali zake zote.

Kwa kuwa *K.M.C.L* walishanithibitishia kwa maandishi ambayo ninayo, kwamba hawana mpango wa kukihamisha Kijiji cha Kakola na kauli hiyo inathibitishwa na vitendo kama vile kujenga *AMREF Centre* na Shule ya Msingi Kakola kusaidiwa ujenzi wa madarasa na *K.M.C.L.* Kwa kuzingatia para hapo juu, naitaka Serikali itoe kauli leo kwamba Kijiji cha Kakola hakitahamishwa na hivyo Wananchi wa Kakola waendelee kupata haki zao za kikatiba bila kulazimishwa na Sheria ya Madini Na 5 ya mwaka 1998 kifungu cha 96(2) kuomba kibali kwa ajili ya kujiendeleza.

Aidha, naitaka Serikali leo imruhusu *DED* wa Kahama apeleke wataalam wake wakapime viwanja kwa ajili ya Wananchi wa Kakola ambao tayari wameshalipia gharama mbalimbali za upimaji wa viwanja hivyo ili Wananchi waweze kujenga majengo mazuri na ya kudumu na waishi bila kubughudhiwa kwamba wamo kwenye eneo la mtu mwingine, ambaye kimsingi kama nilivyosema hapo juu mwenye eneo ameshanithibitishia kwa maandishi kwamba eneo hilo yeye hana kazi nalo na wala halihitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba majibu ya kina kabla ya kuunga mkono hoja hii. Ahsante.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba na mimi nichukue nafasi hii kuchangia kwenye hoja hii muhimu ya Waziri wa nishati na madini. Kabla sijaendelea napenda niseme kwamba naiunga mkono hoja hii asilimia mia moja. *(Makofi)*

Katika kipindi cha Bunge hili tangu Mheshimiwa Waziri wa Fedha alipotoa hotuba ya bajeti yake mpaka Mheshimiwa Waziri wa Mipango na Mheshimiwa Waziri Mkuu na leo pia wakati tunawasilisha bajeti yetu na jana wakati wa Wizara ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Bunge lako Tukufu na Waheshimiwa

Wabunge wamechangia kwa kina mambo mbalimbali yanayohusu Wizara ya Nishati na Madini. Napenda nichukue nafasi hii kusema kwamba Serikali yenu hii ni sikivu, imesikia. Michango ya Waheshimiwa Wabunge ni mingi sana, Mheshimiwa Waziri atakapokuja hapa ataweza kutaja kwa majina, hatutaweza kupitia kila lililosemwa, lakini tutajitahidi kuchukua machache ya ujumla na baadaye tutaweza kutoa majibu kwa kila Mheshimiwa Mbunge kwa lile alilouliza. Kwa upande wangu, mimi ningependa nichangie maeneo machache ya ujumla ya madini na migodi kuchangia fedha kwenye Halmashauri, umeme Vijijini, Makao Makuu ya Wilaya yaani kufikisha umeme, bei ya umeme, *IPTL,* kukatika kwa umeme na mambo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti kama nilivyoanza kusema, napenda nilihakikishie Bunge lako Tukufu kwamba Serikali ni sikivu na imesikia na kuhusu Mikataba ya madini, napenda niseme kwamba kwanza hakuna kinachofichwa kwa maslahi ya mtu yeyote binafsi. Isipokuwa napenda nichukue nafasi hii nielezee tu kwamba uwekezaji kwenye sehemu ya madini ni sehemu ya sera yetu inayotokana na Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi na pia kwa upande wa Serikali ni sera yetu ya ndani kwa kukaribisha na pia ni sera yetu ya nje kama nilivyosema awali, inayotokana na Ilani. Pia uwekezaji unahusu wakati tuliokuwanao huu wa utandawazi, yaani *globalization* ambapo Makampuni makubwa yanashindana na ni washiriki kwa kiasi fulani, kwa Kiingereza wanasema ni *known state actors 29.8* katika mahusiano ya Kimataifa yakishirikiana na Serikali zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia uwekezaji huo unahusu pia ushindani wa kuvutia vitega uchumi katika dunia hii ya utandawazi ambapo nchi zinashindana kuvutia wawekezaji na wenye mitaji mikubwa kuangalia mambo mbalimbali katika maamuzi yao ya kutoa vitega uchumi. Mifumo ya kodi, amani na usalama, utulivu wa sera za kodi yaani *fiscal stability,* mwelekeo wa nchi, sera na misimamo ya nchi na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nia ya Serikali siku zote imekuwa ni kuhakikisha kwamba tunapata manufaa makubwa kutokana na raslimali muhimu ya madini. Lakini kutokana na uwezo wetu wa ndani kuwa mdogo, nia hiyo pia imekuwa ni kuhakikisha kwamba tunawakaribisha wawekezaji kulingana na sera yetu na kuwahakikishia kwamba sisi ni tulivu na tuna sera tulivu na kwamba pia tunaheshimu Mikataba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, kama nilivyoanza kusema kutokana na michango mizuri sana na ni muhimu sana Waheshimiwa Wabunge tangu tumeanza Bunge hili na hata kabla ya Bunge hili. Napenda nichukue nafasi hii niseme kwamba Serikali imesikia na kwamba haya mazuri yote yaliyozungumzwa sasa tutakwenda kuyafanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimezungumza pia kuhusiana na mambo ya madini, suala mahususi lililoulizwa kama Halmashauri zinanyimwa pesa ambazo zinapaswa kuwa katika mikataba ya madini takriban dola laki mbili kwa mwaka sawa sawa na shilingi milioni 200.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda niseme kidogo tu juu ya muundo wa mikataba hii ya madini kwa ujumla, kwamba miundo ya mikataba hii imesanifiwa kwa mfumo mmoja unaofanana fanana kwa maana ya kwamba ni *Modern Agreements* zinazofanana. Mikataba hii ni ya kiutendaji ambapo masuala muhimu yaliyomo ni kama vile hati za Kampuni kupata leseni baada ya kuingia mkataba na Serikali. Maelezo ya masuala ya kodi mbalimbali yaani *Physical Terms.* Masuala ya kibenki na uhamishaji wa gawio la faida, masuala ya wafanyakazi wa mgodi na haswa wale wanaotoka nje na wafanyakazi wa ndani na matukio yanayoweza kupekejea mkataba kuvunjika na mengineyo.

Katika mikataba hii ambayo inafanana fanana kipo kipengele kinachozungumzia utozwaji, uwezo wa Halmashauri kutoza kodi za kiujumla yaani *over general nature,* ili mradi na hili ndiyo muhimu kwamba kodi hizi haziwabagui na kuwalenga wao wenye migodi peke yake haziingilii kodi zinazotozwa na Serikali Kuu kama vile kodi ya mapato yatokanayo na kiwango cha uzalishaji na kadhalika na jumla ya kodi zote hizi zisizidi dola laki mbili kwa mwaka. Sasa hiki kipengele ni *captive,* siyo kwamba wenye migodi *automatically* maana yake wanatakiwa watoe shilingi milioni 200 kwa kila Halmashauri kule kwenye sehemu walizopo.

Lakini kama nilivyosema awali kwa kuwa suala lote hili la kuchangia kwenye Halmashauri na maeneo ambayo migodi ilipo na nchi nzima kwa ujumla, na masuala yote yanayohusu madini, mrahaba na mengineyo ambayo yamekuwa yakichangiwa, kama tulivyosema awali tumesikia, na tumechukua ushauri wote wa Waheshimiwa Wabunge, tumekubali kuchukua ushauri huo, tumekubali kuufanyia kazi Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu umeme vijijini. Nakubaliana sana na Waheshimiwa Wabunge kwamba umeme ni nyenzo muhimu sana ya maendeleo na kwa kweli hatuwezi kuzungumzia maendeleo ya kisasa bila ya umeme na ndiyo sera yetu. Lakini napenda pia niseme kwamba ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge tumekuwa tukitoa mapendekezo ya kutokupelekwa umeme hapa na pale katika maeneo yetu na wakati mwingine tukitoa mifano ya hapa na pale.

Napenda niwahakikishie ndugu zangu kwamba hakuna upendeleo katika kusambaza umeme vijijini. Sera yetu ya Nishati inaainisha kwamba vijiji, miji, vitongoji na kando kando mwa njia za umeme. Kwa hiyo, kadri inavyowezekana viweze kupatiwa umeme. Sera hii pia inaainisha sehemu za uzalishaji, Makao Makuu ya Wilaya na kadhalika. Pia waweze kupatiwa umeme na kadhalika. Tatizo ni kwamba baadhi ya miradi imekuwa na programu kwa mfano inafikisha umeme kwenye makao makuu ya Wilaya ambapo ndiyo kitovu muhimu cha kusambaza umeme vijijini, zimekuwa zikitenga fedha na wakati mwingine baada ya kufikisha Wilayani sehemu zingine za vijijini zimekuwa haziwezi kufikishiwa umeme kutokana na fedha kukosekana.

Lakini kama ambavyo nimekuwa nikijibu katika Bunge lako Tukufu ni kwamba ni nia ya Serikali kuhakikisha kwamba miradi ile ambayo haijakamilika ikamilike na ile ambayo iko ndani ya uwezo wa Shirika la *TANESCO* kifedha na kiufundi tumewaagiza kwamba pia ni miradi ambayo wajitahidi kuikamilisha kwa sababu vinginevyo kwa kweli inakuwa ni hasara, kama kuna mahali ambapo nguzo zimechimbiwa na nyaya zimefungwa lakini shughuli nyingine hazijakamilika kwa kweli inakuwa ni hasara kwa upande wa Shirika. Kwa hiyo, tumewaagiza kwamba watoe kipaumbele kwenye maeneo ambayo miradi haijakamilika ikamilishwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, umeme kwenye Makao Makuu ya Wilaya, kama nilivyosema awali Serikali inatekeleza Sera inayotokana na Ilani ya Uchaguzi ambayo tumesema kwamba Makao Makuu ya Wilaya yote yapatiwe umeme. Kwa mujibu wa takwimu tulizokuwa nazo mwaka 2000 kwa Wilaya kati ya 14 hadi 17, kumi na saba ukiongeza Wilaya ambazo hazina umeme wa Gridi ya Taifa lakini ilikuwa na umeme wa ushirika, kwa Wilaya kama 14. Katikati hapa baina ya 2000 na sasa kuna Wilaya nyingi tu ambazo zimepata umeme na nyingine ambazo ziko katika hatua za mwisho kabisa kupata umeme kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge wa Ukerewe leo alisimama hapa na kutoa pongezi zake za dhati kwa Mheshimiwa Rais na kwa Serikali yake, kwamba umeme sasa utafika Ukerewe. *(Makofi)*

Kwa mujibu wa takwimu za awali ingelikuwa si kwa kuongezeka kwa Wilaya kwa hakika sasa hivi tungekuwa tumeshakwenda karibuni zaidi ya nusu ya ahadi ambayo tulikuwa tumeitoa hapo awali. Lakini kama mnavyofahamu WaheshimiwaWabunge Wilaya hizi zimeongezeka lakini pamoja na kuongezeka ni dhamira ya Serikali kuhakikisha kwamba makao makuu ya wilaya yanapatiwa umeme. Niseme tu kwamba kama ambavyo nimewahi kusema siku moja wakati najibu swali hapa Bungeni, naona sasa hivi kuna mpango ambao tunaushughulikia na kwa sababu haujakamilika kabisa kabisa, si vizuri niutolee maelezo ya kina lakini nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba tunatambua kwamba kuna baadhi ya makao makuu ya Wilaya hayana umeme, na kwamba tuliahidi hivyo na kwa kadri ya uwezo wa fedha utakavyotuwezesha, tuna wajibu wa kuhakikisha kwamba ahadi hiyo inatekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la bei ya umeme kuwa juu. Ni kweli kwamba bei iko juu, lakini ningependa kulikumbusha Bunge lako Tukufu kwamba pia Serikali imekuwa ikijitahidi kukabiliana na tatizo hili. Kwa mfano, mwaka 2002 Serikali ilifanya marekebisho ili kuweza kuhakikisha kwamba viwanda vyetu vinakuwa ni vya ushindani ukilinganisha na viwanda vya nchi jirani na kama ambavyo kwa Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini ametoa takwimu katika hotuba yake kwamba palikuwa na punguzo kwa kiasi cha asilimia 16 ya marekebisho ya bei ya umeme. Na kama ambavyo tumesema, kutokana na marekebisho yale ya mwaka jana, tunakaribiana sana na nchi zingine hizi na kwa upande wa nchi za Afrika Mashariki kwa kweli bei ya umeme kwa maana ya ujumla nafahamu kwamba Waheshimiwa

Wabunge na Mwenyekiti wa Kamati alizungumza kwa ufasaha kabisa kwamba kunakuwa na mazingira mengine ambayo pengine hayafanani.

Ni kweli tunakubali. Lakini ni kwamba kulingana na takwimu ambazo zimeonyesha kwenye kitabu cha hotuba ya Bajeti, tunalingana lingana na nchi hizi ambazo ni za Afrika Mashariki kwamba hapa Tanzania ni senti 7.6 za Kimarekani, Kenya ni senti 8.4 na Uganda ni senti 8. Lakini tunakubali kwamba pamoja na ulinganisho huu bado tuna haja ya kuhakikisha kwamba viwanda vyetu vinakuwa na bei nafuu ya umeme kwamba wananchi wetu wanakuwa na bei nafuu ya umeme ili waweze kutumia nishati hii muhimu na kuondokana na matatizo yanayotokana na kutokuwa na nishati muhimu kama hii.

Lakini ningependa pia nichukue nafasi hii kwa ajili ya taarifa tu ya Waheshimiwa Wabunge kwamba baadhi ya matatizo yaliyosababisha bei hii ya umeme kuwa kubwa ni kutokana na vituo vilivyoko nje ya Gridi yaani hizi *diesel generators,* zinazotumia dizeli. Kwa mfano, hivi vituo ambavyo vinatumia dizeli, vinachangia asilimia 7 tu ya mapato ya shirika ya Umeme nchini. Lakini yanatumia asilimia 34 ya gharama za shirika. Na ndiyo maana kwamba imo katika maslahi ya shirika na Serikali kwa ujumla kuhakikisha kwamba umeme unasambazwa kwenye maeneo hayo yanayotumia dizeli ili kuweza kuondokana na hasara hii kubwa.

Lakini pia kuna matatizo ya uchakavu wa vifaa kama mita, waya na uvujaji wa umeme na ndiyo maana hivi sasa kuna mradi mkubwa unaendelea nchi nzima wa kufanya audit za mita na kurekebisha na kubadilisha vifaa ambavyo vimechakaa ili kuhakikisha kwamba umeme unasafirishwa na kusambazwa kwa utaratibu unaokubalika. Pia kama ambavyo Waheshimiwa Wabunge mmesema ni kweli kwamba kuna malipo ambayo yanafanyika kwa mitambo ambayo ni ghali ni muhimu sana lakini ni ghali kama ya *IPTL* ambayo pia tunalipa kiasi cha shilingi bilioni 2.6 kwa mwezi na pia pengine Waheshimiwa Wabunge mngependa kufahamu kwamba pamoja na kazi kubwa ambayo *TANESCO* inafanya lakini kutokana na uchumi wetu kutokuwa mkubwa sana kama ambavyo tungependa kwa sasa vifaa vya umeme bado inabidi vilipiwe kodi. Na pia kuna gharama kubwa ya kuchukua umeme kutoka kwenye nchi moja jirani kwa mfano umeme huu ambao tunauchukua kutoka Uganda. Tunauchukua kwa senti 12 kwa *unit* ya umeme.

Sasa hivi majadiliano yanaendelea kuhakikisha kwamba gharama hizi zinashuka na tunafanya hivyo kwa nchi zingine ambazo tunauziana nao umeme. Umeme wa Zambia ni rahisi ukilinganisha na Uganda lakini pia tunafanya nao majadiliano kupunguza bei ya umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kama nilivyosema awali inaendelea na majadiliano hayo na hivi sasa *TANESCO* inakamilisha tathmini kwa msaada wa Benki ya Dunia ya kuhakikisha kwamba kutathmini hizi bei za umeme na namna gani zinaweza zikashushwa ili kuhakikisha kwamba uchumi wetu unanufaika kwa matokeo ambayo tunataraji kwamba yatakuwa mazuri katika kushusha bei za umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la *IPTL* ni suala ambalo limezungumzwa kwa muda mrefu. Napenda niseme yafuatayo:- Kwanza *IPTL* ni kituo cha umeme binafsi yaani ni *IPP, Independence Power* na ni sera yetu ya nishati kuwa miradi ya umeme hii ya watu binafsi iweze kukaribishwa hapa nchini. Na siyo *IPTL* tu peke yake hata Songosongo au Songas pia ni *IPP* na vituo hivi vya uzalishaji umeme vya binafsi vina mambo mawili ambayo tunapaswa kuyafahamu.

Kwanza, kunakuwa na mkataba wa ununuzi wa umeme yaani power purchase agreement lakini pili, katika mikataba ile, lazima patakuwa na *capacity charge* au gharama ambayo inabidi ulipe kwa kuwepo ile mitambo na pili, *energy charge* ile ambayo gharama unayolipa kutokana na matumizi ya umeme unaotumia siku hadi siku kwa mwezi hadi mwezi. Kwa hiyo haya yanafahamika kwamba ndiyo mambo ambayo kwa hakika katika *IPP* zote hizi, ambazo hizi ziko hapa nchini mambo haya yote inabidi lazima yawepo lakini nataka niseme kuhusu *IPTL,* kwamba *IPTL* ilianzishwa zamani, mwaka 95 yaani kwa mikataba yake.

Wakati nchi yetu iko katika hali mbaya sana ya mgao wa umeme. La pili, hivi sasa tunaweza kuepuka mgao kutokana na kuwepo *IPTL* ambayo ina uwezo wa megawati 100. Pengine Waheshimiwa Wabunge mngependa kujua, kwamba kutokana na hali ya ukame ambayo imekuwa ikituandama katika kipindi cha mwaka mmoja sasa, hali ya maji katika bwawa tunalolitegemea sana, linalotoa karibuni

asilimia 80 ya uzalishaji wa umeme wa maji yaani Mtera imeanza kupungua. Na kina cha maji cha sasa hivi ni mita za ujazo 694.44 na kiwango cha chini ni mita 690 na cha juu ni 698.5.

Ninachotaka kusema ni kwamba tunaweza au tunaepuka mgao kutokana na ukweli kwamba sasa hivi *TANESCO* inabidi wanunue umeme kutoka kwenye *IPTL*. Na kutokana na gharama hizi ambazo tunakubali kwamba gharama za mradi wa *IPTL* ni kubwa lakini mazingira yake ni kama ambavyo nimeyaeleza jinsi ilivyoingia hapa nchini. Serikali kwanza ilipeleka suala zima la gharama kwenye kituo cha kimataifa cha kusuluhisha masuala ya uwekezaji yaani *International Center for Settlement of Investment of Disputes* na kuweza kupata hukumu ambayo imepunguza hii *capacity charge* kutoka dola milioni 4.5 kwa mwezi hadi kufikia dola milioni 2.6 za sasa kwa mwezi. Kwa hiyo Serikali imekuwa makini kuhakikisha kwamba gharama hizi kwa kweli tunazipunguza. *(Makofi)*

Lakini pili, Serikali sasa hivi kama ambavyo Mheshimiwa Waziri amesema imo katika utaratibu wa kuendelea kutafuta uwezekano wa kupunguza hii *capacity charge* na ikiwezekana kuununua mtambo mwingine, mtambo wenyewe kulingana na hali ya mazungumzo yatakavyokwenda. Tumewesaliana na Serikali ya Malysia na nataka tuhakikishe kwamba gharama hizi ambazo ni kubwa basi zinashuka na pia pamekuwa na mazungumzo na *IPTL* wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo limezungumzwa sana na Waheshimiwa Wabunge ni suala la kukatika katika umeme. Suala la umeme lina sehemu tatu kubwa. Suala la uzalishaji yaani generation usafirishaji, transmission usambazaji distribution.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli tumeshawahi kujibu hapa Bungeni kwamba tatizo kubwa hasa linatokana na uchakavu wa vifaa katika mfumo mzima wa umeme katika kuzalisha na hasa kusafirisha na kusambaza umeme. Na ukosefu wa matengenezo ya uhakika katika mifumo hiyo ya umeme. Pia tuliwahi kusema hapa Bungeni kwamba wizi wa vifaa vya umeme vile waya, mafuta ya transformer na mengineyo yamechangia na matukio mengine ya dharura ambayo yako nje ya uwezo wa Shirika yaani natural calamities pia yamekuwa yamechangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia ni suala zima la kusafisha njia za umeme na ndiyo maana kama mnavyofahamu hivi sasa Shirika la Umeme *TANESCO* liko katika mpango mkubwa siyo tu wa kubadilisha vifaa lakini pia wa kusafisha zile njia za umeme kukata miti ambayo iko katika njia za umeme. Sisi tunathamini sana mazingira. Lakini ukweli ni kwamba unapokuja kwenye suala la umeme ni kama vile barabara ambapo unabidi uwe na sehemu ya reserve kwenye umeme njia zile za umeme chini yake lazima njia ziwe safi. Vinginevyo ama umeme unapotea au inahatarisha maisha ya watu, inahatarisha maisha ya mitambo. Kwa hiyo, hili ni suala ambalo ndiyo maana sasa hivi *TANESCO* wanashughulika katika kusafisha njia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nilithibitishie Bunge lako Tukufu kwamba sasa hivi *TANESCO* inafanya matengenezo makubwa kutokana na makusanyo mazuri ambayo imekuwa ikiyapata, inanunua vifaa na tumeshawahi kusema hapa Bungeni kwamba takribani shilingi bilioni 7 zimeshatumika sasa hivi katika kununua vifaa na wanafanya matengenezo muhimu na kuna mradi mkubwa unaondelea katika kutekeleza ukarabati wa vituo vyote vya Gridi ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na haya pamekuwa na mambo mengine mahususi ambayo yametajwa na Waheshimiwa Wabunge kuhusu maeneo yao. Kama ambavyo tumesema awali itakuwa siyo rahisi kupitia mchango wa kila Mheshimiwa Mbunge hadi Mbunge, lakini tutatoa majibu mahususi kwa maeneo mbalimbali, kila mtu ametoa maeneo yake kwa mfano Mheshimiwa Mongella hapa alikuwa anazungumzia suala la Ukerewe anataka athibitishiwe.

Napenda nichukue nafasi hii nikuthibitishie kwamba ratiba ya upelekaji umeme Ukerewe iko pale pale. Na nataka pia niwathibitishie ndugu zangu wa Urambo na Serengeti kwamba upelekaji umeme kwenye makao makuu ya Wilaya hizi uko pale pale na tunarataji kwamba miradi hii itakamilika muda mfupi ujao. Lakini kuna mengine ambayo yanaendelea sasa hivi Ngara, Biharamulo hadi Chato kwa Mheshimiwa Magufuli na maeneo mengine na tutajitahidi kadri iwezekanavyo kuhakikisha kwamba na maeneo mengine pia yanapata kipaumbele. Kuna maeneo yametajwa mengine na Mheshimiwa Mudhihir

kule Mchinga, Bukene, Mafia kwenye michanga ya maandishi, kwa Mheshimiwa Mwandoro na maeneo mengi ya Waheshimiwa Wabunge. Lakini napenda nichukue nafasi hii kwanza nimwombe sana Mheshimiwa Kahumbi, sijui kama yupo saa hizi? *(Kicheko)*

Kwamba tatizo la Bukene ni kweli kabisa nilikwenda, nalifahamu, amenitembeza pale Bukene. Mimi tatizo hili nalifahamu sana, kama maeneo mengine ambayo pia niliweza kufanya ziara. Namwomba Mzee Kahumbi pamoja na yote haya, lakini atupe nguvu za kuendelea kufanya kazi ili tuje kumhudumia na yeye. Ningeweza, ningesema hata Kinyamwezi au Kisukuma hapa. *(Kicheko)*

Ningesema *beebee uli ndugu* yaani *zinyagamshile.* Ndiyo! *(Kicheko)*
Mheshimiwa Mzee Kahumbi, ndugu yangu wewe, Mzee wangu, kubali yaishe Mzee Kahumbi. *(Makofi/Kicheko)*

Ningesema hivyo hivyo kwa ndugu yangu Mheshimiwa Mabina, basi hata weweMheshimiwa Mabina, Mswalie Mtume Bwana Mabina. *(Kicheko)*

Ningesema hivyo hivyo. *Zingayaishie Mabina.* *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya ni baadhi tu ya mambo ambayo nimepata nafasi kuyachangia na mimi kabla sijamaliza naomba nichukue nafasi hii kwa kweli niwashukuru wapiga wa Wilaya ya Kibaha kwa imani kubwa ambayo wamenipa ya kuwa Bungeni sasa kipindi cha pili na najua sasa hivi wana tatizo la maji. Lakini namshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo kwa kulishughulikia kikamilifu suala hili la maji na nina imani nayo kwamba tatizo hili litapata ufumbuzi. Baada ya kusema haya, naomba nirejee kuwaomba Waheshimiwa Wabunge wote kwamba ndugu zangu tunawaomba sana sana na kwamba mliyoyasema yote sisi tumeyasikia, tumeyakubali na wale watani zangu leo siku yangu. Leo nimewakopesha. Lakini ninawaomba ndugu zangu, *zinyagaishile* .

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi naomba nianze majumuisho yangu kwa kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote na wananchi ambao wanatusikiliza leo kwa jinsi ambavyo wameonyesha msisimko hasa kuhusu Sekta ya Madini ya nchi yetu ambayo imeibuka kwa haraka katika kipindi cha miaka mitano, sita hivi iliyopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru vile vile wapiga kura wa jimbo langu, wananchi wa jimbo langu la Same Mashariki kwa baraka zao na sala zao na kura zao ambazo wanaendelea kunipa na zimeniwezesha kuwa hapa leo nikihudumia Taifa letu. Kama alivyosema Mheshimiwa Naibu Waziri, Dr. Msabaha, hoja zenu zilikuwa nyingi sana na ni hoja za msingi kabisa hasa hasa kwenye sekta ya Madini. Sekta hii Waheshimiwa Wabunge mnafahamu ilikuwepo wakati wa Ukoloni, tukaupata uhuru, tukaichukua sekta hiyo sisi wenyewe, tukawa na mashirika kama *STAMICO,* Minjingu na kadhalika.

Mashirika haya yakafifia kama mashirika mengine ya umma. Mheshimiwa Mbunge mmoja aliuliza akasema kwa nini Serikali haiendi *World Bank* ikakopa, ikaendeleza miradi hii ya madini. Miradi ya namna hiyo ni miradi yenye risk nyingi sana na utakuta huwezi kukopa kama Serikali ukaingia kwenye biashara ya namna hiyo. Maana hatari ya kupoteza ni kubwa sana.

Kwa hiyo, Serikali inakopa *World Bank,* mabenki ya *Africa Development Bank* kwa huduma za kijamii mara nyingi. Tulipokuwa wajamaa tulikuwa tunakopa kwa shughuli hizo mnakumbuka. Serikali ilikuwa inakopa, iendeshe biashara na ndizo hizo, *well*, uchumi wa kijamaa na ndizo hizo ambazo zimetufikisha hapa tulipo. Sasa tumebadilisha tumeingia kwenye mfumo huu wa Sekta binafsi hasa kwenye madini tunajifunza.

Afrika ya Kusini ina historia ya miaka 100 na bado wanajifunza. Juzi juzi hapa baada ya kupata uhuru nao wakatazama mikataba yao na taratibu zao za kuchimbua madini na faida ya madini katika nchi yao, wakaona lazima wabadilishe. Tunaiga ndugu zanguni. Sisi hapa tunaiga kutokana na wenzetu mbele yetu. *We don’t want to re-invent the wheel,* kule ambako wenzetu walikosea sisi tunataka tukuepuke na

tuweze kupata faida katika Taifa letu hasa pato letu la Taifa kutokana na rasilimali hii ambayo kama mnavyosema inamalizika haraka.

Kwa hiyo, michango yenu tunaithamini sana, maana wengi mnajua, wengi mmesafiri na mnaelewa ni kitu gani kinatokea nchi zingine. Sasa sisi kama Serikali kama alivyosema mwenzangu, tunasikia, na tunatekeleza yale ambayo tunaweza kuyatekeleza. Kwa hiyo, tunawashukuru sana kwa michango hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, waliochangia katika hoja hii ni wengi 13 walichangia kwa kuzungumza na tisini na nne walichangia kwa maandishi. Naomba niwataje wale ambao walichangia kwa kuzungumza. Kwanza kabisa ni Mheshimiwa William Shellukindo, Mbunge wa Bumbuli, na Mwenyekiti wa Kamati yetu ya Uwekezaji na Biashara.

Wengine waliochangia ni Mheshimiwa Isaac Cheyo, Mheshimiwa Dr. Lucy Nkya, Mheshimiwa Mwanamkuu M. Kombo, Mheshimiwa James Msalika, Mheshimiwa Ernest Mabina, Mheshimiwa Mbaruk Mwandoro, Mheshimiwa Stephen Kahumbi, Mheshimiwa Frank M. Mussati, Mheshimiwa Felix Mrema, Mheshimiwa Ismail J.R. Iwvatta, Mheshimiwa Balozi Getrude M. Mongella na Mheshimiwa Ali Machano Mussa. *(Makofi)*

Waliochangia kwa maandishi ni Mhehimiwa Esha H.Stima, Mheshimiwa Elizabeth N. Batenga, Mheshimiwa Ibrahim W. Marwa, Mheshimiwa Bakari S. Faki, Mheshimiwa Philip A. Magani, Mheshimiwa Ally A. Karavina, Mheshimiwa Emmanuel E. Kipole, Mheshimiwa Faustine K. Rwilomba, Mheshimiwa Remedius E. Kissassi, Mheshimiwa Job Y. Ndugai, Mheshimiwa Lucas L. Selelii, Mheshimiwa Edigar D. Maokola-Majogo, Mheshimiwa Paul P. Kimiti, Mheshimiwa Khadija S. Ngozi, Mheshimiwa Paschal C. Degera na Mheshimiwa Bahati A. Abeid,

Wengine ni Mheshimiwa Dr. Thadeus M. Luoga, Mheshimiwa Oscar T. Mloka, Mheshimiwa Sijamini M. Shaame, Mheshimiwa Esther K. Nyawazwa, Mheshimiwa Dr. James M. Wanyancha, Mheshimiwa Herbert J. Mntangi, Mheshimiwa Mchande S. Mchande, Mheshimiwa Omar Juma Omar, Mheshimiwa Anne S. Makinda, Mheshimiwa Mossy Suleiman Mussa, Mheshimiwa Mgana I. Msindai na Mheshimiwa Philip S. Marmo.

Wengine ni Mheshimiwa Kidawa Hamad Saleh, Mheshimiwa Biatus R. Magayane, Mheshimiwa Mwadini Abass Jecha, Mheshimiwa Dr. L. Gama, Mheshimiwa Hamza A. Mwenegoha, Mheshimiwa Abu T. Kiwanga, Mheshimiwa Fatma Said Ali, Mheshimiwa Alhaj Abdallah Shaweji, Mheshimiwa Jacob D. Shibiliti, Mheshimiwa Kijakazi Khamis Ali, Mheshimiwa Mudhihir M. Mudhihir na Mheshimiwa Profesa Pius P. Mbawala.

Wengine ni Mheshimiwa Profesa Simon Mbilinyi, Mheshimiwa Juma S. Kidunda, Mheshimiwa Mohamed A. Abdulaziz, Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar, Mheshimiwa Dr. Aaron D. Chiduo, Mheshimiwa Shamsa Selengia Mwangunga, Mheshimiwa Hezekiah N. Chibulunje, Mheshimiwa Ali Said Salim, Mheshimiwa Omar S. Kwaangw', Mheshimiwa Ireneus N. Ngwatura, Mheshimiwa Halimenshi R. M. Mayonga, Mheshimiwa Yussuf Kombo Juma na Mheshimiwa Profesa Henry R. Mgombelo.

Wengine ni Mheshimiwa Henry D. Shekiffu, Mheshimiwa Anthony M. Diallo, Mheshimiwa Raphael N. Mlolwa, Mheshimiwa Abdillah O. Namkulala, Mheshimiwa Venance M. Mwamoto, Mheshimiwa Rainald A. Mrope, Mheshimiwa John E. Singo, Mheshimiwa Jeremiah J. Mulyambatte, Mheshimiwa Issa Mohammed Suleiman, Mheshimiwa Kilontsi M. Mporomyi, Mheshimiwa Profesa Jumanne A. Maghembe, Mheshimiwa Abdallah Khamis Feruzi na Mheshimiwa Profesa Daimon M. Mwaga.

Wengine ni Mheshimiwa Khalid S. Suru, Mheshimiwa Njelu E.M. Kasaka, Mheshimiwa Robert K. Mashala, Mheshimiwa Charles H. Kagonji, Mheshimiwa Arid M. Uledi, Mheshimiwa Damas Pascal Nakei, Mheshimiwa Dr. Batilda S. Burian, Mheshimiwa Shaib Ahmad Ameir, Mheshimiwa Zahor Juma Khamis, Mheshimiwa Frank Michael Mussati, na Mheshimiwa Benedicto M. Mutungirehi.

Waheshimiwa wengine waliochangia kwa Maandishi ni Mheshimiwa John L. Mwakipesile, Mheshimiwa Abdula S. Lutavi, Mheshimiwa Anthony K. Choya, Mheshimiwa Nazir M. Karamagi, Mheshimiwa Capt. Theodos J. Kasapira, Mheshimiwa Parseko V. Kone, Mheshimiwa Mbaruk Mwandoro, Mheshimiwa Salma Khamis Islam, Mheshimiwa Gwassa A. Sebabili, Mheshimiwa Ruth B. Msafiri, Mheshimiwa Maria D. Watondoha, Mheshmiwa Anne K. Kilango (Malecela), Mheshimiwa Zahor lJuma Khamis, Mheshimiwa Mohammed Rajab Soud, Mheshimiwa Jackson M. Makwetta, Mheshimiwa Mohamed H. Missanga na Mheshimiwa Paul E. Ntwina. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mbunge ambaye amechangia mwisho lakini kwa uzito mkubwa ni Mheshmiwa Dr. Ibrahim Msabaha, Naibu Waziri wa Nishati na Madini. Namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa maelezo ambayo ametoa kuhusu hoja mbalimbali na narudia tena kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge kwamba hoja zilikuwa nyingi hasa kwenye maandishi na kama alivyosema tutawajibu mmoja mmoja kwa maandishi mara tu tukimaliza shughuli zetu hizi hapa Bungeni.

Lakini niseme tu la jumla lingine kwamba Mheshimiwa Mwenyekiti wetu wa Kamati ya Biashara na Uwekezaji, Mheshimiwa William H. Shellukindo - Mbunge wa Bumbuli, alishauri kwamba labda kuwe na Semina wakati muafaka kati ya Waheshimiwa Wabunge na Wawekezaji wa Sekta ya madini.

Jana tulijaribu kukaa nao lakini kilikuwa ni kikao ambacho hakikuwa rasmi, kiliandaliwa na Mheshimiwa Leonard Derefa. Sasa Mheshimiwa William Shellukindo ameshauri kwamba labda tuwe na kikao rasmi cha siku moja au mbili hapa Bungeni, tukae na wawekezaji wa madini na wadau mbalimbali ili tuweze kuelezana, kufahamishana na kuelimishana kuhusu sekta hii, vipengele vyake mbalimbali, mirabaha, kodi zake, faida tunazozipata, faida wanazopata wao na ni namna gani tunaweza kuboresha ushirikiano huu katika Sekta hii ya Madini. Kwa hiyo, hilo sisi kwa upande wetu tumeliafiki na tutawasiliana na Mwenyekiti huyo ili tuweze kuandaa semina hiyo kwa wakati unaofaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba nizungumzie mambo matatu au manne hivi ambayo Mheshimiwa Dr. Ibrahim Msabaha hakuyagusia.

Kwanza kabisa ni kuhusu fidia kule katika Mgodi wa Geita. Wakati mgodi ule ulipoanza kuna wananchi ambao ilibidi wahamishwe sehemu ile yenye madini. Hili pia limetokea kwenye Mgodi wa Afrika ya Mashariki na sehemu nyingi. Ni haki yao wananchi kama wale kulipwa fidia kufuatana na taratibu za Serikali. Lakini kule Geita kulitokea matatizo kwamba fidia ambayo ilitolewa na wenye mgodi, kwa bahati mbaya haikuwafikia wastahili wote kwa wakati, jambo hili limewakera kwa muda mrefu. Wiki iliyopita nilibahatika kuwa kule na Waheshimiwa Wabunge wa sehemu ile na tukawa na mkutano wa hadhara, jambo hilo lilijitokeza kabisa kwa wananchi kwamba kwa nini sisi hatupati fidia yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wale wanaodai wengi siyo kosa lao, wenye makosa ni wale ambao ulikuwa ni wajibu wao kuzigawa fedha hizo kwa wanaostahili kulipwa. Lakini jambo hili limechukua muda mrefu likichunguzwa na Serikali na sasa ninafurahi kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge kutoka kule na hasa wananchi wa kule na hasa wale ambao wanahusika kwamba, Serikali imelifikisha mahali pazuri ambapo uamuzi utatolewa na tutalimaliza ili tuondoe kero hiyo kwa wananchi ambao hawana sababu ya kubughudhiwa na kero ya aina hiyo.

Kwa hiyo, tutalimaliza mapema iwezekanavyo. Naomba niliachie hapo kwa sababu sina majina wala kitu chochote leo. Napenda niseme tu kwamba ndiyo nia ya Serikali na liko katika ngazi za juu na tutalimaliza na wananchi waweze kuarifiwa kama hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, naomba nizungumzie kuhusu utafutaji wa mafuta hapa Tanzania. Kuna imani na sisi tuna imani katika Wizara yangu na wataalam wetu kwamba labda kuna mafuta hasa Baharini na Pwani yetu hii ya Tanzania. Vipimo vyote, dalili zote na vigezo vyote vinaonyesha ya kwamba kuna mafuta. Kuna Mheshimiwa Mbunge mmoja nadhani amesema leo kwamba kila akipita pita ananukiwa nukiwa harufu ya mafuta ya taa na mafuta ya petroli.

Sasa kwa kweli kipimo cha pua siyo cha kutegemea sana ukitaka kuwekeza kwenye mafuta. Lakini vipimo vya kitaalam vile vile vimeonyesha ya kwamba kule Pemba na kule Unguja na hasa kutoka Mtwara mpaka Lamu huko Kenya kuna dalili za mafuta. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, utafutaji wa mafuta ni kitu ambacho ni ghali sana na kinachukua muda mrefu sana. Kila nchi hata nchi kubwa, ukubwa kwa maana ya uwezo kama Nigeria, nao wanategemea utafutaji wa mafuta hufanywe na makampuni makubwa zaidi. Kampuni kama Shell International ndiyo wenye uwezo na Bajeti za kuweza kwenda kutumbukiza mahali. Kisima kimoja kinaweza kugharimu dola 15, 20 au dola 40, milioni yaani kisima cha kutafuta mafuta. Kwa hiyo, sisi wenyewe kusema labda tutafute kutokana na Bajeti yetu hatuwezi, ni lazima tuwahamasishe wawekezaji wakubwa ili waje watusaidie kutafuta kama mafuta yapo na yapo kiasi gani ili waanze. Baada ya kuyatafuta, baada ya drilling ni lazima waanze sasa kuchimba kuyatoa pale ikiwa yapo ya kutosha kibiashara yaani *Commercial Quantities*. Kama wakiona yapo lakini ni kidogo hawataendelea na shughuli hiyo lakini wanapoteza pesa, ni pesa zao sisi hatuweki hata senti moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tusipofanya hivyo wenzetu, jirani zetu kama Kenya sasa hivi wamechangamkia sana utafutaji wa mafuta maana wanajua jiolojia ni ile ile. Kwa hiyo, tukichelewa sisi tutapata hasara ya kwamba tutaachwa na Bajeti hizo hizo zitakwenda kutafuta mafuta sehemu nyingine na sisi tutabaki kungoja Bajeti za miaka mingine au tutaachwa kabisa kwa sababu hatuamui upesi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo ni nini? Tatizo ni kwamba Sheria yetu ya kutafuta mafuta ya mwaka 1980 inahitaji kurekebishwa, kuna vipengele vichache vichache vya kurekebishwa. Vipengele hivyo vinahusu kwa mfano ukubwa wa vitalu unachompa mtafutaji wa mafuta, faini utakayompiga kwa mfano kama atakuwa mbabaishaji na malipo atakayolipa kwa kila kitalu unachompa. Sasa vitu kama hivyo bila kuibadilisha hiyo Sheria wawekezaji wanasema hatuji maana Sheria tuliyonayo ya mwaka 1980 ni ya zamani sana na haiwapi imani, *doesn't give them confidence* ya kuwekeza mapesa mengi namna hiyo kama vile vipengele vidogo vidogo havikusahihishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vipengele hivyo tukivileta hapa Bungeni kama tulivyotaka kwenye Bunge lililopita, tukivipitisha havisemi nani atachukua kiasi gani na pia nani atapata faida gani, vinaruhusu tu wale waje wawekeze, wachimbue yale mafuta. Sasa sisi kama Taifa tutakaa, tuseme mafuta yamegunduliwa tutagawana namna gani, huyu sungura sasa tumemshika yupo hapa tumeishamuua, tugawane nani ale mguu, nani ale kichwa na pia nani ale sikio. Hilo siyo la sasa hivi na hilo halihusiani na hii Sheria. Kwa hiyo, ninachoomba ni kwamba tuelewane, Sheria hiyo ije Bungeni ijadiliwe, ipitishwe ili tuweze kusaini mikataba watu kama Shell na watu kama *Petrobras* wa Brazil waje waanze kutumia pesa zao, watuhakikishie kama mafuta yapo ama hayapo. Tukielewana hivyo basi Muswada uletwe. Sasa tuna tofautiana kati ya SMZ na SMT, ndiyo ukweli wenyewe. Lakini mazungumzo yanaendelea na wiki ijayo Jumanne mimi nitakutana na Mheshimiwa Waziri mwenzangu wa Zanzibar, Mheshimiwa Sadati ili kuweza kulisukuma jambo hilo ili tuelewene, Muswada uje hapa upitishwe ili tuanze kutafuta mafuta na yakipatikana tuamue tunagawana namna gani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tutashukuru kama Waheshimiwa Wabunge wa pande zote mtasaidia kutoa hiyo understanding ili tuweze kulisukuma hili ili tutafute mafuta kwa haraka na tusije tukakosa raslimali nyingine ambayo iko ardhini. Tutagawana namna gani tutajadili baadaye. Tuna Kamati yetu ya Mheshimiwa William Shellukindo ambayo inashughulika na mambo ya fedha, tuna Wizara zetu na pia tuna Serikali zetu mbili, hili halitatushinda kwa kweli kama tutakuwa tumefikia hatua hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie vile vile kuhusu umeme uliokatwa siku chache kwenda Zanzibar. Shirika la *TANESCO* ni Shirika la Umma mia kwa mia, halijabinafsishwa bado. Tulichofanya mpaka sasa hivi ni kutafuta Management ambayo inasaidiana na Watanzania ili kuweza kuliendesha shirika hilo. Shirika hili tumelipa majukumu manne. Kwanza, kukusanya mapato kwa uhakika kabisa kabisa, hakuna kumhurumia Mheshimiwa Daniel Yona kwa sababu ni Waziri wa Nishati na Madini au Wizara fulani kwa sababu ni Wizara ya Jeshi au Ofisi fulani kwa sababu ni Ofisi nyeti, kila mmoja anayetumia umeme alipie. Kama ni mtu binafsi, kama mimi nyumbani nilipie, nisipolipa nikatiwe, kama ni Ofisi ya Serikali na huku Bara tumekwishafanya hivyo, mwezi Juni mwaka jana Jeshi tuliwakatia au tuseme walikatiwa, polisi walikatiwa. Ikulu walibakiza Saa Mbili tu wakatiwe lakini wakawahi kwenda

kuzitafuta hizo pesa huko zilikokuwa, maana wana Bajeti zao za kulipia umeme, maji na pia kulipia simu, wakatafuta pesa wakalipa. Ikulu hawakukatiwa lakini kwa kweli hakuna ambaye angezuia wangekatiwa kwa sababu wanatumia na wana Bajeti na wana *Accountants* wao, kwa hiyo ni wajibu wao kulipa bill ambazo zimegharimiwa na Shirika la Umma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa *TANESCO* tumewapa kazi hiyo mojawapo ya kukusanya fedha kwa uhakika kila ilipo bila kumwonea mtu. Ndiyo maana hata *bill* zao tumewaambia sasa hivi ziwe ni za uhakika, wasimwonee mtu yeyote. Lakini wana roho vile vile, *they have heart,* hawaendi tu na kukata mara moja na hasa kwenye Mashirika na kwenye Mawizara. Mara nyingi wanakwenda wanakaa wanazungumza na mteja wao kwa sababu *they want the client,* hawataki kumpoteza mteja mkubwa. Mara nyingi wanakaa, ukiwauliza watakwambia tumekaa na mteja huyu, Kiwanda hiki au Wizara hii tukazungumza namna ya kulipa madeni kama unataka kulipa kidogo kidogo ili mradi mteja na yeye awe mkweli. Sasa kama mteja utasema mimi nitalipa kesho, nitalipa kesho kutwa hulipi, nitalipa lakini ukilipa labda kama ni *Cheque* haifiki au ina *bounce.* Hawa wanafanya biashara, tumewatuma kufanya hivyo ili tuweze kuliboresha Shirika letu, tupate fedha za kutosha na pia tupate nishati ambayo mmesema ninyi Waheshimiwa Wabunge wote hapa kwamba inahitajika katika kukuza uchumi wetu. Tuwasaidie *TANESCO* kukusanya madai ya halali pale pote ambapo wametoa huduma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa *TANESCO* inafanya biashara ya umeme kule Unguja na Shirika lile la Umeme Zanzibar. Ndiyo maana kidogo natofautiana na wenzangu wakisema, tumeikatia Serikali ya Zanzibar umeme. Wizara yangu mimi ikakatiwa umeme hatusemi tumeikatia Serikali ya Tanzania, tunasema Wizara ya Nishati na Madini imekatiwa umeme kwa sababu kama ninavyosema tuna Bajeti yetu, tuna wajibu wa kulipia siyo Serikali zima ambayo imekatiwa. Siyo Serikali ya Zanzibar na hapakuwa na mpango, premeditated wa kuwakatia umeme Zanzibar. Ni kwamba biashara hii inayofanywa na mashirika haya mawili na haikuanza jana, imeanza miaka mingi na utaratibu ambao ulikuwa unatumika tangu mwaka jana hasa walioelewana, Bodi hizi mbili *TANESCO* na Shirika lile la Umeme Zanzibar ni kwamba, jamani eeh madeni yale makubwa ya Zanzibar yatatazamwa na Serikali pole pole. Sasa *from now on June* mwaka 2002 mlipe *current bills, bill* yako ya sasa. Kukawa na matatizo kidogo, bado jamaa wakashindwa kulipwa, wakati mwingine wakapewa muda, wakaambiwa *okay* mtalipa tarehe fulani mwezi unaofuata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayo *sequence of events* ambayo ilitufikisha hapo tulipofika wiki iliyopita. Hii imetengenezwa na *TANESCO.* Sasa Mheshimiwa Sadati tulipozungumza kuhusu suala hili juzi, alisema na yeye anachunguza upande wake ili aone kwa nini ilifikia hatua hiyo, ni jambo la kusikitisha lakini kwa nini lilifika hapo? Mimi nilipouliza kwa upande wangu nikaambiwa ya kwamba mambo yalikuwa hivi na hivi. Mwenzangu anachunguza kwa upande wake kwamba ilikuwaje wale wakaruhusu mpaka wakafikiwa na hatua ya kukatiwa umeme? Mara nyingi waliposhindwa siku za nyuma walikaa na waliposhindana kabisa walikuja hata Serikalini kuzungumza na Wizara ya Fedha kwa mfano, wasaidiwe kama ni fedha kidogo ili waweze kuendelea kupata umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ukweli nilionao kwa kifupi tu, nadhani nina muda bado.

**MWENYEKITI - MHE. ANNE S. MAKINDA:** Ndiyo na unaulizwa ilikuwaje?

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Sawa!! Kwa kifupi ni hivi, Mashirika ya *TANESCO* na *Zanzibar State Fuel Corporation* yalikubaliana Julai, 2002 kuwa *SFPC* ndiyo lile shirika la kule itakuwa inalipa *current bills* zake siku 15 baada ya kupokea ankra, *point* ya kwanza hiyo. *TANESCO* ilitambua kuwa shirika lile wasingeweza kulipa *bill* kikamilifu na wakatoa miezi mitano kwa *SFPC* kujenga uwezo huo. Walipoingia *Net Group* ndiyo hiyo *discipline* ikaanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, Bodi ya Mashirika yetu mawili zilikubaliana kutotoza riba kwenye deni la nyuma, madeni ya nyuma tukasema hakuna riba. Aidha, *SFPC* iliagizwa ifuatilie na *TRA* kuhusu kusamehewa kodi ya *VAT.* Ilitajwa na Mheshimiwa Mbunge mmoja kwamba wanalipa *VAT* lakini walielewana Bodi mbili kwamba hilo lichukueni Hazina kama mnaweza kusamehewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 30 Mei, 2003 *SFPC,* Shirika lile lilitoa hundi bila kuwa na fedha Benki. Hundi Na. 222432 ya Shs. 364,594,500/= kwa ajili ya *bill* ya mwezi wa Aprili, huo ni mwisho wa Mei *bill* ya Aprili inatolewa na *Cheque* inakuja ina *bounce, Cheque* hiyo haikukubaliwa na Benki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tano, kati ya hundi tatu moja Na. 222436 yenye thamani ya Shs. 174,992,750/= ilikataliwa na Benki. Ile *Cheque* iliporudi zikaandikwa nyingine tatu, mbili zikapita ndogo ndogo sasa, hiyo moja ika-*bounce* tena. Tarehe 17 Julai Wakuu wa Mashirika mawili haya, waliwasiliana tena kuhusu *bill* kutolipwa na *TANESCO. TANESCO* ikatahadharisha kuwa *bill* isipolipwa umeme utakatwa Saa Sita Mchana siku ya tarehe 21 Julai, 2003 kwa hiyo waliarifiwa. Tarehe 17 walipewa *notice,* tarehe 17 mpaka tarehe 21 kwamba tutakata siku hiyo Saa Sita. Sasa kama jamaa wale wangejipiga piga kila mahali wakaenda wanakojua wenyewe labda wangezipata pesa lakini ngoja msikie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkurugenzi Mkuu wa *SFPC* hakuleta taarifa yoyote *TANESCO* na ndiyo maana umeme ukakatwa Saa Saba Mchana na kurudishwa Saa Kumi na Dakika Tano Jioni baada ya kufanya malipo ya zile pesa ambazo zilikuwa zimebaki. Hapa kuna mengine ambayo hayakuandikwa kwa mfano Shirika lile liliiambia Benki yake, liliwaambia hawa, Benki yetu itatuma pesa yaani B*ank Transfer* moja kwa moja kutoka Benki yetu, *Peoples Bank* kuja *NBC,* hazikufika. Kwa hiyo, *TANESCO* wakaona eeh tuna mteja hapa ambaye hataki kulipa, *Cheque* zina *bounce* ahadi hazikamiliki *time* imefika. Sasa *TANESCO* wakasema na hili tulielewe, *TANESCO* hawakusema tukate umeme Zanzibar moja kwa moja, tulikatie hili Shirika umeme moja kwa moja, walisema tutawafanyia mgao. Huku Bara tunao mgao unatokea mara kwa mara tukiwa na tatizo fulani. Hatuwakatii Zanzibar *twenty four hours,* ni masaa machache kila siku mpaka walipe, kwa bahati nzuri siku hiyo hiyo wakalipa. *For only a few hours* umeme haukupatikana lakini *those few hours bill* ikalipwa, umeme ukarudishwa na sasa tunaendelea na hali nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni jambo la kusikitisha kama nilivyosema nitakutana na Mheshimiwa Waziri wenzangu wiki ijayo ili tuone chanzo chake na tutafute namna ambapo tutazuia jambo hili lisitokee tena. Lakini kwa kweli vyombo vyetu ni vyetu hivi, ni watoto wetu wawili, mashirika haya mawili, *they have to behave commercially* maana ni mashirika ya kibiashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi huku Bara tumezoea, mimi kwangu simu tunakatiwa, sijui wenzangu Wizara nyingine lakini tunakatiwa mara kwa mara kwa sababu bill hatukulipa upesi. Ni mashirika yetu na tunayafundisha kufanya kazi kwa uaminifu kwa hiyo ni lazima tufanye hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi nyingine ya *Net Group* au ya *TANESCO* tuliyowapa, ni kupunguza gharama ambazo ni *unnecessary costs* na hilo wanaanza kufanikiwa ndiyo maana mapato yao sasa hivi yameongezeka kiasi ambacho tunaweza sasa kufikisha umeme sehemu nyingi. Bado hatujafika kila mahali lakini uwezo unaongezeka na ni kwa sababu ya *discipline* hiyo ambayo imefika pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo nilisema nilieleze hivyo na nitakapokutana na Mheshimiwa Waziri labda atakuwa na maelezo mengine lakini nia yetu itakuwa kwamba jambo hili halitatokea tena kwa sababu tutatafuta taratibu za kuweza kulizuia moja kwa moja. Nadhani hilo nimeligusia vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nigusie jambo la *environment* ambalo Waheshimiwa Wabunge wengi walikuwa na wasiwasi kwamba labda uchimbaji wa madini unaharibu *environment.* Ni kweli lakini katika mikataba tuliyonayo hilo ni jambo ambalo tunalitilia mkazo sana. Kabla mtu hajapewa, kabla mchimbaji hajapewa leseni ya kuchimbua ni lazima awe na *environmental impact assessment* ambayo inatengenezwa na wataalam *independent* na inapitishwa na *NEMC.* Kuna *NGOs* siku hizi za nje na za ndani ambazo zinalinda mazingira kwa dhati kabisa, haziruhusu mazingira yakaharibiwa ovyo ovyo. Mheshimiwa Rais wetu ameanzisha tuzo ya mgodi kila mwaka ambayo unakuwa na mpango mzuri wa kulinda mazingira na tuzo hilo wanalipigania sana wachimbaji mgodi kwa sababu ni sifa kwao, inawapa sifa Kimataifa. Kwa hiyo, hiyo nayo ni hatua mojawapo ambayo inatusaidia kulinda mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini wananchi wenyewe na ninyi Waheshimiwa Wabunge ambao mnatoka sehemu hizi za migodi, tunashukuru kwamba mnakuwa macho mkiona kuna dalili za kuharibu mazingira au mna mawazo ambayo yatatusaidia kuwashawishi hawa wawekezaji tuyalinde mazingira yetu wakiondoka tusiachiwe mashimo, basi tunashukuru kwa kupokea ushauri huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mashimo yaliyopo sehemu mbalimbali mengine ni kwa sababu ya wachimbaji wadogo wadogo, wale inakuwa vigumu sana kuwadhibiti maana anachimba hapa leo, kesho kaondoka, humpati ukamwambia njoo uzibe shimo lako. Kwa hiyo, hiyo inatusumbua kidogo. Lakini jinsi wanavyoungana kuwa vikundi basi tunaweza kuwafuatilia na kuwabana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nigusia moja tu ambalo lilisemwa kwamba kwa nini hatupo kwenye Dar es Salaam *Stock Exchange,* Makampuni ya Madini hayapo kwenye *Dar es Salaam Stock Exchange.* Ili uweze kuandikishwa kwenye *Dar es Salaam Stock Exchange* lazima uwe na kile ki-*record* cha faida. Makampuni haya mengine mengi bado hayajaanza kupata faida. Kwa mfano Afrika ya Mashariki limeanza hata mwaka halijamaliza, mengine bado yanapata hasara na mnasikia mara kwa mara kwamba yanabadilisha *ownership* kwa mfano Afrika ya Mashariki imeuzwa sasa. Wanauza kwa sababu wanaona kungojea mpaka wapate faida, wagawane gawio, *dividend* itachukua muda mrefu. Kwa hiyo, wanauza kwa mwekezaji mkubwa zaidi mwenye uwezo ambaye yeye anaweza kuwekeza zaidi na kungoja muda mrefu ndiyo apate faida yake. Kwa hiyo, wale ambao watakuwa tayari watakuja kuandikisha shares zao katika *Dar es Salaam Stock Exchange, AFGEM* tunasikia karibu wataanza kufanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri juu ya *Tanzanite* ambayo Mheshimiwa Felix Mrema ameutaja na mawazo yake mengi kutoka Arusha, tumeyachukua na tutauzingatia katika kuwawezesha Watanzania hasa sasa kwamba tumeamua kuwa tusipeleke madini yetu ya *Tanzanite* ghafi nje ya nchi. Lakini tutafanya kwa utaratibu ili tusije tukaharibu soko na kuwaharibia ndugu zetu kipato chao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *fiscal regimes* ambazo tunazo Mheshimiwa Dr. Ibrahim Msabaha alizigusia. Mkitazama lile jedwali linaonyesha mrabaha na kodi zile ni *fiscal regimes,* ndugu zangu naomba mzitazame *in totality,* usitazame mrabaha tu, ile *column* ya mrabaha utakuta nchi ambayo ina mrabaha mdogo labda kodi nyingine zinakuwa kubwa, utakuta nchi ambayo ina kodi kubwa inakuwa na mrabaha mdogo. Kwa hiyo, utazame na *all column* ukitaka kulinganisha na nchi nyingine ndiyo utapata picha kamili kwamba sisi *regime* yetu siyo *too soft but we had to start that way,* ilibidi tuanze hivyo ili tuwavutie hao wawekezaji waje nchini wawekeze hapa.

Mheshimiwa Balozi Getrude Mongella kusema tusifungue migodi mingine. Mimi nadhani eeh hapo umetubana sana kwa sababu kwa kweli mimi nadhani tuboreshe mikataba yetu, tuboreshe mafao yetu na maelewano yetu na wale wawekezaji. Lakini tusizuie kuanza migodi mingine maana ndiyo riziki aliyotupa Mwenyezi Mungu, sasa sisi tusipoichimbua na kuwaachia watoto wetu mali hiyo basi tutakuwa hatujafanya lolote. Kwa hiyo, tufanye yote ili tuweze kwenda mbele.

Kuhusu Mzee Ngoma, huyu Mzee Ngoma ni Mpare na anatoka Makanya, namfahamu, ameshaniona siyo kwa sababu mimi ni Mpare lakini kwa sababu ninatoka sehemu hizo na mimi. Na ukweli kama alivyosema Mheshimiwa Arcado Ntagazwa ni kwamba yule Mzee alilipwa. Alipewa ngao, alilipwa fedha na pia alipewa cheti na hayo tuliagizwa wakati ule na Mheshimiwa Rais wa wakati huo, Marehemu Mwalimu Julius K. Nyerere mwenyewe. Alipewa pia vitalu kwa kuchimba yeye mwenyewe kule Mererani. Sasa mimi tumekwishaonana naye mara moja au mara mbili na Mheshimiwa Mbunge wake Mheshimiwa John E. Singo pale vile vile nadhani wanafahamiana. Sielewi kwa nini inasemekana kwamba hatumtambui, tunamtambua maana alipewa cheti, *as far as were are concerned* ndiye aliyegundua *Tanzanite.* Nadhani hilo la Mzee halina utashi, hakuonewa, alipewa fedha za wakati ule, ni fedha nyingi ukizifananisha na za wakati huu na tulimpa vitalu ambavyo *I hope* anavitumia sasa hivi ili aweze kupata faida zaidi kutokana na madini hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, ni faida tunazozipata kutokana na madini. Nataka tena niwarudishe kwenye lile jedwali mojawapo pale tulipoandika *economic benefits* au faida tunazipata kutokana na Sekta yetu ya Madini. Katika kufuatilia kuona kwamba kweli tunapata na hili tumelifanya kwa makusudi ili kuwachokoza ninyi Waheshimiwa Wabunge, lile jedwali linaonyesha ajira tangu tulipoanza kuchimba madini kwa dhati mwaka 1997 hivi mpaka leo, ajira ya Watanzania imepanda kutoka ngapi mpaka wangapi. Wakati huo tulikuwa na watu kama 2,000 tu hivi, sasa hivi tuna watu 5,000. Mchango wa kuwasomesha au kuwaelimisha Watanzania katika kazi za madini tumeweka katika jedwali lile. Makampuni haya yanatumia kiasi gani kila mwaka kutoa elimu kwa Watanzania katika Sekta ya

Madini, michango katika *social community project,* kiasi gani mwanzo na kiasi gani kimefikiwa kwa wakati huu, mwaka hadi mwaka na kiasi gani wananunua hapa nchini vyakula na vifaa, *goods and services.* Yote hayo tumezitaka takwimu hizo tuziweke mle mzitazame ili tuweze kutoa hoja zenye uhakika. Kwa mfano kama tunasema hawanunui kiasi cha kutosha ni kwa sababu gani? Tutasaidiana kutafuta majibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kodi wanazolipa ni kiasi gani ukilinganisha na mapato yao. *Share* tunayoipata sisi kama Taifa maana ni kodi, mrabaha ni sehemu moja tu, kodi nyingi sana ambazo wanalipa, tumeweka pale. Sasa zitazameni, tupeni ushauri Waheshimiwa Wabunge pale ambapo mnafikiria tunaweza kuboresha tutakaa nao ili tuweze kuzungumza na kuwaambia jamani hapa kidogo mngetuongeza. Lakini tuwe na utaratibu wa ku-*dialog* nao ili wasi-*feel* kwamba labda sisi nia yetu ni waanze *and then* tunanyakua au tunawanyanyasa au tunawakatisha tamaa wengine ambao watakuja kuwekeza hapa nchini. Tunao uwezo wa kubadilisha na kuboresha maslahi ambayo Taifa letu linapata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 58 - Wizara ya Nishati na Madini**

Kifungu 1001 - *Administration and General ...* ... Shs. 984,107,500/=

**MWENYEKITI - MHE. ANNE S. MAKINDA:** Haya wote mliosimama mtapata adhabu kwa kuendelea kusimama mpaka muorodheshwe wote. *(Kicheko/Makofi)*

**WABUNGE FULANI:** Sawa!!

**MWENYEKITI - MHE. ANNE S. MAKINDA:** Haya yuko Mheshimiwa Kidawa Hamid Saleh, Mheshimiwa Raynald A. Mrope, Mheshimiwa Kisyeri W. Chambiri, Mheshimiwa Benedicto M. Mutungirehi, Mheshimiwa Capt. Theodos J. Kasapira, Mheshimiwa Halimenshi K. R. Mayonga, Mheshimiwa Dr. James M. Wanyancha, Mheshimiwa Ibrahimu W. Marwa, Mheshimiwa Emmanuel E. Kipole, Mheshimiwa Jeremiah J. Mulyambatte na Mheshimiwa Martha M. Wejja.

Wengine waliosimama kutaka maelezo ni Mheshimiwa Dr. Thadeus M. Luoga, Mheshimiwa Dr. Diodorus B. Kamala, Mheshimiwa Felix C. Mrema, Mheshimiwa Kilontsi M. M. Mporogomyi, Mheshimiwa Parseko V. Kone, Mheshimiwa James P. Musalika, Mheshimiwa Ernest G. Mabina, Mheshimiwa Kabuzi F. Rwilomba, Mheshimiwa Maria D. Watondoha, Mheshimiwa Nazir M. Karamagi, Mheshimiwa Jackson M. Makwetta, Mheshimiwa Lucas L. Selelii, Mheshimiwa Yusuf na Mheshimiwa Ireneus N. Ngwatura.

Waheshimiwa Wabunge, tuelewane, muda wetu ni mpaka saa mbili kasoro robo. Dakika kumi kabla ya kuahirisha kwa dakika moja tunamaliza vifungu vilivyobaki, ndio utaratibu, guarantee guillotine.

**MHE. KIDAWA HAMID SALEH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nina ombi dogo tu kwa Mheshimiwa Waziri, naomba aje alithibitishie Bunge lako hili Tukufu...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kidawa, naomba tukubaliane kwamba badala ya kuwa dakika tano tutumie dakika mbili na nusu kwa sababu hawa waliorodheshwa ni wangapi?

**MHE. KIDAWA HAMID SALEH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, moja tu. Naomba Mheshimiwa Waziri aje alithibitishie Bunge lako hili Tukufu kuwa haelewi kuwa Serikali nzima ya Mapinduzi ya Zanzibar na asasi zake inategemea kupata umeme kutoka Shirika moja tu la *Zanzibar State Fuel Corporation* ambalo nalo linapata umeme kutoka chanzo cha *TANESCO?*

**MWENYEKITI:** Kanuni pia inatuambia suala moja likishazungumzwa halirudiwi, nadhani mnaifahamu.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa swali lake. Namhakikishia kwamba naelewa kabisa kwamba umeme Zanzibar unatokana na Shirika lile ambalo nalo linaupata kutoka *TANESCO.* Ndio maana nasema tutakaa tuone ni namna gani tunahakikisha kwamba umeme haukatwikatwi tena sehemu za Zanzibar katika siku zijazo.

**MHE. RAYNALD A. MROPE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Mheshimiwa Waziri anatueleza juu ya *IPTL* hakuwa amezungumzia sawasawa juu ya *capacity charges.* Kwa sasa hivi *capacity charges* hizi maana yake tunalipa bilioni 3.6 kila mwezi na kwa mwaka tutalipa 43.2 kwa na kwa miaka 20 tutalipa *trilion* moja. Sawa suala hili ndio limepelekwa kwenye International Tribunal kwa upande ule wa pili wa Serikali yaani Mahakama halafu Serikali Kuu nayo pia imepeleka *PCB* na *CID* kwenda ku-*check* mambo yale lakini kwa upande wa Wabunge tunaohusika na wananchi walioathirika sana katika mizengwe ya *IPTL* bado hatujafanya kitu. Tuunde Tume iende kulizamia jambo hili ili wahusika wote waliosababisha hasara kubwa kwa Tanzania waweze kuadhibiwa na waweze kuwajibika kisiasa je, mko tayari? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Kwanza, una maswali mawili, uundaji Tume ni hoja inayopatikana katika kifungu 104(1) hizo ni hoja mbili sisi tunataka moja tu ni ipi hiyo? Mheshimiwa Waziri acha ya kifungu jibu nyingine.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama alivyosema Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba Waheshimiwa Wabunge tuelewane jambo moja ukishakubali mpango wa *IPTL* kuzalisha umeme kwa kutegemea mwekezaji binafsi aitwe Songosongo, *IPTL,* Mchuchuma, Ruhuji kama sio Serikali inayotoa fedha zake kujenga mradi basi inaitwa *IPTL* ikashakuwa *IPTL* inakuwa na aina mbili za gharama moja ni hiyo *capacity charge* na nyingine ni *energy charge.* Kama sasa hivi ilivyo *IPTL* tunaanza kuitumia kwa sababu ya ukame uliopo na karibu tutazalisha megawatt 100 yaani *full capacity* ukitumia yote *full capacity* unaokoa fedha, inakuwa na faida, inakuwa na maana lakini kama kulikuwa na maji wakati wote basi hutumii na yule aliyewekeza anakuambia lazima unilipe kwa sababu nimekuwekea mtambo na ni juu yako kuutumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile labda niwaeleze Waheshimiwa Wabunge kama *IPTL* kesho tungehitaji umeme na akashindwa kuzalisha umeme kwa sababu yoyote ile anatulipa hiyo hiyo 2.6 milioni *dollar per month it both ways* akishindwa ku-*deliver* kwetu tunam-*charge* tukishindwa kuchukua umeme anatu-*charge* na huu ndio mtindo unaotumika duniani kote kwa kutumia *IPTL.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo la Tume nitakuachia wewe lakini tuelewane vile vile *IPTL* ninavyofahamu imechunguzwa na *PCB,* Polisi na hakuna kilichotokea maana kukifanyika uchunguzi katika vyombo vyetu hivyo kunachukuliwa hatua. Mikataba ilisainiwa kihalali kabisa na Kiserikali kabisa na tulipokwenda kwenye *arbitration* tukapunguziwa kutoka kile kiasi ambacho walidai wale mpaka hiyo 123 na ndio inayotumika sasa hivi kuhesabu ile *capacity charge.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani maelezo hayo kwa sasa yatasaidia.

**MHE. RAYNALD A. MROPE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sijaridhika na maelezo kwa hiyo naiomba Kamati hii iagize Bunge liunde Tume yaani natoa hoja kwa mujibu wa Kifungu cha 65 cha Kanuni iundwe Tume ili iweze kwenda kwa undani juu ya suala hili. *(Makofi)*

**MHE. PHILLIP S. MARMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunajaribu kushughulikia suala la Mheshimiwa Mbunge la kutoa hoja, Kifungu cha 104, kifungu hiki kinasema kwamba, bahati mbaya Kanuni ile ukurasa huo haupo. Kifungu cha 104 kinasema: “Kamati Teule yawezwa kuundwa na Bunge kwa madhumuni maalum kwa hoja mahsusi itakayotolewa kwa ajili hiyo na kuafikiwa. Kamati Teule yaweza pia kuundwa endapo baada ya Bunge kujadili hoja fulani litaamua kupeleka jambo fulani litakalotokana na hoja hiyo

kwenye Kamati Teule ambapo utaratibu wake utakuwa kama ifuatavyo. Mara tu baada ya hoja iliyokuwa ikijadiliwa kuamuliwa neno hapo mara tu hoja iliyokuwa ikijadiliwa kuamuliwa Mbunge yeyote mwenye nia ya kutoa hoja chini ya Kanuni hii aweza kusimama mahali pale na kutoa taarifa ya mdomo kwamba anakusudia kuleta hoja ya kuunda Kamati Teule. Baada ya hapo Mbunge huyo atatoa taarifa ya hoja yake kwa maandishi kwa Katibu na hoja hiyo itashughulikiwa wakati unaofaa kwa kuzingatia mpangilio wa shughuli uliowekwa na Kanuni ya 24(3)". Kwa hiyo, basi tunategemea Mheshimiwa Mrope ataleta hoja hiyo. *(Makofi)*

**MHE. KISYERI W. CHAMBIRI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho wa mwaka 2002, Kampuni ya *AMGM* ambayo inachimba dhahabu Tarime ilichukua eneo jipya kwa ajili ya kuchimba dhahabu kwa hiyo iliwataka wananchi wahame. Lakini kitu cha kushangaza ni kwamba kabla wananchi hao hawajahama mali yao ilianza kuharibiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa nina picha chache moja ni shamba ambalo lilivurugwa nyingine ni picha ambapo Askari wetu wanasimamia kuhakikisha kwamba wananchi mashamba yao yanavurugwa na nyingine picha ambayo inaonyesha kwamba hao wananchi ambao hawajahama wamezungushiwa uzio kwa hiyo wako jela kinyume cha kupenda kwao. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Waziri ndiye anatoa leseni za watu kuchimba dhahabu, ninachoomba Waziri afanye awaamrishe hawa watu aliowapa leseni waondoe jela yao kwa wananchi hawa, picha ndio hii, kusudi hawa wananchi ambao wako katika sehemu yao waweze kupata uhuru kamili kabla hawajalipwa hizo fidia zao maana yake sifikiri ni jambo la kiungwana kumzungushia mtu ndani ya *fence* halafu baadaye awe jela ndio ahame hii inapingana na Katiba yetu na ni kinyume cha haki za binadamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kwamba hao wananchi toka mwezi wa kumi na mbili wamezuiwa kulima na wako jela hawawezi kufanya shughuli yoyote basi pia waangalie utaratibu hiyo kampuni itakayotumia waweze kuishi mpaka watakapoenda eneo jipya. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri sababu hao ni watu wako na unawapa leseni naomba uweze kushughulika na utoe majibu jinsi utakavyosaidia wananchi ambao wako ndani ya uzio.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri!

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Taarifa!

**MWENYEKITI:** Taarifa, ndio za Serikali na jibu.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla hujamruhusu Mheshimiwa Waziri...

**MWENYEKITI:** Unajibu wewe ni Serikali.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Aah. Nilikuwa natoa taarifa kwamba hao anaosema wamezungushiwa kwenye uzio na anasema kwamba wako jela kwa mujibu wa utaratibu wetu wa Magereza hiyo siyo jela. Jela ziko kwenye Magereza maalum ambayo yanajulikana.

*(Hapa Wabunge Walizomea ikiwa ni ishara ya kupinga taarifa hiyo)*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tumesikia taarifa ambazo Mheshimiwa Mbunge ambazo amezitoa tunamwomba atupatie vielelezo vyote ili tulishughulikie suala hili kikamilifu kwa lengo ya kuhakikisha kwamba haki inatendeka. *(Makofi)*

**MWENYEKITI**: Mheshimniwa Mbunge, nadhani utapeleka vielelezo vyote kwa Mheshimiwa Waziri halafu atatueleza jinsi mlivyoshughulikia. Sasa ni Mheshimiwa Mutungirehi!

**WABUNGE FULANI:** Bado!

**MHE. KISYERI W. CHAMBIRI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba nitapeleka vielelezo lakini muda haungojei mtu na Serikali yetu tunaelewa inavyoshughulikia mambo huwa inachukua muda murefu, sasa muda huo wa kushughulikia na njaa ile ya watu itashughulikiwaje? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, unaweza pia ukaleta vielelezo mezani hapa au upeleke leo!

**MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niko kwenye *vote* hiyo hiyo, programu ya 10, 250100. Katika mchango wangu wa maandishi, nilimwuliza Mheshimiwa Waziri kwamba mwaka jana iliundwa Tume ya *General Mboma* kuchunguzwa kuwekwa nembo katika madini ya *Tanzanate* lakini mpaka sasa hatujapata taarifa hiyo. Kwa kupitia Bunge hili Tukufu, namwomba Mheshimiwa Waziri kwa sababu zilitumika hela za wapiga kura na walipa kodi kuunda Tume hiyo na kuigharamia atupe maelezo juu ya Tume hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata Mheshimiwa Rais anapokuwa anaunda Tume mbalimbali amekuwa akitoa matokeo kwa hiyo tunadhani walioko chini yake lazima watuambie taarifa hizo kama tunazipata. Sasa nataka kujua kama Mheshimiwa Waziri ataitoa kwenye Bunge hili likiwa linaendelea ili na wananchi waweze kuipata?

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Tume hiyo ya *General Mboma* iliundwa na ilindwa na Waziri wa Nishati na Madini na *General Mboma* amemaliza kazi yake ameripoti kwa Waziri na hatua zimeanza kuchukuliwa kutekeleza yale ambayo yanahitaji kutekelezwa kutokana na ripoti hiyo kwa mfano kuifanya sehemu ya Mererani kuwa *controlled area,* kuweka vitambulisho na masharti mbalimbali ambayo yatasaidia kuboresha uchimbaji wa *Tanzanite* kule Mererani. Kwa hiyo, Tume hiyo tuinatekeleza na kama nilivyosema ilikuwa ni ya Waziri sikujua kwamba inatakiwa iletwe Bungeni kwa sababu yoyote ile lakini tunatekeleza yale ambayo yanahitaji kutekelezwa ili tuweze kuboresha sekta hiyo ya madini.

**MHE. BENIDICTO M. MUTUNGIREHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, yeye anasema ilikuwa ni ya Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Rais aliunda Tume ya Warioba ya Rushwa, ameunda Tume ile iliyokwenda Zanzibar lakini ametoa matokeo hayo kwa wananchi. Sasa katika uwazi na ukweli ndio tunaomba na sisi tujue kilichochunguzwa na Tume hiyo ili tuweze kujiridhisha kwamba yanatekelezwa na kama tunaweza basi tuwe tunauliza maswali kutokana na mwanga tulioupata sisi wananchi, vyombo na ndio maana tunafuatilia. Kwa hiyo, sio jibu kwamba wanatekeleza kule kimya kimya ila tunataka na sisi tujue kilichokuwa kinaendelea.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakubali kwamba tutaleta taarifa ya Tume hiyo mapema iwezekanavyo hapa Bungeni. *(Makofi)*

**MHE. CAPT. THEODOS J. KASAPIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nazungumzia program ya 10, *Sub Vote 1100,* mshahara wa Waziri. Alipokuwa katika ziara ya Wilaya ya Ulanga tulipata matatizo ya kuzimiwa umeme akiwa pale kwa muda wa masaa saba, narudia, Waziri Mkuu wa nchi hii akiwa Mahenge umeme umezimwa kwa muda wa masaa saba lakini umeme huu umeendelea kuzimika mara kwa mara toka jana mpaka hivi ninavyozungumza Mahenge hakuna umeme. Hivi sasa Mheshimiwa Waziri anakubali kutuma mafundi kwenda Mahenge wala sio Mafundi wa Morogoro mafundi wa Dar es Salaam wa Morogoro ndio waliomzimia umeme Waziri Mkuu... *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, unasema ulizimwa au ulikatika?

**MHE. CAPT. THEODOS J. KASAPIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti au niseme umekatwa kwa makusudi na *TANESCO? (Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali haipendi wananchi wake wawe katika shida na kutokana na tatizo ambalo amelisema sasa hivi basi tutachukua kuhakikisha kwamba tatizo hilo linafanyiwa kazi.

**MHE. CAPT. THEODOS J. KASAPIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni *Captain* wa Jeshi, nataka jibu la hakika, nasema mafundi waende Mahenge kesho. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi ninavyozungumzia hakuna umeme. Narudia tena, mafundi waende Mahenge, kesho, na shukuru sana. *(Kicheko/Makofi)*

**MWENYEKITI:** Kama wewe *Captain* wa Jeshi hapa sio Jeshini, Waziri amesema atashughulikia suala hili sasa naomba tumwamini.

**MHE. HALIMENSHI K.R. MAYONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Mheshimiwa Waziri Mkuu alipokuja Kigoma, kwanza nimshukuru amekuwa akitembea sana lakini tangu nimekuwa Mbunge mwaka 1990 Mawaziri wa Nishati na Madini mpaka aliyepo sasa hivi hawajafika Mkoa wa Kigoma...

**MBUNGE FULANI:** Hawajui.

**MHE. HALIMENSHI K.R. MAYONGA:** Hawajui ila Waziri Mkuu yeye amekuwa akifika na tatizo analoambiwa ni umeme wa *grid* haupo. Hivi katika Tanzania hii inapokuwa Mikoa mingine yote ina umeme wa *grid* ukaubakiza Mkoa wa Kigoma, ni manamba? Sasa umeme wa *grid* unaenda lini, mwambie ajibu. *(Kicheko/Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, naomba msitoe hotuba mwulize maswali mwelezwe. *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kuhusu kutembelea Kigoma, napenda kutoa ahadi kwamba tutakwenda Kigoma baada ya Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili kuhusu umeme wa *grid,* hivi tunavyozungumza kuna mradi wa kufanya tathmini au *survey* kutoka Tabora kwenda Kigoma kwa ajili ya kupata tathmini ya uhakika ya kufikisha umeme wa grid Mkoa wa Kigoma ni mradi ambao unafanyiwa kazi sasa hivi.

**MHE. HALIMENSHI K.R. MAYONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hayo majibu yanaanza lini maana akisema Tabora, Tabora, inaanza lini je tathmini hiyo na *feasibility study* imeshafanyika? Kwa sababu ni muda mrefu wanakuambia upembuzi yakinifu ni hoja zinazojengwa humu Bungeni anapokuja Waziri Mkuu, Rais inakuwa ni *embarrassment* sisi tunapata taabu. Hebu ajaribu kufupisha huo muda, tuelewe tu hilo.

**MWENYEKITI:** Kwanza ukubali utamkaribisha, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tathmini inayofanywa ndio itakayotuwezesha kuhakikisha kwamba zinapatikana fedha za kufikisha umeme Kigoma. Tathmini hiyo inafanywa sasa kutokana na mradi ambao tayari upo ambao utatekelezwa mwaka huu wa kupeleka umeme Urambo - Kaliua na kutoka Kaliua ndio tathmini hiyo inafanywa kuupeleka Kigoma. Napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba tunajua umuhimu wa kupeleka umeme Kigoma na kazi hii hivi sasa ndio inaanza kufanywa.

**MHE. DR. JAMES M. WANYANCHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nachangia nilimueleza Mheshimiwa Waziri kwamba mradi wa kupeleka umeme Serengeti umekuwa katika bajeti ya 2001/2002, 2002/2003 na leo umo ndani lakini kazi hiyo haijaanza na hakuna lolote ambalo naona linafanyika. Namwomba Mheshimiwa Waziri anihakikishie hapa ndani leo kazi ya kusambaza nguzo inaanza lini na umeme utawaka lini mji wangu wa Mugumu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niliwambia Mheshimiwa Waziri kwamba migodi ya Tanzania tumeianzisha vibaya na kila mtu analia, hatuna share mle ndani, hatupati ruzuku yoyote. Nikamweleza kwamba tuunde Tume ya kuchunguza mikataba ile na mikataba mipya isianzishwe mpaka Tume hiyo imemaliza kazi?

Mheshimiwa mwenyekiti, je, Waziri anatuhakikishia kwamba Tume hiyo itaundwa? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** La pili tunasema sio Waziri aunde Tume wenye shida ni Waheshimiwa Wabunge, kifungu 104 kinaruhusu kufanya hivyo. Mheshimiwa Waziri kwa sehemu ya kwanza ya swali.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumthibitishia Mheshimiwa Dr. Wanyancha kwamba umeme wa kwenda Serengeti kama ambavyo nimejibu wakati nachangia ni mpango wa uhakika na baada ya taratibu zote hizi kukamilika za kupata mkandarasi na kadhalika tunatarajia kwamba ujenzi utaanza kabla ya mwisho wa mwaka huu.

**MHE. DR. JAMES M. WANYANCHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hajazungumzia Tume, sasa natoa hoja kwamba Tume kwa ajili ya kuchunguza suala hili iundwe kwa kufuata Kanuni ya 104.

**MWENYEKITI:** Haya, tunaendelea, Mheshimiwa Marwa.

**MHE. IBRAHIMU W. MARWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Katika mchango wangu wa maandishi nilieleza malalamiko ya wakazi wa mji wa Musoma ambao kwa muda mrefu wamepeleka maombi yao ya kuunganishwa umeme na *TANESCO* haijafanya hivyo kwa zaidi ya miaka mitatu.

Nilipojaribu kufuatilia suala hilo, uongozi wa *TANESCO* Mara walinieleza kwamba zinahitajika kama shilingi milioni 100. Makusanyo ya mwezi ya Mkoa ni zaidi ya Sh. 200 milioni lakini maombi haya hayajashughulikiwa kwa kipindi cha zaidi ya miaka mitatu.

Je, Waziri anaweza kunihakikishia kwamba tatizo hili ambalo limekuwepo kwa muda mrefu linatafutiwa ufumbuzi kwa maana kwamba *TANESCO* Makao Makuu waruhusu sehemu ya fedha zinazokusanywa katika makusanyo ya Mkoa ziweze kutumika kukamilisha uunganishaji wa umeme kwa hawa wakazi wa mji wa Musoma Mjini?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa hilo ni jambo mahsusi la wateja kwenye eneo lake, namwomba Mheshimiwa Marwa baada ya hapa tuwasiliane ili tujue namna ya kulitatua suala hilo.

**MHE. EMMANUEL E. KIPOLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Sheria ya Madini ya mwaka 1998 tafsiri ya madini inajumuisha na udongo. Kwa kawaida madini kabla hayajaondoka nchini yanatakiwa kulipiwa ile *royalty* kwa sababu udongo unaotoka nchini haulipiwi *royalty* napenda kupata maelezo ni nani aliyeamua kuvunja sheria hii? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, udongo ambao unapelekwa nje ni udongo ambao umechanganya *gold, silver and copper* na hasa hasa unatoka Kahama ndiko ambao kuna miamba ya namna hiyo na wale wenye kiwanda pale hawana uwezo kutenganisha madini hayo.

Lakini udongo huo ukishapelekwa Japan madini hayo yakishatenganishwa wanaambiwa ni kiasi gani cha dhahabu, *silver* na *copper* halafu *royalty* inalipwa kutokana na kiasi hicho ambacho kinapatikana na rekodi hizo zinawekwa wakati wote na tunafuatilia hatuna wasiwasi kwamba labda *royalty* itapotea katika kiasi hicho.

**MHE. EMMANUEL E. KIPOLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, jibu la Mheshimiwa Waziri halihusiani na swali langu. Nimesema kwamba kile kiasi cha dhahabu kinachochambuliwa kule ndicho tu kinacholipiwa hiyo royalty lakini ule udongo mwingine ambao kwa tafsiri ya sheria nao ni madini haulipiwi na haurudishwi! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashauri kama alivyokuwa ameshauri Mheshimiwa Mongella kwamba bora basi zoezi hili lisimame ili tulifanyie uchambuzi wa kina. *(Makofi)*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda niifahamishe Kamati yako Tukufu kwamba Sheria ya Madini inasema wazi ni kipi kitalipiwa mrahaba au mrabaha yote ni hayo hayo. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, udongo sio miongoni mwa yaliyoainishwa kulipiwa mrabaha. Kama alivyoeleza Mheshimiwa Waziri, udongo ambao unasafirishwa, kinachotafutwa kwa madhumuni ya Sheria ya Madini ili Serikali ipate haki yake ni yale madini ambayo yanakwenda kutenganishwa yaani shaba, dhahabu na fedha.

**MHE. EMMANUEL E. KIPOLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu bahati nzuri sheria hiyo ninayo hapa, lakini kwa bahati mbaya muda wako hauturuhusu, lakini kifungu cha 86(1) kinasema: "Madini yatalipiwa mrahaba kwa maana ya *minerals"*. Lakini ukienda kwenye tafsiri ya *minerals* kwa vyovyote ukiisoma inakwambia udongo umo kwenye hiyo. Sasa mimi sijaridhika na majibu yote, kama yapo mengine ya ziada naomba.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda tu nimsisitizie Mheshimiwa Kipole, udongo hata yeye anapojenga nyumba yake nimwulize anapokwenda kuuchukua Serikali haimtozi *royalty,* ndiyo ukweli lakini .....

*(Hapa Waheshimiwa Wabunge walizomea)*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Ngonjeni niendelee.

**MWENYEKITI:** Naomba mumsikilize.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Ninachosema hapa tafsiri sahihi ya Sheria ya Madini na masuala ya royalty ni madini ambayo yameainishwa kwa madhumuni ya kulipita *royalty.* Sasa udongo kwa maana yake anayoipatia siyo sehemu ya kulipia *royalty* na siyo madini, napenda tuelewane kabisa hapa.

**MHE. PARSEKO V. KONE -** Kuhusu utaratibu.

**MWENYEKITI:** Kanuni gani?

**MHE. PARSEKO V. KONE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kulingana na kanuni za Bunge kifungu 56(1) kinasema hivi: "Mbunge anayependa mjadala unaoendelea juu ya hoja yoyote uahirishwe hadi wakati wa baadaye aweza kutoa hoja kwamba mjadala sasa uahirishwe na atataja anataka mjadala uahirishwe mpaka lini". *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa....

**MWENYEKITI:** *Order.* Mheshimiwa Mbunge soma na kifungu kingine cha pili, hapo hapo.

**MHE. PARSEKO V. KONE:** Cha pili hicho ni cha kwako kwa sababu kinasema: "Kama Spika atakuwa na maoni kwamba kuwasilishwa kwa hoja hiyo ni kinyume cha utaratibu wa uendelezaji bora wa shughuli za Bunge aweza kukataa". Sasa hilo ni lako, ndiyo maana mimi nimetoa hoja hiyo wewe ukubali au ukatae. *(Makofi/Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge hoja ya kusitisha haipo. Tunaendelea na orodha ya wale waliotaka kuzungumza. Kwa hiyo, tunaendelea na Mheshimiwa Mulyambatte, ahaa Mheshimiwa Kipole.

**MHE. EMMANUEL E. KIPOLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sijaridhika na hayo majibu, basi naomba tupitishe kwa pungufu ya shilingi moja yangu.

**MHE. JEREMIAH J. MULYAMBATTE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nimechangia kwa maandishi nilikuwa nimemwuliza Mheshimiwa Waziri kwamba huu usombaji wa mchanga ambao Mheshimiwa Kipole ameusema hili nilikuwa nimesema kwamba watu wanafanya *sampling* kuchukua udongo ambao una almasi. Wilaya ya Meatu mpaka sasa hivi kuna watu ambao wanachimba almasi, lakini wanajifanya kwamba wanachukua mchanga wenye almasi wanakwenda kupima sehemu za Uholanzi. Sasa nikaomba anipe maelezo, lakini alipojibu ni kwenye upande wa dhahabu. Lakini kwenye almasi kama kuna mtu ambaye anasomba udongo huo pamoja na almasi hiyo huyo tunamweka katika sheria gani, anayechukua udongo wetu pamoja na almasi yetu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mulyambatte, kufuatana na kifungu 49(10) ndiyo suala alilokuwa anazungumzia Mheshimiwa Kipole, kwa hiyo hupaswi kurudia. Mheshimiwa hilo ni suala la mchanga na udongo ambalo Mheshimiwa Kipole amezungumza sidhani kama Waziri atakuwa na majibu mengine zaidi ya yale aliyojibu mwanzo.

**MHE. MARTHA M. WEJJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mimi ninaomba Waziri aniambie amechukua hatua gani kwa huyu msomi aliyebobea kuandika *cheque* kupeleka benki ili achukue pesa akalipie umeme, ni hatua gani imechukuliwa kwa sababu tayari ameshatutia dosari Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwamba tunabagua Serikali ya Zanzibar na Serikali ya Tanzania Muungano? Wakati huo huo watu wakaandamana, baada ya kukatwa umeme na pesa zikapatikana baada ya saa chache tu kupita? Kwa nini hakufanya hiyo kazi kabla ya muda huo? Naomba jibu kamili.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Wejja suala hili lilishughulikiwa na Mheshimiwa Kidawa, kwa hiyo wewe unarudia.

**MHE. MARTHA M. WEJJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani. Kidawa kauliza mambo mengine, mimi nazungumzia habari ya *cheque* na mwandika cheki. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyoeleza mapema, wiki ijayo nitakutana na Mheshimiwa Waziri Saddat wa Nishati kule Unguja na hilo ndilo moja ya mambo ambayo tutayazungumzia kuona ilikuwaje *cheque* ikaandikwa ambayo ili-*bounce* na kutufikisha katika hali hii ya kusikitisha kuhusu umeme wa Zanzibar.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge niliwaambia ikifika kasoro dakika kumi tunafunga kazi hii ndiyo utaratibu. Mheshimiwa Njelu Kasaka, Kanuni za Bunge.

**MHE. NJELU E. M. KASAKA:** Kanuni ya 86(3) na (7) ya Kanuni hiyo hiyo nataka kusema kwamba mwenendo unaotawala Kamati ya Bunge zima nasema Kanuni Namba (3): "Mjumbe yeyote anayetaka kutoa hoja kwamba majadiliano ya Kamati ya Bunge Zima yaahirishwe mpaka wakati mwingine wa baadaye, anaweza kutoa hoja hiyo wakati wowote kwa maneno yafuatayo: Kwamba Waziri anayehusika atoe taarifa, yeye Waziri atoe taarifa kwa Bunge juu ya maendeleo ya kazi ya Kamati hii na kuomba ruhusa Kamati hii ikutane tena baadaye". *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kanuni ndogo ya (7) ya kanuni hiyo 86 inasema: "Kamati ya Bunge Zima yaweza kuamua, Kamati ya Bunge Zima yaweza kuamua baada ya hoja kutolewa kwamba shughuli hiyo iliyo mbele yake wakati huo irudishwe au ipelekwe kwanza katika Kamati ya Kudumu inayohusika. Kwa sababu suala hili linaonyesha *interest* kwa watu wengi, lina manufaa kwa Bunge na nchi nzima liahirishwe, natoa hoja hii liahirishwe. *(Makofi)*

*(Hapa Wabunge fulani walisimama kuunga mkono hoja)*

**MWENYEKITI:** Naomba Waheshimiwa Wabunge, mkae wakati Spika anaongea. Mheshimiwa Mbunge anazungumzia Kamati ya Bunge Zima, Kamati ya Bunge Zima inahusiana na Miswada. Sasa ni

wakati wa fedha ni Kamati ya Matumizi ya Fedha. Kwa hiyo, Kanuni zinazotumika ni za matumizi ya fedha.

Muda umekwisha, kwa hiyo tunatumia kifungu 122 ambacho kinasema: "Iwapo jambo au shughuli yoyote haikuwekewa masharti katika kanuni hizi Spika ataamua desturi na utaratibu wa kufuata katika jambo au shughuli hiyo na uamuzi huo pia utaingizwa katika kitabu cha maamuzi ili kuongoza mwenendo wa baadaye".

Kwa hiyo, ninachoamua sasa waliosimama kuzungumzia kifungu walikuwa karibu 30, sasa thelathini maana yake ni kama siku nyingine ya kujadili Mswada. Kwa hiyo, kwa uamuzi huu sasa tunapitisha fungu moja tu la mwisho kitabu cha nne na cha pili.

Fungu 58 - Wizara na Nishati na Madini ... Shs. 25,365,980,000/=

*(Fungu lililotajwa hapo juu lilipitishwa na Kamati bila mabadiliko yoyote)*

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 58 Wizara ya Nishati na Madini**

Fungu 58 - Wizara ya Nishati na Madini ... ... Shs. 102,091,552,300/=

*(Fungu lililotajwa hapo juu lilipitishwa na Kamati bila mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa taarifa kwamba Kamati ya Matumizi imeyapitia Makadirio ya Wizara ya Nishati na Madini, kwa mwaka wa fedha 2003/2004, Kifungu kwa Kifungu....

*(Hapa Waheshimiwa Wabunge walizomea)*

**MWENYEKITI:** Sema Fungu kwa Fungu.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ngoja nianze tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa Taarifa kwamba Kamati ya Matumizi imeyapitia makadirio ya Wizara ya Nishati na Madini kwa mwaka wa fedha 2003/2004, fungu kwa fungu na kuyapitisha bila mabadiliko yoyote. Hivyo naomba kutoa taarifa kwamba sasa Bunge lako Tukufu liyakubali makadirio haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Wizara ya Nishati na Madini Kwa Mwaka 2003/2004 Yalipitishwa na Bunge)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge kama alivyosema Spika asubuhi Wizara hii inatakiwa ipewe zaidi ya muda wa siku moja. Kwa hiyo, hilo alili- *note* asubuhi Mheshimiwa Spika. Kwa hiyo, matatizo haya ni kwa sababu muda uliokuwepo ni mfupi. Kwa hiyo, watu wengi wangeweza

kuzungumza, kwa sababu wamekuwa zaidi kuliko wale ambao walipewa nafasi ya kuzungumza. Kwa hiyo, inaeleweka tatizo hili linatokana na kwamba Wizara ni kubwa inahitaji muda zaidi wa siku moja. Sasa naahirisha Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 01.43 Usiku Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Ijumaa Tarehe 25 Julai, 2003 Saa Tatu Asubuhi)*